

# **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Ishirini na Tano – Tarehe 19 Julai, 2006**

*(Mkutano Ulianiza Saa Satu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama kawaida tuna baraka za kuwa na wageni. Pale kwenye *Speakers Gallery* wapo wageni ninaowathamini sana nao ni Viongozi wa Kitaifa wa Chama cha Walimu hapa Tanzania, wakiongozwa na Ndugu Gracian Mkoba, Kaimu Rais wa Chama cha Walimu Tanzania. Aonyeshe mkono, yule pale.

Ndugu Yahya Msurwa, Katibu Mkuu wa Chama cha Walimu Tanzania. Yule pale. Ndugu Mahomed Hutali Mweka Hazina Taifa wa Chama cha Walimu. Halafu wenyeji wao ni Ndugu Lucas Luhobo, Mwenyekiti wa Wilaya nadhani hapa Dodoma na Ndugu Sudi Mercy, Katibu wa CWT Wilaya. Ahsanteni sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia Wajumbe wa Bodi ya Vyama vya Akiba na Mikopo *SACCOS* kutoka Jimbo la Chilonwa kwa Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje.

Naomba pale walipo wasimame. Mheshimiwa Manju Msambya anaye mgeni kwenye *Gallery* ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma. Ahsante sana. *(Makofi)*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA):** Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007.

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:** Maoni ya Kamati ya Huduma za Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007.

**MHE. PHARES K. KABUYE - MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI:** Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu kwa Mwaka wa Fedha uliopita, Pamoja na Maoni kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007.

### **MASWALI NA MAJIBU**

Na. 233

**MHE. ALYOCE B. KIMARO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Hospitali ya Wilaya ya Moshi katika Mji Mdogo wa Himo hasa ikizingatiwa kuwa Wilaya hiyo haina hospitali ya Serikali?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce Beni Kimaro, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Wilaya ya Moshi Vijijini haina Hospitali ya Wilaya. Wananchi wa Wilaya ya Moshi Vijijini wapatao 401,369 wanapata huduma za Afya katika Hospitali nne, hospitali teule mbili za Kilema katika Kijiji cha Rosho na Hospitali ya Kibosho zilizoko chini ya dhehebu la Katoliki. Pia zipo Hospitali ya Marangu katika kijiji cha Marangu Arisi, inayomilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kulutheri Tanzania na Hospitali ya TPC iliyoko chini ya Kampuni ya Sukari ya TPC. Pia viro vituo viwili vya Afya vya Mwika katika Kijiji cha Msae na Kituo cha Afya cha Kirua katika kijiji cha Kwamare. Vituo vyote vinamilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Moshi Vijijini. Vilevile zipo Zahanati 32 za Serikali, Zahanati 26 za Mashirika ya Dini na Zahanati 12 za watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa Serikali haina mpango wa kujenga Hospitali ya Wilaya katika Wilaya ya Moshi Vijijini. Hata hivyo, Serikali kupitia Halmashauri ya Moshi Vijijini katika mipango yake kwa mwaka 2006/2007 imetenga jumla ya Sh.50,000,000/= ili kuanza ujenzi wa Kituo cha Afya katika Mji Mdogo wa Himo. Fedha hizo zitapatikana kupitia mradi wa kuimarisha Serikali za Mitaa *LGDCG*. Katika mipango ya baadaye ya Halmashauri itazidi kukipanua kituo hicho na kuwa Hospitali ya Wilaya hatua kwa hatua kulingana na hali ya upatikanaji wa fedha. Kwa wakati huu nawashauri wananchi wa Wilaya ya Moshi Vijijini waendelee kutumia Vituo vya Huduma za Afya viliwyopo katika Wilaya hiyo.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa, Serikali imekubali itajenga Kituo cha Afya katika Mji Mdogo wa Himo. Je, Serikali iko tayari kutoa ramani ya Hospitali ya Wilaya ili kwa kupitia wafadhili ambao wananchi watatafuta tuenze kujenga hiyo Hospitali sambamba na hicho Kituo cha Afya?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMI (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOAA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, Wizara inazo ramani za aina zote za Vituo vya kutolea Huduma za Afya kuanzia Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali za Wilaya na Mkoa. Kwa hiyo, ningependa kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba tunayo ramani na tutashukuru kama atatutafutia wafadhili na tuko tayari kutoa ushauri kwa sababu ramani zinaweza zikatofautiana kufuatana na mazingira hospitali inapojengwa.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Waziri wa Afya na Ustawi na Jamii na Naibu Waziri wa TAMISEMI. Naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa hospitali nyingi zilizoko Mkoani Kilimanjaro ni za Taasisi na za watu binafsi; na kwa kuwa Hospitali ya Mkoa ya Mawenzi sasa imechakaa na haiwezi tena kuhudumia watu inavyopaswa. Je, Serikali haionti kuwa ni wakati muafaka sasa wa kukarabati hospitali ile ili iwe kwenye hadhi ya kuwa hospitali itakayomudu kuwashudumia wananchi wa Kiliamanjaro kwa bei nafuu, na kwa msaada wa Serikali kuliko ambavyo wananchi wanateseka kwenye hospitali za watu binafsi na Taasisi? (*Makofi*)

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, tuna fungu kupitia TAMISEMI la kukarabati hospitali zetu zote za Mkoa na hiyo itajumuisha Hospitali ya Mawenzi. Ahsante.

Na. 234

#### **Watumishi wa Halmashauri**

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali iliamua kupeleka maendeleo karibu na wananchi; na kwa kuwa, ili lengo hilo litimie panahitajika watumishi wenyewe sifa za kufanya kazi hizo:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia motisha watumishi wanaofanya kazi katika maeneo yenye mazingira magumu ili kuweza kuwashikilia (*retain*)?
- (b) Pamoja na mahitaji makubwa ya watumishi katika Halmashauri; je, ni kwa vigezo vipi au mazingira yapi ambapo Mkurugenzi anaajiri

watumishi wa muda (*temporary staff*) kufanya kazi hizo na anatakiwa ashirikishe Mamlaka zipi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkoo, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mbunge wa Kilindi, lenye sehemu (a) na 9b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, uzoefu umeonyesha kuwa Mazingira magumu katika kazi yanaweza kutohana na kukosekana kwa vitendea kazi na kwa hiyo kumfanya Mtumishi atekeleze majukumu yake kwa shida au matatizo ya miundombinu hasa barabara kwa maeneo ambayo hayafikiki kwa urahisi na hivyo kusababisha kupatikana kwa taabu huduma muhimu za kijamii au kukosekana kabisa. Ili kuhakikisha kuwa watumishi wanakuwa na mazingira mazuri ya kufanya kazi katika ngazi ya Halmashauri, Serikali imekuwa ikifanya yafuatayo:-

- (i) Kuhakikisha kuwa barabara katika maeneo yanayohusika zinapitika.
- (ii) Kuhimiza ujenzi wa nyumba za kuishi watumishi.
- (iii) Kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi.
- (iv) Pia kutoa fursa kwa watumishi wote kujiendeleza katika fani mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, aidha, wote tunafahamu kuwa Serikali imekuwa ikiongeza mishahara ya watumishi mara kwa mara ili kuongeza uwezo wao kifedha. Vilevile hivi sasa Mheshimiwa Rais ameunda Kamati ya kuangalia upya suala zima la mishahara ya watumishi. Hivyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge na watumishi wote kwa ujumla kuwa na subira ili Kamati hiyo itakapokamilisha kazi yake tutapata mapendekezo ya motisha mbalimbali kwa watumishi ikiwa ni pamoja na wale wafanyakazi wanaofanya kazi katika mazingira magumu.

(b) Mheshimiwa Spika, taratibu za kutoa ajira katika Utumishi wa Umma zimefafanuliwa katika Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002 ikisomwa pamoja na kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 kama ifuatavyo:-

(i) Kwa mujibu wa taratibu ya uendeshaji Na.13(1)(d),(e) na (g) Katibu Mkoo, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ndiye mwenye mamlaka ya kutoa vibali vyta ajira ya kudumu na mikataba ya muda kwa nafasi zilizopo katika Ikama ya mwaka husika.

(ii) Baada ya Halmashauri husika kupata kibali cha ajira kwa nafasi zinazopaswa kujazwa. Halmashauri inatakiwa kuzitangaza nafasi hizo na kuchuja waombaji wenyе sifa kwa kutumia Bodi yake ya ajira kwa ajili ya kufanya usaili.

(iii) Halmashauri kabla ya kutoa ajira ya muda ni lazima ijiridhishe kuwa ajira hiyo ni ya kazi ya muda au ya msimu ina ulazima au haihitaji mfanyakazi wa kudumu au mtumishi wa kudumu.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake. Lakini hata hivyo nina maswali mawili madogo ya nyongeza. La kwanza, nakubali kabisa alivyosema tuwe na subira, lakini tuko kwenye Awamu ya Kasi mpya. Subira kwa kweli kwetu kule bila Watumishi hatuwezi kuendelea. Sasa nilikuwa naomba kwa sababu huwezi kumtoa mtumishi Mjini ukamleta akakaa kwenye nyumba ya udongo na barabara yenyewe ni mbovu ni mpaka apande baiskeli na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali kwa makusudi mazima na Mheshimiwa Naibu Waziri akubaliane na mimi kwamba watutazame kwa jicho la pekee Wilaya ya Kilindi kwa sasa mpaka hapo baadaye tutakapopata watumishi, ili na sisi tuweze kusimama kwa miguu yetu. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwa hilo anagalau msukumo wa mwaka mmoja?

La pili, nataka kupata ufanuzi. Jibu tu lilikuwa kwamba kwa kweli kwa ujumla watumishi wa *temporary* hawatakiwi kuwepo. Hili suala limepitwa na wakati. Tayari yameishafanyika, yaliyofanyika na kwa bahati nzuri tayari wameishaajiriwa. Lakini naona siyo utaratibu mzuri Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba mtu anakaa pale kwa *temporary* akisubiriwa kuajiriwa. Kwa sababu ajira ni ya wazi kwa wakati huu. Kwa hiyo, naona hilo tulichukulie ni kosa lilitotokea, lakini limekwisha kurekebishwa na tumepata fundisho.

Mheshimiwa Spika, hilo la kwanza, naomba Mheshimiwa Naibu Waziri akubaliane na mimi kama kweli wanaweza wakatusaidia kwa wakati huu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA;** Mheshimiwa Spika, analolisema Mheshimiwa Beatrice Shellukindo ni kweli. Lakini nataka nikumbushe tu kwamba uamuzi wa kugawa Handeni katika maeneo mawilil ili Kilindi iwe ni Wilaya peke yake na Halmashauri peke yake ilikuwa ni baada ya kutambua kwamba tusipofanya hivyo Kilindi inaweza ikachukua muda mrefu kusonga mbele.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa nataka kwanza Mheshimiwa Mbunge appreciate hilo kwamba ulikuwa ni uamuzi mzito na wa busara sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaelewa kabisa kwamba Kilindi ina matatizo mengi na yote lazima yafanyiwe kazi. Lakini ninalomwomba Mheshimiwa Beatrice Shellukindo ni vizuri tukaenda basi hatua kwa hatua. Tutajitahidi kama Serikali kuona linalowezekana,

lakini kwa kasi anayoitaka na kwa hali ya kifedha tuliyo nayo tutakuwa tunasema uongo kama tutamwahidi kwamba tutakwenda kwa kasi anayoitarajia kwa sasa. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge, kidogo avute subira, lakini tunatambua na tunajitahidi kusaidia kadri itakavyowezekana. Hili la kazi za muda kwa kweli ni katika mazingira kama ya Kilindi tu ndiko tulikolazimika kuchukua hatua kama hiyo ili katika zile hatua za mwanzo angalau tuwe na watu wanaosaidia kusukuma shughuli za maendeleo. Lakini tunakubaliana naye ni jambo ambalo si vizuri likaingia katika utaratibu wa kudumu na sasa tunajizatiti kwa uhakika zaidi kuisaidia Kilindi kuwe na watumishi wa kutosha watakaosaidia kuendesha Halmashauri.

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Naibu Waziri amesema ipo Tume imeundwa na sisi tunashukuru kwamba itatoa matokeo yatakayowafaidisha wafanyakazi. Lakini vilevile amesema wafanyakazi wamekuwa wakiongezwa mishahara. Mishahara ikiongezwa inaongezwa kwa wafanyakazi wote na haifanyi kazi ya kutatua mazingira magumu wanamoishi wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, Jimbo langu mimi ni la Kigoma Kusini hasa Kusini mwa Jimbo lenyewe. Usafiri ni tatizo na bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri amesema usafiri ni moja ya maeneo ya mazingira magumu. Je, Wizara itasaidia vipi kutatua tatizo la watumishi wanaoishi Mwambao mwa Ziwa Tanganyika Kusini mwa Jimbo la Kigoma Kusini ili na wenyewe wajione ni watumishi sawasawa na watumishi wa sehemu nyingine ambapo mazingira yao ya kazi ni magumu sana hasa walimu? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi kwamba barabara ni tatizo mojawapo ambalo linafanya wafanyakazi wengi wasiende katika sehemu hizo. Lakini Serikali imejizatiti. Waheshimiwa Wabunge, mmepitisha Bajeti ya fedha za *Road Fund* jumla ya shilingi bilioni 23 na fedha hizo zitagawiwa katika Wilaya mbalimbali na katika Halmashauri mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge, katika mipango yao ahakikishe kwamba fedha hizo zinatengeneza zile barabara korofi ambazo zinaleta kikwazo kwa watumishi mbalimbali wakiwemo pamoja na walimu. Pia Serikali inajitahidi na kuwahimiza Halmashauri na wananchi kwamba wajenge mazingira mazuri ya walimu ikiwa ni pamoja na nyumba za walimu ili walimu waweze kubaki katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, kadhalika Serikali sasa hivi inajitahidi kuunda Tume ili kuangalia wale watumishi wanaofanya kazi katika mazingira magumu. Ili kuangalia kwamba je, kuna posho yoyote ambayo inaweza ikawasaki wale wafanyakazi wanaoishi katika mazingira magumu. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge tushirikiane katika kujenga mazingira mazuri kwa walimu pamoja na wafanyakazi wengine.

### **Upekuzi wa Askari kwa Raia Wanawake**

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, mara nyingi inapotokea hitaji la kupekuliwa mtuhumiwa, Askari wa kiume peke yao ndio hutumiwa, hata kama upekuzi huo unahusisha chumba cha mtuhumiwa wa kike:-

- (a) Je, Serikali haioni kwamba, kitendo hicho kinachofanywa na Askari ni kinyume cha Sheria na ukiukwaji wa haki za binadamu?
- (b) Je, Serikali haioni kwamba, huo ni unyanyasaji wa kijinsia?
- (c) Je, hali hiyo inafanyika kwa makusudi au ni kutokana na upungufu wa Askari wa kike. Kama ni kutokana na upungufu, kwa nini Serikali isitoe nafasi za ajira zaidi kwa vijana wa kike ili kukidhi haja hiyo na hivyo kuepuka unyanyasaji huo wa kijinsia?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, kabla ya kumjibu Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mbunge wa Viti Malaum, swali lake ningependa kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mwendo wa Mkosa ya Jinai (*Criminal Procedure Act*) Na. 20 ya mwaka 1970 kifungu cha 26 inaeleza kuwa endapo pana ulazima wa mwanamke kupekuliwa, basi ni lazima upekuzi huo ufanywe na mwanamke, ili heshima na utu wa mwanamke uzingatiwe.

Aidha, msisitizo wa aina hiyo pia umetolewa katika Kanuni za Polisi (*Police General Orders*) Na. 272 kifungu Namba 4 kwamba endapo Askari Polisi wa kike atakuwa hayupo kufanya upekuzi, kazi hiyo itafanywa na mwanamke mwingine kwenye eneo la faragha ambapo siyo rahisi kwa mtu mwingine kuona kinachofanyika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, sasa naomba kumjibu Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kitendo cha upekuzi kikifanywa na Askari wa kiume kwa mwanamke ni ukiukwaji wa haki za binadamu. Endapo itabainika kuwa Askari wa kiume amemfanya upekuzi mwanamke, atakuwa amefanya kosa la jinai na kwenda kinyume na kanuni muhimu za Jeshi la Polisi hivyo, atapaswa kuchukuliwa hatua kali za kisheria kwa kukiuka maadili ya kazi yake.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba pale itakapotokea Askari mwanamume akafanyia upekuzi mwanamke siyo tu amefanya unyanyasaji wa jinsia bali pia amevunja sheria na anapaswa kuchukuliwa hatua kali za kisheria.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika swali (a) na (b) kuwa sheria hairuhusu kufanya upekuzi wa aina hiyo. Kila Askari Polisi amefundishwa sheria za msingi za ukamataji na upekuzi ambazo ziko wazi. Iwapo kuna tukio la aina hilo basi huo ni ukiukwaji wa maadili mema ya utendaji kazi katika Jeshi la Polisi ambako kutakuwa kumefanywa kwa utashi wa Askari na si kwa maelekezo ya Jeshi la Polisi au upungufu wa Askari wa kike. Hivyo, Askari wa kiume hawezi kusingizia kutokuwepo Askari mwanamke kwa vile sheria inatoa ruhusa kazi hiyo kufanywa na mwanamke mwininge kwenye eneo la faragha.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na yenye ufasaha.

Lakini naomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba kwa sababu vitendo hivi vimezoleka kufanyika na hakuna hatua zozote zinazochukuliwa dhidi ya wanaohusika. Namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri alithibitishie Bunge hili Tukufu kwamba vitendo hivyo kuanzia sasa havitofanyika na pindi vikifanyika sheria zinazohusika zitachukua mkondo wake.

**SPIKA:** Sijui inakuwaje pale ambapo Askari mwanamke ndiyo anampekua mwanamume. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba mpaka sasa hatujapokea lalamiko lolote la Askari mwanamume kumpekua mwanamke na kama nilivyosema sheria inazungumza wazi kwamba atakayefanya hivyo atakuwa amefanya makosa. Kama Mheshimiwa Mbunge anamjua aliyefanya hivyo atueleze ili utaratibu wa sheria upate nafasi. Sisi siku zote tutasimamia sheria na kuhakikisha kwamba vitendo hivyo havifanyiki.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maumbile ya mwanamke na mwanamume, Jeshi la Polisi halipendelei kwa Askari wa kike kumfanyia upekuzi mwanaume kutokana na athari zake. (*Kicheko*)

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mimi mwenyewe binafsi nilikuwa ni Askari vilevile wa Polisi, sijapata kuona wala kusikia kitendo hicho kinafanyika katika Jeshi la Polisi. Lakini kwa vile yeye mwenyewe amekiri na amesema kwa mujibu wa sheria ni kinyume cha haki za binadamu. Je, kwa Askari mwanamke kumpekua mwanaume nayo si haki za binadamu vilevile?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri amekwisha kulijibu hilo.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri ningependa kuuliza. Kwa kuwa kuna uhaba mkubwa wa Askari wa kike kwa mfano, katika Kituo cha Polisi cha Bumbuli hakuna Askari wa kike hata mmoja. Je, Waziri anayehusika hawesi kufanya utaratibu wa kutumia mgambo wa kike wakawa kama mashahidi wakati anapohitajika kupekuliwa mwanamke katika Kituo cha Polisi?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAI:** Mheshimiwa Spika, Sheria inaruhusu mwanamke yoyote ule kumpekua mwanamke mwenzake. Kwa maana hiyo, mgambo wa kike anayo haki kabisa ya kusimamia ushahidi pale anapohitajika kufanyika hivyo. Aidha, katika Jeshi la Polisi kuna Askari wa kike 6,643 ambao tunaamini wanakidhi haja sana. Katika kipindi cha mwaka huu Askari wa kike waliomaliza mafunzo walikuwa ni 478. Kwa hiyo, pale ambapo kuna upungufu tutahakikisha tunaziba upungufu huo ili mambo yaende vizuri. (*Makofii*)

Na. 236

#### **Udhibiti wa Hakimiliki**

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR** aliuliza:-

Kwa kuwa, wasanii ni kioo cha jamii kwa sababu wanaelimisha, wanafurahisha na kutangaza jina la Tanzania nje ya nchi kupitia nyimbo, michezo ya kuigiza, maonyesho ya vazi la Taifa, kwaya, mashairi na kadhalika:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuelimisha juu ya udhibiti wa hakimiliki ya kazi zao?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar kwamba kazi za sanaa ni moja ya shughuli muhimu katika kukuza elimu, burudani, utamaduni na michezo. Aidha, sanaa huajiri watu wengi ambao huzalisha mali na kuchangia sehemu kubwa ya Pato la Taifa. Katika baadhi ya nchi zilizoendelea shughuli za sanaa huchangia asilimia 6 hadi 8 ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1999 Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ijulikanayo kama *Copyright and Neighbouring Act No. 7* ya mwaka 1999 ili kuboresha ulinzi na ukuzaji wa kazi hizo. Sheria hii ilianza kutumika tarehe 31 Desemba, 1999. Kifungu cha 46 cha Sheria hii kilianzishwa Chama cha Hatimiliki Tanzania yaani *Copyright Society of Tanzania (COSOTA)*.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya chombo hiki ni pamoja na kukuza, kulinda haki za watanzi wa sanii na wachapishaji na kuwaelimisha na kuhamasishwa wanachama wake, asasi na umma juu ya masuala mbalimbali ya hakimiliki.

Mheshimiwa Spika, *COSOTA* inatoa elimu kwa njia ya redio, televisheni, semina kwa wadau mbalimbali kuhusu udhibiti wa hakimiliki kwa wasanii.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza hivi.

Kwa kuwa wasanii ni watu muhimu sana na kwa kuwa mpaka hivi sasa kuna baadhi ya wasanii wanalamikia kuhusu ukiukwaji wa hakimiliki ya kazi zao. Hata kama kimeundwa hicho Chama cha *COSOTA*. Sasa nauliza je, wasanii wamefaidikaje juu ya elimu itolewayo na *COSOTA* na Serikali inawasaidia vipi kutatua matatizo ya wasanii hao?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, tangu *COSOTA* ianzishwe mwaka 2001 imeshafanya Semina katika mikoa 16 Tanzania Bara. Semina hii imewaelimisha na kuwahamasisha wasanii, watanzi pamoja na wachapishaji. Semina hii imezalisha ama imewafanya wasanii hawa na wachapishaji 850 kujiunga na *COSOTA*.

Kwa hiyo, wale wasanii 850 tayari wamesha-rejestra kazi zao 4,100 pale *COSOTA* na sasa hivi zinalindwa na Sheria hiyo Na. 7 ya mwaka 1999. Licha ya hivyo sasa hivi *COSOTA* inashughulikia makusanyo ya mrahaba (*royalties*) kwa ajili ya kuwagawia wale watu ambao wametoa kazi zao katika maeneo ya starehe na majumba mengine kama mahoteli.

Kwa hiyo, sasa hivi Serikali kupitia *COSOTA* bado inaendeleza Semina katika mikoa mingine na vile vile imeajiri watu katika kila mkoa kwa ajili ya kukusanya mirahaba na pia Serikali kwa kupitia *COSOTA* inatoa taarifa mbalimbali za kanuni na sheria za *COSOTA* kupitia redio, televisheni na magazeti.

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja dogo la nyongeza.

Japokuwa *COSOTA* ipo na Mheshimiwa Waziri amesema ipo na inafanya kazi yake. Lakini naomba Mheshimiwa Naibu Waziri akubaliane nami kwamba *COSOTA* haitoshi na haifanyi kazi yake ile inavyotakiwa kisawasawa. Kwa sababu wasanii wetu huu ni ukweli usiofichika kwamba wanafanya kazi kubwa sana katika mazingira magumu lakini wamekuwa wakiibiwa sana, tena sana kazi zao. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuiongezea *COSOTA* watu wengine wa kusaidia kazi au kuweka ulinzi wa kutosha kuwasaidia vijana hawa ukizingatia kwamba wamejiajiri wenywewe. Yaani wameisaidia Serikali katika kujipatia ajira wenywewe. Sasa ni kazi ya Serikali kutoa ulinzi

wa kutosha kwa wasanii hawa ili kulinda kazi zao na wafanye kazi katika mazingira mazuri? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, chombo hiki kimeanza kazi mwaka 2003 na kama nilivyosema kwamba sasa hivi kinaendesha Semina na tayari watu 850 wameshajiunga na chama hiki na kinafanya kazi yake vizuri. Sasa hivi ni kwamba tu tunaongeza vifaa pamoja na ofisi kwenye mikoa kusudi waweze kufanya kazi vizuri. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge asubiri tu mambo yatakuwa mazuri. Sasa hivi labda nipende kumjulisha kwamba kuna malalamiko zaidi ya 80 ambayo yamewasilishwa. Kwa hiyo suala kubwa ni kwamba watu wapate elimu waweze kuelewa maana ya kutunza hatimilki watumiaji na wale ambao wanazalisha.

Kwa mfano sasa hivi *COSOTA* imetengeneza *sticker* inaitwa *Hakigram* ambayo inawekwa kwenye kaseti za *video* pamoja na kanda za kaseti za kawaida kusudi wananchi waweze kuelewa maana ya kutumia hakimiliki. Ahsante. (*Makofi*)

Na. 237

### **Survey ya Sampuli ya Kilimo**

**MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, sasa ni karibia miaka kumi (10) au zaidi tangu *Survey* ya mwisho ya sampuli ya kilimo ilipofanyika mwaka 1994/1995 na kwa kuwa, madhumuni ya *Survey* hiyo ni kupima kwa vitendo maeneo ya uzalishaji ya kilimo na tija ili kuhakiki takwimu za maeneo ya uzalishaji katika Wilaya na Mikoa na hatimaye Kitaifa:-

Je, Serikali sasa ina mpango gani wa kufanya *survey* mpya ili kupunguza dosari za takwimu za uzalishaji wa mazao ya chakula?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Vita Rashidi Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kupata takwimu za uzalishaji za Kilimo, njia kuu mbili hutumika, njia ya kwanza ni ya kutumia vipimo halisi katika sampuli iliyochaguliwa na njia ya pili ni ya mahojiano na wakulima kwa kutumia madodoso. Upatikanaji wa takwimu kwa njia ya kwanza, ulifanyika mwaka wa 1994/1995 kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwa kutumia ufadhili wa Benki ya Dunia. Hata hivyo, *Survey* kwa njia hii ilionekana kuwa ya gharama kubwa.

Mheshimiwa Spika, katika kutafuta namna ya kupata takwimu hizo kwa gharama ndogo bila kuathiri ubora wa takwimu, mwaka 1996 ulifanyika ulinganisho wa takwimu zilizopatikana kwa njia ya kupima na zile zilizopatikana kwa njia ya mahojiano. Matokeo ya ulinganisho huo yalionyesha kuwa takwimu zilizopatikana kwa kupima kwa vitendo zilikaribia kulingana na zile zilizopatikana kwa mahojiano kwa kiwango cha ubora wa kuridhisha. Kwa vile gharama za kupata takwimu hizo kwa mahojiano zina gharama ndogo, *survey* zilizofanyika baada ya ile ya 1994/1995 zimekuwa zikitumia njia ya mahojiano.

Baada ya *survey* ya mwaka 1994/1995, *survey* zimekuwa zikifanyika kila mwaka mpaka mwaka 1999/2000 na *survey* zote hizo zilitumia njia ya mahojiano katika kukusanya takwimu sahihi za uzalishaji wa mazao ya chakula.

Mheshimiwa Spika, mbali na kukusanya takwimu kwa njia hizo mbili nilizozitaja, Serikali inaangalia uwezekano wa kutumia teknolojia ya *Geographical Positioning System (GPS)*, ambayo hutumia satelaiti, kama njia mbadala ya kutuwezesha kupata takwimu za uzalishaji wa mazao kwa urahisi na usahihi zaidi. (*Makofi*)

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa takwimu za sasa za makadirio kama alivyosema Mheshimiwa Waziri za mahojiano ya kutumia madodoso ambazo hazitupi uhalisi wa tani za mazao ya chakula tunayovuna kiwilaya na kinchi ili kupanga vyema mipango yetu iliyosahihii kwa wananchi wetu. Je, Serikali itakubaliana nami iko haja ya kufufua mpango wa *crop cutting survey* kwa kila mwaka wa mavuno ili kupata kiasi halisi cha mavuno ya chakula?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE):** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimpongeze na kumshukuru sana Mheshimiwa Vita Kawawa kwa umakini wake wa kufuatilia takwimu za sekta za kilimo. Kwa sababu hizo zinatuwezesha kufanya mipango yetu na utekelezaji wake kwausahihi wake zaidi. Lakini kuhusu pendekezo lake la kwanza tutumie ile *crop cutting survey* nataka kusema tu kwamba Serikali inaweza kuangalia uwezekano wa kufufua mpango huo ili mradi tu kama mpango huo utakuwa na gharama nafuu pamoja na kutupatia takwimu za usahihi zaidi. Lakini niongeze tu kwamba pamoja hizi *survey* zinazofanyika kila mwaka lakini pia hufanyika tathmini ya mara kwa mara ya kuhakiki mavuno yaliyopatikana ili kuweza kupima hali ya upatikanaji wa chakula nchini.

**MHE. DR. CHRISTANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba idadi ya mavuno yanayopatikana yanatokana pia na kasoro ya wananchi kutumia mbolea kwenye ardhi bila ya kuwa na uhakika kwamba mbolea hiyo ndiyo ingetumika katika maeneo hayo kwa maana kwamba hivi sasa Serikali hajifanya uchunguzi ni aina gani ya mbolea na itumike mahali gani na kwa ardhi gani?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE):** Mheshimiwa Spika, nataka tu nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba endapo wakulima watalima bila kufuata kanuni bora pamoja na utumiaji wa mbolea zinazostahili kusema kweli mazao yatakuwa ni hafifu.

Sasa katika jibu langu la msingi hapa nilipokuwa nazungumzia habari za *survey*, *survey* hizi zinazingatia mambo mengi ikiwa ni pamoja na kuangalia ukubwa wa maeneo, ubora wa maeneo, pamoja na udongo unaostahili, ili kuwezesha kanuni bora za kilimo pamoja na upatikanaji wa mbolea uweze kutumika ili kuweza kupata mazao yanayostahili.

Kwa hiyo, Serikali iko katika hatua mbalimbali za kuhakikisha kwamba jambo hilo linafanikiwa ili tuweze tukapata mazao ya kutosha.

Na. 238

### **Ujenzi wa Barabara ya Dodoma – Iringa**

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, barabara ya kutoka Dodoma kwenda Iringa ni kiungo kikubwa cha mawasiliano na ni muhimu sana kwa uchumi katika Mikoa ya Kusini na ya Kaskazini; na kwa kuwa, tangu Bunge la 1995 – 2000 Serikali imekuwa ikitoa ahadi kuwa barabara hiyo ingetengenezwa kwa kiwango cha lami mara baada ya upembuzi yakinifu:-

- (a) Je, upembuzi yakinifu kwa barabara hiyo umefanyika?
- (b) Kama umefanyika, Je, ujenzi wa barabara hiyo utaanza na kumalizika lini?
- (c) Kama bado haujafanyika, Je, Serikali ina sababu gani za msingi za kutokamilisha jukumu hilo?

Kwa kuwa, barabara ya kutoka Dodoma kwenda Iringa ni kiungo kikubwa cha mawasiliano na ni muhimu sana kwa uchumi katika Mikoa ya Kusini na ya Kaskazini na kwa kuwa, tangu Bunge la 1995 – 2000 Serikali imekuwa ikitoa ahadi kuwa barabara hiyo ingetengenezwa kwa kiwango cha lami mara baada ya upembuzi yakinifu:-

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Jones Galinoma, Mbunge wa Kalenga, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara imekamilisha taratibu za kupata Kampuni ya kufanya usanifu wa kina wa barabara ya Dodoma – Iringa chini ya ufadhili wa *Nordic Development Fund (NDF)*. Hivi sasa uchambuzi wa Makampuni yenye sifa unaendelea utakaofuatiwa na uuzaji wa nyaraka za zabuni ambapo Mkataba wa Usanifu wa kina unategemewa kusainiwa mwanzoni mwa mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, chini ya mpango huu mpya, ni matarajio yetu kuwa mradi utatekelezwa mapema baada ya kuamua kufanya usanifu wa kina moja kwa moja ukifuatiwa na ujenzi wa kiwango cha lami baada ya upatikanaji wa fedha za ujenzi.

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Je, Wizara hii inafahamu kwamba mradi huu umeagizwa katika Ilani ya CCM na umeagizwa na Rais.. Inafahamu kwamba ni juzi tarehe 25 Juni, 2006 Mkutano Mkuu wa Chama umeagiza mradi huu ushughulikiwe. Kama ndivyo inakuwaje bado tunapeleka tarehe mbele ikifahamika kwamba katika muda wa miaka kumi iliyopita ni barabara kiasi cha kilomita 6 tu kutoka Iringa kuja Dodoma ndizo zilizotengenezwa.

Kwa kiwango hicho itapita miaka 40 au 50 bado tunazungumza habari ya upembusi. Kwa nini bado tunazungumza habari ya upembusi, kwa nini tusiweke umuhimu zaidi tuweze kuondoa tatizo hili.

Na swali ambalo linaandamana na hilo ni kwamba kutokana na ubovu wa barabara hii mazao au chakula kutoka Mikoa ya Kusini inapelekwa nchi za nje badala ya kuja katika Mikoa ya Kati, Mikoa ya Kaskazini ni kwa sababu ya ubovu wa hiyo barabara. Kwa nini tusiipe barabara hii umuhimu unaostahili. Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, Serikali inajua sana umuhimu wa barabara hiyo. Na Serikali inakumbuka sana ahadi ambayo iko kwenye Ilani ya Uchaguzi, ahadi ya Rais na vile vile ahadi zilizotolewa wakati wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nimesema katika jibu langu la msingi kwamba barabara hii itajengwa hivi karibuni na ili kujenga barabara lazima hatua ambazo nimezitaja za usanifu wa kina zifanyike.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimesema narudia kumweleza Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wote wa maeneo ya Dodoma na Iringa kwamba ahadi ya Serikali ya kujenga barabara hii katika kipindi hiki cha Ilani ya Uchaguzi 2005/2010 lazima itatekelezwa. Kwa hiyo tuwe na hakika kwamba barabara hii itatekelezwa ndani ya kipindi hiki.

### **Kubomoka kwa Barabara Zilizojengwa kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO** aliuliza:-

Kwa kuwa, barabara zilizotengenezwa kwa kiwango cha lami huwa zinabomoka kwa muda mfupi baada ya kufanyiwa matengenezo, na inapotokea hivyo wala hazifanyiwi ukarabati kwa haraka hivyo husababisha usumbufo mkubwa kwa wenye magari, foleni ndefu na ajali zisizo za lazima:-

Je, kunakuwa na muda gani kwa Mkandarasi kuhudumia barabara iliyokwishatengenezwa?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mbunge wa Viti Maalum , kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara za lami hujengwa kwa kuzingatia viwango vya kitaalam (*design standards*) na ujenzi wake hufanywa kwa kuzingatia viwango vya ubora (*Technical Specifications*). Viwango hivyo ndivyo vinavyotofautisha ubora wa barabara. Barabara zikijengwa kwa kuzingatia viwango hivyo zinatarajiwa kudumu kwa kipindi maalum (*design life*) kabla ya kuhitaji kufanyiwa ukarabati au matengenezo makubwa.

Mheshimiwa Spika, barabara za lami za aina ya *surface dressing* (yaani lami nyepesi) kipindi chake cha kudumu kama imetumika vizuri ni miaka mitano hadi saba. Aidha, zile zilizojengwa kwa kiwango cha lami aina ya *Asphalt Concrete* (yaani lami nzito) kipindi chake cha kudumu kama imetumika vizuri hakipungui miaka kumi na tano (15).

Aidha, gharama za ujenzi wa lami ya aina ya *Asphalt Concrete* ni kubwa ikilinganishwa na ile ya *surface dressing*.

Mheshimiwa Spika, barabara nyingi zilizojengwa kwa kiwango cha lami huanza kubomoka baada ya kipindi chake cha uhai kupita. Hivyo kabla ya kuanza kubomoka, yanatakiwa matengenezo makubwa ya kuongeza uhai ili ziweze kutumika kwa muda mrefu zaidi. Kwa bahati mbaya kipindi hicho cha kufanya matengenezo makubwa kinapofika matengenezo hayo mara nyingi hayafanyiki ipasavyo kutokana na ufinyu wa fedha zinazotengwa kwa ajili ya kazi hiyo katika Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, zipo pia sehemu za barabara ambazo huharibika mapema kabla ya muda wake kutokana na matumizi mabaya ya barabara kwa mfano, kupitisha magari yenye uzito unaozidi uwezo wa barabara husika, kumwaga mafuta (*oil, diesel* na kadhalika) kwenye lami, shughuli za binadamu kama kupitisha huduma za mabomba ya

maji masafi na machafu, umeme, simu na kadhalika hasa kwenye miji ambapo mamlaka husika hukata barabara kuitisha huduma hizo bila kufanya matengenezo sahihi katika sehemu walizokata na hivyo kuanzisha kubomoka kwa barabara husika.

Mheshimiwa Spika, Mikataba yetu ya ujenzi wa barabara ambayo inazingatia taratibu za Kimataifa huweka kipindi cha mwaka mmoja kwa Mkandarasi kuangalia ubora wa barabara kwa gharama zake baada ya ujenzi kukamilika yaani (*defect liability period*).

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ametueleza kwamba kuna viwango tofauti vyatami ambavyo vinatengeneza barabara katika nchi yetu. Lakini tunashuhudia kwamba kuna barabara ambazo zinatengenezwa kwa muda mfupi tu hata huo mwaka mmoja haujafika labda miezi 6 tu zinaanza kutoboka na kuanza kuleta athari na usumbufu kwa wananchi.

Je, ili kudhibiti ubora wa barabara zetu Mheshimiwa Waziri haoni kwamba sasa umefika wakati wakandarasi ambao wanajenga barabara hizo watoe muda maalum pamoja na huo wa mwaka mmoja ambao umetueleza kwa kutengeneza barabara hizi na pale ambapo inaonekana mkandarasi hakutengeneza kwa muda ule kama ulivyosema wa mwaka mmoja. Je, Serikali inachukua hatua gani kwa mkandarasi yule?

Lingine nauliza kwamba je ni kwa nini barabara za mijini hadi sasa hazitengenezwi barabara ndogo ndogo za pembeni ambazo zitasaidia wananchi wanaotembea kwa miguu na baiskeli kupita ili kupunguza ajali?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, Sheria za Mikataba ya ujenzi wa barabara zinaelekeza kwamba mjenzi atumie muda wa mwaka mmoja baada ya kukabidhi barabara kuhakikisha kwamba barabara haiharibiki na anafanya matengenezo hayo kwa gharama zake. Hii ni sheria na tumekuwa tukiizingatia tunafanya matengenezo haya kwa gharama zake.

Hii ni sheria tumekuwa tukiizingatia lakini lakini pale ambapo hata baada ya kipindi hicho barabara inazidi kuharibika Serikali imekuwa ikichukua hatua za kisheria za kukabiliana na wajenzi wa aina hiyo. Moja ni kuangalia kwamba mkandarasi kama huyo hapewi kazi nyingine tena. Lakini kubwa ni kwamba katika kipindi kile wataalamu wa Wizara vile vile wanahakikisha kwamba barabara ile kweli inakidhi matakwa.

Mheshimiwa Spika, inawezekana hatua zikawa zinachukuliwa bila ya watu wengine ambao hawahuksiki na mkataba kwa maana ya Wizara pamoja na mkandarasi kufahamu, lakini hatua hizo zimekuwa zikichukuliwa. Hatuwezi kuongeza kipindi hicho cha *defect liability period* zaidi ya mwaka mmoja kwa sababu ndiyo Sheria za Kimataifa zinavyosema. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie kwamba kwanza kitu ambacho Wizara

itakuwa inafanya na imekuwa ikifanya kwa kweli ni kuhakikisha kwamba inateua Makandarasi ambao wana historia ya ujenzi wa barabara bora na pale inapotokea matatizo kama hayo basi sheria inachukua mkondo wake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutenga maeneo ya watembea kwa mguu kupita. Kwa kweli ndiyo hasa nia ya ujenzi wa barabara hasa katika miji yetu. Katika hifadhi ya barabara katika miji yetu ukiangalia upana ule vile vile kuna nafasi ya kuweka maeneo ya kutembea kwa miguu. Lakini naelewa kwamba kutokana na ukosefu wa fedha Mamlaka zetu za miji zimekuwa zikishindwa kutengeneza vizuri barabara hizo.

Lakini kwa kweli hifadhi ya kutengeneza barabara au njia kwa ajili ya watembea kwa miguu huwa zipo isipokuwa ukosefu wa fedha. Ningependa nisisitize kwamba uwezo unapokuwepo Mamlaka zetu za Miji ziweze kutengeneza vile vile barabara za watembea kwa miguu ili kupunguza ajali kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. ANNE K. MALECELÀ:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa uzembe uliokuwa unasababisha maghorofa yaporomoke ndio chanzo hicho hicho kinachosababisha barabara zetu za lami zisiwe imara. Na kwa kuwa baada ya Serikali kuchachamaa sasa Wakandarasi na Wajenzi wa Maghorofa wamekuwa makini.

Je, Serikali Kuu haioni kwamba kuna umuhimu sasa wa kufanya ukaguzi wa barabara zetu za lami ikiwezekana zote ili kujua ni kiasi gani nchi yetu inajengewa barabaa ambazo hazina hadhi inayostahili? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ningependa kulihakikishia Bunge lako kwamba majengo yote ya heshima yaliyokuwa yanajengwa katika nchi hii yamekukwa na usimamizi mzuri na madhubuti mojawapo ni jengo hili. (*Makofi*)

Majengo yaliyokuwa yanakumbwa na tatizo alilolieza Mheshimiwa Mbunge ni majengo yaliyoanza kienyeji na yakaendelea kujengwa kienyeji na kwa mbinu ambazo sio za kawaida.

Mheshimiwa Spika, barabara hujengwa na Serikali na Serikali ina taratibu za ujenzi wa barabara hizo ambazo tumekuwa tukizieleza hapa usanifu, *detail design* hii yote inalalamikiwa hapa kama lile swali la leo asubuhi la Mheshimiwa Galinoma kwamba mbona hizi *design* haziishi. Ni katika kuhakikisha kwamba kila inchi ya barabara vipimo vyake vinajulikana na ujenzi wake unakuwa kulingana na vipimo.

Barabara hizi pamoja na kwamba sisi Wizara ndiyo tunaosimamia na kujenga, lakini wako Wahandisi wote mnatoka kwenye barabara hizi, kuna Wahandisi mara nyingine ni watu wa humu ndani Bodi za Uhandisi zinazohusika na wa nje na wa Wizara wote watatu wanamsimamia yule mjenzi.

Kwa hiyo, tuna uhakika kabisa kwamba barabara inapokamilika na kukabidhiwa Wizarani yaani inakabidhiwa Serikali, barabara ile imesimamiwa vizuri kwa kila hali. Ila inawezekana kuna maadui wawili wa barabara na nadhani hili ndilo la maana. Adui wa kwanza ni watumiaji wa barabara kutofuata vipimo vya Malori na Mabasi.

Mheshimiwa Spika, ukichukua hii njia hapa kati ya Morogoro na Dodoma hivi nyuma mtakuwa mmeona barabara inanepanepa hivi kazi ile ilifanyika vibaya ni sisi Wizara wenye tuligundua na tumemlazimisha yule mkandarasi kurudia kulingana na vipimo vilivyokuwako. Kwa sababu kati ya Dodoma na Dar es Salaam malori makubwa yanayoleta mizigo hapa Dodoma ndiyo yamekuwa yakiharibu hii barabara na sasa tumerudia na ya pili tumeweka vipimo vya kupima uzito barabarani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachotaka kulihakikishia Bunge lako Tukufu ni kwamba kwa kweli yale mambo ya kienyeji mpaka maghorofa yanaanguka hayafanyiki kwenye barabara. Ila tutashukuru kama tulivyoshukuru viongozi wa Morogoro tukiambiwa kwamba kuna mchezo fulani kwenye barabara ili tuweze kuufuutilia na kuudhibiti mara moja. (*Makofi*)

Na. 240

### **Mafanikio ya Elimu Katika Shule Nchini**

**MHE. SUSAN A. LYIMO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Hayati Baba wa Taifa aliwahi kusema kuwa: “Kulangua elimu ni dhambi” na kwa kuwa, matokeo ya mitihani ya Kidato cha nne kwa miaka ya hivi karibuni yameonyesha kuwa, Shule za Seminari zinazoendeshwa na Taasisi za Kidini zinaongoza kwa kufaulisha wanafunzi kwa kiwango kikubwa kuliko shule nyingine na kwa kuwa, watoto wanaosoma katika shule hizo ni wale ambao wazazi wao wanao uwezo wa kuwalipia katika shule hizo na ndio wanaoendelea na elimu ya juu:-

- (a) Je, Serikali haioni kuwa, kwa utaratibu huo inajenga tabaka la watoto wa matajiri kuendelea na elimu ya juu?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa ruzuku kwa shule binafsi ili wazazi wenye uwezo wa kati waweze kufaidi shule hizo?
- (c) Kwa kuwa, Serikali imedhamiria kuongeza idadi ya wanafunzi kwa mpango wa MMEM/MMES bila kuangalia ubora wa elimu hiyo; na kwa kuwa, Walimu pia wanachangia kwa kiasi kikubwa, katika kutoa elimu bora inayowawezesha wanafunzi wengi zaidi kufaulu;

Je, Serikali haioni kuwa, uwiano kati ya ubora wa elimu na matokeo mazuri ya mitihani unatokana pia na kutowaandaa Walimu kikamilifu kwa

kuwapatia mafunzo ya ualimu kwa wakati muafaka na ndiyo maana matokeo mazuri ya elimu bora hayaonekani katika shule nyingine?

## **NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MWANTUMU**

### **A. MAHIZA) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suzan Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, shule yoyote inaweza kufanya vizuri katika Mitihani kama ina Walimu wa kutosha wanaojituma na wanafunzi wanaojituma ipasavyo na kusimamiwa kwa karibu. Kufaulu vizuri kwa wanafunzi wa Seminari hakujengi tabaka la watoto wa matajiri kuendelea na Elimu ya Juu.

Seminari nyingi zina madhumuni maalum na kwa kawaida hazitozi ada kubwa. Wanaosoma katika Seminari ni pamoja na wa hali ya kawaida na wengi wao hubaki kuendelea na mafunzo ya dini. Aidha, katika mitihani ya kidato cha 6, mara nyingi Shule za Serikali zinazoongoza katika matokeo na hivyo wengi wanajiunga na Vyuo vya Elimu ya Juu.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua na kuthamini mchango wa Sekta Binafsi katika kuisaidia Serikali kutoa elimu kwa raia wake. Kupitia MMES, Shule zisizo za Serikali ambazo haziendeshwi kibashara na siyo Seminari zinaweza kupewa ruzuku kwa ajili ya kununulia vifaa vya kujifunza na kufundishia kutegemea uwezo wa fedha uliopo. Aidha, Serikali inasaidia katika kutoa huduma za ukaguzi wa shule, mitihani ya Kitaifa na kuandaa Walimu wanaaoajiriwa katika shule hizo.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia MMEM na MMES lengo si kuongeza idadi ya wanafunzi tu, bali pia kuongeza ubora wa elimu kwa kuandaa na kuongeza Walimu, vifaa vya kufundishia na kujifunzia, madarasa na nyumba za Walimu katika Shule za Msingi na Sekondari. Ubora wa elimu unapimwa kwa vigezo vingi, ikiwemo Mitihani ya Kitaifa.

Kwa kigezo cha Mitihani, ubora wa elimu inayotolewa unaonekana katika ufaulu wa wanafunzi wa Darasa la Saba, Kidato cha Nne, na Sita kuongezeka kila mwaka tangu kuanza kwa MMEM na MMES. Aidha, Walimu wa kufundisha ngazi zote mbili wanaandalowiwa kwa wingi zaidi na kwa ubora wa hali ya juu.

Pia mafunzo kazini yanatolewa kwa Walimu wa madaraja yote. Hata hivyo ni kweli kuwa tunahitaji kuongeza Walimu wengi zaidi na mafunzo kazini. (*Makofii*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nitaongeza dakika tano kwa kipindi cha maswali kwa sababu tulianza na matangazo ya wageni.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa vyuo vya elimu ya juu, Serikali imeamua kuwapa mikopo hata wanafunzi walioko kwenye vyuo binafsi je, Wizara itakubaliana nami kwamba sasa ni wakati muafaka kwa Wizara kuanzisha mikopo kwa wanafunzi wa sekondari ili wanafunzi wengi zaidi waweze kuendelea na masomo yao ya sekondari kwani wengi wao wanaoacha wana uwezo kiakili lakini wazazi wao hawana uwezo kifedha?

Swali la pili, kwa kuwa Wizara huwa inatoa motisha kwa wanafunzi walifanya vizuri katika mitihani yao ya kidato cha nne na kidato sita. Je, Wizara inawapatia motisha gani walimu ambaa wamewasaidia wanafunzi hao wafanye vizuri zaidi?

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu sehemu ya kwanza ya swali la nyongeza la Mheshimiwa Susan Lyimo kama ifuatavyo. Mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu lengo lake ni kuwakopesha vijana waliokatika vyuo vya elimu ya juu vya umma na sio vyuo vya elimu ya juu binafsi na hii itafafanuliwa zaidi nitakapotoa maelezo yangu ya Bajeti siku ya ijumaa wiki hii, tarehe 22 Julai, 2006.

**SPIKA:** nadhani sehemu ya pili haijajibwa, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundii.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHAZA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba walimu nao hihitaji kupewa motisha na kwa maeneo mbalimbali motisha zimekuwa zikitolewa na hivi karibuni mkoa wa Dodoma ni mionganoni mwa mikoa iliyotoa motisha kwa wanafunzi shule yenye, walimu na watendaji wote wa ngazi ya Wilaya ambaa waliofanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii kutoa rai kwa Halmashauri na mikoa yote kuwapongeza na kutoa tuzo za watumishi bora walimu wote ili waweze kutusaidia kuelemisha watoto wetu kwa, Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya.

Na. 241

### **Sheria ya Ardhi**

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE** aliuliza:-

Kwa kuwa Sheria ya Ardhi iliyopo sasa inatambua kuwa ardhi ni mali ya Serikali na hivyo hulipwa fidia ya mazao na uendelezaji uliofanyika kwenye ardhi endapo itabidi matumizi ya ardhi hiyo au kumilikisha eneo husika kwa mtu au asasi na kwa kuwa wananchi wengi sana wameathirika kutokana na mashamba waliyokuwa wakiyatumbia kwa kilimo, malisho, kuni na kadhalika. Kumilikishwa kwa wawekezaji wa madini:-

(a) Je, ni lini Serikali itarekebisha Sheria hiyo ili utoaji wa fidia kwa ardhi uangalie pia athari zingine (kama kilimo cha mazao yasiyo ya kudumu, malisho,

uchimbaji mdogo mdogo wa madini na kadhalika), zinazotokana na ardhi kumilikishwa kwa taasisi au kampuni badala ya kuangalia tu mazao au uendelezaji uliofanyika kwenye ardhi husika?

(b) Je, Serikali inajiuhusisha vipi kuwatafutia wachimbaji wadogo wadogo maeneo mengine ya kuchimba madini ya dhahabu na madini mengine wakati maeneo yao yanapomilikishwa kwa wawekezaji wakubwa wa nje?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, Mbunge wa Msalala, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali haina mpango wa kuzifanya marekebisho Sheria za Ardhi za mwaka 1999, kwa kuwa zinaelekeza wazi utaratibu wa ulipaji wa fidia kwa wananchi kutokana na ardhi yao kuchukuliwa kwa ajili ya manufaa ya umma. Katika kipindi hiki, Serikali inatekeleza Mkakati wa Kutoa Elimu kwa Umma kuhusu matakwa ya Sheria hizo nchi nzima ili wananchi waliowengi waweze kuzielewa. Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Namba 4 ya mwaka 1999 fungu la 3 (g) na Kanuni za Sheria hiyo zinazoitwa *The Land Assessment of the Value of Land for Compensation Regulation* za Mwaka 2001 zinazoelekeza ulipaji wa fidia na kwa wakati kwa wananchi waliopoteza maslahi katika ardhi husika. Fidia itakayolipwa itajumuisha thamani ya ardhi na uboreshaji usio hamishika, posho ya usumbufu, posho ya safiri, posho ya upangaji na kupoteza faida. Vile vile kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na.5 ya mwaka 1999 fungu la 3(g) na Kanuni za Sheria hiyo ya mwaka 2002, fungu la 13 linaelekeza wazi kuhusu ulipaji wa fidia. Kutokana na matakwa ya Sheria hizo na Kanuni zake wananchi watakoondolewa kwenye maeneo yao wanastahili kulipwa fidia. Fidia itazingatia mazao ya aina zote (Mazao ya kudumu na yasiyo ya kudumu), majengo thamani ya ardhi na posho ya usumbufu. Aidha inaelekezwa kuwa pale panapo kuwa na mimea ya mazao ya musimu, mwananchi anapewa muda wa kusubiri mazoa yapevuke na kuvunwa. Kwa upande wa wafugaji na wachimbaji wadogo wa madini kama wanaikalia ardhi ile kwa mujibu wa Sheria za Ardhi, nao wanastahili fidia.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali hajijuhishi na kuwatafutia maeneo mengine ya kuchimba madini ya dhahabu na madini mengine wachimbaji wadogo wakati wanapoondolewa katika maeneo yanayomilikishwa kwa wawekezaji wakubwa. Kazi ya kubaini maeneo ya uchimbaji wa madini inafanywa na wachimbaji wenyewe. Hata hivyo, ofisi za madini zilizoko hapa nchini huwasaidia wadau wa sekta ya madini kupata taarifa mbalimbali zinazohusu maeneo yenye madini yaliyowazi ambayo yanafaa kwa utafutaji na uchimbaji wa madini wanayohitaji.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa kuna maeneo mengi ya Kata za Kinaga Buliga na Ngaya ambayo yamechukuliwa na Serikali kwa ajili ya bomba kuu la maji kutoka Mwanza kuja

Kahama na bahati mbaya wananchi wale hawajajua ni kiasi gani na lini watalipwa fidia ya maeneo yao. Je Serikali inaweza ikawaambia ni lini na kiasi gani watalipwa?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi ni kwamba kutokana na Sheria ya Ardhi Namba 4. *The Land Assessment of the Value of Land for Compensation* ni kwamba endepo Serikali itachukua eneo kwa ajili ya shughuli za Umma Serikali inawayibika kulipa fidia. Ninachotegema sasa ni kwamba *evaluation* inafanyika na ikishafanyika inaletwa Serikalini au Wizarani kwangu ili *Chief Valier* aweze *ku-certify* na baada ya hapo inarudishwa pamoja na malipo kwa Wilaya ili wanakijiji waweze kulipwa. Kama haijafanyika ninamwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutufatilia na kuhakikisha kwamba wananchi walioondolewa kwa ajili ya miradi ya Umma wanalipwa mali zao ipasavyo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha. Swalii la Mheshimiwa Profesa Mwalyosi tutalipanga kesho. Ndilo lililosalia. Matangazao wapo wageni Madiwani wanane kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kahama, ni wageni wa Mheshimiwa Maige na Mheshimiwa Lembeli, wale pale, karibuni sana Waheshimiwa Madiwani. (*Makofi*)

Upande wangu wa kushoto bado tunao vijana wetu pamoja na walimu wa kutoka Hijra *Seminary* ya mjini Dodoma. Jana niliita sekondari naomba kulekebisha ni *Hijra Seminary* karibuni tena. Napenda kuwafahamisha wageni kwamba Bunge shughuli zake sio hiki kipindi cha Maswali tu naona kunatabia ya wananchi kutokuja jioni kuona shughuli nyingine za Bunge. Kwa hiyo, walimu na wageni wengine, mkitaka kuona upeo mzima wa shughuli za Bunge basi pia inawezekana mkaja hata jioni, mkashuhudia hayo mengine. Kuna mgeni mmoja mashuhuri na muhimu sana kwa mwenzetu mmoja naye si mwingine bali ni Bibi Musalika, Mke wa Mbunge wa Nyang'wale, Mheshimiwa James Msalika, karibu sana. Basi nadhani pengine ametoka. Mheshimiwa William Kusila, Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama anawatangazia wajumbe wa Kamati hiyo kwamba kutakuwa na Mkutano leo tarehe 19 Julai, 2006 saa tano asubuhi, Chumba Namba 219.

Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, anawatangazia wajumbe wa Kamati yake kwamba leo watakuwa na Kikao muhimu cha kuongea na *TRA*, nadhani linahusu lile suala la mafuta. Kikao kitafanyika saa saba mchana, chumba namba 133, ghorofa ya kwanza, jengo la utawala. Wajumbe tafadhili msikose mnaelewa jinsi ambavyo bei za mafuta zinazozungumzwa. Kwa hiyo, kikao hiki ni sehemu ya kupata ufanuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, anawatangazia wajumbe kwamba saa tano asubuhi katika ukumbi Namba 231, ghorofa ya pili, jengo la utawala kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo. Mheshimiwa Athuman Janguo, Mwenyekiti wa Wabunge wa Mkoa wa Pwani anatangazia kwamba mnaombwa Wabunge wote kutoka mkoa wa Pwani mkutane kwa muda mfupi sana mara baada ya kipindi hiki cha Maswali na Majibu. (*Makofi*)

## **HOJA ZA SERIKALI**

### **Makadirio ya Matumizi ya Serikali ya Mwaka 2006/2007 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi**

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii iliyochambua makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako likubali kujadili na kupitisha makadirio ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kupitia CCM kwa kura nyingi kuwa Rais wa Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nampongeza kwa kuchaguliwa na Mkutano Mkuu Maalumu wa CCM kuwa Mwenyekiti wa Taifa wa CCM. Pia nampongeza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa tena kuwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na baadaye kuthibitishwa na Bunge kwa kura nyingi kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nakupongeza wewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa kuchaguliwa na Waheshimiwa Wabunge kuongoza Bunge letu. Nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa kwa kuingia Bungeni. Napenda pia kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kuteuliwa kushika nyadhifa hizo muhimu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kutumia nafasi hii, kumshukuru Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kunituea, na kunipa heshima kubwa ya kuwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kazi ambayo ni kubwa na yenye majukumu muhimu kwa Taifa letu. Nawashukuru pia Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) na Chama cha Walimu Tanzania (CWT) kwa kunifikisha hapa nilipo.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii vilevile kuwapongeza na kuwashukuru Mheshimiwa Dkt. Juma Alifa Ngasongwa (MB), Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa hotuba yake ambayo imetoa tathmini, mwenendo na mwelekeo wa uchumi wa Taifa kwa jumla; na Mheshimiwa Zakhia Hamdani Meghji, Waziri wa Fedha, kwa hotuba yake iliyoelezea kwa ufasaha Bajeti ya Serikali ya mwaka 2006/2007. Bajeti hii imetoa kipaumbele kwa sekta muhimu katika kukuza uchumi ikiwemo Sekta ya Elimu ambayo inao wajibu mkubwa katika Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA) wa kuboresha ufanisi wa nguvu kazi ya taifa kwa njia ya elimu. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu Edward Ngoyai Lowassa, kwa Hotuba yake ya bajeti iliyofafanua mambo muhimu ya elimu yaliyoamuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwa Naibu Mawaziri wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Mwantumu Bakari Mahiza,

Mbunge wa Viti Maalumu Mkao wa Tanga na Mheshimiwa Ludovick John Mwananzila, Mbunge wa Jimbo la Kalambo, kwa ushirikiano, uaminifu na uadilifu wao waliounesha kwangu na kwa viongozi wetu Wakuu Serikalini na kwa watumishi wenzetu wote Wizarani.

Napenda pia kutoa shukrani zangu kwa Katibu Mkoo wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundsi Profesa Hamisi Omar Dihenga na Naibu Katibu Mkoo Ndugu Oliver Paul Mhaiki, pamoja na Afisa Elimu Kiongozi Ndugu Ricky Abiudi Mpama kwa ushirikiano walionipa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na shukrani zangu zote hizo, napenda pia kutoa shukrani zangu kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Omari Shaban Kwaangw', Mbunge wa Babati Mjini, kwa ushauri na maelekezo waliyoyatoa ya kuboresha Bajeti na utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundsi baada ya uchambuzi wao wa kina.

Mheshimiwa Spika, Majukumu ya Wizara, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundsi imekabidhiwa kutekeleza na kusimamia majukumu yafuatayo:-

- (a) Elimu ya Awali.
- (b) Elimu ya Msingi.
- (c) Elimu ya Sekondari Kidato cha 1 hadi 6.
- (d) Elimu itolewayo kwa wenyewe mahitaji maalum.
- (e) Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi.
- (f) Mafunzo ya Ufundsi.
- (g) Mafunzo ya Ualimu Daraja A na Stashahada.
- (h) Kuhakiki na kupima ubora wa elimu kwa kuendesha ukaguzi wa shule na kutoa mitihani ya kitaifa ya Darasa la IV, VII, Kidato cha 2, 4 na 6 na mitihani ya Elimu ya Ualimu na Ufundsi.
  
- (i)Kufanya Utafiti, Kupanga na kuratibu mipango ya elimu.
  
- (j)Kutoa miongozo ya uendeshaji na kusimamia kazi za Taasisi na Mabaraza ya Wizara ambayo ni:-

- (i) Taasisi ya Elimu Tanzania (TET);
- (ii) Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW);
- (iii) Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA);
- (iv) Mamlaka ya Mafunzo ya Ufundsi Stadi (VETA);
- (v) Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania (TLSB); na
- (vi) Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM).

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu hayo Wizara inaongozwa na:-  
(a) Sera ya Elimu na Mafunzo, 1995.(b)Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na rekebisho Na 10. la mwaka 1995.(c)Sheria Na. 1 ya Mafunzo ya Ufundsi ya mwaka 1994.(d) Dira ya Maendeleo ya Tanzania, 2025.(e)Mkakati wa Kukuza Uchumi na

Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA).(f)Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Mipango ya Mwaka 2005/2006, na Malengo ya Mwaka 2006/2007. Kwa kuwa huu ni mwanzo wa Serikali ya Awamu ya Nne inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, ningependa kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa, Wizara yangu itasimamia na kutekeleza maelekezo yaliyomo katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Maelekezo hayo yanasisitiza kuimarisha ubora wa Elimu ya aina na fani zote ili kuondokana na uchumi ulio nyuma na tegemezi.

Katika kufanikisha azma hii, mkakati madhubuti umewekwa ili kupanua Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari, Vyuo vya Mafunzo ya Ualimu na Ufundi kama ilivyoainishwa katika Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu (*Education Sector Development Programme (ESDP)*) ambapo utekelezaji wake unajidhihirisha katika Programu za MMEM na MMES. Aidha, utekelezaji katika maeneo mengine unakusudiwa kutekelezwa kwa kuyaendeleza mafanikio yaliyopatikana katika Serikali ya Awamu ya Tatu.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Elimu ya Msingi, Utekelezaji wa Malengo ya Elimu ya Msingi Mwaka 2005/2006. Mwaka 2005/2006 ulikuwa mwaka wa tano wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (2002 – 2006). Pamoja na utekelezaji wa mpango huu, miradi ya Shule Zenye Mazingira Yanayomjali Mtoto, Kukomesha Ajira Mbaya kwa Watoto na mradi wa Lishe Shulenii ilitekelezwa. Aidha, kupitia MMEM ambaao ni mpango endelevu kazi zifuatazo zimetekelizwa:

- (a) Kuongeza idadi ya wanafunzi katika Shule za Awali kutoka wanafunzi 638,591 mwaka 2005 hadi 669,137 mwaka 2006. Hili ni ongezeko la wanafunzi 30,546 sawa na asilimia 4.8.
- (b) Kuongeza idadi ya Shule za Msingi kutoka 14,257 mwaka 2005 hadi 14,700 mwaka 2006. Hili ni ongezeko la shule 443 sawa na asilimia 3.1.
- (c) Kuongeza idadi ya Wanafunzi wa Shule za Msingi kutoka wanafunzi 7,541,208 mwaka 2005 hadi wanafunzi 7,959,884 mwaka 2006. Hili ni ongezeko la wanafunzi 418,676 sawa na asilimia 5.6.
- (d) Kuandikisha wanafunzi Darasa la kwanza 982,640 sawa na asilimia 74.6 ya lengo la kuandikisha wanafunzi 1,316,727 wenyewe umri wa miaka saba (7).
- (e) Kusimamia Walimu Wanafunzi 7,286 walio katika mafunzo kwa vitendo na kuwapanga katika Halmashauri mbalimbali nchini. Aidha, wanachuo 10,510 wanaendelea na mazoezi ya vitendo shuleni katika Halmashauri zote.

- (f) Kupandisha kiwango cha kufaulu Darasa la IV kutoka asilimia 85.7 mwaka 2004 hadi asilimia 87.8 mwaka 2005. Aidha, Darasa la VII ufaulu umepanda kutoka asilimia 48.6 mwaka 2004 hadi asilimia 61.8 mwaka 2005.
- (g) Kuimarisha ubora wa elimu kwa kutoa ruzuku ya uendeshaji wa shule shilingi 55,669,928,754.00 kwa Halmashauri zote. Kati ya fedha hizo shilingi 22,270,000,000.00 ni kwa ajili ya kununua vifaa vyta kufundishia na kujifunzia. Kitaifa, uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi umefikia wastani wa kitabu kimoja kwa wanafunzi watatu (1:3).
- (h) Kukamilisha ujenzi wa vyumba vyta madarasa 2,692 kwa kutumia Ruzuku ya Maendeleo ya shilingi 8,345,200,000.00.
- (i) Kujenga nyumba za Walimu 1,856 hususan maeneo ya vijijini kwa Ruzuku ya Maendeleo ya shilingi 6,681,600,000.00.
- (j) Kununua madawati 39,620 kwa kutumia Ruzuku ya Maendeleo ya shilingi 792,585,000.00.
- (k) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya MMEM sehemu ya Sekta ya Elimu (*Education Sector Review*) mwaka 2006 kwa ngazi zote na ripoti ya Kitaifa imekamilika.

Mheshimiwa Spika, Malengo ya Mwaka 2006/2007. Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu inakusudia kuweka msukumo maalumu katika utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo (1995) ya kuwa kila shule ya Msingi iwe na Darasa la Elimu ya Awali.

Mheshimiwa Spika, lengo la Wizara ni kuandikisha watoto 1,321,124 wenye umri wa miaka 5 hadi 6 katika Darasa la Awali mwaka 2007. Katika kutekeleza azma hii, Wizara inawahimiza wananchi na Halmashauri zote kushiriki katika ujenzi wa madarasa, kuwaafuatisila na kuwaandikisha watoto wenye umri stahili ifikapo Januari 2007. Aidha, Wizara yangu itatekeleza kazi zifuatazo:-

- (a) Kuendelea kutoa Ruzuku ya Maendeleo ya shilingi 3,010,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vyta madarasa 860.
- (b) Kuandikisha watoto 1,166,737 wa Darasa la Kwanza Januari 2007 wenye umri wa miaka 7 na waliobaki wa miaka 8 na 9 wa mwaka 2005.

- (c) Kujenga nyumba za Walimu 500 hasa vijijini ili kuboresha makazi kwa Walimu.
- (d) Kuajiri Walimu wapya 7,337 ili kuweza kukabiliana na ongezeko kubwa la uandikishaji watoto Darasa la Kwanza.
- (e) Kujenga majengo ya vyoo vyaa kutosha kwa kila shule.
- (f) Kujenga matangi ya kuvuna maji ya mvua katika shule zenyne upungufu.
  
- (g) Kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Elimu ya Msingi Kwa Walioikosa (MEMKWA).
  
- (h) Kuendelea kutoa Ruzuku ya Uendeshaji kwa ajili ya kuimarisha wastani wa uwiano wa kitabu kimoja kwa wanafunzi watatu (1:3) kwa vitabu vyaa kiada vyaa kufundishia na kujifunzia ili kukidhi ongezeko la wanafunzi na hatimaye kufikia kitabu kimoja kwa mwanafunzi mmoja (1:1).
- (i) Kujenga majiko 27 katika shule za Wilaya ya Mpwapwa na kujenga matangi 4 ya maji katika shule za Mkoa wa Singida zilizo kwenye Mpango wa Lishe Shulenii.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Miradi ya Elimu ya Msingi katika mwaka 2005/2006, Idara imetekeleza miradi ifuatayo:-

Mradi wa shule zenyne mazingira yanayomjali mtoto (*Child Friendly Schools Project (CFS)*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu kwa kushirikiana na UNICEF imeendesha mradi wa uhamasishaji jamii juu ya shule inayomjali mtoto. Jumla ya shule 622 katika wilaya za Kisarawe, Masasi, Songea (V), Musoma (V), Ngara na Makete zinashiriki katika mradi huo ambao unaendelea hadi mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2005/2006, Wizara imetekeleza yafuatayo:-

- (a) Kuhamasisha na kushirikisha viongozi wa Wilaya, Kamati za Shule na Jamii kuhakikisha mazingira ya kumjali mtoto yanapatikana katika Wilaya zenyne mradi.

- (b) Kuchagua Walimu wa Ushauri Nasaha katika Wilaya zenyeye mradi.
- (c) Kuendesha mafunzo kwa Walimu 275 kuhusu Mbinu Shirikishi za Ufundishaji katika shule zinazomjali mtoto.

Mheshimiwa Spika, Malengo ya Mwaka 2006/2007mwaka 2006/2007, mradi umelenga kutekeleza yafuatayo:-

- (a) Kufuatilia matumizi ya Mbinu Shirikishi za Ufundishaji katika shule zinazomjali mtoto.
- (b) Kufuatilia na kutathmini ushiriki wa viongozi wa Wilaya, Kamati za Shule na Jamii katika kuleta mazingira ya kumjali mtoto katika shule za mradi.
- (c) Kutathmini mahitaji ili mradi uweze kuenezwa katika Wilaya nyingine nchini.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kukomesha Ajira Mbaya ya Watoto Kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi kwa Walioikosa (MEMKWA). Katika mwaka 2005/2006 Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani kupitia *ILO/IPEC* ilihudumia vituo 372 katika Halmashauri za Simanjiro, Arumeru, Arusha (M), Urambo, Iramba, Kondoa, Mufindi, Iringa (V), Ilala, Kinondoni na Temeke kwa lengo la Kukomesha Utumikishwaji wa Watoto ambapo jumla ya watoto 13,344 wameondolewa katika ajira mbaya na kupewa Elimu ya Msingi.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Lishe Shulen. Katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu kwa kushirikiana na *World Food Programme (WFP)* imeteketeza mradi wa Lishe Shulen katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Singida na Manyara. Mradi huu umeanza mwaka 2000, awamu ya kwanza ya mradi itakamilika ifikapo Desemba 2006. Shule zinazonufaika na mradi huu ni 330 zikiwemo 15 za bweni ambazo ni Engoruke Juu, Ketumbeine, Sinya, Longido, Kibaya, Kijungu, Ndredo, Arash, Endulen, Malambo, Nainokanoka, Bwigiri, Kigwe, Embort na Simanjiro. Aidha, jumla ya wanafunzi 169,503 wanafuwaika na mradi huu. Mbali na lishe, shule husika zinapata msaada wa kujengewa madarasa, ofisi za walimu, vyoo, visima vyatya maji na majiko. Awamu ya pili ya Mpango huu itaanza mwaka 2007 na kumalizika mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Elimu ya Sekondari kutokana na upanuzi wa Elimu ya Msingi na ufaulu wa wanafunzi wa Shule za Msingi, Elimu ya Sekondari imepanuliwa kwa msaada mkubwa wa nguvu za wananchi kwa kujenga majengo ya shule. Aidha, katika kupanua Elimu ya Sekondari, Wizara inaendelea kuweka msisitizo wa kuongeza idadi ya wanaojiunga na Elimu ya Sekondari kufikia asilimia 50 ya Rika Lengwa ifikapo mwaka 2009. Vilevile, Wizara yangu inaweka msisitizo katika kuongeza usawa kwa jinsi, makundi mbalimbali ya wenye ulemavu na yenye tofauti ya mapato katika wilaya zote, ikiwa ni pamoja na kuimarisha usimamiaji wa elimu na kuhamasisha ujenzi wa Shule za Sekondari za kutwa hususan maeneo ambayo hayana shule za kutosha.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Malengo ya Elimu ya Sekondari Mwaka 2005/2006. Katika mwaka 2005/2006 sambamba na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES), mradi wa *Prevention and Awareness in Schools of HIV and AIDS (PASHA)* na Mradi wa Pili wa Elimu (*Education II Project*) pia imetekelezwa. Kwa ujumla mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

(a) Kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaojiunga na Kidato cha 1 kutoka 180,239 mwaka 2005 hadi 243,359 mwaka 2006 ambalo ni ongezeko la wanafunzi 63,120 sawa na asilimia 35.0. Shule za Serikali zimeandikisha wanafunzi 196,391 na Zisizo za Serikali wanafunzi 46,968 wa Kidato cha 1 mwaka 2006. Idadi hii inaongeza asilimia ya wanafunzi wa Kidato cha 1 hadi 4 kufikia asilimia 13.4 ya Rika Lengwa (*NER*) la miaka 14 – 17. (*Makofî*)

(b) Kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaojiunga na Kidato cha 5 katika Shule za Serikali kutoka 15,509 mwaka 2005 hadi 18,211 mwaka 2006 wakiwemo wavulana 10,777 na wasichana 7,434. Hili ni ongezeko la wanafunzi 8,501 sawa na asimilia 87.5 ikilinganishwa na mwaka 2005. Katika Shule Zisizo za Serikali wanafunzi 9,569 wamejiunga na Kidato cha 5 wakiwemo Wavulana 5,511 na Wasichana 4,058 (Angalia Kiambatisho A, Kielelezo Na. 10).. Idadi ya wanafunzi walio Kidato cha 5 hadi 6 mwaka 2006 katika Shule za Serikali na Zisizo za Serikali ni 45,427.

(c) Kuongezeka kwa idadi ya Shule za Sekondari kutoka 1,745 mwaka 2005 hadi 2,289 mwaka 2006 sawa na ongezeko la asilimia 31.2. Idadi ya Shule Zisizo za Serikali ni 599 sawa na asilimia 26.2 ya shule zote. (*Makofî*)

(d) Kuongezeka kwa idadi ya wasichana wa Kidato cha 1 hadi 4 kutoka 231,808 mwaka 2005 hadi kufikia 299,353 mwaka 2006. Hili ni ongezeko la wasichana 67,545 sawa na asilimia 29.1. Idadi ya Wasichana Kidato cha 1 hadi 4 imefikia asilimia 47.5 ya wanafunzi wote mwaka 2006.

(e) Kuongezeka kwa idadi ya wasichana Kidato cha 5 hadi 6 kutoka 12,763 mwaka 2005 na kufikia 18,191 mwaka 2006 sawa na ongezeko la asilimia 42.5. Idadi ya Wasichana katika ngazi hii ni asilimia 40 ya wanafunzi wote.

(f) Kuongezeka kwa idadi ya Wasichana wanaojiunga Kidato cha 1 hadi 6 kutoka 244,571 mwaka 2005 hadi kufikia 317,544 mwaka 2006. Hili ni ongezeko la asilimia 29.8 .

(g) Kufungua Shule mpya za Serikali katika Mikoa yote ambapo hadi kufikia Mei 2006 shule 488 zimefunguliwa.

(h) Kuongezeka kwa idadi ya Shule za Sekondari za Serikali zinazotoa Elimu ya Kidato cha 5 na 6 kufikia 104. Shule zilizoongezeka mwaka 2006 ni Kilosa (Wavulana), Bwiru Boys, Nyakato (Wavulana), Chang'ombe (Mchanganyiko), Babati (Wasichana) na Kazima (Wasichana). Shule Zisizo za Serikali zinazotoa elimu ya Kidato cha 5 na 6 ni 162. Kwa hiyo idadi ya Shule za Sekondari zenyenye Kidato cha 5 na 6 mwaka 2006 ni 266.

(i) Kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wa Shule za Sekondari Kidato cha 1 hadi 6 kutoka 524,325 mwaka 2005 hadi kufikia 675,672 mwaka 2006. Hili ni ongezeko la wanafunzi 151,347 sawa na asilimia 28.9.

(j) Kugharimia watoto 33,873 toka familia zenyenye kipato duni kwa lengo la kuwapatia watoto wote fursa sawa za elimu.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha Elimu ya Sekondari Wizara imechukua hatua mbalimbali kwa misingi ya kuwaendeleza Walimu Kitaaluma na Kitaalamu kwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu ambapo:-

(i) Walimu 6 wanasoma Shahada ya Uzamili na Walimu 49 wanasoma Diploma ya Juu ya Elimu (*PGDE*) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (*Makofii*)

(ii) Walimu 91 wanasoma Shahada ya kwanza ya Hisabati (*B.Ed. - Mathematics*) Chuo Kikuu cha Tumaini.

(iii) Walimu 72 wamelipiwa sehemu ya gharama za mafunzo yao ya Chuo Kikuu Huria.

(iv) Walimu 320 walipatiwa mafunzo ya muda mfupi ya mbinu shirikishi katika ufundishaji wa Sayansi na Hisabati. Aidha, Walimu 3,194 wameajiriwa na kupangwa kufundisha katika Shule za Sekondari za serikali.

Mheshimiwa Spika, Malengo ya Mwaka 2006/2007, katika mwaka 2006/2007, kwa kushirikiana na wazazi na wadau wengine wa elimu, Wizara yangu itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuchangia ujenzi wa vyumba vya madarasa mapya 1,637 kwa gharama ya shilingi 11,459,000,000.00 kwenye Shule za Sekondari Kidato cha 1 hadi 4 zinazojengwa na wananchi na madarasa 128 katika Shule za Sekondari Kidato cha 5 hadi 6.

(b) Kuchangia ujenzi wa nyumba za walimu 1,000 kwa gharama ya shilingi 9,000,000,000.00 kwenye Shule za Sekondari.

(c) Kuchangia ujenzi wa maabara 40 kwa gharama ya shilingi 560,000,000.00 katika shule za Sekondari Kidato cha 1 hadi 6.

(d) Kujenga vyoo katika shule 60, hosteli 5 na maktaba 30 kwa gharama ya shilingi 500,000,000.00.

(e) Kukarabati shule 30 kati ya 100 za Kitaifa.

(f) Kukarabati miundombinu kwenye shule zenyenye mahitaji maalumu. Shule hizo ni Korogwe Wasichana, Tabora Wasichana, Moshi Ufundu, Kazima, Pugu na Rugambwa.

(g) Kugharimia Elimu ya Sekondari kwa wanafunzi 45,873 wanaotoka katika familia zenyenye kipato duni wakiwemo 33,873 wanaoendelea kulipiwa.

(h) Kuwajengea uwezo wa Kimenejimenti Wakuu wa Shule, Bodi za Shule, Kamati za Uendeshaji za *Shule* (*School Management Teams*) pamoja na Maafisa walioko Makao Makuu ya Wizara.

(i) Kuendesha mafunzo kwa ajili ya viongozi wa ngazi ya Mkoa na Wilaya ili kuwashirikisha kikamilifu katika ufuatiliaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari katika maeneo yao.

(j) Kugharimia Walimu 200 mafunzo ya Shahada ya Kwanza katika Chuo Kikuu Huria.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Elimu ya Sekondari Mwaka 2005/2006. Miradi miwili ifuatayo imetekelizwa na Wizara yangu sambamba na MMES kwa lengo la kuboresha Elimu ya Sekondari.

Mradi wa *Prevention and Awareness in Schools of HIV and AIDS (PASHA)*

Mradi huu ulianza rasmi Julai 2003 kwa majoribio katika mkoa wa Tanga na unalenga kutoa Elimu dhidi ya UKIMWI shulenii. Kazi zifuatazo zimetekelizwa katika mwaka 2005/2006:-

(a) Kutoa mafunzo ya kujenga uwezo katika mada za kuzuia maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI kwa walimu 160 wa Mkoa wa Tanga.

(b) Kutoa mafunzo ya mbinu shirikishi za ufundishaji wa mada za UKIMWI, Ushauri Nasaha na Jinsia kwa Walimu 80 wa somo la *Biology*.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Pili wa Elimu (*Education II Project*). Katika kuboresha ufundishaji wa masomo ya Sayansi na Hisabati katika Shule za Sekondari, mwaka 2005/2006 Mradi wa Pili wa Elimu ulitekeleza yafuatayo:-

(a) Kutoa mafunzo kazini kwa wawezeshaji wa masomo ya Sayansi na Hisabati yaliyowashirikisha Wakaguzi 42, Wakufunzi 91, Wakuu wa Shule 125 na Walimu wa Shule za Sekondari 1,169.

(b) Kupeleka vitabu vya masomo ya Sayansi na Hisabati katika Shule za Sekondari 224 kwenye Wilaya 80 vyenye gharama ya shilingi 1,562,081,640.00.

(c) Kujenga maabara kwenye Shule za Sekondari za Oldonyosambu, Chalao, Matola, Igunga, King'ori, Kaliua, Zingibali na Kyela kwa gharama ya shilingi 969,150,147.00.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007 Mradi wa Pili wa Elimu ya Sekondari utatekeleza yafuatayo:-

(a) Kukamilisha ujenzi wa maabara za Sayansi katika Shule za Sekondari za Mangaka iliyopo Masasi, Inyonga iliyopo Mpanda na Kilangalanga iliyopo Kibaha kwa kutumia Wahandisi wa Wizara.

(b) Kusambaza vifaa vya maabara katika Shule za Sekondari 12 zilizojengewa maabara na mradi. Shule hizo ni Kilangalanga, Mangaka, Matola, Mogabiri, Manga, Chalao, King'ori, Inyonga, Oldonyosambu, Kongwa, Meatu na Makiba.

(c) Kutathmini uboreshaji wa ufundishaji na uongozi uliofanywa katika shule zinazofundisha masomo ya Sayansi na Mpango wa Elimu ya Watu Wazima katika Wilaya 12 za Mradi.

(d) Kutayarisha ripoti ya hitimisho la Mradi.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Elimu ya Ualimu Utekelezaji wa Malengo ya Elimu ya Ualimu Mwaka 2005/2006. Idara ya Elimu ya Ualimu katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) iliendelea kutoa mafunzo Tarajali na Kazini kwa walimu wa Daraja A na Stashahada. Kutokana na Mipango hiyo mikakati iliwekwa ya kuandaa walimu bora ambao watatosheleza mahitaji ya shule za Awali, Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu. Mwaka 2005/2006 Idara ya Elimu ya Ualimu imetekeleza yafuatayo:-

(a) Kuimarisha Mtandao wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa:-

Kuweka Mtandao wa TEHAMA katika Vyuo vya Ualimu. Hatua iliyofikiwa ni maandalizi ya maabara katika vyuo 32 vya Serikali. Kuunganisha mtandao wa *internet* Chuo cha Ualimu Morogoro. Kununua kompyuta na *satellite* kwa ajili ya vyuo 31 vilivyobakia. Kuajiri wataalamu watano na kutoa mafunzo kwa wakufunzi 28.

(b) Kutenganisha Vyuo vya Ualimu; vyuo 14 kuwa vya Stashahada na 18 kuwa vya Daraja A.

(c) Kuandaa rasimu ya kwanza ya muhutasari wa TEHAMA kwa Vyuo vya Ualimu.

(d) Kuwapatia mafunzo wanachuo Tarajali 4,130 wa Daraja A.

(e) Kuwapatia mafunzo shulenii wanachuo Tarajali Daraja A mwaka wa pili.

- (f) Kuwapatia mafunzo ya Stashahada Wanachuo Tarajali 4,400.
- (g) Kufanya mtihani Walimu 21,000 walioko kazini wa Daraja B/C ili waweze kuhitimu Daraja A.
- (h) Kuwapatia mafunzo Walimu wa Cheti; Elimu Maalum 90, Elimu ya Awali 250 na Sayansi Kimu 100.
- (i) Kusomesha Walimu 60 Stashahada kupitia Elimu kazini katika Fani za Sanaa za Jukwaani na Ufundii, Michezo na Muziki.
- (j) Kutoa mafunzo ya ufundishaji na ujifunzaji wa njia shirkishi kwa Walimu wa Shule za Msingi 41,945.
- (k) Kudhamini Wakufunzi 280 kwa mafunzo ya Shahada ya Ualimu katika Chuo Kikuu Huria.

Mheshimiwa Spika, Malengo ya Mwaka 2006/2007, maendeleo endelevu ya elimu yanahitaji kuwepo kwa walimu wa kutosha katika shule zote. Katika kukabiliana na tatizo la upungufu wa walimu na kujenga uwezo wa kitaalamu, mwaka 2006/2007 Idara ya Elimu ya Ualimu itatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kuandaa miundombinu na Mtandao wa TEHAMA.
- (b) Kutoa mafunzo ya Ualimu Tarajali Daraja A 7,200 kwa ajili ya Shule za Awali na Msingi.
- (c) Kutoa mafunzo ya Stashahada ya Ualimu 4,000 na Mafunzo maalumu ya mwezi mmoja 3,500 kwa lengo la kukidhi mahitaji ya walimu katika shule za Sekondari.
- (d) Kuendeleza Walimu 26,000 wa Daraja B/C kwa utaratibu wa moduli kufikia Daraja A ifikapo mwaka 2007.
- (e) Kugharimia Wakufunzi 314 wanaosoma Chuo Kikuu Huria.
- (f) Kugharimia na kuandaa muhtasari wa kufundishia TEHAMA kwenye Vyuo vya Ualimu.
- (g) Kuandaa Mkakati wa Menejimenti na Kuendeleza Walimu (*Teacher Development and Management Strategy*).
- (h) Kukarabati Vyuo 10 vya Ualimu.

Mheshimiwa spika, Idara ya Ukagazi wa Shule, Utekelezaji wa Malengo ya Ukagazi wa Shule Mwaka 2005/2006. Katika kuhakikisha kuwa sera, sheria, kanuni na viwango vilivyowekwa vinazingatiwa katika mfumo wa elimu nchini, Wizara yangu

inahusika na ukaguzi wa Shule za Awali, Msingi, Sekondari, Vituo vya Elimu Maalumu, Ufundu Stadi, Elimu ya Watu Wazima na Vyuo vya Ualimu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2005/2006 Idara ya Ukaguzi wa Shule ilikagua jumla ya asasi za elimu 15,515 sawa na asilimia 78 ya lengo la kukagua Asasi 19,905 kwa mwaka. Katika kuboresha ukaguzi wa shule Wizara imenunua magari 18 na kompyuta 80 kwa ajili ya Wakaguzi wa Shule Wilayani.

Aidha, Idara imeendesha mafunzo ya awali kwa wakaguzi wapya 127 na mafunzo ya Menejimenti kwa Wakaguzi Wakuu wa Shule wa Wilaya 120. Vilevile, Idara imefanya ukarabati katika ofisi 31 za ukaguzi wa Shule Wilayani. Kazi nyingine zilizofanyika katika mwaka 2005/2006 ni:-

(a) Kupitia na kuboresha Mwongozo wa Mafunzo na Kiongozi cha Mkaguzi wa Shule.

(b) Kuendesha mafunzo kuhusu Uchambuzi wa Mihtasari na matumizi ya mbinu shirikishi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa Wakaguzi wa Shule wa masomo ya English, Kiswahili, Physics, Chemistry, Biology na Ualimu.

(c) Kufanya ukaguzi maalum wa vyuo na shule mpya 600 kwa ajili ya kufuatilia tuhuma mbalimbali na kuongeza mikondo.

(d) Kufanya utafiti kuhusu ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Hisabati katika Shule za Msingi na Vyuo vya Mafunzo ya Ualimu Daraja A. (*Makofî*)

(e) Kusimamia na kuendesha Mtihani wa Kidato cha 2.

Mheshimiwa Spika, Malengo ya Mwaka 2006/2007, kwa madhumuni ya kuhakikisha ubora na kudhibiti viwango vya elimu itolewayo, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kufanya ukaguzi katika Asasi za Elimu 20,112.

(b) Kutoa nakala 1,000 za Mwongozo wa Mafunzo ya Awali ya Ukaguzi na nakala 1,000 za Kiongozi cha Mkaguzi wa Shule.

(c) Kusimamia na kuendesha Mtihani wa Kidato cha 2.

(d) Kuboresha mazingira ya kazi kwa Wakaguzi wa Shule kwa:-Kukarabati Ofisi 20 za Ukaguzi wa Shule.Kununua vifaa vya ofisi kama vile samani na kompyuta kwa Wilaya 20.Kutoa mafunzo juu ya Mtaala mpya kwa Wakaguzi wote 1,064. Kununua magari matano kwa ajili ya ofisi za kanda.

(e) Kuendesha mafunzo ya Elimu dhidi ya UKIMWI kwa wafanyakazi wote wa Idara ya Ukaguzi wa Shule.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Afisa Elimu Kiongozi ni mhimili wa utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo, utoaji wa Nyaraka na Miongozo mbalimbali kwa ajili ya kuboresha Elimu na Mafunzo ya Ufundu. Aidha, Ofisi inaratibu utoaji wa Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari, Ualimu na Elimu ya Watu Wazima, Elimu kwa Radio, Usajili wa Shule na Elimu Maalumu. Vilevile, Ofisi ya Afisa Elimu Kiongozi inasimamia Mpango wa Elimu dhidi ya UKIMWI, Ushauri Nasaha na Elimu ya Mazingira. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Elimu ya Watu Wazima. Utekelezaji wa Malengo ya Elimu ya Watu Wazima Mwaka 2005/2006. Kitengo cha Elimu ya Watu Wazima huratibu utoaji wa Elimu ya Watu Wazima nchini, Elimu Nje ya Mfumo Rasmi wa Shule, Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Watoto Walioikosa (MEMKWA) na Elimu ya Wafanyakazi. Katika mwaka 2005/2006 Kitengo cha Elimu ya Watu Wazima kimetekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendesha mafunzo kwa wawezeshaji ngazi ya vituo 1,166 kuhusu uanzishaji na uendeshaji wa Mpango wa Uwiano Kati ya Elimu ya Watu Wazima na Jamii (MUKEJA).

(b) Kuchapa moduli 2,280 kati ya 513,000 za MUKEJA na kuzisambaza katika Halmashauri 97.

(c) Kupanua shughuli za MUKEJA kutoka vituo 80 mwaka 2005 hadi vituo 1,140 mwaka 2006 na kuongeza uandikishaji wa washiriki kutoka 675,000 mwaka 2005 hadi 1,892,368 mwaka 2006.

(d) Kuendesha mafunzo kwa wawezeshaji 3,949 wa vituo vya Mpango wa Elimu ya Msingi Kwa Walioikosa (MEMKWA).

(e) Kuwapatia mafunzo ya kujenga uwezo watendaji 42 wa Kituo cha Kisomo Mwanza.

Mheshimiwa Spika, Malengo ya Mwaka 2006/2007, katika mwaka 2006/2007, Kitengo cha Elimu ya Watu Wazima kitatekeleza yafuatayo:-

(a) Kufuutilia utekelezaji wa Waraka wa Elimu Na. 3 wa Mwaka 2006, unaoelekeza kuhusu Utekelezaji wa Mkakati wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi.

(b) Kuchapa seti 4,800 za moduli za MUKEJA za awamu ya pili na kuzisambaza katika Halmashauri 97.

(c) Kufuutilia na kuratibu utoaji wa mafunzo ya Wawezeshaji wa MEMKWA na MUKEJA katika Halmashauri 97.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Elimu Maalumu Utekelezaji wa Malengo ya Elimu Maalumu Mwaka 2005/2006, jukumu la Kitengo cha Elimu Maalumu ni kuratibu shughuli zote za Elimu kwa ajili ya watu wenye ulemavu hususan kupanga na kusimamia uimarishaji na upanuzi wa huduma za elimu kwa wenye ulemavu. (*Makofi*)

Katika jitihada za kuongeza nafasi kwa watoto wenye ulemavu kuandikishwa shulenii, Wizara yangu inatekeleza mfumo mpya wa Elimu Jumuishi ambao unatumia shule za kawaida kuandikisha na kutoa elimu kwa watoto wenye ulemavu kusoma kwa pamoja na watoto wasio na ulemavu. Katika mwaka 2005/2006, Kitengo cha Elimu Maalumu kimetekeleza yafuatayo:-

- (a) Kununua mtambo wa kuchapisha vitabu vya Wasioona.
- (b) Kuchapisha aina 13 za vitabu vya mitaala katika Braille.
- (c) Kukamilisha rasimu ya Mwongozo wa kufundishia Elimu Jumuishi.
- (d) Kutoa Mafunzo ya Elimu Jumuishi kwa Walimu 936 wasio na taaluma ya Elimu Maalumu katika Halmashauri 39.
- (e) Kuwapatia wataalamu 60 wa Elimu Maalumu mafunzo ya muda mfupi katika fani za Wasioona, Viziwi, Ulemavu wa Akili, Wenye Otizim na Viziwi Wasioona.

Mheshimiwa Spika, Malengo ya Mwaka 2006/2007, katika mwaka 2006/2007, Kitengo cha Elimu Maalumu kitatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia Wanafunzi Wenye Ulemavu wa Akili, Wasioona, Wenye Uoni Hafifu, Wenye Otizim, Viziwi, Viziwi Wasioona, Ulemavu wa Viungo na Albino.
- (b) Kuchapa aina 13 za vitabu vya kiada zenye nakala 600 kila moja kwa Shule za Msingi, aina 8 zenye nakala 400 kila moja kwa Shule za Sekondari na aina 2 zenye nakala 400 kila moja kwa Vyuo vya Ualimu.
- (c) Kuchapa Mwongozo wa Mwezeshaji wa Mafunzo ya Elimu Jumuishi.
- (d) Kuendesha Mafunzo ya Elimu Jumuishi kwa Walimu 1,200 katika Halmashauri 50.
- (e) Kuendesha mafunzo ya muda mfupi kwa wataalamu wa Elimu Maalumu kwa Wasioona na Wenye Uoni Hafifu 50, Wenye Ulemavu wa Akili na Wenye Otizim 50 na Viziwi na Viziwi Wasioona 50.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Usajili wa Shule Utekelezaji wa Malengo ya Usajili wa Shule Mwaka 2005/2006. Wizara yangu imeendelea kuwashamasisha

wananchi na wadau mbalimbali kuendelea kujenga shule ili kuisaidia serikali katika kutimiza malengo ya kuwapa watoto wote nafasi ya kupata elimu.

Aidha, Wizara inaendelea kutoa wito wa kuzisajili shule kwa kuzingatia vigezo na taratibu zinazotakiwa kwa shule zote mpya kuwa na viwango vinavyostahili. Hali hii itasaidia kuondoa wasiwasni kwa wazazi ambao wanaamua kupeleka watoto wao katika Shule Zisizo za Serikali na za Wananchi. Katika mwaka 2005/2006, Kitengo cha Usajili wa shule kitatetekileza yafuatayo:-

- (a) Kusajili Shule Zisizo za Serikali 109.
- (b) Kutoa vibali vya kujengwa kwa Shule Zisizo za Serikali 84.
- (c) Kuthibitisha Wenye Shule na Mameneja wa Shule 106.
- (d) Kutoa vibali vya kuanzisha shule 482 zilizojengwa kwa nguvu za Wananchi.
- (e) Kutoa leseni za kufundisha kwa waombaji 631.
- (f) Kutoa mafunzo kwa Watendaji wa elimu 213 kuhusu taratibu za kusajili shule.
- (g) Kukusanya na kuhakiki takwimu za Walimu walio kazini kutoka Halmashauri 80 kama hatua ya awali ya kuwasajili.

Mheshimiwa Spika, Malengo ya Mwaka 2006/2007, katika mwaka 2006/2007 Kitengo cha Usajili wa Shule kitatetekileza yafuatayo:-

- (a) Kusajili shule Zisizo za Serikali 150.
- (b) Kuchambua maombi 100 ya kuthibitishwa Meneja na Mwenye Shule Zisizo za Serikali.
- (c) Kuchambua maombi 80 ya vibali vya kuanzisha Shule za Sekondari zilizojengwa kwa nguvu za Wananchi.
- (d) Kuchambua maombi 400 ya leseni za kufundishia.
- (e) Kuendesha mafunzo kuhusu taratibu za usajili wa Shule na Walimu kwa Watendaji 200 kutoka Halmashauri 7.
- (f) Kukusanya takwimu za Walimu walio kazini kutoka Halmashauri 60.

- (g) Kuchapisha nakala 4,000 za vyeti vya Usajili wa Walimu.
- (h) Kuratibu utafiti kuhusu ubora wa elimu kwa nchi 15 za Kusini mwa Afrika *Southern Africa Consortium for Monitoring Education Quality (SACMEQ III)*. Nchi shiriki katika utafiti wa SACMEQ ni Botswana, Kenya, Lesotho, Malawi, Mauritius, Mozambique, Namibia, Sychelles, South Africa, Swaziland, Tanzania (Bara), Tanzania (Zanzibar), Uganda, Zambia na Zimbabwe.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Elimu kwa Redio Utekelezaji wa Malengo ya Elimu kwa Redio Mwaka 2005/2006, katika harakati za kuboresha Elimu ya Msingi, Sekondari, Ualimu na Mafunzo ya Ufundishaji, Wizara yangu inatilia mkazo Elimu kwa njia ya Redio. Aidha, Elimu kwa Redio hutoa taarifa na kuhamasisha wananchi na wadau wa elimu juu ya utekelezaji wa mipango ya elimu. Katika mwaka 2005/2006, Kitengo cha Elimu kwa Redio kimetekeleza yafuatayo:-

- (a) Kuandaa na kutangaza Vipindi 52 vinavyohusu Mbinu Shirikishi za ufundishaji, Vipindi 52 vya ‘Boresha Elimu’ na Vipindi 216 vya masomo ya *English*, Kiswahili na Maarifa ya Jamii kwa Darasa la V, VI na VII.
- (b) Kutafsiri, kuhariri na kuchapisha nakala 150,000 za Mwongozo wa kufundishia Elimu ya Mazingira kwa Shule za Msingi.
- (c) Kutoa mafunzo kwa Walimu 97 wa Shule za Msingi na Sekondari na Wakaguzi wa Shule 30 kuhusu utumiaji wa Mwongozo wa Mkakati wa Ujanishaji Shule.
- (d) Kutayarisha na kuchapa nakala 2,000 za Mwongozo wa Ushauri Nasaha kwa ajili ya Shule za Sekondari na Vyuo vya Ualimu.
- (e) Kutoa mafunzo ya Ushauri Nasaha kwa Walimu 382 wa Shule za Sekondari na Vyuo vya Ualimu.

Mheshimiwa Spika, Malengo ya Mwaka 2006/2007, katika mwaka 2006/2007, Kitengo cha Elimu kwa Redio kitatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kuandaa na kutangaza vipindi 52 vya ‘Boresha Elimu’, vipindi 52 vya Ufundishaji kuhusu Mbinu Shirikishi na vipindi 432 vya masomo ya *English*, Kiswahili, Sayansi, Jiografia, Historia na Uraia kwa Darasa la V, VI na VII.

- (b) Kuendesha semina kwa Walimu 1,260 na Wakaguzi wa Shule 756 kutoka Kanda 6 za elimu kuhusu utumiaji wa Mwongozo wa Elimu ya Mazingira.
- (c) Kuhariri na kuchapa nakala 200,000 za kufundishia Elimu ya Mazingira.
- (d) Kutoa mafunzo ya Ushauri Nasaha kwa Walimu 1,000 wa Shule za Sekondari na Vyuvo vya Ualimu.
- (e) Kuchapa nakala 9,000 za Mwongozo wa Ushauri Nasaha.
- (f) Kutafsiri Mwongozo wa Ushauri Nasaha kutoka Kiingereza kuwa Kiswahili.
- (g) Kukamilisha kitini cha mada ngumu za Elimu ya Mazingira kwa Shule za Msingi.

Mheshimiwa Spika, Elimu Dhidi ya UKIMWI. Ugonjwa wa UKIMWI unaendelea kuathiri nguvu kazi ya Taifa letu wakiwemo Wafanyakazi, Walimu na Wanafunzi wanaosoma katika Shule za Msingi, Sekondari na Vyuvo vya Ualimu na Ufundii. Ili kukabiliana na tatizo hili, Wizara yangu imeandaa na inatekeleza mkakati na mwongozo kuhusu Elimu ya UKIMWI katika Mashule, Vyuvo vya Ualimu na katika sehemu za kazi. Aidha, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii itashirikiana na Wadau wengine wa Elimu katika kuwasaidia Walimu na Wafanyakazi walioathirika na ugonjwa wa UKIMWI.

Katika mwaka 2005/2006, Kitengo cha Redio Sehemu ya Elimu Dhidi ya UKIMWI kimetekeleza yafuatayo:-

- (a) Kutoa mafunzo kwa Waelimishaji Wenza 60 katika Asasi na Idara za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii.
- (b) Kutoa Elimu Dhidi ya UKIMWI kwa Walimu 1,200 wa Shule za Msingi.
- (c) Kusambaza vitabu 205,521 vya mafunzo ya Elimu Dhidi ya UKIMWI katika Shule za Msingi na Vyuvo vya Ualimu.
- (d) Kutoa mafunzo kwa Walimu wa Sekondari 451 wanaofundisha masomo yanayobeba mada za VVU na UKIMWI kutoka Kanda za Kaskazini Mashariki, Kaskazini Magharibi na Kusini.
- (e) Kufuutilia utekelezaji wa Elimu ya Familia katika Shule 30 za Sekondari katika Kanda ya Kati.

- (f) Kutoa mafunzo kwa Waelimishaji Rika 120 kutoka Shule 16 za Sekondari za Mkoa wa Pwani.
- (g) Kuratibu masuala yanayohusu UKIMWI kwa kushirikiana na Idara na Asasi za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Kitengo cha Redio Sehemu ya Elimu Dhidi ya UKIMWI kitakeleza yafuatayo:-

- (a) Kutayarisha vitabu vya Elimu ya kujikinga na VVU na UKIMWI kwa ngazi zote.
- (b) Kuchapa na kusambaza maandiko ya mafunzo ya Elimu ya Kujikinga na UKIMWI katika Shule na Vyuo vya Ualimu.
- (c) Kuendesha mafunzo kwa Walimu 2,000 wa masomo yanayobeba mada za VVU na UKIMWI Shule za Msingi katika Kanda 8 za Kielimu chini ya usimamizi wa Wakaguzi Wakuu wa Shule wa Kanda.
- (d) Kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya programu ya UKIMWI.
- (e) Kuendesha mafunzo ya Elimu ya Familia kwa walimu 777 wa masomo chukuzi ya Elimu ya Familia na Wakuu wa Shule za Sekondari 250 kutoka Kanda ya Nyanda za Juu.
- (f) Kuboresha na kuhariri rasimu za masomo chukuzi manne ya Elimu ya Familia kwa wanafunzi wa Shule za Sekondari.
- (g) Kufuatilia utekelezaji wa Elimu ya Familia katika Shule za Sekondari 30 Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Sera na Mipango Utekelezaji wa Malengo ya Idara ya Sera na Mipango Mwaka 2005/2006. Upangaji mzuri wa mipango ya Elimu unahitaji ufuatiliaji, tathmini na utafiti unaoridhisha ili kupata mafanikio yanayokusudiwa. Katika kulifanikisha hili, mwaka 2005/2006, Idara ya Sera na Mipango imetakeleza yafuatayo:-

- (a) Kufanya utafiti kuhusu vigezo vya ubora wa shule za msingi mkoani Singida kutohana na matokeo yasiyoridhisha ya kumaliza Elimu ya Msingi.
- (b) Kufanya utafiti juu hali ya elimu nchini (2000 - 2004) na kutoa Makadirio ya mahitaji muhimu katika kufikia malengo ya elimu kwa wote mwaka 2015.

- (c) Kukusanya ripoti za tafiti zilizofanywa katika ngazi ya Elimu ya Msingi, Sekondari na Mafunzo ya Ualimu (1995 – 2005).
- (d) Kufanya ufuatilliaji na tathmini katika Halmashauri 121, Shule za Msingi 605 na Shule za sekondari 491 kuhusu utekelezaji wa mipango ya kazi na matumizi ya fedha.
- (e) Kusimamia ukarabati wa shule za Sekondari 18 za Kiara, Weruweru, Dr. Salmin Amour, Kilakala, Kibiti, *Jangwani Girls*, Korogwe, Shinyanga, Nganza, Rugambwa, Mwenge, Mataka, Mikumi, Kibasila, Iyunga, Tambaza, Minaki, Ndanda na Vyuo vya Ualimu vya Katoke, Mpuguso, Mhonda, Ilonga na Vikindu.
- (f) Kutayarisha Programu za Mipango ya Muda Mfupi, Muda wa Kati na Muda Mrefu za Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari, Ualimu na Elimu ya Watu Wazima.
- (g) Kufanya mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo (1995).
- (h) Kutoa ithibati 50 kwa vitabu vya kielimu na zana za kufundishia shulen na vyuoni.
- (i) Kutayarisha tovuti ya Wizara na kuunganisha intaneti katika Idara zote zilizoko Makao Makuu ya Wizara.
- (j) Kutoa miongozo ya ujenzi *Construction Guidelines, Construction Technical Handbooks, Detailed Working Drawings Handbooks, Guidelines for Monitoring Construction, Procurement Guidelines* kwa Wakuu wa Shule, Vyuo vya Ualimu na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Malengo ya Mwaka 2006/2007, katika mwaka 2006/2007. Idara ya Sera na Mipango itatekeleza kazi zifuatazo:-

- (a) Kufanya utafiti wa maendeleo ya taaluma ya uongozi kwa baadhi ya Shule za Msingi nchini Tanzania, mwenendo wa mdondoko (*drop-out*) wa wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekondari kuanzia mwaka 1995 hadi 2005 na athari za ada katika utoaji wa elimu ya sekondari.
- (b) Kufanya ufuatiliaji na tathmini, katika Shule na Vyuo vya Ualimu kuhusu matumizi ya fedha na utoaji wa huduma za Elimu na Mafunzo ya Ufundii.
- (c) Kuboresha Rasimu ya Mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995 ili kuingiza masuala ya Mafunzo ya Ufundii.

- (d) Kukamilisha andiko la Pili la Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM II) na kuchapa kitabu cha Takwimu za Msingi za Elimu Tanzania 2007 (*Basic Education Statistics in Tanzania 2007*).
- (e) Kuandaa Mapitio ya Matumizi ya Fedha za Umma (*Public Expenditure Review (PER)*), Mpango wa Kati wa Matumizi ya Fedha (*Medium Term Expenditure Framework (MTEF)*) za Wizara.
- (f) Kukarabati baadhi ya majengo ya shule za Sekondari 20, Vyuo vya Ualimu 10, ofisi za ADEM na ofisi za Kanda 3 za Mpango wa Matengenezo (*Physical Planning and Maintenance Zones*).
- (g) Kutoa ithibati 80 kwa vitabu vya kielimu na zana za kufundishia Shulen na Vyuni.
- (h) Kuimarisha Hifadhi na Mpangilio wa Taarifa za Kompyuta (*Database*) na kumbukumbu za Wizara.
- (i) Kuendesha mafunzo ya matengenezo na dhana ya utunzaji wa majengo na mazingira kwa Wakuu wa Shule na Vyuo katika Kanda 8 za elimu.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Mawasiliano na Habari Utekelezaji wa Malengo ya Mawasiliano na Habari Mwaka 2005/2006, katika kudumisha Utawala Bora, Uwazi na Uwajibikaji, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na vyombo vya habari na Wadau wengine wa elimu ili kuelezea umma kuhusu mafanikio na changamoto zinazojitokeza katika Sekta ya Elimu na kuhamasisha ushiriki wa wananchi katika kutekeleza mipango ya Elimu. Katika mwaka 2005/2006 Kitengo cha Mawasiliano na Habari kimetekeliza yafuatayo:-

- (a) Kuratibu utoaji wa habari za kielimu katika Vyombo vya Habari na kupiga picha za video na mnato katika matukio mbalimbali ili kufahamisha jamii kuhusu maendeleo ya Sekta ya Elimu na kuweka kumbukumbu za Wizara.
- (b) Kutayarisha matangazo 34 ya Redio na Televisheni ili kuifahamisha na kuhamasisha jamii kuhusu mikakati, mafanikio na changamoto za Wizara katika kutekeleza Mipango ya Elimu.
- (c) Kutengeneza na kusambaza nakala 327,239 za Jarida la *Ed-SDP (Education Sector Development Programme Newsletter)* kwa Kanda 8 za Elimu kwa ajili ya kuhamasisha jamii na Wadau wa elimu ili kushiriki katika utekelezaji wa Programu za Elimu.
- (d) Kuandaa vipindi 26 vya Redio na Televisheni kwa kushirikiana na vyombo vya habari ili kuelezea Sera na Utekelezaji wa Programu za MMEM na MMES.

(e) Kuandaa na kusambaza kalenda 50,000 na vipeperushi 50,000 kwa ajili ya Programu za MMEM na MMES.

Malengo ya Mwaka 2006/2007, katika juhudi za kuhakikisha kuwa wananchi na wadau wa elimu wanaelewa majukumu, mipango na programu mbalimbali zinazotekeliza na wizara yangu, katika mwaka 2006/2007 Kitengo cha Mawasiliano na Habari itatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kuratibu utoaji wa habari katika Vyombo vya Habari na kupiga picha za video na mnato katika matukio mbalimbali ili kufahamisha jamii kuhusu maendeleo ya elimu na kuweka kumbukumbu za Wizara.
- (b) Kutayarisha matangazo 40 ya Redio na Televisheni ili kuifahamisha na kuhamasisha jamii kuhusu mikakati, matatizo na mafanikio ya Wizara katika kutekeleza Mipango ya Elimu.
- (c) Kutengeneza na kusambaza nakala 330,000 za Jarida la *Ed-SDP* kwa Kanda 8 za elimu kwa ajili ya kuhamasisha jamii na Wadau wa elimu ili kushiriki katika utekelezaji wa Mipango ya Elimu.
- (d) Kuandaa vipindi 50 vya Redio na Televisheni kwa kushirikiana na vyombo vya habari ili kuelezea Sera na utekelezaji wa Programu za MMEM na MMES.
- (e) Kuandaa na kusambaza kalenda 50,000 na vipeperushi 50,000 kwa ajili ya kuelimisha jamii kuhusu mafanikio na matatizo ya utekelezaji wa programu za MMEM na MMES.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Utawala na Utumishi Utekelezaji wa Malengo ya Utawala na Utumishi Mwaka 2005/2006. Idara ya Utawala na Utumishi pamoja na kuratibu masuala ya Programu ya Kuboresha Utumishi wa Umma katika Wizara, pia husimamia ajira za watumishi, maslahi, kujenga uwezo, kusimamia sheria, kanuni na taratibu za utumishi. Katika mwaka 2005/2006, Idara ilishughulikia ajira za watumishi wasio Walimu 170 na Walimu wapya 2,872 kati ya nafasi 3,524 za Shule za Sekondari na Vyuo vya Ualimu.

Aidha, Wizara ilishughulikia maslahi mbalimbali ya watumishi 3,498 yakiwemo marekebisho ya mishahara 2,767, mirathi 60, viinua mgongo 17 na malipo ya kustaafu 199.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, jumla ya watumishi 2,417 walipatiwa mafunzo mbalimbali ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi kama inavyoonesha katika Kiambatisho C, Kilelezo Na. 5. Mafunzo haya yalilenga katika kuwajengea uwezo watumishi ili waweze kumudu majukumu waliyokabidhiwa.

Mheshimiwa Spika, Malengo ya Mwaka 2006/2007, katika mwaka 2006/2007, Idara itatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kuajiri watumishi 9,769 wakiwemo Walimu 9,500 na watumishi wasio walimu 269.
- (b) Kugharimia mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi kwa Watumishi 150.
- (c) Kuthibitisha kazini watumishi 220 wasio walimu.
- (d) Kupandisha madaraja watumishi 1,347 wasio walimu.
- (e) Kuendelea kushirikisha Sekta Binafsi katika kutoa huduma za Usafi, Ulinzi, Upishi na Mapokezi.
- (f) Kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Tathmini ya Utendaji Kazi wa Watumishi kwa utaratibu mpya unaolenga kuweka malengo na matokeo katika utendaji kazi (*Open Performance Review and Appraisal System (OPRAS)*) kwa watumishi wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (*ADEM*) Utekelezaji wa Malengo ya *ADEM* Mwaka 2005/2006. Katika kuimarisha mafunzo ya uongozi wa elimu nchini, Wizara yangu kupitia Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (*Agency for the Development of Educational Management (ADEM)* hutoa mafunzo, huduma ya ushauri wa kitaalamu na kufanya utafiti katika masuala ya uongozi na uendeshaji wa taasisi za elimu. Katika mwaka 2005/2006, *ADEM* imetekeliza yafuatayo:-

- (a) Kutoa mafunzo ya Stashahada ya Uongozi wa Elimu kwa Viongozi 98 wa Idara mbalimbali za Elimu hususan Walimu Wakuu, Waratibu Elimu Kata, Maafisa wa Elimu ngazi ya Wilaya, Walimu wa shule za Awali, Msingi, Sekondari na vyuo, Wafanyakazi katika mashirika yasiyo ya kiserikali (*NGOs*) yanayoshughulikia masuala ya elimu na Mameneja na wamiliki wa Shule Zisizo za Serikali.
- (b) Kutoa mafunzo ya mwezi mmoja kwa Wakuu wa Shule na Wakuu wa Shule Wasaidizi wa Sekondari za Serikali na Zisizo za Serikali 128.
- (c) Kuendesha mafunzo ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa Waratibu wa Elimu Kata 228 kutoka katika Wilaya za Temeke, Bagamoyo, Korogwe, Iramba, Magu, Maswa, Mbozi na Masasi.
- (d) Kutoa mafunzo ya mwezi mmoja ya Uongozi na Uendeshaji Elimu kwa Maafisaelimu Mikoa ya Rukwa, Dodoma, Mara, Iringa, Pwani, Arusha na  
Dar es salaam na kwa Maafisaelimu Wilaya za Temeke, Mkuranga, Kibondo, Makete, Ilala, Maswa, Mvomero, Bariadi, Sengerema, Moshi,

- Sumbawanga, Mpanda, Arusha, Kigoma, Mbeya, Mpwapwa, Iringa, Kilombero, Kisarawe, Mbeya (M) Liwale, Tabora, Rufiji, Hanang, Kibaha, Tunduru, Chunya, Singida (M), Mbozi, Bagamoyo, Pangani, Mbulu, Tandahimba, Ngara, Newala, Kondoa, Sikonge, Mbarali, Arusha (Jiji), Iringa (M), Mwanga, Rombo, Kasulu na Iramba.
- (e) Kutoa mafunzo ya Cheti cha Uongozi wa Elimu kwa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi 224 kutoka Kanda 8 za Elimu yaliyofanyika katika vyuo vya Ualimu vya Butimba, Bunda, Mrutunguru, Katoke, Tabora, Morogoro, Mandaka, Marangu, Korogwe na Kinampanda.
- (f) Kutoa mafunzo ya Uongozi na Uendeshaji Elimu kwa Wakaguzi wa Shule za Msingi 256 kutoka Wilaya mbalimbali.
- (g) Kufanya tafiti 3 za kielimu kwa kushirikiana na nchi za Malawi, Afrika ya Kusini na Uganda. Tafiti hizo ni: Uboreshaji wa Uongozi, Tabia za Viongozi na Mifano Bora ya Uongozi.

Mheshimiwa Spika, Malengo ya Mwaka 2006/2007, katika mwaka 2006/2007, *ADEM* itatekeleza kazi zifuatazo:-

- (a) Kutoa mafunzo ya Stashahada ya Uongozi wa Elimu kwa Viongozi 150 wa Idara mbalimbali za Elimu yanayowahuju Walimu Wakuu wa Shule za Msingi, Waratibu Elimu Kata, Maafisa wa Elimu ngazi ya Wilaya, Walimu wa Shule za Awali, Msingi, Sekondari, Wafanyakazi katika mashirika yasiyo ya kiserikali (*NGOs*) na Mameneja na wamiliki wa shule Zisizo za Serikali.
- (b) Kuendesha mafunzo ya Uongozi na Menejimenti ya mwezi mmoja kwa Wakuu wa Shule wapya na Wasaidizi wa Shule za Sekondari za Serikali na Zisizo za Serikali 120 kutoka Kanda zote.
- (c) Kutoa mafunzo ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa Waratibu wa Elimu Kata 2,300 kutoka Wilaya za Mpwapwa, Nachingwea, Mbinga, Urambo, Kasulu, Sumbawanga (M), Sumbawanga (V), Njombe, Kilombero, Same, Monduli, Karagwe, Singida (M), Singida (V), Dodoma (V), Ilala, Mkuranga, Kilosa, Mwanga, Lushoto, Arumeru, Babati, Geita, Tarime, Bukoba (M), Bukoba (V), Iringa (M), Iringa (V), Mbeya (J), Mbeya (V), Mtwara Mikindani, Songea (M), Songea (V) na Lindi (M).
- (d) Kutoa mafunzo ya mwezi mmoja ya Cheti cha Uongozi na Uendeshaji Elimu kwa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi 1,000 katika kanda zote za kielimu kupitia Vyuo vya Ualimu.
- (e) Kutoa Mafunzo ya miezi mitatu ya Cheti cha uongozi wa Elimu kwa Wakuu wa Shule za Sekondari 100 kutoka Kanda zote za kielimu.

- (f) Kuendesha mafunzo ya *OPRAS* kwa Maafisa Elimu Mkoa na Wilaya, Wakuu wa Shule za Sekondari, Wakaguzi wa Shule (W) na Makatibu wa Idara ya Utumishi wa Walimu. Mafunzo hayo yataendeshwa katika Kanda za Nyanda za Juu, Magharibi, Ziwa na Kanda ya Kaskazini.
- (g) Kutoa mafunzo ya mwezi mmoja ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa Maafisaelimu wa Wilaya Taaluma, Vifaa na Takwimu 40 kwa mikoa ya Tabora na Pwani.
- (h) Kutoa mafunzo ya Uongozi na Uendeshaji Elimu kwa Wakaguzi wa Shule za Msingi 200 kutoka kanda zote za kielimu.
- (i) Kutoa mafunzo ya wiki mbili ya Uongozi wa Elimu kwa wajumbe wa Bodii za Shule za Sekondari 1,000 kutoka Kanda zote za kielimu.
- (j) Kutoa mafunzo ya wiki mbili ya Uendeshaji kwa Timu za Menejimenti za Shule za Sekondari 1,400 kutoka kanda zote za kielimu.
- (k) Kuendesha tafiti za kielimu kwa kushirikiana na nchi za Malawi, Zambia, na Afrika ya Kusini. Tafiti hizo zinahusu Uboreshaji wa Uongozi, Kutathimini Mahitaji ya Mafunzo, Tabia za Viongozi, na Mifano Bora ya Uongozi katika Shule za Msingi.

Mheshimiwa Spika, Taasisi na Mabaraza ya Wizara. Taasisi na Mabaraza yaliyo chini ya Wizara yangu yanafanya kazi kwa ushirikiano ili kufanikisha utoaji wa elimu bora. Kila Taasisi na Baraza limetekeleza kazi zilizopangwa kwa kuzingatia malengo na mipango ya elimu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW). Utekelezaji wa Malengo ya TEWW mwaka 2005/2006, katika jitihada za kufuta ujinga na kujiendeleza katika mfumo usio rasmi, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) inaendelea kutoa elimu kwa vijana nje ya shule, wafanyakazi na watu wazima ambao hawakupata nafasi ya kujiendeleza katika mfumo rasmi. Ili kukamilisha malengo haya mwaka 2005/2006 Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima imetekeleza yafuatayo:-

- (a) Kuendesha mafunzo ya Stashahada ya Elimu ya Watu Wazima kwa Wanachuo 223 na Stashahada ya Juu ya Elimu ya Watu Wazima kwa wanachuo 63.
- (b) Kutoa mafunzo ya Elimu ya Sekondari kwa Walioikosa kwa Njia ya Elimu Masafa kwa walengwa 13,000.
- (c) Kuandika na kurekebisha masomo ya Kiswahili, *Civics, History, Geography, Mathematics, English na Biology* kama yanavyotolewa kwa njia ya Elimu Masafa hatua ya kwanza na ya pili yaweze kuwa katika mfumo wa moduli.

- (d) Kuchapa majarida ya “*Studies in Adult Education No. 62*” na “*Journal for Adult Education No. 14*” kwa ajili ya kuelimisha jamii na wanachuo wa Taasisi.
  - (e) Kutoa mafunzo ya Cheti cha Sheria kwa wanafunzi 168.
  - (f) Kutoa mafunzo ya kuwaendeleza wafanyakazi ya muda mfupi na mrefu kwa wafanyakazi 116.
  - (g) Kuajiri watumishi 16 wa kada mbalimbali.
- Mheshimiwa Spika, Malengo ya Mwaka 2006/2007, katika mwaka 2006/2007, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima itatekeleza yafuatayo kwa lengo la kuimarisha utoaji wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu ya Kujiendeleza nje ya mfumo rasmi kwa walioikosa:-
- (a) Kutoa mafunzo ya Stashahada ya Juu kwa walengwa 124 na Stashahada ya Kawaida ya Elimu ya Watu Wazima kwa walengwa 260.
  - (b) Kutoa Elimu ya Sekondari kwa Walioikosa kwa Njia ya Masafa au Posta kwa walengwa 30,000 kwa mikoa yote.
  - (c) Kuandika na kurekebisha masomo ya *English*, Kiswahili, *Geography* na *History* hatua ya tatu ili yaweze kuwa katika mfumo wa moduli.
  - (d) Kuchapa moduli za masomo ya *Civics*, *English*, Kiswahili, *History*, *Geography*, *Mathematics* na *Biology* za Elimu kwa Masafa hatua ya pili.
  - (e) Kuandaa na kuchapa majarida ya *Studies in Adult Education (SAED)* No. 63, *Journal of Adult Education Tanzania (JAET)* No. 15, na *Alumni News Letter* kwa ajili ya kufahamisha jamii kazi za Taasisi.
  - (f) Kuongeza idadi ya Wanachuo wa Cheti cha Sheria kutoka 168 hadi 200.
  - (g) Kutoa mafunzo ya kuendeleza Wafanyakazi wa Taasisi katika Mafunzo ya Shahada ya Urdaktari wa Falsafa 1, Shahada ya Uzamili 4, Elimu ya Sekondari 40 na Mafunzo ya Muda mfupi 60.
  - (h) Kufanya ukarabati wa chumba cha studio Makao Makuu na kujenga Kituo cha Masomo eneo la Kisota Dar es Salaam na kununua nyumba mbili kwa ajili ya ofisi za mikoa ya Mwanza na Shinyanga ambapo hakuna majengo ya Taasisi.
  - (i) Kuimarisha kazi za TEWW kwa kuweka mtandao wa intaneti katika vituo 21 vya Elimu ya Watu Wazima katika mikoa yote na kuajiri watumishi 72 wa kada mbalimbali.

- (j) Kununua magari 5 kwa ajili ya kanda ya Ziwa, Mashariki, Magharibi, Kaskazini Magharibi na Kusini.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) Utekelezaji wa Malengo ya TET Mwaka 2005/2006, katika kutoa elimu iliyo bora na inayoendana na wakati Wizara yangu kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inaendelea kuimairisha mitaala na mihutasari ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari, Ualimu na Elimu Maalumu. Aidha, TET inaendelea kubuni, kutengeneza na kuweka ubora wa vifaa vyta kufundishia na kujifunzia.

Mwaka 2005/2006 Taasisi ya Elimu Tanzania iliendelea na ukuzaji wa mitaala kwa ngazi mbalimbali kwa kutekeleza yafuatayo:-

- (a) Kuandika miongozo minne ya kufundishia masomo 9 ya Shule za Msingi.
- (b) Kuandika miongozo ya kufundishia katika shule za Awali na Elimu Maalumu.
- (c) Kutayarisha miongozo mitatu ya masomo ya Stadi za Kazi, Sayansi na Maarifa ya Jamii kwa ajili ya Darasa V-VII.
- (d) Kufaragua (*improvise*) vivunge vyta masomo ya *English*, Kiswahili na Haiba/Michezo na kuandika miongozo yake.
- (e) Kuandika miongozo miwili ya kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia katika Shule za Elimu ya Awali.
- (f) Kutathmini ufundishaji wa masomo sita ya MEMKWA katika wilaya za Ngara, Kisarawe, Musoma (V), Makete, Songea (V) na Masasi.
- (g) Kufanya mapitio kwenye vitabu, miongozo na mihutasari 6 ya MEMKWA.
- (h) Kuendesha semina 3 za kitaaluma kwa wakuza mitaala kuhusu matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), intaneti na tovuti.
- (i) Kutafiti na kutathmini njia za kufundishia na kujifunzia zinazotumika shulenii. Utafiti na tathmini umefanyika katika mkoa wa Singida kwa ufadhili wa *ADEA, CIDA, UNICEF* na *UNESCO*.

- (j) Kutoa mafunzo kwa Walimu wa Shule za Msingi 1,400, Sekondari 180, Wakufunzi 20 wa Vyuo vya Ualimu, Maafisaelimu 240 na Wakaguzi 286 kuhusu ufundishaji wa masomo yaliyomo katika mitaala iliyorekebishwa. Mafunzo hayo yamefanyika katika kanda zote kwa kiwango cha asilimia 75.

Mheshimiwa Spika, Malengo ya Mwaka 2006/2007, katika mwaka 2006/2007, TET itatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kuendesha mikutano ya paneli za masomo 10 kwa Shule za Msingi na Sekondari.
- (b) Kufaragua zana za kujifunzia na kufundishia kwa ajili ya Shule za Elimu ya Awali.
- (c) Kuandaa Mitaala na Mihutasari ya Ualimu, ngazi ya Cheti na Stashahada ili iendane na mitaala iliyorekebishwa.
- (d) Kuandika Miongozo ya kufundishia masomo ya Sekondari ya Kidato cha 1 hadi 4 kulingana na mtaala mpya.
- (e) Kufuutilia utekelezaji wa Mitaala ya Elimu ya Msingi na Sekondari.
- (f) Kuandaa vipindi 6 vya Redio na Televisheni vya kufundishia masomo ya Shule za Msingi kwa Darasa la III na IV.
- (g) Kuchapa na kusambaza kwa Wadau wa Elimu Mwongozo wa Taifa wa Ukuzaji Mitaala.
- (h) Kurekebisha vitabu 12 vya MEMKWA vya mwaka wa tatu.
- (i) Kutoa mafunzo kwa wawezeshaji kwa ajili ya upanuzi wa shughuli za MEMKWA katika wilaya ya Makete.
- (j) Kutoa mafunzo kwa Wakuza Mitaala 15 na wafanyakazi waendeshaji 10 wa Taasisi ya Elimu Tanzania katika maeneo yao ya kitaalamu.
- (k) Kuendesha Semina 3 za kitaalamu kwa wafanyakazi wote wa TET kuhusu utumiaji wa TEHAMA.

- (l) Kuchapisha na kusambaza matoleo manne ya Jarida la “*Tanzania Educational Journal*”, Kalenda ya 2007 na kuanzisha utumiaji wa tovuti ya TET ili kuelimisha jamii kuhusu kazi za TET.
- (m) Kufanya utafiti kuhusu mbinu zinazotumika kufundisha masomo katika Shule na Vyuo vya Ualimu.
- (n) Kuendesha mafunzo yahusuyo Mitaala iliyorekebishwa kwa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari, Wakufunzi wa Vyuo vya Ualimu na Wakaguzi wa Shule.
- (o) Kuandika mihutasari ya Historia, Uraia na Jiografia kwa ajili ya Shule za Msingi, *Physics* na *Chemistry* kwa ajili ya Shule za Sekondari.
- (p) Kudurusu mihutasari ya masomo ya Sekondari ya Kidato cha 5 hadi 6.
- (q) Kudurusu mihutasari ya masomo ya *Bible Knowledge, Divinity, Islamic Studies* na *Arabic Language*.
- (r) Kuandaa mwongozo wa kurekebisha masomo ya michepuo ili kuainisha masomo ya Ufundı, Kilimo, Biashara, Sayansi Kimu na Mafunzo ya Ufundı Stadi yanayotolewa na *VETA*.
- (s) Kununua gari moja kwa ajili ya kazi za *TET*.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Huduma za Maktaba (*Tanzania Library Services Board (TLSB)*) ina jukumu la kuanzisha, kutunza na kuendeleza Maktaba za Umma, Shule, Mashirika na Taasisi nyingine.

Katika mwaka 2005/2006, Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania imetekeleza kazi zifuatazo:-

- (a) Kuongeza vitabu 8,965 kutoka kwa Wafadhili.
- (b) Kuongeza Wanachama 9,626 wa huduma za maktaba.
- (c) Kukamilisha ujenzi wa Awamu ya Pili wa Maktaba ya Dodoma.
- (d) Kukamilisha Awamu ya Kwanza ya ujenzi wa majengo ya Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka Bagamoyo ambapo ujenzi umekamilika kwa asilimia 85.

- (e) Kutayarisha Hema za Kusomea Jumuiya katika vituo vya Bagamoyo, Kigoma, Kilimanjaro, Musoma, Morogoro, Dodoma, Iringa, Sumbawanga, Lindi, Mtwara, Mbeya na Tanga.
- (f) Kuendesha semina 2 na Hema za Kusomea 8 kuhusu VVU na UKIMWI. Semina na Hema zilifanyika Bagamoyo, Dar es Salaam, Musoma, Morogoro, Iringa, Sumbawanga, Moshi, Kigoma, Lindi na Tanga.
- (g) Tamasha la Wiki ya Vitabu katika mikoa ya Pwani, Dodoma, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Mtwara, Morogoro, Rukwa, Shinyanga na Tabora.

Mheshimiwa Spika, Malengo ya Mwaka 2006/2007: Mwaka 2006/2007, *TLSB* itatekeleza yafuatayo katika Mpango wa kuendeleza maktaba nchini:-

- (a) Kuimarisha na kuboresha huduma kwa kuongeza machapisho 40,000 katika mikoa 18 yenyе maktaba.
- (b) Kutoa nakala 2 za orodha ya Vitabu na Machapisho mengineyo yanayochapishwa nchini (*Tanzania National Bibliography (TNB)*).
- (c) Kuendeleza ujenzi wa Awamu ya Tatu wa Maktaba ya Dodoma kwa kujenga ukumbi wa mikutano.
- (d) Kuendeleza ujenzi wa Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka Bagamoyo.
- (e) Kukarabati majengo ya maktaba za mikoa ya Ruvuma, Mtwara, na Kagera.
- (f) Kuboresha maktaba za Shule za Sekondari 21 na Vyuo vya Ualimu 10 kwa kutoa mafunzo ya Ukutubi kwa watumishi husika.
- (g) Kuanzisha maktaba mpya katika mikoa ya Singida, Pwani na Manyara.
- (h) Kununua magari 3 kwa ajili ya kuboresha huduma za *TLSB*.
- (i) Kuendesha semina 18 na Hema za Kusomea 8 kuhusu UKIMWI katika mikoa 18 yenyе maktaba. Aidha, Hema za Kusomea (*Reading Tents*) zitaendeshwa katika vituo vya Bukoba, Songea, Mtwara, Tabora, Shinyanga, Kilosa, Njombe na Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Mitihani la Tanzania: Utekelezaji wa Malengo ya Baraza la Mitihani la Tanzania Mwaka 2005/2006; Baraza la Mitihani la Tanzania (*National Examination Council of Tanzania (NECTA)*) ni mamlaka yenyе kuendesha

mitihani ya Kitaifa ya kumaliza Elimu ya Msingi Tanzania Bara, Elimu ya Sekondari Kidato cha 4 na 6, Ufundu, Ualimu Daraja A na Stashahada.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2005/2006 Baraza la Mitihani la Tanzania limetekeleza malengo yafuatayo:-

- (a) Kuendesha na kutoa matokeo ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi 2005.
- (b) Kukamilisha Uendeshaji wa Mtihani wa Ualimu na Ufundu iliyofanyika Mei, 2005 na kutunuku Stashahada na Vyeti kwa wahitimu.
- (c) Kuendesha Mtihani wa Kidato cha 4, Ualimu Daraja A na Mtihani wa Maarifa iliyofanyika Oktoba, 2005 na Mtihani wa Kidato cha 6 ulifanyika Februari, 2006.
- (d) Kusimamia uendeshaji wa mitihani itolewayo na Bodi za nje ya nchi.
- (e) Kukamilisha Awamu ya Kwanza ya ujenzi wa Kituo cha Usahihishaji Mitihani, Mbezi Wani na kuanza Awamu ya Pili ya ujenzi.
- (f) Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi yenyenye lengo la kupunguza maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI, Kifua Kikuu, Malaria, Ukoma na Kisukari.

Mheshimiwa Spika, katika Mtihani wa Kitaifa wa Kumaliza Elimu ya Msingi mwaka 2005, kati ya watahiniwa 493,946 waliofanya mtihani, wakiwemo wasichana 240,585 na wavulana 253,361, waliofaulu walikuwa 305,062 sawa na asilimia 61.8. Wasichana waliofaulu walikuwa 131,312 sawa na asilimia 54.5 na Wavulana walikuwa 173,750 sawa na asilimia 68.5. Mwaka 2004 watahiniwa 499,241 walifanya mtihani, waliofaulu walikuwa 243,043 sawa na asilimia 48.7. Wasichana waliofaulu 104,077 sawa na asilimia 41.8 na Wavulana waliofaulu 138,966 sawa na asilimia 55.7. Takwimu zinaonesha kuwa kuanzia mwaka 2000 idadi ya watahiniwa waliofaulu imekuwa ikiongezeka.

Mheshimiwa Spika, katika Mtihani wa Kitaifa wa Kidato cha 4 mwaka 2005, kati ya watahiniwa 82,697 waliofanya mtihani, waliofaulu katika Daraja I - IV walikuwa 70,305 sawa na asilimia 85.02 ikilinganishwa na matokeo ya mwaka 2004, ambapo kati ya watahiniwa 63,370 waliofaulu walikuwa 57,970 sawa na asilimia 91.5. Watahiniwa waliofaulu Daraja I - III mwaka 2005, walikuwa 28,166 sawa na asilimia 34.03 ikilinganishwa na watahiniwa 23,929 sawa na asilimia 37.8 waliofaulu mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, katika Mtihani wa Kitaifa wa Kidato cha 6 mwaka 2005, kati ya watahiniwa 16,884 wakiwemo wasichana 5,863 sawa na asilimia 37.7 na wavulana 11,021 sawa na asilimia 65.3, waliofaulu katika Daraja I - IV walikuwa 16,362 sawa na asilimia 96.9 kati ya hao wasichana walikuwa 5,709 sawa na asilimia 97.4 na wavulana

walikuwa 10,653 sawa na asilimia 96.7. Mwaka 2006 kati ya watahiniwa 21,126 waliofanya mtihani, waliofaulu katika Daraja I – IV walikuwa 20,343 sawa na asilimia 96.3. Mwaka 2006 waliofaulu katika Daraja I - III walikuwa 18,295 sawa na asilimia 86.6 ikilinganishwa na 14,461 sawa na asilimia 88.4 ya waliofaulu mwaka 2005

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006 Mitihani mingine iliyoendeshwa na NECTA ilikuwa ni pamoja na Ualimu na Ufundu. Katika mitihani ya Ualimu ya mwaka 2005 waliofaulu na kutunukiwa vyeti kati ya watahiniwa 11,269 walikuwa 11,092 sawa na asilimia 98.4. Mwaka 2004, watahiniwa walikuwa 14,411. Waliofaulu na kutunukiwa vyeti walikuwa 14,104 sawa na asilimia 97.9. Katika Mitihani ya Elimu ya Ufundu ya mwaka 2005 waliofaulu walikuwa 420 kati ya 834 sawa na asilimia 50.3. Aidha, NECTA ilisimamia Mitihani ya Nje kwa niaba ya Taasisi za Uingereza, ikiwamo ya Chuo Kikuu cha London, Lincolnshire Institute of Purchasing and Supply, Chartered Institute of Marketing, The Royal Institute of Chartered Surveyors, The Institute of Chartered Secretaries and Administrators, Association of Chartered Certified Accountants, The Association of International Accountants, The Institute of Chartered Shipbrokers na London Association Board of Royal School of Music.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kulitaarifu Bunge lako kuwa Mitihani ya Kitaifa ya Darasa la VII, Kidato cha 4, 6 na Ualimu iliendeshwa bila kuwako uvujaji. Aidha, NECTA iliboresha mazingira ya kazi kwa kutekeleza yafuatayo:-

- (a) Kukamilisha awamu ya pili ya ujenzi wa mabweni ya kituo cha usahihishaji wa mitihani kiweze kumudu ongezeko la watahiniwa.
- (b) Kununua mashine mbili za uchapaji Mitihani na kusimikwa vipoza joto katika jengo la Chapa na Uchapaji.
- (c) Kununua kompyuta 54 na vifaa vyake kwa ajili ya kuandaa na kutoa matokeo ya mitihani.
- (d) Kuweka mtandao wa Kompyuta (*Local Area Network-LAN*) na kusimika mtambo wa kisasa wa tovuti kwa madhumuni ya kutoa huduma bora.
- (e) Kutoa mafunzo kwa wadau wote wanaoshughulikia mitihani.

Mheshimiwa Spika, Malengo ya Mwaka 2006/2007: Katika mwaka 2006/2007, NECTA imojiandaa kuendesha Mitihani yote ya Kitaifa kwa ufanisi unaohitajika, ikiwa ni pamoja na kusimamia mitihani itolewayo na Bodi 9 za Mitihani ya Nje. Aidha, NECTA itatekeleza malengo yafuatayo:-

- (a) Kutafiti, tathmini, usanifu na ukuzaji mitihani mbalimbali ya Kitaifa.

- (b) Kuendesha mitihani ya Kumaliza elimu ya msingi, Maarifa, Kidato cha Nne na cha Sita, Mtihani wa Ualimu Daraja A na Stashahada ya Ualimu.
- (c) Kuendesha Mitihani ya Cheti cha Ufundu Sanifu na Stashahada ya Juu ya Uhandisi kwa niaba ya Baraza la Taifa la elimu ya Ufundu.
- (d) Kusimamia Mitihani ya Nje inayofanywa na watahiniwa binafsi hapa nchini.
- (e) Kukamilisha ujenzi wa kituo cha kusahihishia mitihani.
- (f) Kutoa mafunzo yenye lengo la kupunguza maambukizi ya virusi vya UKIMWI, kifua kikuu, malaria, ukoma na kisukari.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu Stadi: Utekelezaji wa Malengo ya *VETA* Mwaka 2005/2006. Katika mwaka 2005/2006, (*Vocational Education and Training Authority (VETA)*) imetekeleza yafuatayo:-

- (a) Kuanza kuchora ramani za ujenzi na kutayarisha zabuni kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa Vyuo vya Ufundu Stadi vya Shinyanga, Mpanda, Tabora na Ulyankulu na ujenzi wa vyuo vipyta vya Singida na Arusha.
- (b) Kuongeza idadi ya Wasichana wanaojiunga na Vyuo Vya Ufundu Stadi vya *VETA* na visivyo vya *VETA* katika kozi ndefu na fupi kutoka 20,627 mwaka 2004/05 hadi 35,996 mwaka 2005/2006.
- (c) Kuanzisha Mpango wa Kuendeleza Walimu wa Ufundu Stadi Kitaaluma (*Skills Up-grading*). Walimu 64 wamepelekwa katika viwanda 9 vilivyopo Dar es Salaam.
- (d) Kuimarisha utekelezaji wa Mfumo Mpya wa Mafunzo (*Competence Based Education and Training*) kwa kutoa mafunzo ya Walimu, ukarabati wa karakana na uboreshaji wa vifaa vya kufundishia. Jumla ya shilingi 598.66 milioni zimetolewa kwa Vyuo Vya Ufundu Stadi vilivyosajiliwa na *VETA* kwa ajili ya kununulia vifaa vya mafunzo (*tools and equipment*). Fedha hizi zimegawiya katika Kanda.
- (e) Kukuza mafunzo ya kozi ndefu katika vyuo vinavyomilikiwa na *VETA*. Jumla ya vijana 10,741 wamepatiwa mafunzo katika ufundi stadi. Aidha, vyuo vingine vya Ufundu Stadi vilivyosajiliwa na *VETA* vilitoa mafunzo ya muda mrefu kwa vijana 31,849.
- (f) Kutoa mafunzo ya kozi fupi kwa washiriki 38,901 kutoka vyuo vya *VETA*.

- (g) Kukuza mafunzo ya Walimu wa Ufundu Stadi yanayotolewa na Chuo cha Ualimu wa Ufundu Morogoro kwa utaratibu wa kutoa mafunzo wakati Mwalimu akiwa katika kazi (*off-campus*).
- (h) Kutoa mafunzo ya Stadi za Maisha kwa vijana 10,741 katika vyuo vyote vya *VETA* na visivyo vya *VETA*.
- (i) Kutoa mafunzo kwa vijana 90 wenye ulemavu katika stadi za useremala, ushonaji nguo, ushonaji viatu, batiki na uhazili.
- (j) Kuimarisha uendeshaji wa Mitihani ya Ufundu Stadi na Biashara (*Trade Test* na *NABE*). Jumla ya watahiniwa 20,920 walifanya mitihani hii katika madaraja mbalimbali na kati yao 11,409 sawa na asilimia 54.4 walifaalu.
- (k) Kuimarisha Mitihani katika Mfumo wa Mafunzo unaotumika (*Competence Based Assessment*). Jumla ya wanafunzi 5,872 walifanya mitihani hii na 5,166 walifaalu.
- (l) Kuimarisha ushirikiano na Zanzibar katika suala la utoaji Mitihani ya Ufundu Stadi na Biashara. Jumla ya watahiniwa 384 kutoka Zanzibar walifanya mitihani mwaka 2005 na 210 walifaalu.
- (m) Kutoa mafunzo ya Ufundu Stadi kwa watoto 3,000 walio chini ya umri wa miaka 18 wenye lengo la kuwaondoa katika ajira mbaya. Mafunzo haya yalifanyika katika Wilaya za Ilala, Kinondoni, Temeke, Iramba, Kondoa, Iringa, Simanjiro, Arusha na Urambo.

Mheshimiwa Spika, Malengo ya Mwaka 2006/2007: Katika mwaka 2006/2007 *VETA* itatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kukamilisha ukarabati kwa kufunga vifaa katika Vyuo vya Ufundu Stadi vya Mara, Kagera, Dakawa, Mikumi, Songea, Oljoro na Kigoma.
- (b) Kuendelea kukarabati Vyuo vya Ufundu Stadi vya Shinyanga, Mpanda, Tabora na Ulyankulu.
- (c) Kuanza ujenzi wa vyuo vipyaa vya Singida, Arusha, Lindi, Manyara, Pwani na Dar es Salaam.
- (d) Kuhamasisha na kusaidia Vyuo vya Ufundu Stadi vya Asasi Zisizo za Kiserikali, Watu Binafsi na Taasisi za Kidini ili viweze kukuza na kuboresha mafunzo yanayotolewa.
- (e) Kuandaa Mkakati wa utekelezaji wa Mpango wa Uanzishaji wa Vyuo vya Ufundu Stadi kila Wilaya.

- (f) Kuboresha viwango vya mafunzo yanayotolewa kwa kutoa mitaala inayolingana na mahitaji ya soko la ajira.
- (g) Kutoa mafunzo ya taaluma (*skills upgrading*) ya ualimu kwa Walimu wa Ufundu Stadi waliopo na wale wanaotarajia kujiunga na kazi ya ualimu wa ufundu.
- (h) Kukuza na kuboresha mafunzo yanayotolewa kwa sekta isiyo rasmi ikiwa ni pamoa na sekta ya Kilimo ili kutoa fursa kwa walengwa kujipatia stadi na kukuza ajira na kuboresha Kilimo.
- (i) Kupanua utekelezaji wa utaratibu mpya *Integrated Training for Entrepreneurial Promotion (INTEP)* unaolenga Sekta isiyo rasmi kwa kubaini fursa za kiuchumi zilizopo katika jamii na kutoa mafunzo kulingana na fursa hizo.

Mheshimiwa Spika, Changamoto Katika Utekelezaji: Katika kutekeleza Malengo, Mipango na Programu mbalimbali za elimu zilizopangwa, Wizara yangu imekabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- (a) Kuwepo kwa pengo la fedha kwa programu za MMEM na MMES. Pengo la fedha katika programu hizi limesababisha kutofanyika kwa baadhi ya kazi muhimu zilizopangwa kama vile ujenzi wa vyumba vya madarasa, nyumba za walimu na maabara na hivyo kuathiri utekelezaji wake.
- (b) UKIMWI bado ni tishio katika maendeleo ya Elimu ambapo unaathiri Walimu, wafanyakazi, wanafunzi na jamii kwa ujumla ambayo ni nguvu kazi ya Taifa.
- (c) Upanuzi wa Vyuo vya Ufundu hauendi sambamba na mahitaji ya wahitimu wanaomaliza Elimu ya Msingi na Sekondari.

Mheshimiwa Spika, Maamuzi Muhimu: Katika mwaka 2006/2007 Wizara yangu itatekeleza maamuzi yafuatayo:-

- (a) Ajira ya Walimu itakuwa ya moja kwa moja mara wanapohitimu vyuo bila kusailiwa. Aidha, Walimu wastaifu wenye afya nzuri inapobidi wataajiriwa kwa mkataba katika kukabiliana na upungufu wa Walimu. Wahitimu wa Kidato cha 6 na Vyuo Vikuu wasiokuwa na taaluma ya Ualimu wataajiriwa na kupewa mafunzo maalumu ili kukabiliana na uhaba wa Walimu. Mkakati huu ni wa muda mfupi.
- (b) Kwa kutambua kuwepo kwa baadhi ya maeneo kuwa na mazingira magumu ya kazi kwa Walimu, Wizara yangu itafanya mapitio ya Muundo

wa Utumishi wa kada ya Walimu (*Scheme of Service*) pamoja na kutoa kipaumbele kwa maeneo yenyе mazingira magumu.

- (c) Serikali itaendelea kugharimia wanafunzi wanaotoka katika familia zenyе kipato duni kwa kuzingatia taratibu na kanuni zinazowabainisha wanafunzi wa aina hiyo ikiwa ni pamoja na kudhibiti ukiukwaji wa taratibu unaonufaisha wasiostahili.
- (d) Wizara itaendelea kushusha madaraka ya uendeshaji na usimamizi wa Shule za Sekondari hatua kwa hatua kwa kuzijengea uwezo na hatimaye kuzipatia madaraka zaidi Bodi za Shule, Halmashauri na Mikoa. Hali hii inaweza kuimarisha na kudhibiti ubora wa majengo na unununzi wa vifaa mbalimbali vya shule ikiwa ni pamoja na kusogezza huduma karibu na wadau wa elimu. Kuanzia mwaka 2006/2007 kila Wilaya itakuwa na Mratibu wa Elimu ya Sekondari.
- (e) Mipango ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi na Sekondari (MMEM na MMES) ni endelevu. Aidha, rasimu ya andiko la Awamu ya Pili la MMEM 2007 – 2011 imeshaandaliwa ili kufikia malengo ya Elimu kwa Wote (*EFA*) na Malengo ya Milenia (*MDGs*). Kwa misingi hiyo programu ya MMEM ni endelevu na Wadau wa Elimu wanatakiwa kuendelea kusimamia utekelezaji wake.
- (f) Wizara itaendelea kusisitiza suala la michezo shulenii hususan kuwepo kwa viwanja, vifaa na Walimu wa michezo. Aidha, Wizara yangu itashirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo katika kuhakikisha kuwa kunakuwepo na Mpango Kabambe wa kuibua vipaji vya Wanamichezo Shulenii ikiwa ni pamoja na kuangalia uwezekano wa kuwa na shule zenyе mchepuo wa michezo.
- (g) Wizara itaanzisha Baraza la Ushauri wa Elimu (*National Education Advisory Council*) kwa ajili ya kutoa ushauri kwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundı.
- (h) Wizara itaendelea kutoa Elimu ya kujikinga na VVU na UKIMWI kwa wanafunzi, walimu, wafanyakazi na jamii kwa ujumla. Aidha, Wizara itaendelea kubaini na kutayarisha mikakati ya kutoa huduma, faraja na ushauri nasaha kwa walioathirika, yatima na kuelimisha walemaavu.
- (i) Kuimarisha Shule za Kitaifa ili kujenga Umoja wa Kitaifa kwa Wanafunzi.

- (j) Wizara itaweka mkazo katika utoaji wa Elimu Maalumu kwa kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia yanayozingatia usawa kwa walemau kupata elimu bora.
- (k) Madeni ya Walimu yanayohusu Uhamisho, Likizo, Matibabu na Posho ya Kuanza Kazi ya Walimu ya kipindi kilichopita hadi Januari 2006 yameshachambuliwa na kuhakikiwa. Uhakiki huu umebaini deni halali la Shilingi 855,107,220.00 ambalo litaanza kulipwa mwaka wa fedha wa 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, Shukrani Na Pongezi: Nachukua nafasi hii kuwashukuru wananchi wote kwa ushiriki na michango yao ya hali na mali katika utekelezaji wa Mipango ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı.

Aidha, nawapongeza viongozi wote wa ngazi mbalimbali pamoja na Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Madiwani kwa kushiriki kwao katika kufanikisha utoaji na uendeshaji wa Elimu na Mafunzo ya Ufundı. (*Makofisi*)

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani za pekee kwa Wahisani mbalimbali kwa kuchangia utekelezaji wa Mipango ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı. Wahisani hao ni Uswidı, Uingereza, Ufaransa, Ireland, Japan, Norway, Finland, Canada, Uholanzi, Ujerumanı, China, Jamhuri ya Watu wa Korea, Ubeligiji na Umoja wa Nchi za Ulaya (EU).

Aidha, mashirika yaliyochangia Elimu na Ufundı ni pamoja na Benki ya Dunia (WB), WFP, UNICEF, UNESCO, ILO, UNFPA, UNDP, Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB), NORAD, GTZ, DFID, Sida, CIDA, EU, JICA, USAID, JOVC, VSO, CELTEL, CBP, OPEC, DANIDA, Peace Corps, Book Aid International, Aga Khan Education Foundation, Plan International, Sight Servers International, UNAIDS, World Vision, Ireland Aid, Care International na mashirika mengineyo.

Pamoja na misaada hiyo, utekelezaji wa Mipango ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı kwa mwaka 2005/2006 haungefanikiwa na kukamilika katika kiwango nilichoelezea bila jitihada, ushirikiano na uongozi wa pamoja katika Wizara yangu.

Natoa shukrani zangu za dhati kwa Wakurugenzi wa Idara zote, Viongozi wa Elimu na Mafunzo ya Ufundı katika ngazi mbalimbali, Walimu na Wafanyakazi wengine wote wa Wizara yangu kwa ushirikiano walionipa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı; na katika maandalizi ya Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu pia kwa Wenyeviti, Wakurugenzi Watendaji, Makatibu Watendaji na Wajumbe wa Mabaraza na Taasisi zote zilizo chini ya

Wizara yangu na Wafanyakazi wengine wote katika ngazi mbalimbali kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuimarisha na kuendeleza Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Aidha, natoa shukurani na pongezi kwa uongozi wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Chama cha Mameneja na Wamiliki wa Shule Zisizo za Serikali (*TAMONGSCO*), Chama cha Wachapaji na Asasi za Kiraia (*Civil Society*) kwa ushirikiano wao mzuri na ari yao ya kushirikiana na Wizara katika kutatua matatizo mbalimbali.

Napenda kuwashukuru viongozi wa matawi ya TUGHE na CWT Makao Makuu ya Wizara kwa ushirikiano na ushauri wao katika kushughulikia masuala ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Bajeti ya Wizara Mwaka 2006/2007. Baada ya kueleza yote hayo, ninaomba sasa Bunge lako lijadili hoja yangu pamoja na kuzingatia Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii na kupitisha makadirio ya matumizi ya shilingi 239,650,710,000/= ili kuwezesha Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kutekeleza mipango ya mwaka 2006/2007 kati ya fedha hizo:-

- (a) Shilingi 133,964,077,900/= zinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi; na
- (b) Shilingi 105,686,632,100/= zinaombwa kwa ajili ya Mipango ya Maendeleo ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naafiki!

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa, kwa sababu ambazo siyo lazima nizieleze, sasa mimi nitatoka na ataingia Naibu Spika. (*Makofii/Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaazna kazi, naomba nisome Kanuni mojawapo. Nasoma Kanuni 126, Waheshimiwa Wabunge naona hawana kitabu. Kanuni Namba 126 inasema kwamba: “Iwapo jambo au shughuli yoyote halikuwekewa masharti katika Kanuni hizi, Spika ataamua desturi na utaratibu wa kufuatwa katika jambo au shughuli hiyo na uamuhi huo pia utaingizwa katika Kitabu cha Maamuzi ili kuongoza mwenendo wa baadaye“.

Waheshimiwa Wabunge, sasa, katika miaka yote tumekuwa hapa Bungeni, Spika huwa anakaa katika kiti. Akitoka Naibu anakaa katika kiti au Wenyeviti tulio wachagua. Lakini katika taratibu hizo hizo kwamba Spika, anaweza kuwa au anaweza asiwe , isipokuwa Naibu Spika, lazima awe . (*Makofii*)

Lakini akiishaingia humu Bungeni Spika anakuwa mmoja wa sisi Wabunge. Sasa, Spika, siku nyingine anakuwa na shughuli zozote zile anazofanya ofisini kwake amalize. Sasa, Dodoma ni mahali padogo sana, Spika itabidi asikilize kwenye *microphone* zilizoko kule ofisini. Kwa hiyo, tumefikiria kwamba kwa sababu ya nafasi ya kuwa Spika ni na hakuna Kanuni yoyote humu ndani inamzuia Spika asiweze kukaa ndani ya Bunge akasikiliza ila anaweza kukaa lakini asiongoze kikao anakokaa wala asiulize swali wala asijadili kitu chochote. Kwa hiyo, tumeamua kwamba kiti kile peke yake kama anachokaa Naibu Spika kule, Spika akiwa hana shughuli zingine anaweza kukaa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, tunamshukuru Mbunge wa Ruangwa, Mheshimiwa Sigifrid Ng'itu, kwa kumwachia Spika kiti. (*Makofi*)

Baada ya hapo, namwita Mwenyekiti wa Kamati iliyojadili Wizara hii Mheshimiwa Omar S. Kwangw'. (*Makofi*)

**MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe mwenyewe kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı kwa mwaka wa fedha 2005/2006, na Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı, kwa mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kuchukua fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Babati Mjini, kumpongeza Mheshimiwa Jakaya M. Kikwete kwa kuchaguliwa kwake kuliongoza Taifa akiwa Rais wa nchi yetu na Mwenyekiti wa CCM na pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kwake kuwa Makamu wa Rais. Vile vile naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Edward N. Lowassa, , kwa kuchaguliwa kuwa wa Monduli na kuteuliwa kwake kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pamoja nao nawapongeza viongozi wote waliochaguliwa na walioteuliwa katika ngazi mbalimbali. Nawatachia wote kila laheri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa kwake. Vile vile naomba nikupongeze wewe kwa kuchaguliwa kwako kuwa Naibu Spika wa Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ilichambua Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı, katika maeneo yafuatayo:-

Taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati na malengo ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı kwa mwaka wa fedha 2005/2006.

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wi zara na Mpango wa Maendeleo, kwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malengo na Dira na Dhima ya Wizara. Kamati imeridhika na dira ya Wizara inayolenga kuwa na Mtanzania aliyeelimika kwa kiwango cha juu, mwenye maarifa, mahiri, na anayekomaa kiutamaduni ili aweze kukabiliana na changamoto za kitaifa na kimataifa katika nyanja za kisiasa, kijamii na kiuchumi ifikapo mwaka 2025. Aidha, Kamati inaunga mkono dhima ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu inayolenga kuhakikisha kuwepo mazingira mazuri ya kisheria na kiutendaji yatakayowezesha wadau wote wenyewe nia na uwezo wa kutoa elimu iliyo bora, washiriki kupanua elimu hiyo katika ngazi zote na kutoa fursa sawa kwa wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Malengo ya Bajeti ya Mwaka 2005/2006: Kamati inaipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu kwa mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa malengo ya bajeti ya mwaka 2005/2006 hasa katika utekelezaji wa Mpango wa MMEM unaohusu ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu, matundu ya vyoo, ununuvi wa samani na uboreshaji wa mazingira ya kufundishia na kujifunzia na upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

Vilevile kwa mafanikio yaliyofikiwa katika kuandikisha wanafunzi katika Shule za Msingi hasa darasa la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Matatizo Katika Utoaji Wa Elimu Bora: Matatizo ni mengi na kwa sababu ya muda tunatoa maoni kwenye maeneo machache tu, mengine yatasemwa vizuri na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Moja, Kuacha shule: Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kuandikisha wanafunzi wengi wa darasa la kwanza chini ya MMEM, kumekuwapo na kuacha shule kwa wanafunzi na kushindwa kuendelea na masomo na hivyo kupunguza matazamio ya Umma na ya Serikali kuanzisha mpango wa MMEM.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakati Kamati yangu ikichambua Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu, ilibaini kuwepo kwa matukio ya kuacha shule kwa wanafunzi na kupunguza lengo la Serikali la kuona kuwa watoto wote wenyewe umri wa kuanza shule wanaandikishwa kuanza Elimu ya Msingi na wote wanaendelea na masomo hadi darasa la saba kwa asilimia 100.

Aidha, matazamio ya jamii na Serikali ni kutekeleza mipango ya MMEM na MMES ili asilimia 50 ya wanafunzi waweze kuendelea na Elimu ya Sekondari hadi kidato cha nne, na asilimia 25 wajiunge na Elimu ya Sekondari hadi kidato cha sita na hatimaye asilimia 12.5 wajiunge na Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuthibitisha ukubwa wa tatizo la kuacha shule katika Elimu ya Msingi, Kamati yangu ilipewa takwimu na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu kwa wanafunzi wa mkoa wa Morogoro tu walioacha shule na kupata mimba katika kipindi cha mwaka 2005 kama ifuatavyo:-

<b>Wilaya</b>	<b>Waliopata mimba</b>
Kilosa	99

Kilombero	102
Manispaa	4
Morogoro	48
Mvomero	24
Ulanga	123
<b>Jumla</b>	<b>400</b>

Pamoja na jedwali hilo hapo juu, kamati ilielezwa kuwa kuanzia Januari hadi Aprili mwaka huu wa 2006, wanafunzi 90 wamethibitika kupata mimba mkoani Morogoro, na wanafunzi 415 walipata mimba katika mkoa wa Mtwara mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu hizi ni za mikoa miwili tu na hazijumuishi wanafunzi wa kiume ambao nao huacha shule na kujihusisha na vitendo vingine katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, picha tunayopata kutokana na takwimu hizi ni kuwa watoto wanaoacha shule ni kikwazo kwa mafanikio ya jitihada za Serikali za kuongeza na kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika Elimu ya Msingi na pia kuboresha na kuongeza idadi ya shule za Sekondari.

Tabia ya wanafunzi kuacha shule haiwezi kufumbiwa macho; kwani hatima yake ni kuongezeka kwa idadi ya watu wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu na hii itakuwa na maana ya kupunguza vita dhidi ya ujinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tatizo la kuacha shule kwa wanafunzi shulenii, Kamati inashauri Serikali katika ngazi zake zote kuchukua hatua madhubuti kuona kuwa wote walioandikishwa na kuanza darasa la kwanza wanafanikiwa kumaliza darasa la saba kwa kuweka mkazo katika kuwaelimisha wazazi na sasa wakati umefika kwa Serikali na jamii kuzingatia kanuni ya uandikishaji na mahudhurio shulenii ya 2002 iitwayo *The Primary School Compulsory Enrolment and Attendance Rules 2002*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tatizo la wasichana kufaulu kwa kiwango cha chini kuliko Wavulana: Kumekuwepo na takwimu za wasichana kufaulu kwa kiwango cha chini kuliko wavulana katika shule za Msingi na Sekondari katika mitihani ya kitaifa kama takwimu ya elimu ya Msingi ya mwaka 2002 kwa mikoa michache kama inavyoonyesha hapa chini:-

<b>Mikoa</b>	<b>Wavulana</b>	<b>Wasichana</b>	<b>Wastani wa jumla</b>
Mara	40.0%	6.0%	28.0%
Mwanza	41.0%	17.0%	30.0%
Lindi	40.7%	22.9%	31.5%
Pwani	33.6%	17.6%	25.6%

Kigoma	38.5%	12.2%	25.2%
Shinyanga	25.0%	10.0%	17.0%
Manyara/Arusha	33.0%	23.0%	28.0%

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi ni takwimu za miaka michache iliyopita, hivyo ni muhimu kujua hali ikoje sasa (2006) kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri Serikali kuwa kila shule ya msingi ipewe malengo mahsusini namna ya kuondoa tatizo la wanafunzi wa kike kufaulu kwa kiwango cha chini na taarifa au takwimu za namna ya kuondoa tatizo hili ziwe zikitolewa kila mara kwa wadau wote. Pamoja na hali hii, Kamati inatoa pongezi maalum kwa wasichana waliofaulu vizuri sana katika mitihani yao mpaka wakapewa zawadi na tuzo hivi karibuni katika Ukumbi wa Karimjee Dar es Salaam, Maoni yetu ni kuwa “Wasichana wanawenza na Taifa liwawezeshe”. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango Wa Kuimarisha Elimu Ya Sekondari (MMES): Kamati inapongeza Serikali kwa kutekeleza mpango maalum wa kuimarisha Elimu ya Sekondari (MMES) kwa lengo la kuendeleza na kulinda mafanikio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) kuanzia mwaka 2004/2005. (*Makofi*)

Ni matarajio ya Kamati kuwa Serikali pia itaanza mapema maandalizi kwa Vyuo vya Elimu ya Juu ili kupokea mafanikio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapongeza Serikali ya awamu ya nne kwa kuanza kwa kasi nzuri katika kuongeza na kuimarisha Elimu ya Sekondari ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa watoto wengi wanaostahili kujunga na Elimu ya Sekondari wanapewa nafasi katika shule zilizopo na kujenga shule mpya za Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kuwa katika kutekeleza mpango wa MMES Serikali iwe makini na kuona kuwa matatizo au mapungufu yaliyojitokeza wakati wa kutekeleza mpango wa MMEM hayatokei katika mpango wa kuimarisha Elimu ya Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaamini kuwa ujenzi na upanuzi wa Elimu ya Sekondari utafanikiwa kwa ubora unaotakiwa na kwa gharama nafuu iwapo wananchi watashirikishwa katika ujenzi ikiwa ni pamoja na kuwashawishi wachangie nguvu zao pale inapowezekana kama kufyatua na kuchoma matofali kwa ajili ya kujengea vyumba vya madarasa, badala ya kutumia fedha yote kuititia makandarasi kujenga madarasa na nyumba za walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapongeza Serikali kwa kuanzisha mpango mzuri wa kuandaa walimu wa shahada ya kwanza kwa ajili ya kufundisha katika shule za

Sekondari ambazo zinaongezeka nchini kote kwa kupandisha hadhi Chuo cha Ualimu Changombe - Dar es Salaam na Sekondari ya Mkwawa- Iringa kuwa Vyuo Vikuu Vishiriki vya Ualimu vya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa lengo la kutoa wahitimu wengi wa ngazi ya shahada ili kukidhi mahitaji ya mpango wa MMES.

Mheshimiwa Naibu Spika, Aidha, Kamati inashauri kuwa pamoja na kazi nzuri inayofanywa ya kuimarisha elimu chini ya MMEM na MMES kwa mkopo toka Benki ya Dunia, ni vema Serikali ikatafakari uwezekano wa kuanzisha mipango endelevu ya kuimarisha na kuendeleza mafanikio haya (*Sustainable Development*) kwa fedha zetu za ndani kama tunavyotumia fedha zetu za ndani kwa miradi maalum kama ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kupunguza ada kwa shule za Sekondari, bado utaratibu wa kulipa ada unaleta adha kwa watoto ambao wazazi wao hawana uwezo na hivyo wengi kuacha Shule. Kamati inashauri kuwa, Serikali itafute utaratibu mzuri zaidi wa kukusanya ada badala ya utaratibu unaotumika wa Wakuu wa shule kukusanya ada na mara kadhaa kuwarudisha wanafunzi nyumbani kufuata ada. Hali hii husababisha wanafunzi kukosa masomo na hivyo inaweza kushusha ubora wa kiwango cha taaluma kwani sasa tumefikia mahali kuwafanya Wakuu wa shule kuwa kama wakusanya ushuru badala ya kusimamia taaluma mashulenii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kuwa Serikali ihangaike na mzazi zaidi kulipa ada ya shule ya watoto wake ili Wakuu wa shule waache watoto wasome; watoto wasiangaliwe kama walipa kodi, kamwe hawastahili kabisa adha hii ya kurudishwa nyumbani kila wakati kwani ada inaweza kukusanywa na Halmashauri au kwa kutumia wakala. Aidha, kuanzishwe mikataba kati ya wazazi na Serikali na siyo kati ya watoto na shule au Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine la Elimu ni wanafunzi kushindwa katika masomo ya Hisabati na Lugha. Katika mazingira ya ulimwengu wa sasa ambao unatawaliwa na matumizi ya sayansi na teknolojia, Hisabati na Lugha ni muhimu sana. Somo la Hisabati husaidia katika kufikiri na kurahisisha na somo la Lugha ni ufunguo wa masomo mengine yote. Serikali isimamie kwa karibu kwa kutoa kipaumbele kwa masomo ya Sayansi, Hisabati na lugha kwa kuwepo walimu katika masomo hayo, ili wanafunzi wanapochaguliwa kuendelea na masomo ya elimu ya juu waweze kuwasiliana vizuri na walimu wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uongozi wa Sekondari: Kutokana na kuongezeka kwa shule za Sekondari kwa wingi na kwa kutekeleza sera ya kuwa na shule za Sekondari kwenye ngazi ya kila Kata, kunahitaji muundo au utaratibu mpya utakaoweza kusimamia na kuhudumia shule za Sekondari. Hivyo Kamati inashauri kuwa Serikali ianzishe utaratibu wa utawala utakao ratibu Elimu ya Sekondari ngazi ya Wilaya lakini vile vile kwa kuzingatia kuwa elimu ya sekondari bado iendelee kuwa chini ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hapa nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundii kwa kusema hili katika Bajeti yake. Kwa kweli tunampongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika ziara za Kamati Mikoani na taarifa kutoka kwa Wadau kwenye maeneo mbalimbali imedhihirika kuwepo udhaifu wa uongozi na vilevile baadhi ya Wakuu wa Shule za Sekondari kutoshirikisha vizuri walimu na wanafunzi katika maamuzi mbalimbali na hatimaye kushusha taaluma na pia kusababisha migogoro na migomo baridi shulenii. Kamati inashauri kuwa Wizara sasa ichukue hatua za makusudi kurekebisha hali hiyo kwa kujipanga upya.

Aidha, kwa ngazi ya Wizara Kamati inashauri kuwa isiwakumbatie Wakuu wa Shule ambaa shule wanazosimamia zinashuka kitaaluma mwaka hadi mwaka kwa sababu tu ya udhaifu wa uongozi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukaguzi wa Shule. Ukaguzi wa shule ni muhimu katika kutathmini maendeleo ya shule na kubaini maeneo yanayohitaji kuboreshwa. Aidha, ukaguzi wa shule ni njia ya kuleta uwajibikaji katika uendeshaji wa shule. Kamati inatoa ushauri ufuataao:-

- (a) Kasi ya ukaguzi iongezwe kwa kutoa mafunzo zaidi kwa Wakaguzi ngazi za Wilaya na Kanda, kwani idadi ya wakaguzi wanaopewa mafunzo kila mwaka haiendani na kasi mpya katika kuboresha elimu. (*Makofi*)
- (b) Serikali itenye fedha zaidi kwa ajili ya kufanikisha ukaguzi na kuondoa vishawishi vyovoyote kutoka kwa wale wanaokaguliwa.
- (c) Taarifa za Ukaguzi zirejeshwe kwenye Halmashauri, Kamati za shule na wadau wengine ili maeneo yenye udhaifu yaweze kuboreshwa na hatua zaidi kuchukuliwa. Hatua hizo zisicheleweshwe kwa urasimu wowote.
- (d) Idara ya ukaguzi ipewe kipaumbele kwa kuondolewa tatizo la usafiri hasa magari walau kila Halmashauri ipewe gari moja kama kweli tumedhamiria kusimamia ubora wa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Mitihani la Taifa; Kamati inafahamu Baraza la Mitihani la Taifa linafanya kazi nyeti ambayo inabidi ifanyike kwa tahadhari kubwa na katika mazingira sahihi. Aidha, tunaipongeza Serikali kwa kuimarisha utendaji wa Baraza la Mitihani la Taifa kufikia kiwango cha sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo Kamati imebaini kuwa Baraza la Mitihani inakabiliwa na matatizo ambayo ni pamoja na kuchakaa kwa vyombo vyakusafirishia mitihani, kuchakaa kwa magari na upungufu wa vitendea kazi ambavyo

haviwiani na ongezeko la wanafunzi. Pia wataalam waaminifu wengi zaidi wanahitajika sasa ili kuongeza ufanisi wa kazi hii nyeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia kuwa Serikali imeimarisha Elimu ya Msingi na Elimu ya Sekondari na kuongeza idadi ya watahiniwa, vivyo hivyo ukubwa wa kazi za Baraza la Mitihani unaongezeka. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuimarisha na kuboresha uwezo wa Baraza hilo ili liweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. (*Makofi*)

Aidha, Kamati inashauri Serikali kusaidia Baraza hilo kukamilisha ujenzi wa jengo maalum kwa ajili ya kusahihishia mitihani ambalo ujenzi wake umesimama kwa ukosefu wa fedha. Kamati inaamini kuwa tatizo kubwa pengine siyo fedha bali ni maamuzi yetu katika kupanga vipaumbele vyetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Elimu Tanzania (TET): Taasisi ya Elimu ni chombo mahsus kwa ajili ya kuandaa na kukuza Mitaala ya Elimu kuanzia ngazi ya Shule za Awali, Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu, kudhibiti ubora wa zana zinazotumika kutekeleza mitaala, kutunga na kuchapisha mihtasari, kuunda na kusambaza zana za kufundishia mashulenii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kuwa Taasisi ya Elimu Tanzania ipewe madaraka ya kushirikiana na vyombo mbali mbali vinavyohusika na elimu katika kuandaa mitaala ambayo inakubalika na kukidhi mategemeo ya umma wa Tanzania.

Aidha, Taasisi hiyo itengewe Bajeti inayolingana na majukumu yake na ipewe jukumu la kutunga na kuthibitisha vitabu vya kufundishia katika ngazi za elimu zinazohusika kuziandalia mitaala. Vilevile mabadiliko ya mitaala yanapotokea wapo watu wanaoweza kutumia mwanya huo kuandika vitabu kwa lengo la kuuza na kupata faida tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kuwa Taasisi ya Elimu Tanzania ianzishe ushirikiano wa karibu zaidi na Taasisi kama hii ya Zanzibar, kwa sababu kwa ngazi ya Elimu ya Sekondari wanafunzi hutahiniwa kwa kutumia mitihani inayotungwa na Baraza la Mitihani la Taifa linalozingatia mitaala inayoandalishi na Taasisi ya Elimu Tanzania. Hivyo, ili kuwatendea haki watahiniwa wa Zanzibar ni vema kuwepo makubaliano kati ya pande zote mbili kuhusu mitaala inayotumika nchini kote katika ngazi zilizotajwa hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri Taasisi ya Elimu kuwa iwapo kutajitokeza kwa Serikali au wadau kutaka mabadiliko makubwa ya msingi katika mitaala inayotumika katika shule zetu, ni vyema ikashirikisha wadau wakuu na wanataluma wa elimu kutoka kwenye ngazi za msingi. Pia Kamati ya Bunge ishirikishwe tangu hatua za awali badala ya utaratibu wa kuwashirikisha wadau hatua za mwisho ambapo ikitokea jamii kukataa mabadiliko, itakuwa gharama kubwa kwa walipa kodi na pengine kuvurugika kwa utaratibu mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Elimu ya Ufundu (*Vocational Training*) ni muhimu kwa kuwezesha wahitimu kujajiri wenye na pia kupata taaluma muhimu ambazo wahitimu wanaweza kuzitumia katika maisha yao ya kila siku. Kamati inashauri kuwa Serikali ifanye juhudhi za makusudi za kuimarishe na kupanua Vyuo vya Ufundu Stadi kwa kuvifanya ukarabati, kupanua karakana zake na kuhakikisha kuna vifaa vya kisasa na vyatofu kutoa taaluma zinazokidhi mahitaji ya jamii na kwa kiwango cha juu sambamba na ongezeko la mahitaji ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapongeza utaratibu wa Serikali wa kujenga Vyuo vya Ufundu *VETA* kwa kila Mkoa na kwa kuanza utekelezaji wa kujenga vyuo hivyo kwa Mikoa mitatu iliyokuwa imebakia ya Lindi, Pwani na Manyara. Hata hivyo Kamati inashauri kuwa Serikali ione umuhimu na ulazima wa kujenga vyuo vya *VETA* katika kila Wilaya katika harakati za kuongeza ajira. (*Makofisi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Elimu Ya Watu Wazima, Kamati inapenda kuishauri Serikali kufanya juhudhi za makusudi kufufua Elimu ya Watu Wazima kwani ingawa Bunge limekuwa linaidhinisha fungu kila mwaka, Elimu ya Watu Wazima imekuwa haipewi uzito unaostahili wakati tunashuhudia idadi ya wasiojua kusoma na kuandika ikiongezeka. Kamati inashauri kuwa Kamati za Elimu ya Watu Wazima, zifufuliwe katika ngazi zote, pamoja na kuwashirikisha washikadau wote yaani Halmashauri za Wilaya, Mashirika yasiyo ya Kiserikali na watu binafsi katika kukusanya na kutumia rasilimali zilizopo kwa ajili ya kufanikisha Elimu ya Watu Wazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, ione umuhimu wa kuanzisha mikakati ya kuleta mabadiliko yanayoendana na wakati katika kutekeleza majukumu yake, kama kuanzisha tovuti yake na kurahisisha mawasiliano kati yake na wanafunzi kwa kutuma masomo kwa njia ya mtandao wa kompyuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani, mwisho naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu, Mheshimiwa Margreth Sitta (Mbunge) na Naibu Mawaziri wake Mheshimiwa Ludovick Mwananzilla (Mbunge) na Mheshimiwa Mwantumu Mahiza (Mbunge), kwa ushirikiano wao wakati wa kujadili taarifa ya utekelezaji wa malengo ya bajeti ya mwaka 2005/2006 pamoja na Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu, kwa mwaka wa 2006/2007.

Aidha, nawapongeza wataalam wote wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu wakiongozwa na Katibu Mkuu Profesa Hamis Dihenga, kwa ushirikiano waliotoa wakati Kamati ilipokuwa inajadili Fungu 46.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii kwa umakini na ushiriki wao wakati wa kujadili taarifa ya utekelezaji wa malengo ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu, kwa mwaka wa fedha wa 2005/2006 na kufikiria Makadirio ya Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2006/2007. (*Makofisi*)

Mheshimiwa Spika, kwa heshima naomba niwatambue wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii waliochambua Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundsi Fungu 46 kwa kutaja majina yao kuwa ni Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, ambaye ndiyo Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mheshimiwa Profesa Feetham Banyikwa, Mheshimiwa Hasnain Dewji, Mheshimiwa Meryce Emmanuel, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa, Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Phares Kabuye, Mheshimiwa Janet Kahama, Mheshimiwa Mariam Kasembe, Mheshimiwa Sameer Lotto, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mheshimiwa Khadija Saleh Ngozi, Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mheshimiwa Faustine Rwiombwa, Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mheshimiwa Fatma Abdalla Tamim na mimi mwenyewe kama Mwenyekiti wao. (*Makofi*)

Mwisho nampongeza Katibu wa Bunge, Ndugu Damian Foka na ofisi yake kwa kuhudumia vizuri Kamati hii wakati inachambua Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundsi kwa mwaka 2006/2007. Aidha, nawapongeza Makatibu wa Kamati hii Ndugu Theonest Ruhilabake na Ndugu Lina Kitosi, kwa umahiri wao katika kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. PHARES K. KABUYE - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kutoa maoni juu Kambi ya Upinzani.

Kabla sijaendelea naomba niseme kwamba kuna siku moja niliaga kwamba nakwenda nyumbani kwenye kesi na inawezekana mnaponiona hapa mkaniita mwongo, bahati nzuri kesi imeahirishwa mpaka hapo tutakapoambiwa tena. Kwa hiyo, msishangae kuona bado niko pamoja na ninyi tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua wasaa huu kwa mujibu wa Kanuni zetu za Bunge kifungu cha 43(5) (b)(c) na 81(1) Toleo la mwaka 2004, kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani (vyama mbadala) kuhusiana na Bajeti ya Elimu na Mafunzo ya Ufundsi kwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile hotuba hii imewasilishwa mezani, naomba inukuliwe ilivyo katika *Hansard* hata kama sitakuwa nimemaliza kuisoma yote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote naomba uniruhusu kutoa shukrani kwa chama changu cha siasa cha *TLP* kilichoniruhusu kwenda kwa wananchi kuomba kura na wananchi wa Jimbo la Biharamulo Magharibi walionipa kibali cha kuwa sauti yao katika Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumshukuru Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni kwa kunateua kuwa Waziri Kivuli wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis. Nitajitahidi kuonyesha kuwa hawakufanya makosa katika uteuzi huu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kuwahakikishia Watanzania kuwa tutajitahidi kwa kadri ya uwezo wetu kuunga mkono jithada zote zenye lengo la kuwapatia wananchi wa Tanzania elimu bora itakayowawezesha kupambana na mazingira yao ili waishi katika maisha bora na kuendeleza kizazi cha Mtanzania. (*Makofî*)

Katika Taifa lolote lenye nia ya kujiendeleza, sekta ya elimu ni sekta muhimu sana ambayo ndiyo yenye haki ya kupewa kipaumbele cha kwanza katika mipango ya maendeleo. Ni elimu bora tu ndiyo imekuwa msingi imara kwa Mataifa yote yaliyoendelea na yanayoendelea duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, historia ya Taifa letu inaonyesha kuwa sekta ya elimu ni moja ya sekta nyeti ambazo zimekuwa uti wa mgongo wa ujenzi wa Taifa letu. Sekta hii ilitumika ipasavyo katika kuwajengea vijana wa nchi hii dhamira ya uzalendo kwa nchi yao, kujenga moyo wa Utanzania ultiotukuka, kujenga viongozi wa baadaye kama ndugu yetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na zaidi kujenga wasomi waliotukuka kama hayati Profesa Chachage Seth Chachage ambaye ametutoka hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sera ya elimu kwa wote katika miaka ya 1970, kwa nia iliyothabiti kabisa ya kuwasaidia Watanzania kuondokana na adui ujinga, umaskini na maradhi, Serikali yetu ilianzisha mikakati ya utekelezaji wa sera ya elimu kwa wote yaani *Universal Primary Education (UPE)*, ambayo ilipitishwa mwaka 1974 na kuanza kutekelezwa mwaka 1977.

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi wa kufanya elimu kuwa haki ya wote, wenye uwezo na wasio na uwezo, makupe kwa makabwela, walala heri kwa walalahoi, ulikaribishwa kwa shangwe kubwa na Watanzania. Ni wazi kuwa mkakati huo ulifanikiwa kuongeza idadi ya wanaojua kusoma na kuandika mionganii mwa jamii yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo mafanikio ya sera hiyo hayakuweza kufikia malengo haswa ya sera hiyo ya kuondoa adui ujinga, umaskini na maradhi. Ni ukweli usiopingika kuwa hali ya ujinga, umaskini na maradhi bado ni mbaya sana hadi hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huu ambapo tunajitahidi kutekeleza sera kama hiyo ya elimu kwa wote, ni wajibu wetu kuyatambua, kuyapitia na kuyaolewa yale yote yaliyokosewa hapo mwanzoni. Moja ya sababu kubwa ya matatizo mengi yaliyoyitokeza wakati ule ni kutoshirikiswa walengwa. Mkakati huo kama ilivyo wa sasa, ulitekelezwa kwa muono na fikra za watawala kwa kupitia matakwa ya sera za chama kimoja bila ya kujali umuhimu wa walengwa wa mkakati wenyewe yaani wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokuhusisha kwa karibu walengwa katika kuandaa na kusimamia mkakati huo ndiko kulipelekea matatizo kama vile kukosekana kwa majengo na vifaa vya kutosha nya kufundishia, kutumika kwa walimu waliokosa vigezo rasmi ambao vile hawakutosheleza mahitaji yaliyotokana na idadi kubwa ya wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima ielewewe kuwa sisi hatupingi nia ya Serikali kutekeleza wajibu wake wa kuwapatia elimu Watanzania wote bila ya ubaguzi wa aina yoyote. Ukweli ni kuwa tunawapongeza kwa kuzinduka na kugundua ubaya wa dhambi ya kuwatelekeza baadhi ya Watanzania katika kuwapa haki yao ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo linakuja pale Serikali inapoamua kuparamia mipango mikubwa na nyeti kama hii bila ya kufanya maandalizi ya kutosha na hii inatokana na tabia ya ndugu zetu kupenda kuchukua maamuzi makubwa kwa ajili ya mafanikio ya kisiasa tu hata pale ambapo yanakuwa maamuzi ya kitaalamu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatma ya taaluma ya elimu nchini, suala la walimu wasio andaliwa vizuri kufundisha ni moja ya tatizo lililojitokeza wakati wa utekelezaji wa mkakati wa mwaka 1974. Ni wakati huu ndipo taaluma ya ualimu iligeuzwa kuwa taaluma ya waliokosa nafasi ya kuendelea na elimu ya juu na hivyo kuishushia hadhi kabisa taaluma hiyo. Kana kwamba taaluma hii haina nafasi yake katika dunia ya taluma zilizotukuka. Hali hii ilipelekea kuwa na Watanzania wengi wanaojua kusoma na kuandika, lakini waliokosa upeo wa kutosha wa kielimu unaohitajika kupambana na adui ujinga, maradhi na umaskini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni miaka kadhaa sasa Watanzania wamekuwa wakilalamika kuhusu uwezo finyu wa wasomi wanaotoka katika vyuo vyetu vya elimu ya juu. Ukiiondoa matatizo mengi yanayovikumba vyuo vyetu vya elimu ya juu, lakini ni wazi mzizi wa tatizo hili ni mfumo wa elimu ya msingi ambayo wengi wao ama wamepitia wakati wa mpango wa kwanza wa *UPE* ama walimu wao ni matunda ya mpango huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu ndio watekelezaji wakuu na muhimu katika utoaji wa elimu bora. Kama walimu hawakuandaliwa vizuri kimaisha na mazingira yao ya kazi na mahali wanapoishi, hata kama Serikali itajenga madarasa mazuri na mengi kiasi gani bado elimu itakayotolewa haitakidhi viwango vya kuitwa elimu bora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii sio tu imeshusha kabisa hadhi ya taaluma ya ualimu, lakini pia imesabisha kushuka kwa ubora wa elimu tunayowapa vijana wetu wa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa maendeleo ya elimu ya msingi (*MMEM*) tafiti mbalimbali zilizofanyika kuangalia mwenendo wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (*MMEM*) wa mwaka 2001 zikiwemo zile za Serikali na za mashirika yasiyo ya Kiserikali, zinaonyesha mapungufu mengi katika mpango huo hadi hivi sasa. Kutokana na tafiti zilizofanywa na Chama cha Walimu Tanzania (*CWT*)

na shirika lisilo la Kiserikali la HakiElimu mwaka 2003, unaonyesha kuwa katika mpango mzima wa *MMEM* suala uboreshaji wa mazingira ya walimu halikutiliwa mkazo wa kutosha. Wakati walimu wanaongezewa mzigo mkubwa wa kufundisha wanafunzi waliozidi kiwango cha kawaida, bado hali ya maslahi yao ikiwa mshahara ama posho, ni duni mno. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu kwa Serikali yetu kutumia tafiti hizi kuangalia upya mbinu za utekelezaji wa azma ya kutowa elimu ya bure kwa Watanzania wote, badala ya kuzidharau na kuzidhihaki kama ilivyojitekeza katika suala la HakiElimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya shule zetu vijijini, wakati mpango wa *MMEM* umejitahidi kulivalia njuga suala la ujenzi wa majengo ya madarasa na vyumba vya walimu, bado hali ya shule za vijijini inatia mashaka. Wakati shule za mijini zinaongezewa uwezo wa kimajengo ili kuweza kuhimili mikiki ya kuongezeka ghafla kwa idadi ya wanafunzi, shule za vijijini bado hazijapewa msisitizo unaohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile shule za vijijini zimeendelea kuwa nyuma katika mgawanyo wa idadi ya walimu kulingana na mahitaji ya wanafunzi. Hili linatokana na Serikali kushindwa kuja na mbinu mahsus ya kuboresha mazingira ya kuwavutia walimu kwenda kufundisha vijana wetu huko vijijini. Tatizo la mazingira duni likiwemo lile la ukosefu wa nyumba za kuishi walimu wetu ni moja ya sababu za upungufu huo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha kuwa vijana wa Kitanzania waishio vijijini wanapata haki sawa ya elimu bora na wenzao wa mijini, tunapendekeza Serikali itekeleze mambo yafuatayo:-

- (i) Kufuatilia kwa karibu miradi ya nyumba za walimu vijijini kwa kuzipa kipaumbele katika mgawanyo wa fedha za shughuli hiyo.
- (ii) Kuunda kamisheni maalumu itakayopewa jukumu la kuandaa, kusimamia na kutekeleza mpango wa ujenzi wa nyumba bora za walimu vijijini ili kupunguza mianya ya ubadhirifu na kuongeza ufanisi wa zoezi hilo. (*Makofii*)
- (iii) Kutoa posho maalumu za kuvutia kwa walimu watakaokuwa tayari kwenda kufundisha vijijini kwa muda mrefu ikiwemo hata uwezekano wa mkopo usio na riba wa ujenzi wa nyumba katika maeneo yao wanayotoka. (*Makofii*)
- (iv) Kuondoa baadhi ya kodi katika mishahara ya walimu wa vijijini ili kuwaongeza tija ya utumishi wao kwa Taifa letu. (*Makofii*)

Hata hivyo, wakati tafiti hizo zinaonyesha kuwa utekelezaji wa majengo, 2003, *MMEM* ilikuwa imetumia asilimia 47 ya matumizi yake, wakati nyanja zingine kama mafunzo ilikuwa imetumia 1.8% na wakati kamati za shule zikiwa na 5%. Hii inaonyesha wazi kuwa umuhimu wa kuwaendeleza walimu wetu kitaaluma bado haujatiliwa mkazo

unaotakiwa. Inasikitisha kutamka hapa kwamba idadi kubwa ya walimu wetu wamekuwa hawasaidiwi vya kutosha wakitaka kujiedeleza kitaaluma na wanapotaka kwenda kusoma ili kuongeza elimu huambiwa wajilipie wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya kumjengea mwalimu mazingira bora ya utendaji kazi, madawati na mfumo mzima wa vyoo ni muhimu sana, wakati *MMEM* inaanizishwa mahitaji ya madawati yalikuwa ni 1,897,253 lakini mpaka takwimu hizi zinachapishwa 2004, madawati yaliyokuwepo ni 549,083 na kati ya vyoo 253,617 vilivyohitajika ni vyoo 100,770 tu vilivyo kuwepo wakati huo na hapa yalikuwa ni mafanikio ya miaka mitatu. Hatujui kwa mwaka na nusu mpaka sasa takwimu hizo zimebaki pale pale au zimepungua?

Mheshimiwa Naibu Spika, vitendea kazi katika shule zetu vitabu ni moja ya mahitaji muhimu sana kwa mwalimu na mwanafunzi. Ukosefu wa vitabu katika shule zetu unachangia kwa kiasi kikubwa ukosefu wa utamaduni wa kujisomea mionganoni mwa Watanzania. Ni shule chache sana za msingi na Serikali ambazo zina maktaba rasmi. Dhana ya maktaba imefanywa kuwa ni maalumu kwa elimu ya juu tu. Hili ni kosa kubwa kufanywa na Taifa ambalo tayari limekumbwa na utamaduni wa kutojisomea mionganoni mwa wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa usambazaji wa vitabu na mahitaji mengine kwa njia ya zabuni zinazotolewa na kamati za shule hasa shule za msingi nao vile vile una mapungufu makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kamati nyingi za shule zetu zinakosa ujuzi wa kutosha kutekeleza jukumu hilo na mengineyo ambayo kihistoria hawakuwa nayo. Haya yote yamepelea shule nyingi kupata vitabu vyenye thamani duni, vinavyochakaa haraka na vingine visivyoendana na mahitaji ya mitaala rasmi. Vile vile inasabibisha kuongezeka kwa mazingira ya rushwa na ubadhifuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali kama hiyo, tunaitaka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii ifanye yafuatayo:-

(i) Itoe taarifa rasmi kuhusu hasara iliyotokea hadi sasa kutokana na kubadili mfumo wa ununuzi wa vitabu na mahitaji mengine ya shule za msingi nchini kuanzia mwaka 2001 hadi sasa.

(ii) Itoe taarifa rasmi kuhusu uchunguzi wa rushwa na ubadhifuru katika kamati za shule uliotokana na mtindo wa zabuni za kamati za wazazi. (*Makofi*)

(iii) Serikali ieleze Watanzania ni hatua gani zimechukuliwa hadi hivi sasa kwa wahusika.

(iv) Iwaeleze Watanzania hali halisi ya uboreshaji wa mazingira ya shule zetu zaidi ya idadi ya wanafunzi na madarasa, kwa miaka mitatu iliyopita kulingana na malengo yaliyowekwa mwaka 2001.

(v) Serikali itwae tena jukumu la kusambaza vitabu na vifaa vingine vya kufundishia katika mashule yetu. (*Makofit*)

Mhehimiwa Naibu Spika, uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi, idadi ya wanafunzi ambao kila mwalimu anatakiwa kufundisha imekuwa ikiongezeka kila mwaka tangu kuanzishwa kwa mpango wa *MMEM*. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa zinaonyesha kuwa idadi imekuwa kama ifuatavyo: mwaka 2001 - 1 mwalimu mmoja anafundisha watoto 46, mwalimu mmoja anafundisha watoto 53, mwalimu mmoja anafundisha watoto 53, mwaka 2003 mwalimu mmoja anafundisha watoto 57 na mwaka 2004 mwalimu mmoja anafundisha watoto 59. Baadhi ya Mikoa kama vile Shinyanga, Kigoma, Mwanza, Manyara, Tabora na Kagera zina hali mbaya zaidi zikiwa na uwiano wa mwalimu na wanafunzi ni kuanzia 1:64 mpaka 87 kwa Mkoa wa Shinyanga. Tatizo hili lipo katika shule za Mijini na Vijijini. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya ufuatiliaji ya Taifa ya mwaka 2004 inaonyesha kuwepo na upungufu wa walimu 57,640 wakati uwezo wa vyuo vyetu kwa sasa ni kutoa walimu wahitimu 12,000 kwa mwaka. Hapo bado taarifa hiyo haikuzingatia ukweli juu ya walimu wanaostaafulu, wanaoacha ajira ya Serikali na kujiunga na shule za watu binafsi na wale wanaofariki kutokana na ugonjwa wa *HIV/AIDS* na vifo vya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyuo vya elimu ya ualimu huku tukitambua umuhimu wa kuongeza walimu ili kukidhi mahitaji yanayotakana na mpango wa elimu kwa wote, tunaamini Serikali bado haijaweza kuja na mkakati imara zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzishwa ghafla kwa kile tunachokiita Vyuo Vikuu vya Ualimu, kama hivi karibuni tulivyoshuhudia mfumuko wa kampasi kadhaa za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam si mbinu bora ya kutatua tatizo hili. Chuo Kikuu sio majengo na watu bali ni mfumo uliosheheni vigezo vya kitaaluma ikiwemo wahazili waliokidhi matakwa na sio kama hali tunayoshuhudia hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtindo wa kuibuka tu na kutaka kuonyesha umahiri wa kuwa na idadi kubwa ya wanaoitwa wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu bila hata kukamilisha mahitaji muhimu ni hatari kwa Taifa letu. Hii sio tu inashusha hadhi ya elimu ya juu bali pia inajenga wasomi legelege ambao wanaweza kufanya maamuzi yatakaloliangamiza Taifa letu hapo siku za usoni. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hili tunashauri yafuatayo, kwanza, badala ya kukimbilia kuanzisha vyuo vikuu vingi kwa mara moja, Serikali itilie mkazo zaidi katika kuviwezesha vyuo vilivyopo sasa viwe vile vya umma na binafsi.

Pili, Serikali itilie mkazo wa kusomesha wahazili watarajiwa katika masomo ya shahada za uzamili na za uzamivu kwa kutoa kipaumbele cha juu katika utowaji wa mikopo na *scholarship* maalum.

Tatu, Serikali iboreshe maslahi ya walimu mara moja ili kuvutia vijana wengi zaidi ambao ama wamekimbia katika shule binafsi tu ambazo zina walimu wa kutosha au wamekwenda nje ya nchi kutoa huduma ya elimu.

Nne, Serikali ihakikishe wale wote wanaoajiriwa kwa kazi ya uhazili katika vyuo vyetu wanakidhi mahitaji rasmi ya kitaaluma na kimaadili na kuacha mara moja kufanya zoezi la uajiri kwa mtindo wa zimamoto. (*Makofi*)

Mpango wa elimu kwa wale waliokosa (MEMKWA), mpango huu malengo yake ni mazuri lakini tatizo kubwa ni kama lile lililojitokeza kwa mpango wa elimu ya watu wazima tofauti ikiwa ni kidogo sana. Mpango huo kama ilivyo mipango mingine ya Serikali yetu, haukufanyiwa utafiti wa kutosha na kushirikisha walengwa na washikadau wengine. Pamoja na mapungufu mingine, tatizo la ajira ya walimu wanaofundisha katika mpango huu kutoeleweka inaathiri utekelezaji mzima wa mpango huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili Serikali inapaswa kufanya mambo yafuatayo, kwanza, Serikali inapaswa kueleza Watanzania ambao wameonyesha kuvutiwa sana na mpango huo, nini hatma ya ujira wa walimu wanaojihusisha na mpango huo?

Pili, Serikali ianzishe mfuko maalum wa kuwawezesha Watanzania wanaojiendeleza kielimu kuitia mpango huo lakini wanaishi katika mazingira magumu kutokana na kukosa ajira ya uhakika wanapatiwa msaada ama mkopo wa fedha za kujikimu.

Tatu, Serikali itumie zile shilingi milioni mia tano za kwenda katika kila Mkoa kuwakopesha vijana wanaojiendeleza katika mpango huo ikiwa kama sehemu ya ujasiriamali wa kujikomboa katika lindi la adui ujinga na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la matabaka katika mfumo wetu wa elimu, wakati Mwalimu Julius Nyerere anajitahidi kujenga Utanzania tunaojivunia nao hivi sasa, suala la matabaka katika elimu lilikuwa adui mkubwa aliyeogopwa na kila mtu. Vijana wetu wote walitakiwa kujiona wamoja na sawa wawapo shulenii. Tofauti za kimazingira kati ya shule moja na nyingine ilikuwa ni mwiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kuona Serikali yetu kwa makusudi mazima inaacha mfumo wa elimu yetu unatumika kujenga dhana ya matabaka kati ya watoto wetu ingawa Katiba ya nchi yetu na hata ile ya chama tawala inatambua kuwa Tanzania bado ni nchi ya ujamaa. Kushamiri kwa kile kinachoitwa shule za kimataifa na *Academy Schools*, kumeathiri kabisa dhana ya usawa ambayo ndio msingi wa Utanzania wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wetu wanajengewa mazingira ya kujiona bora zaidi ya wengine kutokana na uwezo wa kipato wa wazazi wao wanaoshindana kuonyesha mafanikio yao kiuchumi. Hili sio tu linajenga hisia za matabaka mionganii

mwa vijana wetu lakini pia limegeuka kuwa kishawishi kwa wazazi wengi kutokuwa waaminifu katika shughuli na majukumu yao, iwe Serikalini ama katika sekta binafsi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, shule hizi ambazo zimegeuka kuneemeka kutokana na mfumo unaoruhusu wao kujipangia ada na gharama zingine kubwa bila ya kujali hali ya kweli ya Watanzania walio wengi, ndizo zimekuwa kimbilio la vijana wengi wenye vipaji vikubwa vya kufundisha mara tu wamalizapo masomo ya elimu ya ualimu. Ni shule hizi ambazo zimegeuka kuwa kimbilio la walimu wazofu kutoka shule za serikali ambapo wanaona kuwa taaluma yao haithaminiwi. Ni shule hizi ambazo kuwepo kwa mazingira mazuri ya kielimu, ndizo hivi sasa zimegeuka kuwa chimbuko la vijana wengi wanaofaulu vizuri na kupata viwango vinavyotakiwa kuingia katika vyuo vyetu vya elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kuwa elimu ya juu ndiyo pekee ambayo hivi sasa inaweza kumwezesha Mtanzania kujikomboa na umaskini yeye binafsi, familia yake na jamii yake. Katika hali kama hii ambayo inapendelea wale tu walionacho kupata mafanikio na kuwaacha wasionacho kuendelea na umaskini unaotokana na ukosefu wa elimu bora, ni wazi tunajenga na kuneemesha mfumo hatari wa kimatabaka katika nchi yetu, huku tukitambua nia njema ya kuwepo kwa shule binafsi, tunaamini kuna ulazima wa Serikali kuwa na uwezo wa kufuutilia na kusimamia ada na gharama zake zingine. Vile vile Serikali ichukue hatua madhubuti na za haraka kurekebisha mapungufu yaliyopo katika shule zetu za Serikali. Ni wazi Serikali ikiamua, sifa iliyokuwepo hapo zamani kwa shule za Serikali itarudishwa na Watanzania wasionacho watapata haki sawa ya elimu bora na wenzao walio nacho, ili wao na familia zao kujikwamua kimaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi kilichopita Serikali ilitangaza kuanza tena kutoa ruzuku kwa shule za binafsi. Kutokana na kumbukumbu ni kuwa suala la Serikali kutoa ruzuku sio jipya kwani mwaka 1927 Gavana wa pili wa Tanganyika Sir Donald Cameron, Serikali yake ilitoa ruzuku kwa shule binafsi na shule za misheni. Mpango wa ruzuku hizo umesaidia sana kuboresha mazingira ya elimu katika shule nyingi za binafsi na sasa wamiliki wengi wa shule za binafsi ni watu wenye uwezo mkubwa kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inadhani kama fedha hizo za ruzuku zipo basi zinaweza kusaidia kwa kuwalipia wanafunzi wale ambao wanakosa ada katika shule za Serikali kama liliyvo fungu la kusaidia wanafunzi walio katika mazingira magumu. Kwa njia hii hata wale watoto wa wazazi wasio na uwezo wataweza kupatiwa elimu bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo tunadhani Watanzania wanapaswa kujua mambo kadhaa kama ifuatavyo:-

- (i) Ni jinsi gani mpango huu unaathiri uwezo wa Serikali katika juhudu zake za kuboresha mazingira ya shule za Serikali?

(ii) Wananchi wanapaswa kujua ni kivipi mpango huu hautumiki vibaya kuziwezesha shule binafsi zenyenye kumilikiwa na wakubwa fulani katika serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaipongeza Wizara kwa kutambua matatizo ya baadhi ya familia ambazo zinaishi katika mazingira magumu kutokana na sababu mbalimbali. Tatizo la watoto kupoteza wazazi kutokana na maafa mbalimbali mfano janga la ugonjwa wa *HIV/AIDS* ni moja ya sababu ambazo zinafanya Serikali yetu isikwepe jukumu la kuwawezesha wahusika kupata elimu bora kama wenzao wengine. Mwaka jana Wizara ilitenga fungu kwa ajili ya kusaidia wanafunzi wanaoishi katika mazingira hayo na usimamizi wake kukabidhiwa Halmashauri za Wilaya husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuweza kuboresha utekelezaji wa mpango huu, Serikali inapaswa kuwaeleza wananchi masuala yafuatayo:-

(i) Wizara humpatia kila mwanafunzi kiasi gani na kwa mahitaji yapi?

(ii) Wanafunzi wangapi ambao hadi sasa wamefaidika na mpango huo?

(iii) Wizara inahakikishaje kuwa wote wanaopata fedha hizo ni walengwa hasa?

(iv) Wizara ina maoni gani kuhusu malalamiko kuwa misaada hiyo hutolewa kwa upendeleo na mara nyingi hucheleva kuwafikia walengwa?

(v) Wizara inahakikishaje kuwa tatizo la upendeleo unaotokana na masuala kama ya rushwa, ukabila na tofauti za kisiasa hayaathiri mpango huu ili Watanzania wote wenye kuhitaji msaada huo kufaidika nao?

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaonyesha kuwa tangu mwaka wa fedha 2001/2002 mpaka mwaka 2003/2004, kumekuwepo na ongezeko kubwa la fungu la fedha zinazotengwa kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara hii wakiwemo walimu. Lakini taarifa hizo hizo zinaonyesha kuwa kiasi cha shilingi 1,155,983,749/= zimekuwa hazichukuliwi na wale wanaodhaniwa kuwa ni watumishi wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii inaonyesha wazi kuwa tatizo la kutambua watumishi halali katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundji na hivyo kutenga fedha ambazo hazipaswi kutengwa. Hili linatokea wakati ambapo walimu halali wanaendelea kuteseka kwa kukosa mishahara yao wakati unaopaswa, kunyimwa malimbikizo yao ya posho mbalimbali na hata kunyimwa au kucheleweshewa pensheni zao kwa wale waliostaafu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilieleze rasmi Bunge lako yafuatayo:-

(i) Ni watumishi wangapi hewa waligundulika katika Wizara hii kwa miaka mitatu iliyopita na walimu hewa walikuwa wangapi?

(ii) Nini sababu za kutokea upungufu huo na ni juhudini gani ambazo zimefanyika hadi hivi sasa kulishughulikia suala hilo?

(iii) Wahusika wakuu wa tatizo hilo ni kina nani na wamechukuliwa hatua gani hadi hivi sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hiyo hiyo ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali inaonyesha kuwa kulikuwa na upotevu wa fedha taslimu shilingi 131,133,044.75 na upotevu wa vifaa vya stoo vyenye thamani ya shilingi 85,408,137.65. Fedha hizi ni nyingi kiasi ambacho kingeweza kumaliza baadhi ya matatizo yanayowasibu walimu wetu. Serikali ilieleze Bunge lako nini hatma ya upotevu huo, ni kina nani wanahuksika na upotevu huo, hatua gani zimechukuliwa dhidi yao na ni juhudhi gani zimechukuliwa kuzuia upotevu wa aina hiyo usiendelee kutokea?

Serikali ni lazima iwaajiri walimu ambao tayari wameshapata mafunzo ya nadharia na vitendo na wenye uwezo uliothibitika kuwakabidhi jukumu la kuwajenga vijana wetu kieleimu na kimaadili.

(i) Serikali iache mara moja mpango wake wa kuajiri vijana waliomaliza elimu ya sekondari ya juu tu bila ya kuwapa elimu ya ualimu kwa muda unaofaa wao kuwa walimu bora.

(ii) Serikali iache kuharibu mfumo wa elimu ya ualimu kwa kupunguza muda wa mafunzo wenye kuhitajika kuboresha taaluma hiyo.

(iii) Wizara husika iwe na utaratibu wa kufanya maandalizi ya kutosha kabla ya kuanzisha shule mpya ama kuongeza madarasa kwa kuwa na mpango mrefu wa kuboresha mazingira na mahitaji ya shule hizo ili tuweze kuwa na vijana walio na elimu bora na sio bora elimu.

(iv) Tabia ya Serikali kubadili matumizi ya shule mbalimbali ili kuwa vyuo vya elimu ya juu kama ilivyotokea katika shule za Mkwawa na Mazengo, ni lazima ya watafutiwe suluhu la kudumu bila ya kuathiri juhudhi zao za kielimu.

(v) Mfumo wa utungaji wa mitihani ya Taifa ni lazima upitiwe upya ili uendane na mabadiliko yanayotokea hivi sasa kama vile mpango wa MEMKWA, Elimu ya Ufundji na mipango mingineyo inayochipuka kila siku.

(vi) Suala la kubadilisha mitaala ya elimu ni lazima liwahusishe Watanzania wote ili waweze kuwakilisha maoni yao kwa ukamilifu na waweze kuelewa vyema madhumuni ya mabadiliko hayo.

(vii) Mabadiliko ya mitaala ni lazima iangalie maslahi ya Taifa letu kwa upana wake na kutoacha mawazo ya wachache wanaokubali nguvu za mfumo wa kile kinachhoitwa soko huria kuhodhi shughuli hizo.

(viii) Suala la mfumo wa elimu yetu kuendana na lengo la kujenga Utaifa unaopotea kwa kasi miiongoni mwa vijana wetu ni lazima liangaliwe kwa umakini.

(ix) Serikali ilete Bungeni mpango wa kurudisha mfumo wa elimu inayowezesha wanafunzi wa sehemu moja ya nchi kupata elimu katika sehemu nyingine ya nchi kama ilivyokuwa hapo zamani.

(x) Hatua za haraka zichukuliwe kuliangalia suala la matabaka katika mfumo wa elimu yetu na haswa nafasi ya kuijunga na vyuo vya elimu ya juu vya umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii muhimu ya mwanga wa dunia, kwa kuwa mtu wa kwanza leo hapa. (*Makofi*)

Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwake, si Rais tu lakini Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi kilicho na dhamana ya kuiongoza nchi hii kwa miaka mitano ijayo.

Pia nampongeza Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge na kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu. Nawapongeza pia Mawaziri, Naibu Waziri na viongozi wote, niseme kwa ujumla na kuwapongeza wale ambao wamechaguliwa au wameteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikupongeze wewe kwamba tulikuchagua bila kipingwa kuwa Naibu Spika, lakini kwa heshima kubwa ningetangulia sana kumpongeza sana Mheshimiwa Spika, ambaye kwa pamoja mnafanya kazi nzuri ya kutuongoza ndani ya Bunge mkishirikiana na Wenyeviti wenu wawili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nitoe pongezi kwa anayeongoza Wizara hii Mheshimiwa Margaret Sitta, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu na Naibu Mawaziri wake wawili. Kwa kweli wanamsaidia vizuri sana, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila na Mheshimiwa Mwantumu Mahiza, bila kumsahau Katibu Mkuu, watendaji wote, wakuu wa idara na hasa kwa sababu mimi cha kusema leo naona kama nimeishiwa kwa sababu kwa kweli hotuba hii imeandaliwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii ina takwimu zote muhimu. Hotuba hii ina ufanuzi wa sentensi fupi fupi kiasi kwamba hata ambaye alikuwa na matatizo akiamua kuisoma vizuri atajua Serikali imeamua kufanya nini kwa upande wa elimu kwa miaka mitano ijayo. Nitoe pongezi sana hapo kwa sababu amedhamiria kuendeleza maboresho ya elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mawili, matatu ambayo yalikuwa yamezungumzwa na Mheshimiwa Phares Kabuye, ambaye amemaliza tu kabla ya mimi, siyaingilia ndani lakini nimeona kama ni lawama lawama ambazo nadhani hii hotuba hawajaisoma vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kwa kuweza kuwemo humu ndani. Mimi binafsi naishukuru sana UWT chini ya uongozi wa CCM kwa kuniwezesha kuwa Mbunge, kwa kutumia ule utaratibu wa kwamba huwa wanatoa nafasi zao mbili za Viti Maalum katika kupanua demokrasia na kutuingiza wanawake wenye ulemavu. Nashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalolisema hapa naomba kabisa, natoa rai kwamba hata vyama vingine nya siasa viige mfano huu kwa sababu ulemavu hauna itikadi. Tukiwa humu ndani tutazungumzia mambo ya waliotutuma, nje huko ndiyo majukwaani tunaweza tukashindana. Sasa na wenzetu nao waige mfano huu ili waweze kuingia wengi wa aina yetu yaani wenye ulemavu wa aina mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitajikitika katika kitabu hiki kurasa zile zinazozungumzia Kitengo cha Elimu Maalum, ukarasa wa 31 na 32. Kwa ujumla nimefarijika sana kwamba yale ambayo yalikuwa yananitatiza kidogo kimaandishi nimeanza kuyapatia ufumbuzi wake. Nasema kimaandishi, kwa sababu tunachongoja matendo basi, baada ya kuwapatia hizo fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo elimu kama elimu kama wengine walivyozungumza na ilivyo ni kweli kwamba ni ufunguo wa maisha katika dunia. Elimu ni haki ya msingi iliyofafanuliwa hata kwenye Katiba yetu kwamba kila mtu kwa kweli ana haki ya kupata elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na pongezi zote niseme tangu Uhuru mpaka sasa ni kweli kwamba watoto wenye ulemavu wameongezeka. Sijui kwa kuzaliwa au kwa kupata ajali, kwa hiyo, wameongezeka hapo mimi sifahamu. Nadhani tafiti zinapaswa kuchukua mkondo wake. Lakini wameongezeka kabisa kutokana na tafiti ndogo zilizokwisha kufanywa pamoja na pongezi kwamba wameongezeka kuingia madarasani, lakini pamoja na taarifa nzuri hii bado kuna vikwazo nya mazingira ya kusomea na kujifunzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa na mpango wa *MMEM* ambao sasa hivi unaenda kwenye *Phase II* kama taarifa iliviyotueleza hapa. Lakini nasikitika *Phase I* haikuzingatia kabisa majengo yalivyojengwa na kwa miaka ya nyuma nilikuwa naelezwa kwamba kuna ramani zimepelekwa kwenye Halmashauri kusudi majengo yajengwe hivyo, vyoo vijengwe kwa kustahili. Lakini hakuna kilichofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika sana, watoto walemvu wameshindwa kuingia darasani. Watoto wasioona wanajikongoja pamoja na vifimbo fimbo vyao mpaka wanaanguka. Wale wanafunzi wa ulemavu wa akili, kidogo wakati mwingine huwa kunakuwa kama ni kuchanganyikiwa, anaweza akaanguka ovyo ovyo.

Kwa hiyo, kwa awamu ya kwanza ile nakiri kabisa yaani nasema kabisa hakuna kilichofanyika mpaka nikawa na hoja kwamba basi *MMEM* hii ilikuwa ya watu tu wasio walemvu, sisi tulio walemvu *MMEM* hii haikuwa yetu. Kwa hiyo, nafarijika kwa

sababu nimeona hapa kwamba kutakuwa na kuzingatia uboreshaji wa mazingira ya kufundishia. Naomba hizo ramani na Wahandisi wa kwenye Halmashauri zetu ambao hizo shule au hayo majengo yanapojengwa wasiwe mbali wakague, majengo yasiendelezwe mpaka haya ambayo Wizara imeweza kutoa mwongozo nayo yamefanyika. Vinginevyo *MMEM* itaendelea kuwa ni *MMEM* ya wasio na ulemavu tu na kuwaacha watoto wenye ulemavu nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo nijumlishe moja kwa moja na *MMES* ni madarasa mengi tu sasa yameanza kujengwa na wananchi. Sijui kama mwongozo huu nao umeshafika huko, nachelea kwamba hawa watakaojikongoja kutoka shule za msingi watakuta matatizo yale yale kwenye sekondari. Sasa hapo watafika kweli, wenye ulemavu hawatafika Chuo Kikuu hawa? Wenye ulemavu hawatafika popote.

Kwa hiyo, naomba suala la mazingira ya kusomea na kujifunzia yaendelee kuzingatiwa na Wizara pamoja na kwamba nimefarijika kuona kwamba kuna mwanzo mzuri unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefarijika kwamba kutakuwa na nyongeza pia ya walimu. Lakini elimu kwa majengo tu siyo elimu, *in fact* ni wanafunzi na walimu kwa sababu hata nikiwa chini ya mti nikisoma naweza nikaokota kitu, msingi mkubwa ni walimu. Pamekuwa na jitihada ya kuongeza walimu wa elimu maalum, lakini mimi nasema bado hawatoshelezi kwa sababu Chuo ninachokifahamu ni kimoja tu cha Patandi. Tena nadhani sina uhakika kama wanaishia kwenye hata Stashahada wala sielewi. Lakini hawa wachache wanaosomeshwa Patandi, lazima wahudumie Shule za Msingi 40 za viziwi, shule 31 za wasioona, shule 100 na Vitengo vyake 23 za walemavu wa akili, shule nne za walemavu viziwi wasioona na shule tano za walemavu wa viungo. Hapo sijahesabia shule za sekondari ambazo ni 24 nani anasomesha.

Kwa hiyo, bado tuna kazi kubwa ya kuandaa walimu wa kwenda kufundisha na licha ya kuongeza wingi wao ningeshauri, elimu hii maalum ni taaluma kabisa na ni wachache wanaotaka hata kujitolea kwa sababu ni ngumu pia. Lakini ningeshauri katika ngazi zote za kusomea ualimu iwekwe katika mtaala kwamba kila mwalimu anayesomea ualimu apate dozi ya elimu maalum na wale ambao wanataka kwenda *ku-specialize* ndiyo waingie kwa undani wa elimu hii. Vinginevyo idadi yao haitatimia, kwa sababu watu wanafanya kwa kupenda tu. Sasa tukifanya kwa kupenda hawa watoto watasomeshwa na nani? Ndiyo wazo langu hilo na ushauri wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya kuongezeka ningeomba sana wapewe motisha maalum. Mwalimu anayefundisha mtoto mwenye ulemavu wa aina yoyote ile yeye pale pale ni mzazi, yeye pale pale ndiyo *aid* wa kumshika mkono. Wana matatizo magumu, waongezewa kwa kweli au wawekewe posho maalum ya mazingira magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo ningeshauri Wizara, iandae wataalam wa lugha za alama na wale wa *brail* hata kama si mwalimu *as such* lakini *specifically* hawa waweze kuwaidia hawa walimu wasioona kwa mfano. Si rahisi asaidiwe na mwalimu mwenzake kwa sababu mwalimu huyo ana kipindi, basi pawe na wataalam wa kuweza

kusaidia mambo haya na lugha ya alama kwa viziwi. Wanakataa kabisa habari ya kusema wao watumie kusema, wao wanasema lugha yao ni lugha ya alama. Kwa hiyo, hili nalo liwekwe ama kwenye mtaala wa ufundishaji watu wakaweze kujifunza pale ili angalau watoto hawa waweze kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na matatizo ya vifaa tangu mwaka 2005/2006 mpaka sasa 2006/2007 Wizara imesema kwamba itaongeza ununuzi wa vifaa hivi. Mimi napongeza ununuzi wa vifaa hivi. Mimi hapa niseme tu nawapongeza sana na naomba kweli vinunuliwe. Labda ningependa tu kujua kwani mtavitawanya kwenye shule gani ili angalau niweze kuwashauri Wabunge wenzangu huko majimboni wakaangalie ukweli wa maandishi haya kwamba vifaa hivyo vimenunuliwa kwenye shule zao huko na zimefika. Illa naendelea kushauri kwamba hapa fedha ziendelee kutengwa nyangi kwa sababu vifaa vyta watoto wenye ulemavu ni aghali sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna elimu mpya, mfumo mpya huu wa elimu ya mjumuisho. Nashukuru hapa kuna watu watakaofundishwa sawa sawa, lakini nadhani mwanzo wake hakuwa mzuri, haukueleweka wala kwa wadau, wanafunzi wenyewe, wala walimu, kwa mfano hata Katumba II iliyoko Rungwe, Mbeya wako walimu wanafunzi wasioona, viziwi, wameunda shule moja, hebu uangalieni huo mchanganyiko utakuwaje. Walimu wa *ku-handle* hizo *sections* za ulemavu hawapo wa kutosha eti wanasema ndiyo elimu mjumuisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa elimu mjumuisho ni kuwalundika watoto wenye ulemavu pamoja au ni kuwaweka pamoja na wenzao ili waweze kufaidika. Hapa ndipo ambapo inahitajika wataalam kwa sababu hata mtoto kiziwi ukimweka darasani na wengine amba siyo viziwi lazima pawe na mwalimu pale anayemudu kumtafsiria yale yanayosemwa na huyu mwalimu anayefundisha. Tumewaandaa hao au ni mjumuisho wa maneno tu halafu hatuendi mbali?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kama lilikuwa ni tamko tu huko, tusiige haraka mambo kabla ya maandalizi ya kutosha, vinginevyo itakuwa ni kujidanganya kumbe matokeo yake yatakuwa siyo mazuri sana. Kuna tatizo la watoto wanaendelea mpaka sekondari huko kwamba wasioona hawafundishwi hesabu. Sasa hii inaathiri ufaulu wao. Naiomba Wizara hapa sijui ifanye nini kwa sababu wanaishia *division three*, *division four* kwa sababu usipofaulu hesabu kielimu una mushikeri. Sasa hawa hawapati *division nzuri* na hii inaweza kuathiri hata katika kuchaguliwa kwao kwenda *form five* na kuendelea huko. Hivi hili tunalifanyaje kwa watoto wasioona? Naomba msaada hapo liweze kuangaliwa upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wanafunzi ambao wameweza kuhitimu ualimu aidha kwa *ku-specialize* viziwi na mengineyo lakini imekuwa ni tatizo kuajiriwa. Watendaji Wilayani kwetu hii siyo kwamba waende TAMISEMI na Menejimenti lakini Serikali ni moja tunashauriana wapate mahali, hawapati ajira hawa. Kuna Mheshimiwa mmoja juzi ameniambia alimsomesha mtoto kiziwi mpaka amemaliza ualimu kila akija ofisini kwenu anazungushwa, ajira hapati.

Sasa naomba katika mtindo huu ambao tumeanza kwamba walimu wataajiriwa *straight* na Wizara hawa muwape *priority* kwa kweli ya kuajiriwa kwa sababu ni mambo ya kujisukuma mpaka hatua hiyo ina maana wameshafikia mahali pa kuweza kujitegemea na kwa kweli asiwe mzigo kwa ndugu na jamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisisahau naomba niunge mkono hoja kwa sababu nina mengi hapa ya kusema. Nalipongeza Baraza la Mitihani lakini kama ripoti yetu ilivyosema ninaomba sana sana lile jengo limalizwe lile la kusahihishia litasaidia udhibiti wa mitihani na litasaidia walimu wale wasiwe wanazagaa zaga mbali.

Mimi nilikuwa mwalimu, mwalimu mwengine anapokaa huku na mwengine anapokaa huku *paper zikipotea* mseme Baraza wanavujisha mitihani, kumbe mazingira yenye hayawasaki sana kuweza ku-*control* hivi vitu. Pesa itoke na maamuzi muhimu yafanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, Morogoro imekuwa na matatizo kama tulivyosikia hapa kama Wilaya ya Ulanga ambayo mpaka sasa hivi kati ya wale 90 walio-*drop out* mwaka huu wao 45 wame-*drop out* wale watoto. Oh, nashukuru sana na naomba kuunga mkono hoja. (*Makofî*)

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi na mimi nichangie kidogo hoja hii ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu. Kwanza kabisa napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja Naibu Waziri wake wawili na wataalam kwa hotuba nzuri, katika hotuba ambazo ni nzuri hii ni mojawapo ni nzuri kwa kweli. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hotuba ambayo ina maelezo ya wazi, ina takwimu muhimu. Kwa hiyo, nadhani hata maswali ya kuuliza takwimu yatakuwa yamejibowi, nashukuru sana. Hii ndiyo inatakiwa kweli, elimu lazima iongoze hata katika mambo yake. Kwa hiyo, nashukuru sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiunga kabisa hoja hii. Nina machache tu ya kuzungumza. La kwanza kabisa, napenda kumpongeza sana Waziri pamoja na timu yake kwa kufanya kitu ambacho kilitupa wasiwaso wakati kinaletwa mbele yetu hapa kwenye Bunge kwa bahati nzuri mimi nilikuwepo. Wakati mitaala ya zamani inabadilishwa tulikuja tukaelezwa maneno mazuri hapa ya kitaalam tukakubali kwamba ni kweli huo ni mwelekeo mzuri na wakati wa Bajeti tukazungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka kitu nikisema wakati mwingine ukisema kitu mtu anaweza kudhani unakejeli lakini ukikaa vizuri ukakifikiria utakikuta kina mantiki, kwa sababu wako wataalam wa sera ambao wapo pale ambao pengine walikuwepo wakati ule lakini naamini Bwana Mpama yupo nadhani Bwana Mhaiki yupo, watakumbuka nilivyosema hapa, nikasema baadhi yetu tumeshughulika na masuala ya *policy*, sera za jumuiya au *Public Policy Management* tukasema unapotengeneza sera lazima ufikiri mpaka kichwa kiume na unapoibadilisha hali kadhalika ufikiri mpaka kichwa kiume. Nikauliza mlifanya hivyo na nikazungumza kwa kiingereza, *when making public policies one has to think until it hurts and when un making public policies one has to think equally until it hurts*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nilitaka tu kuacha na hiyo *note* kwamba mmerejesha sera hiyo ambayo ilisitishwa? Je, mlifikiri mpaka kichwa kimeuma? Kama bado basi katika *policy* kuna kupitia *policy*, kuiboresha, kuweka sehemu ambazo kidogo zina dosari. Naisema hii kwa sababu haya mambo ya kubadilisha badilisha haya, maana yake hii Wizara ni mambo ya kitaalam, sasa ni vizuri wanaokuwepo pale wakae wasikilize wataalam, wasahau historia, wasahau chanzo cha mambo mengi yaliyopo pale. Kupapatika huku na kuamua hiki hakifai na hiki na ushabiki mwingine ambao hauna msingi utatuletea matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi Waheshimiwa Wabunge, Waziri aliporudisha hii mitaala sisi tulijisikiaje, maana yake tulikuwepo. Tulijisikiaje sisi? Tulijisikia ovyo sana. Lakini nakumbuka kwamba baadhi yetu tuliliza kwamba haya kweli mmekaa mkayafikiria. Lakini mimi nakubaliana sana na naunga mkono kwamba tumerudi kwenye kitu ambacho tangu kama tungeendelea hivi tulivyo tungepata matatizo makubwa. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii, kwa hatua na juhudii na misaada mingi ambayo tumeipata sisi Waheshimiwa Wabunge na Halmashauri zetu katika suala la kusukuma maendeleo ya elimu ya sekondari. Nadhani miaka miwili tu hii ndipo Serikali kwa kweli ilipokuja kutusaidia. Shule zile za sekondari ambazo ni za Serikali, kwa mfano katika Jimbo la Bumbuli wakati linaanzishwa mwaka 1995 mimi nilikuwa Mbunge wa kwanza, ilikuwa hakuna hata shule moja ya sekondari.

Sasa kwa Lushoto ukizungumza hivyo watu wanaweza kushangaa kuna shule pale Mazinde Juu, Kifungulo, Kongei, Soni Seminari, na kadhalika, zile ni shule ambazo zimejengwa na madhehebu na zinachukua wananchi nchi nzima na hazina upendeleo wowote kwamba sasa hapa tutoe upendeleo kwa eneo hili kuanzia mwaka 1995 wananchi wenyewe baada ya kuchagua kwamba maendeleo ya Jimbo la Bumbuli yataletwa na elimu.

Kwa hiyo, wote tuipe elimu kipaumbele. Sasa hivi jimbo lile lina shule za sekondari za kutwa 10 ni *average* ya shule moja kwa kila mwaka. Ikiwa na maana kwamba nafasi ziliongezeka kuanzia sifuri mpaka nafasi 840 kwa sababu kuna shule moja ina mikondo mitatu badala ya miwili. Sasa jimbo la Bumbuli lina Kata 12, Kata 10 zina shule na mwezi Januari Kata mbili zitakamilisha, kwa hiyo, kila Kata itakuwa na shule yake ya Sekondari. (*Makofî*)

Sasa ombi letu sisi ni kwamba kwa kweli kazi ya Wizara ni kutuhakikishia kwamba walimu wanapatikana na walimu ambaa ni bora na vifaa vyta kufundishia. Wananchi wameshaitikia wito na kujisaidia wenyewe halafu na nguvu ya *MMES* nayo imezidi kuwatia hamasa. Kwa hiyo, nadhani kwa ushirikiano huo tutakwenda mbali. Jambo lingine ambalo nataka kuipongeza Wizara kuna kitu ambacho nataka nikizungumzie lakini baada ya kusikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri hasa pale katika eneo la maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maamuzi muhimu lile amuzi D pale na kwamba sasa pole pole madaraka ya kusimamia na kuendesha shule za sekondari yaende kwenye Halmashauri za Wilaya, ni uamuzi mzuri sana, kwa sababu shule zilizo nyingi Wizara kwa kweli itashindwa kuwa kila mahali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Wizara iwe na yale mambo yenye kazi ya kitaalam yale, kwamba isimamie taaluma, iweke *standards*, ifanye ukaguzi na kuhakikisha kwamba hakuna shule ambayo inafanya vinginevyo na kutizama mitaala hiyo, je, inakwenda na wakati na kuiboresha?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni jambo zuri sana na nadhani Mheshimiwa Waziri wewe na Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, mngekaa, tusingojee mpaka mambo yaye kamilifu yaana mkamilishe kila kitu, ni kwamba kuanzia sasa hivi katika Halmashauri yoyote ile kunapoitishwa Baraza la Madiwani, kitu cha kwanza cha kuzungumza ni maendeleo ya shule za sekondari, hiyo ndiyo *agenda* ya kwanza kabisa, waambiwa hivyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi hicho kitu hakifanyiki utaelezwa vitu vingine vidogo vidogo tu hivi ambavyo kwa kweli havina mchango mkubwa katika maendeleo ya wananchi. Kwa hiyo, *priority* kwa kweli ni elimu ya sekondari, elimu ya msingi wameshakubali na tunakwenda vizuri, lakini sekondari mpaka Serikali ilipoleta *MMES* kwa sababu kuna fedha ndipo sasa na wataalam nao wakasema sasa na sisi tushiriki. Lakini siku zilizopita hizo ni kumbembeleza kwamba hawa wamekuwa *ma-cement* hebu tizameni katika mipango yetu ya maendeleo, hakuna mahali kuna akiba ya *cement*.

Mheshimiwa Naibu Spika, akiba ya *cement* sio kupanga *cement* iwepo, hapana, kwa hiyo, haya mageuzi tunayahitaji hayo kwamba elimu ya sekondari kwa maendeleo katika nchi yetu bila hiyo haitawezekana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo moja ambalo nilitaka kulidokeza hapa ni kuhusu hizi bodi za shule, nadhani tungetizama vile viwango vya wajumbe wa bodi, kwa mfano, mimi katika jimbo langu kuna maeneo yangu ukizungumza habari ya kidato cha nne, watu wanakushangaa kidato cha nne maana yake nini? Hao watu wametoka wapi? Maana yake vidatu vya nne ndio tunaviandaa sasa. Sasa ukitaka mtu wa kidato cha nne ndio aingie kwenye bodi, utampata wapi, hayupo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani tungeweka viwango ambavyo vinalingana na mazingira kwamba katika eneo hilo kwa kweli mtu anauelewa mpana, anaushawishi ndio aingie kwenye hiyo bodi, sasa huyu kijana wa kidato cha nne anaushawishi gani pale kijijini, hao wanaotoka sasa hivi, maana yake kuna wengine wametoka sasa na wapo kwa sababu wamesomea kwenye shule za kutwa, kama hakupata nafasi ya kuendelea atakuwepo kijijini, je, huyu ndio aingie katika bodi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani tungekwenda na wakati na tuache, ma-*DC*, Halmashauri, Mabara na Madiwani, tuangalie ni wajumbe gani wa bodi, kuna wazee wengine kule vijijini hawana kidato, lakini akisimama akizungumza kitu ndio kimekwisha hicho kimekwenda. (*Makofii*)

Sasa tusije tukaenda na vidato hivi tukavuruga hoja nzuri sana. Tukirudi nyuma huko wakati chama cha *TANU* kinashinikiza kuanzisha Chuo Kikuu, ile *Faculty of Law* pale Lumumba, wangapi walikuwa na *degree*, lakini waliofikiria ni hao ambao hawana *degree* ndio walifikiria sasa twende hivyo isije ikafika mahali hata wananchi wakashangaa kwamba tumejenga wenyewe shule, lakini inapokuja hasa kuingia kwenye kuangalia maendeleo yake anasema nyie kaeni tunataka wa vidato. *More than 20 now*, tubadilike zile za Serikali sina matatizo, mimi zile ziko nje, lakini hizo wanazojenga wenyewe za kutwa tuangalie ni nani ambaye ataweza kusaidia zaidi katika sehemu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu ameongezewa jukumu moja la mafunzo ya ufunzi, ni jukumu kubwa sana lakini ni jukumu muhimu sana, katika taarifa yake hii hotuba yake ametuonyesha kuna vyuo vya *VETA* kwa Kanda. Sasa mimi napendekeza kwa kweli sasa tusiende kwenye Kanda, tuende kwenye Mikoa, tumalize kila mkoa uwe na chuo cha *VETA*. Halafu twende kwenye Wilaya, vyuo hivi

kwa kweli ni muhimu sana kwa sababu vinasaidia kujenga vijana waweze kujitegemea na vilevile mafunzo haya yasiwe ya kufundisha halafu wakatoka hivi hivi. Kuwe na utaratibu kabisa wa kuwapatia angalau zana za mwanzoni kabisa za kwenda kuanzia maisha, wajajiri wenyewe kuliko saa hivi. *VETA* imefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri mimi nilipokuja kwenye Bunge hapa toka mwaka 1996 nimekaa kwenye hoteli ya *VETA* hapa, miaka 10 nimekaa pale, ndio kuna hoteli pale inaendeshwa vizuri sana na vijana ambao wamefundishwa na chuo pale juu. Lakini vijana wengine pale wanakatishwa tamaa, wasaidie wale vijana, nimekaa pale miaka kumi, kuna vijana pale wanafanya kazi kwa muda wa miaka sita hana ajira, anaambiwa ni kibarua.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuonyesha masikitiko yangu kwa Waziri wa Kazi aliyetangulia, mwaka 2004 wakati wa bajeti ya mwaka 2004/2005 nilisema kwamba yeche ni Waziri wa Kazi, (*labour laws*) vipi *institution* chini yake inakwenda kinyume cha sheria hizo? Vijana wanakaa pale bila ajira kamili, utafokeaje watu wengine kama wewe mwenyewe unasimamia sheria lakini ndani yako wewe kuna wavunjaji sheria?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuzungumza hapa. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyekiyeza kusimama hapa nikiwa mzima na salama kuweza kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kumpongeza Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu, napenda kumpongeza pia Mheshimwia Samuel Sitta, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Spika wetu wa Bunge hili na pia bila kumsahau mama mwenzangu, mama Anne Makinda kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. (*Makofî*)

Pia napenda kumpongeza mama Margaret Sitta, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi na hali kadhalika mama Mwantumu Mahiza kuwa Naibu Waziri wa Elimu. Kwa kweli wanawake wanadhihirisha kuwa wanaweza. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Yuko na Naibu mwengine pale. (*Kicheko*)

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kumpongeza Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Shukrani za pekee napenda nizipeleke pia kwa Chama changu cha Wananchi (*CUF*) kilichoniteua mpaka leo kuweza kusimama hapa kutetea wananchi wa Tanzania wote wa kwa ujumla. (*Makofî*)

Mimi nitaanza kwa kuzungumzia kuhusu madarasa ya awali, kwa kweli napenda kuipongeza Wizara kwa kuanzisha utaratibu mzima wa madarasa ya awali. Kwa sababu nyumba ilio na msingi bora itajengeka ikiwa imara zaidi, kuliko nyumba ambayo itajengwa kiholela. Kwa hiyo, naamini ikiwa madarasa ya awali yataboreshwa katika hali ilio nzuri, basi nina hakika tutapata wanafunzi amba ni bora amba watalijenga Taifa bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo ni kwamba katika madarasa hayo ya awali, tatizo linakuja kuna ukosefu wa vifaa, madarasa mengi ya awali yanaendeshwa yakiwa hayana vifaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, madarasa mengi ya awali hayana walimu walio na taaluma ile ya kufundisha madarasa ya awali. Kwa hiyo, unapomtoa mwalimu kutoka darasani ambaye anataluma ya msingi, ukimpeleka kule anaona kama unakwenda *kumlet down* katika taaluma yake. Kwa hiyo, anajisikia kuwa bila shaka nikifundisha awali naonekana mimi sio mwalimu bora. Kwa hiyo, tunatakiwa tupate walimu amba wamepata taaluma katika ufundishaji wa hayo madarasa ya awali, ikachangia pamoja na vifaa. Wenzetu wa shule za binafsi, madarasa yao ya awali yanakuwa ni mazuri kutokana na kuwa wana vifaa vya kila namna ya kufundishia na mwanafunzi unapomfundisha kwa vitendo anaelewa zaidi, kuliko unapomfundisha kinadhalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye suala la msingi, tunashukuru kwa kuanzishwa kwa *MMEM*, madarasa tumeyaona, yamejengwa na wanafunzi wamo madarasani, lakini bado tatizo linakuja tuna upungufu wa walimu, walimu imekuwa ni tatizo kwa hiyo, tunaiomba Serikali iwe na juhudhi za makusudi kuhakikisha tunaongezewa walimu katika shule zetu za msingi.

Pia katika hizo hizo shule za msingi pia tatizo linakuja kwa sababu vifaa hatuna, hakuna vifaa, walimu wengi sasa hivi wanafundisha kinadharia tu, hawafundishi kwa vitendo, kutokana na ukosefu wa vifaa na walimu si kuwa hawapendi kutafuta vifaa, lakini kutokana na maslahi yao duni yanawafanya kiasi kwamba hawawezi kutumia fedha walizonazo kujinunulia wenyewe vifaa.

Kwa hiyo, tunaiomba Serikali kama walivyotangaza kwamba maslahi ya walimu au mishahara ya walimu imeongezwa, basi iongezwe katika hali ambayo itaridhisha angalau mwalimu naye pia akitoa chake kidogo kusaidia kununua vifaa atakuwa anacho kinachobaki kumsaidia. Walimu hao hao pia wanatokewa na matatizo ya ukosefu wa nyumba za kuishi, bado niko pale pale, naomba Serikali ikishirikiana na Halmashauri zote za Miji ihakikishe kwamba walimu hususan wa mjini, wanatafutiwa viwanja. Wanaweza kujenga, nina hakika walimu wanaweza kujenga. Kwa hiyo, watafutiwe viwanja ambavyo wataweza kujijengea nyumba zao na hata kama mwalimu atahama, tutawahamasisha walimu hao hao wanaohama, akihama, atakayehamia kuja kum-replace yule anaweza akapangishwa kwenye nyumba ya yule mwalimu ambaye amehama pale ili kuipunguzia Serikali tatizo la nyumba kwa ajili ya walimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu spika, tukija kwenye masuala ya *MMES*, kwa kweli Serikali imejitahidi kuhamasisha raia wote pamoja na Wizara kuhamasisha watu wajenge shule

kwa ajili ya wanafunzi waliokosa nafasi ya kuingia sekondari na hilo na limetekelezwa. Lakini ni kwamba Serikali ilifanya makosa, ilijitahidi kujenga shule bila ya kutafuta walimu, ni sawa sawa na kutangaza vita bila ya kuwa na askari wala silaha, kwa hiyo, Wizara ihakikishe kabla haijafikiria kuhazisha shule, ifikirie kufundisha walimu wa kutosha.

Kama alivyosema Mheshimiwa Mkangaa, shule sio lazima iwe na darasa, mwanafunzi anaweza kusoma popote, lakini kikubwa mwalimu awepo. Hata mtoto akitoka nyumbani akienda kusoma chini ya mti, mzazi utakapoulizwa mtoto wako yuko wapi wewe utasema amekwenda shule huwezi kusema kuwa amenda chini ya mti, lakini shule hapo kwa mfano darasa likikutwa linapiga kelele na mwalimu hayupo wakiulizwa mbona mnapiga kelele, wanafunzi watajibu hakuna mwalimu.

Kwa hiyo, nadhani kwanza Serikali ihakikishe inafundisha walimu wa kutosha ndipo hapo iwe inafuutilia uongozaji wa madarasa. Tutakapofanya hivyo tutakuwa tumetafuta viongozi ambao ni viongozi bora, lakini tukiendelea na kufanya kazi ya zimamoto ya kufungua madarasa yasiyokuwa na walimu matokeo yake tutakuwa na bora viongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuzungumzia kuhusu watoto wanaokwenda shulenii, mwanafunzi mwenye njaa hawezu kufundishika na familia zetu nyingi ziko katika hali duni ya kipato, kwa hiyo, tunachoomba sisi ili mwanafunzi aweze kusoma ni lazima ashibe, naiomba Serikali ihakikishe inawapatia angalau mlo mmoja wanafunzi, mlo mmoja uliokamilika na ni mlo ambao utategemea mazingira yaani chakula kikuu kinachotegemea sehemu ile aliyopo mwanafunzi.

Kwa hiyo, mwanafunzi atakapokuwa ameshiba kwa hiyo, ni rahisi mwanafunzi kusikiliza masomo na hali kadhalika pia utoro utakuwa unapungua, sababu watoto wengine wanatoroka kwa sababu tangu asubuhi hajakula chochote na mpaka saa tisa alasiri inabidi abaki shulenii. Kwa hiyo, utoro utapungua na pia matatizo haya ya mimba yanaweza yakapungua kwa sababu watoto wengine wanatoka nyumbani wakiwa hawakula na wakati mwingine wanadanganywa njoo twende ukachukue *chips* na matokeo ya *chips* anarudi nyumbani akiwa ana mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumalizia kwa kusema kuwa Serikali ihakikishe walimu wanapatiwa vifaa na hata hivyo kuna baadhi ya shule ambazo zina wanafunzi ambao ni walemvu, lakini utakuta wanafunzi hao walemvu hawakutengewa sehemu maalum hususan za kujisaidia. Kwa mfano, utakuta mwanafunzi ni mlemavu anahitaji kwenda kujisaidia, inabidi aende kwenye tundu la choo ambalo halitamwezesha yeze kuchuchumaa inabidi ashike uchafu wa wenzie. Kwa hiyo, Serikali iliangalie hilo kujenga sehemu nzuri ambazo zitawasaidia wanafunzi ambao ni walemvu, ili waweze kujisaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna walimu ambao wanafundisha hawa walemvu kwa mfano kuna wanafunzi ambao wanawafundisha wanafunzi wasioona, mfano hai upo, mwalimu anaambiwa akawachukue watoto, ametoka Tanga Mjini, amekwenda Handeni

kuchukua watoto hana usafiri, hana chochote, mwalimu amepanda lori ameenda kuwachukua watoto ambao hawaoni. Anarudi mwalimu huyo huyo anapanda tena lori na wanafunzi ambao hawaoni kwenye lori ambalo limejaa mizigo, ile ni hatari kwa sababu lolote linaweza likatokea, yule mwanafunzi yupo pale haoni chochote, ninachoomba walimu wanaoshughulika na wanafunzi walemavu, watafutiwe vyombo vyaa usafiri vitakavyowawezesha kuwasaidia watoto wao wale kuwarudisha majumbani wakati wanapokwenda na wanaporudi likizo kutoka shuleni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba nisijichanganyie mada, naomba nikae.

**NAIBU SPIKA:** Nilikuwa nasema katika taarifa ya Umoja wa Mataifa wanasema angalau theluthi moja mahali pa maamuzi wawe wanawake. Hapa angalau theluthi moja katika maamuzi yuko mwanaume mmoja, kwa hiyo, wao wamefanya *reverse*, kwa hiyo, tunawapongeza sana na tunampongeza Mheshimiwa Rais. (*Makofi*)

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia machache kuhusu hii Wizara muhimu ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu. Lakini kabla sijachangia naomba niseme maneno machache ya utangulizi.

Kwanza nimpongeze sana Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu kwa hotuba yake nzuri. Kwa kweli hotuba hii ni ya kipekee na mimi nakubaliana naye. Aidha, napenda nimpongeze sana Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kuifanya ya kuimarisha elimu katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa pongezi hizo, naomba nichangie maeneo machache. Nianze na suala la walimu. Waheshimiwa Wabunge waliotangulia wamesema vizuri sana lakini na mimi nataka nisisitize tu. Juhudi kubwa zimefanyika, labda niseme tu kwamba mimi nachangia zaidi kwenye elimu ya sekondari. Juhudi kubwa sana zimefanyika katika kupanua elimu ya sekondari katika nchi yetu.

Mimi naweza kusema Watanzania wote wametoa nguvu kubwa na rasilimali nyingi kuweza kujenga majengo ya shule za sekondari na kutokana na juhudu hizi, Wizara yetu imekubali kutoa vibali vyaa kufungua shule za sekondari na watoto wetu wakachaguliwa kuijunga shule za sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na takwimu ambazo Waziri amezionyesha katika hotuba yake, katika kipindi cha mwaka 2005/2006 tumefungua shule za sekondari 448. Ni idadi kubwa ya shule kwa kipindi kifupi cha mwaka mmoja, napenda nimpongeze sana Waziri na zaidi zaidi nimpongeze Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa, ambaye ametoa msukumo wa kipekee katika suala hili. Pamoja na jitihada hizi hivi sasa tumezaa tatizo lingine, nalo ni upungufu wa walimu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Margreth Mkanga na Mheshimiwa Mbunge aliyekaa sasa hivi wamelisemea vizuri sana tatizo hili. Lakini na mimi nasema nisisitize kwamba elimu haiwezi kupatikana kwa kukusanya katika majengo ya shule yaliyopo, elimu itapatikana baada ya watoto hawa ama wanafunzi kukutana na walimu, walimu ndiyo wenye elimu, kwa hiyo hatuna sababu ama ni bure kuwaweka wanafunzi shulenii wakati hatuna walimu.

Mimi napenda nichukue mfano wa Wilaya ya Kondo, tumefungua shule za kumi mwaka huu lakini hatujapata walimu mpaka sasa. Sina hakika walimu wangapi sasa hivi wamepangwa lakini tulichofanya ni kuchukua walimu wa shule za msingi kwenda kushikilia shule hizo mpaka hapo tutakapopata walimu kutoka Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba ili hawa watoto wetu wasipoteze muda wao hapa shulenii tunaomba Wizara hii iweke mikakati ya dhati kabisa ya kupeleka walimu haraka iwezekanavyo katika shule zetu zote nchini ili waweze kutoa elimu ambayo imekusidiwa. Kwa baadaye basi ningeshauri tu kwamba pamoja na upanuzi wa elimu ya sekondari kwa maana ya kujenga majengo na kufungua sekondari nyingi katika nchi yetu, mimi nafikiri hatuna budi kufanya maandalizi mapema ya walimu. Kwa hiyo, nashauri kwamba walimu waandalisiwe mapema ili waweze kupangwa katika shule mpya zitakazofunguliwa na aweze kuandaa mazingira mazuri ya kupokea wanafunzi katika shule mpya. Hivi sasa hilo halifanyiki matokeo yake ni kwamba wanafunzi wanatangulia shulenii wanawasubiri walimu. Sasa kwa utaratibu ambao ninaufahamu mimi huo si utaratibu unaofaa. Kwa hiyo, naomba utaratibu ubadilishwe ili walimu watangulie kabla ya wanafunzi shulenii.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nataka kuchangia ni suala la maabara. Hivi sasa katika karne hii ya sayansi na teknolojia masomo ya sayansi lazima yafundishwe kikamilifu na yanaweza kufundishwa kikamilifu na kwa vitendo tu na vitendo vinaweza kufanyakia pale panapokuwa na maabara, kama hakuna maabara elimu ama masomo ya sayansi hayataweza kufundishwa katika shule zetu. (*Makofî*)

Nimejaribu kusoma hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kuhusu ujenzi wa maabara katika shule zetu ama katika nchi yetu, yeye amebaini kwamba kwa kipindi hiki cha mwaka 2006/2007 atajenga maabara 40 tu, hiyo imeandikwa ukurasa wa kumi na tisa. Sasa kwa idadi ya sekondari ambazo zipo 488, zilizojengwa na kufunguliwa mwaka jana, hivi tutachukua muda gani kukamilisha maabara katika shule zetu zote hizi na hizi shule si kwamba zinabaki hizo hizo zinaongezeka mwaka huu katika mwaka 2006/2007 tutaongeza shule za sekondari.

Sasa juhudii za kujenga maabara katika shule zetu za sekondari kwa kweli iwekwe ama iongezwe. Huko nyuma Serikali iliwahi kuahidi kwamba katika shule ya sekondari ambayo itajengwa na kufunguliwa kwa nguvu za wananchi Serikali kuitia Wizara hii ingechangia kujenga maabara kwa kila sekondari ambayo itajengwa na nguvu za wananchi. Lakini hilo halifanyiki sasa, kwa kweli naomba wananchi wanajitahidi kujenga vyumba vyaya madarasa, wanajitahidi kujenga majengo ya utawala, wanajitahidi kujenga nyumba za walimu, lakini suala la maabara tusaidieni, naomba sana hilo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika sambamba na hilo maabara bila umeme nafikiri kuna baadhi ya masomo hayatafundishwa, kwa hiyo, naomba suala la umeme nalo lizingatiwe katika shule zetu za sekondari. Sekondari ambazo zinafunguliwa huko vijijini itakuwa ni vigumu sana kufundisha baadhi ya masomo kwa sababu hakuna umeme, tunaomba basi wakati Wizara itakaposaidia kujenga maabara katika shule zetu za sekondari, basi suala la umeme nalo lipewe kipauumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2004/2005 Wizara ya Elimu ilianzisha mpango ama Mradi wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari, kwa maneno mengine MMES katika mwaka huo Wizara iliweka utaratibu mzuri wa kugawa fedha kwa kila Wilaya ili kusaidia nguvu za wananchi katika ujenzi wa baadhi ya majengo. Napenda nimkumbushe Waziri kwamba Wilaya ya Kondoa mwaka huo iligawiwa, majengo ama fedha kwa ajili ya majengo yafuatayo:-

- (i) Nyumba za walimu tisa ambao tuliahidiwa kupewa shilingi milioni 81.
- (ii) Vyumba vya madarasa 54 na tuliahidiwa kupewa shilingi milioni 378, jumla tuliahidiwa kupewa shilingi milioni 459.

Napenda kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Kondoa nishukuru sana Serikali kwamba kwa upande wa ahadi ya nyumba Serikali imetekeleza ahadi yake ya kutoa shilingi milioni 81 na hizo nyumba zimekwisha kamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda niishukuru Serikali pia ilitoa shilingi milioni 182 kwa ajili ya vyumba vya madarasa 26, nayo yamekwishajengwa na yamekamilika. Ninachotaka kukumbusha ni kwamba katika ahadi ya vyumba 54 bado kuna ahadi ya vyumba 28 bado Wizara hajatekeleza. Naomba basi nimeona katika bajeti ya mwaka huu kuna madarasa zaidi ya 1000 ama kuna fedha ambazo zimetengwa ya madarasa zaidi ya 1,000, naomba basi Waziri atufikirie kutupa fedha mapema iwezekanavyo ya vyumba 28 ili tuweze kukamilisha maboma ambayo tumekwisha yajenga na tunasubiri msaada wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho ambalo ningependa nichangie ni kuhusu ugumu wa mazingira ya maeneo fulani fulani katika nchi yetu. Labda nianze kwa kusema kwamba Serikali ilikuwa imefanya utaratibu mzuri sana wa kuangalia mazingira mbalimbali katika nchi yetu na kujaribu kusaidia pale ambapo kuna ugumu wa aina fulani na hapa napenda nimkumbushe Waziri kwamba katika maeneo yale ya ufugaji ama Serikali iliamua kuwasaidia kwa kuwajengea shule za mabweni, ama shule zenye mabweni, kuanzia elimu ya msingi, sekondari na kuendelea. Lakini pia kuna maeneo mengine pia yana matatizo yanayofanana na maeneo yale ya ufugaji ambayo yanapatikana katika mikoa ya Manyara, na Arusha.

Mimi katika jimbo langu nina tatizo kubwa moja, ni kwamba vijiji ambavyo viko katika jimbo langu viko mbalimbali sana, takribani kilometra 20 mpaka 30 kutoka kijiji cha kwanza na kingine. Tumejitahidi kujenga, sekondari katika kata hizo, lakini wanafunzi wanashindwa kuhudhuria, tatizo ni umbali.

Kwa hiyo, naomba nitoe ombi rasmi hapa kwamba tusaidiwe na sisi kama walivyosaidiwa wafugaji, ama jamii ya ufugaji na mimi naahidi kwamba sisi, kwa maana ya mimi na wapigakura wangu, tutajenga mabweni katika shule hizo, naomba mtusaidie gharama ya chakula katika shule hizo, naomba sana, bila ya hivyo mtatuacha nyuma sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuchangia hayo machache naomba nikushukuru tena kwa kunipa nafasi hii na namwombea kila la kheri Waziri na ninatamka kwamba ninaunga mkono hotuba hii. (*Makofi*)

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi ya awali kabisa kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, nakupongeza wewe binafsi kwa jinsi ambayo umeimudu nafasi yako. Kwa kweli umetudhihirishia kwamba akina mama tunaweza. Baada ya pongezi hizo, niwapongeze pia Mheshimiwa Waziri na sio mwengine, dada yangu Mheshimiwa Magreth Sitta, Manaibu Waziri wote wawili kwa jinsi ambavyo wameimudu Wizara hii. Ni kweli Mheshimiwa Rais amepatia kwa sababu ameteua Waziri na Manaibu wake ambao wametokana na Walimu. Waziri alikuwa Kiongozi Mkuu katika Chama cha Walimu ambacho kinashughulikia masuala ya Walimu. Hivyo Walimu wana imani kabisa sasa Wizara ya Elimu imepata mwenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake kwa jinsi wanavyojitahidi kuisimamia Wizara hii kwa kufanya ziara mbalimbali, kufuatilia kero na kuona jinsi taaluma inavyotolewa huko Mikoani. Mungu awabariki sana. Kazi yao ni nzuri, inahitaji kupongezwa. Siyo hivyo tu, hata maswali hapa Bungeni tunayojibwa na Wizara hii, majibu mazuri sana. Nina imani hata Wabunge wenzangu ni mashahidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, sasa nianze kutoa mawazo yangu katika Wizara hii. Mawazo haya siyo mengi ni kwa sababu Bajeti ni nzuri sana na inatia moyo. Lakini naomba wakati Waziri anafanya majumuisho, maombi yangu yapewe majibu kwa sababu ni maombi ya Walimu, wengine wako hapa wanasubiri, wanasikiliza.

La kwanza, napenda nizungumzie kuhusu chombo cha Walimu ambacho sasa hivi kinajulikana kwa jina la Idara ya Huduma kwa Walimu. Chombo hiki kimekuwa na majina mengi sana. Tulikotoka kiliitwa *UTS*. Tukahama hapo, kikaitwa *TSC* na sasa hivi kinaitwa *TSD* na kiko chini ya Wizara ya Utumishi. Sasa mbona chombo hiki kinayumba na walengwa wake ni Walimu? Kwa nini chombo hiki kisirudishwe kwenye Wizara husika, Wizara Mama ya Walimu ili Walimu waendelee kunufaika na chombo hiki? Kwa sababu ni chombo ambacho kilikuwa kinashughulikia masuala mengi ya Walimu kama masuala ya taaluma, nidhamu, ajira na madaraja. Sasa Walimu wanaanza kupata hofu kwamba hata maslahi yao yanawenza yakapotea. Hata *scale* za mishahara yao inaweza ikapotea. *Scale* zao walizoea kuitwa *TGTS*.

**NAIBU SPIKA:** Naomba wasaidiwe. Balozi wa Marekani anakaa kwenye *VIPs Lounge*. *I will introduce you after you have sitted in the right place. You have to sit in the right place here.*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina imani dakika zangu utazilinda vizuri tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hakika hata maslahi ya Walimu yanaweza yakayumba. Chombo chao cha mishahara kilikuwa kinaitwa *TGTS* na ninapata na wasiwasi kwamba kinaweza kikaitwa *TGS* kitendo ambacho kinawatia wasiwasi Walimu kwamba mashahara na maslahi yao yanaweza yakayumba. Ninaiomba sana Serikali kwamba chombo hiki kirudishwe kwenye Wizara Mama, yaani Wizara ya Elimu mahali ambapo Walimu wapo ili waweze kuyaona matatizo ya Walimu kwa karibu zaidi. Kuipeleka Wizara ya Utumishi, Ofisi ya Rais, jamani huko ni mbali Walimu hawawezi kufika huko. Mimi mwenyewe Mbunge kufika Ofisi ya Utumishi Ofisi ya Rais, siwezi, itakuwa Walimu! Rudisheni chombo hiki kwenye Wizara yao, Wizara Mama ambayo ni Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maombi hayo ambayo ninafahamu Serikali hii inajali hoja za Wabunge, najua hili litatiliwa maanani kabisa.

Naomba sasa nichangie kuhusu suala la ulipaji mishahara Walimu. Naishukuru sana Serikali, inawajali Walimu na tayari mishahara yao sasa inalipiwa kwenye Benki, yaani *NMB* na Mameneja wa Benki hizi wanajitahidi sana kuwashughulikia Walimu. Lakini Ndugu zangu Walimu wapo wengi. Ukienda mwisho wa mwezi Benki ya *NMB*, hata hapa Dodoma, utashangaa! Walimu siku hiyo hawafundishi kabisa, hata waliopo Mjini, yaani ni siku ambayo wanashinda Benki. Ukienda, utawakuta wanahangaika, wengine wajawazito, wagonjwa , lakini wanahitaji mishahara. Ninaiomba sana Serikali ijaribu kulitazama suala hili la ulipaji wa mishahara kwa kina zaidi. (*Makofii*)

Kwa kuwa Benki inatoa huduma nzuri tu, iwe na *Mobile Bank* iwafuate Walimu walipo, kuwe na Vituo Tarafani ili Walimu wapunguziwe gharama za kufuata mishahara. Jamani Walimu wanahangaika na wanatumia nauli zao, wanatembea kwa miguu, wanapanda balskeli. Mtawashawishi Walimu waanze kuolewa ovyo ovyo kwa ajili ya lifti za balskeli kwa kuhangaikia mishahara. Wahurumieni Walimu muwapelekee huduma mahali walipo. Nina hakika kwa kazi yao nzuri, mkiwatamizia haja zao, mkiwijali, watajituma vizuri sana katika nafasi zao kwani wana nafasi nzito katika kuwaelimisha watoto au vijana wa Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuchangia hilo, naomba sasa niongee kuhusu suala la MMES. Naipongeza Serikali kwa mpango wa MMES, ni mpango ambao umekwenda sambamba na mpango wa MMEM.

Mheshimiwa Naibu Spika, MMEM ilikwenda vizuri sana, lakini MMES mimi naona inasusua, kuna sababu gani? Hata mgao wa pesa toka walipotoa mgao wa kwanza

mpaka sasa hivi hakuna mgao mwingine na yapo majengo ambayo hayajakamilika na juhudzi za wananchi zimetumika. Naomba mpango wa MMES uende sambamba na mpango wa MMEM ulivyokuwa. Ukiangalia majengo ya MMEM ni mazuri ajabu, hayafanani na majengo ya MMES wakati MMES wanasona vijana ambao wameshapevuka kielimu, wakubwa na wanastahili wapate hadhi ya majengo yanayostahili na taaluma wanayoipata.

Vilevile, mpango huu wa MMES ni kweli Walimu hawatoshi, hata wale waliopatikana hawajakwenda hata kuripoti. Kwa mfano, Shule hizi zilizofunguliwa juzi, nina mfano mzuri wa Mkoa wa Singida. Mkoa wa Singida, Walimu waliopangiwa ni 129, walioripoti mpaka sasa hivi ni 30. Niambie utoaji wa taaluma wa sampuli hiyo, tutafika tunakokwenda! Ninaomba sana itazamwe kwa kina, ni sababu gani za msingi zinawafanya Walimu wasiripoti? Kuna sababu gani zinafanya Walimu wakimbie Vituo vyao? Sababu zinazowezekana kutatuliwa, zitatuliwe.

Ninamshukuru Mheshimiwa Waziri, amesema katika Bajeti yake nyumba 1000 zitajengwa, hii ni hatua nzuri sana. Tunachoomba tu ni kwamba kasi iongezeke nyumba hizi zijengwe ili Walimu wetu waweze kupata nyumba za kuishi.

Pamoja na miundombinu mingine, mahali Shule za Sekondari zilipo, basi maji yapelekwe, barabara ziwepo na umeme upatikane ili Walimu waweze kushawishika kuishi kwenye mazingira ya Shule wanazopangiwa. Bila kufanya hivyo, mpango wa Serikali hautazaa matunda kama inavyotegemewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule hizi hata vifaa hazina. Wenzangu walishatangulia kusema, Shule hazina vifaa, wanafunzi wanasona katika mazingira magumu, izingatiwe kwamba Shule zimefunguliwa kwa kuchelewa wakati nyingine zilishaanza. Hebu niambie *syllabus* hiyo wataifikiaje wakati *materials* zenyewe zinatafutwa kwa taabu? Mwalimu mwenyewe vitabu anaazima Shule nyingine. Ninaomba basi, kwa kuwa lengo la Serikali ni zuri, tuhakikishe tunakuwa na maandalizi mazuri na vifaa kwa ajili ya utoaji wa taaluma kwa ajili ya Sekondari ambazo ni azma nzuri kabisa ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huo, naomba niongelee kuhusu suala la madeni. Nashukuru kwamba Mheshimiwa Waziri amesema kwamba kuna madeni ambayo tayari yameshafikiwa na Walimu watalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini yapo madeni ambayo Walimu walioomba wamekataliwa, wamepeleka vivuli vya madai yao kwa sababu ni risiti za mwanzo zilipotea na zilipotelea chini ya mafaili chini ya mwajiri. Kwa nini Mwalimu ahukumiwe au anyimwe haki yake wakati vivuli au risiti zimepotelea kwa Mwajiri? Ninaomba wale Walimu ambao vivuli vyao vimekataliwa, Serikali ikubali kwa sababu Walimu hawana hatia waliwasilisha kwa Waajiri wao na zikapotelewa kwenye mafaili humo Ofisini. Sasa itakuwa hatujawatendea haki kama Walimu hawatapata haki zao. Ninaomba sana hili litiliwe maanani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niongelee juu ya posho za kufundishia. Mimi nitarudia kila mwaka. Kazi ya Mwalimu ni ngumu sana na wanaifanya katika mazingira magumu sana na unawaona wewe mwenyewe jinsi wanavyokataa kwenda kuripoti kwenye maeneo magunu. Sasa kivutio kimojawapo cha kuwashawishi Walimu kwenda kufundisha kwenye mazingira magumu ni kuwarudishia posho ya kufundishia. Posho hii siyo sadaka, ina sababu za msingi kabisa. Mwalimu anafanya mambo mengi sana katika kuandaa mada zake za kufundishia pamoja na zana za kufundishia. (*Makofi*)

Zipo Taasisi nydingine za Serikali, akishafanya kazi Ofisini anaiweka hapo hapo, lakini Mwalimu anahama na kazi zake mpaka nyumbani kwenda kuandaa zana za kufundishia na maandalizi ya kazi hizo ni mpaka anunue vitendea kazi, ananunua kwa mshahara huohuo wa Mwalimu. Ninadhani hata hiyo Tume inayohakikisha mishahara iliyoteuliwa na Rais itakuwa imenisikia, hakikisheni mnawarudishia Walimu posho ya kufundisha. Yaani *Teaching Allowance*, mtakuwa mmewatia moyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie kusema kwamba, hawa Walimu waliopangiwa kazi juzi hapa, wana wasiwasi na malipo yao. Haya malipo yana usumbufu sijui watapata kwa nani? Malipo ya mazingira magumu hawajui hata wanalipwa na nani! Namshukuru Waziri kwamba amesema anapeleka Mratibu kwa kila Wilaya atakayehakiki masuala ya Walimu wa Shule za Sekondari. Ninaomba basi, hawa Waratibu wapelekwe haraka ili waweze kuwasaidia Walimu waliopangiwa kwenda kufundisha, wajue watafika kwa nani na malipo yao yanalipwa kwa stahili gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hilo, sasa nizungumzie juu ya Shule za kutwa. Kweli Shule tumejenga nydingi na lengo letu ni zuri tu kwamba wanafunzi wengi waende Sekondari, lakini wasichana wetu tunawaweka katika mazingira gani? Wasichana hawawezi kumudu kusoma Shule za Kutwa. Shule za Kutwa zina vishawishi vingi kwa wasichana wetu.

Ninaomba sana suala hili lipewe kipaumbele, kujenga hosteli za wasichana baadaye ndipo zifuate hosteli za wavulana kwa sababu wasichana wetu wanaishi katika mazingira ya vishawishi. Anapotoka nyumbani mpaka Shule hujui anapambana na mambo gani njiani. Kuna vivutio vyta kila sampuli!

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hakika tukiwapa kipaumbele wasichana kupata hosteli, tutakuwa tumesaidia wasichana kumudu masomo ya Sekondari na kumaliza masomo yao. Mpaka sasa hivi wasichana wengi hawamalizi masomo yao kwa sababu ya vishawishi vyta barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kuhusu suala la ufanisi wa ufundishaji. Ni kweli Shule zetu kimatokeo zinapishana, Shule nydingine zinafaulisha sana na nydingine hazifaulishi. Tafadhalii fanyeni utaratibu wa kuwakutanisha hawa Wakuu wa Shule ili waweze kubadilisha usoefu, wapeane mbinu mbalimbali wanazofanya mpaka wakafaulisha vizuri zaidi kuliko wengine. Ninaamini mkifanya hivyo, Walimu watabadilishana usoefu na hata Shule ambazo hazifaulishi zitafaulisha.

Ni matumani yangu kwamba Waheshimiwa Wabunge hapa kila mmoja anapenda Shule za Mkoani kwake zifafulishe. Hakuna Mbunge anayependa Mkoani kwake kuwe na Shule za kusuasua, wanapenda Shule zote zipate elimu yenye kiwango kinacholingana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, niongelee Shule yangu moja ya Mwenge Sekondari. (*Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakusuhukuru sana na ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, napenda nimirambulish mbele yenu Balozi wa Marekani Bwana Michael Liza na Mkurugenzi wa *USAID*, Bibi Pamela White. Ni wageni wa Spika na wa Serikali. (*Makofi*)

Tunaendelea na Mheshimiwa James Musalika.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nafurahi kwamba umenipa nafasi hii niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya hapo, napenda nimpongeze kwa hotuba yake nzuri sana na bila shaka itatoa mwelekeo mpya katika suala zima la elimu.

Vile vile, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuteuliwa kushika nafasi hiyo, nafasi ambayo ni yake kabisa, nadhani Mheshimiwa Rais ameona kwa kazi alizofanya nzuri huko nyuma za Chama cha Walimu Tanzania. Mimi napenda nimpongeze kwa jinsi anavyotenda kazi kwa kipindi hiki kifupi, tumeona na mimi ni shahidi.

Mimi juzi nilikuwa na tatizo la Wapigakura wangu, nikaenda Ofisini kwake, Mheshimiwa Waziri kwa *speed* ambayo sina hakika nitailinganisha vipi na ya Spika, aliweza kutatua tatizo langu haraka sana, akanipa kikombe cha kahawa na kabla sijamaliza kikombe cha kahawa akawa tayari tatizo langu ameshanitatulia na akaniruhusu kuondoka. Mimi napenda nimpongeze sana kwa hayo yote. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ndiyo uzuri wa Mawaziri akina Mama. (*Makofi*)

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia napenda niwapongeze sana Watendaji Wizarani, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii, ni watu waadilifu na wasikivu, wanasikiliza sana matatizo ya Waheshimiwa Wabunge. Sasa hakika hiki kinatokeaje, ningependa hata Wizara nyingine ziige kazi za watendaji wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijielekeze kwenye hoja yenye. Naomba kwa niaba ya Wapigakura wangu kutoka Jimbo la Nyang'wale, niseme masuala mawili tu

katika siku ya leo nayo ni kuhusu Elimu ya Msingi na Elimu ya Sekondari. Kwenye Elimu ya Msingi, nimeombwa niseme yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utakumbuka kwamba tumekuwa na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) na katika mpango huo, wananchi walitakiwa watoe nguvu zao, wajenge madarasa au maboma ya madarasa na maboma ya nyumba za Walimu ili kutatua matatizo hayo na kwamba Mradi wa MMEM ungekamilisha maboma hayo ya madarasa na nyumba za Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya mpango huu, wananchi wa Wilaya ya Geita waliitikia kwa wito mkubwa sana na wakahamasika na wakakubali kufanya hiyo kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwaka 2004 katika Wilaya ya Geita maboma ambayo ni ya madarasa kwa Shule za Msingi yaliyokuwa yamejengwa na wananchi kwa nguvu zao ni maboma 1113, maboma ya nyumba za Walimu yaliyokuwa yamejengwa kufikia hapo ni maboma 450. Kwa hiyo, Serikali kupitia MMEM pamoja na nguvu za Halmashauri kwa upande wa madarasa au maboma ya madarasa maboma yaliyoezekwa ni 228 tu. Kwa hiyo, maboma ambayo bado hajakamilishwa ambayo sasa hivi ni maboma 885 ya madarasa.

Kuhusu maboma ya nyumba za Walimu maboma yaliyokuwa yamejengwa kwa nguvu za mpango wa MMEM pamoja na Halmashauri ni maboma 231. Maboma ambayo bado hayajaezekwa au kukamilishwa ni maboma 219.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mazingira ya ujenzi yalikuwa kama ifuatavyo:-

Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, Waheshimiwa Wabunge na Madiwani waliwahamasisha wananchi kuitia mpango huu wa MMEM kama Serikali ilivyokuwa imeelekeza. Wananchi wakaitikia, lakini pia na sehemu nguvu ya dola ilitumika kuwasukumua wale ambao walikuwa tayari kushirikiana na Serikali.

Nakumbuka katika Kijiji cha Kaluma, kwa mfano yupo rafiki yangu mmoja anaitwa John Kilimi alikuwa Mwenyekiti wa Kitongoji, hakuonyesha ushirikiano na aliwekwa ndani. Lakini kuna Kijiji cha Bululu Kata ya Kakora siku tunafanya Kikao pale, wazee wakaniomba kwamba tunaomba zoezi la ujenzi wa haya maboma usimame, ilikuwa ni mwezi wa kwanza. Kipindi hicho ni cha njaa kwa sababu pesa tuliyonayo tunanunua chakula na vijana wetu, watoto ambao ndio wanakwenda kuhemea mahali kwagine, sasa hivi wamekimbia nyumba zao kwa sababu inabidi wachangie nguvu ya pesa kukamilisha maboma yale. Mimi sikuwa na jibu la kuwaambia, nikawaambia kwamba nimesikia, lakini Serikali iliendelea kuhamasisha, waliyajenga pamoja na kukimbia nyumba zao lakini waliendelea na kujenga. Sasa ndiyo mazingira ambayo maboma hayo yalijengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wa Wilaya ya Geita kwa kipindi kizima cha mwaka 2004/2005 tumekuwa tukiomba Serikali ikamilishe maboma hayo kwa sababu hakuna Kikao ambacho Mbunge angekwenda kufanya Kijijini bila kuulizwa maboma hayo ambayo ni ahadi ya Serikali kwa wananchi. Tulimwona

Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni na wakati ule Mheshimiwa Mungai, aliahidi kwamba atalifikisha kwa Serikali na atalifikisha kwa Rais Mkapa kwa wakati huo na ahadi tuliyopewa baadaye ni kwamba maboma hayo sasa yatakamilishwa na kutokana na mpango wa kuomba pesa Benki ya Dunia kukamilisha maboma hayo. Lakini mpaka tunakwenda kwenye uchaguzi, maboma hayo yalikuwa hayajashughulikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2004 nimewahi kuuliza swalı hapa Bungeni, lilikuwa limeelekezwa kwenye Wizara ya TAMISEMI kwamba: "Kwa kuwa Serikali iliyahamasisha wananchi na kutumia nguvu kujenga maboma na kuahidi kwamba itayakamilisha na kwa kuwa maboma hayajakamilishwa: Je, Serikali sasa iko tayari kutoa maelekezo kwamba wananchi hao sasa wasichangishwe tena, wasijitolee tena na wasijitoe tena?"

Mheshimiwa Naibu Spika, jibu la Serikali lilikuwa kama ifuatavyo:-

Tulipongezwa sana na Wilaya nyingine ziliambiwa ziige mfano kutoka Geita. Jibu la pili, tukaambiwa kwamba siyo vizuri wananchi wahamasike kuliko uwezo wa Serikali. Sasa Serikali gani inafanya hivyo, inakuwa *double standard* inakuwa inatuambia tujenge halafu inasema tumezidi? (*Makofi*)

Sasa, wananchi wa Jimbo langu ukiwaambia wafanye kazi ya kulima, wanalima sana na nyumba wamejenga. Mmeona sasa leo mnawaambia kwamba mlifanya nguvu kuliko uwezo wa Serikali. Lakini bado tukaendelea kupewa matumaini. Juzi Mheshimiwa nadhani Mabina Mbunge wa Geita aliuliza hapa tena jamani, maboma hayo vipi? Yanabomoka na yanaanza kupata ufa, jibu la Serikali safari hii likawa na lenyewe tofauti kabisa! Akajibiwa kwamba, kama yamepasuka hayo maboma inawezekana yamejengwa bila kuzingatia viwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nalinganisha hii sawasawa na hadithi ya baba mmoja ambaye kila mwaka alikuwa na njaa kwenye nyumba yake, lakini alikuwa na shamba kubwa na vijana wapo. Akasema sasa mwaka huu nataka tulime tuondokane na tatizo la njaa. Akawaambia vijana na akawapa na sheria ndogondogo kwamba mlime. Wakaitikia, wakalima shamba lote, ye ye alisema kwamba ataleta mbegu. Walipomaliza kulima wakamwambia baba sasa shamba tayari tumeshalima, tunaomba mbegu tupande. Akasema mbegu ipo kidogo tu robo hekari tu, wakati shamba ni kubwa sana.

Kwa hiyo, akawapa robo hekari wakapanda. Baada ya mwezi mmoja wakamkumbusha kwamba mzee sasa shamba ni vipi? Tunataka tupande mbegu, mvua ndiyo hizi. Akasema, ninyi hamjui kwamba mimi baba yenu, sina uwezo? Mbona mlilima sana! Ndiyo majibu ya Serikali hayo mbona mlilima sana wakati mnajua sina uwezo? Wakaendelea kumkumbusha tena baada ya miezi miwili, ndiyo ya juzi ya Mheshimiwa Mabina kwamba Mzee, lakini shamba sasa linaanza kuota majani, sasa jibu la safari hii ni kwamba inawezekana mlilima vibaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Geita wanataka Serikali iseme hayo maboma iliyowaahidi wananchi wanayakamilisha lini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye majukwaa tulipokuwa tunaomba kura, Madiwani, Waheshimiwa Wabunge, hata Mheshimiwa Rais, alipofika Wilaya ya Geita aliulizwa kuhusu maboma na jibu lake lilikuwa ni kwamba maboma hayo, jibu letu sisi wanasiasa na kwa kuwa swali lipo kwenye Ilani ya Uchaguzi na majibu yetu yalikuwa ni kwamba, maboma hayo tutayakamilisha. Sasa kura tumeshapewa, wananchi wa Jimbo la Nyang'wale, Geita na Busanda wanataka maboma hayo Serikali iyakamilishe kama ilivyokuwa imeahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije sasa kwenye mpango wa MMEM, lakini nimalizie kwa upande wa msingi kwamba, tunaomba sasa Walimu, tupo watu wengi sana 800,000, tuna Shule nyingi na tuna watoto wengi, kwa hiyo, Walimu hawatoshi wa Shule za Msingi, kwa hiyo, tunaomba tupewe kwa makusudi kabisa tuwe tunachukuliwa kama Mkoa kwenye masuala mengine na Shule ni nyingi.

Sasa nije kwenye upande wa MMES na mimi niseme kidogo kwamba mimi naupongeza sana huo mpango na unaendelea, lakini unaonyesha una mapungufu namna ya usimamiaji wa pesa za ujenzi wa yale madarasa pamoja na nyumba za Walimu. Msimamizi, inaonekana yuko Mkoani. Kule Wilayani, Mkurugenzi hana nguvu na hao wanaojenga amba ni Mkuu wa Shule na Kamati yake. Hana nguvu nao, sasa unajikuta kuna maeneo yamejengwa chini ya kiwango au pengine hela zimetolewa lakini hazijatumika. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba utaratibu wa usimamizi wa pesa hizi uangaliwe upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, yafuatayo mengine ni maombi kwamba Shule nyingi hizi za Kata zilizojengwa kwa mpango wa MMES hazina Walimu na Wabunge wengi sana wamekuwa wakienda Wizarani kuomba walimu. Nashukuru Wizara imechukua hatua, juzi ilifanya *interview* kwa vijana wa *Form Six*, wako kwenye kozi ya mwezi mmoja sasa hivi ili wakafundishe hilo. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Shule ambazo ni mpya na maeneo mengine yako nyuma kielimu, naomba sasa katika mgao muwape upendeleo Geita ikiwemo na Shinyanga, mtupatие upendeleo maalum kwa Walimu, wazibe mapengo.

Sisi *Form Four* tumeangalia matokeo, *Division III na Division IV* kwa sababu hakuna Walimu, sasa hebu tupeni upendeleo na sisi tuonekane hatuna tatizo la kuwa na Walimu. Tuliwaambia hatuna umeme, hatuna barabara, hatuna simu, hatuna maji, sasa hata Walimu! Hebu tupeni Walimu basi, angalau mpare aibu kidogo kwa hilo! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimegundua kwamba Shule nyingi hizi wanasoma masomo ya *arts*, ambayo sasa hivi kwa utaratibu na mtazamo wa duni wa sayansi na teknolojia, tunataka sasa masomo ya sayansi, yaani *physics, chemistry*, hesabu na hiyo lugha, sasa wanafunzi wengi wanasoma *arts* Sekondari. Naomba Wizara ifikirie na ibuni utaratibu wa kuhamasisha wanafunzi sasa wapende hesabu, *Chemistry*, yaani masomo ya sayansi, tutajikuta katika Afrika Mashariki sisi wote tunajifunza lugha tu, historia, *The Roman Empire* na kadhalika wakati sayansi hatuna habari. Kwa hiyo, nafikiri tungewapa motisha Walimu wa Sayansi kwa maana ya maslahi na marupurupu, pamoja na hata wanafunzi wanaoonyesha kwamba wanaweza masomo ya sayansi kama hesabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba kwa haraka sana nimalizie kwamba katika mpango wa MMEM naomba tuwe na *component* ya kununua *generators*, zipelekwe Sekondari za Kata ambazo hazina umeme ili wanafunzi nao wajifunze kompyuta. Unaweza kukuta Wilaya nzima hakuna mwanafunzi anayemaliza *Form Four*, Shule hajui, hata kompyuta hajaiona. Sasa tutakuwa hatuna uwiao mzuri kielimu.

Lakini pia ningependa nisema kuwa, katika mpango huu wa MMEM, kulikuwa na *component* ya *hostel*. Hii MMES ni muhimu sana kwamba ni kweli wanafunzi wanapofika *Form II* wanaolewa kwa sababu ya ugumu wa maisha, wanakuwa wanawekwa nyumba ndogo kwa sababu Shule wanazosoma pale Kijijini, usiku wamepanga kwenye nyumba za hawa ndugu zetu wanakijiji na wana matatizo hayo ya kujikimu.

Kwa hiyo, wanajikuta wanaolewa na kuna Shule, sina takwimu hapa. Kuna Shule walianza kama wanafunzi 20 wakafanya mtihani *Form Four* wawili sasa wanapata matatizo hayo. Serikali ione kwamba, Hostel ni muhimu sana ili wanafunzi hao waweze kumaliza Shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwamba, yaangalieni sana maeneo haya ambayo yapo nyuma kwa sababu hata walimu wanaopangwa kwenda kule kufundisha, wanakwenda kuripoti na kurudi Mjini, hawataki kukaa huko. Sasa tunaomba kwamba muwe mnawapa kipaumbele vijana wa maeneo yale ambao kwanza wengine huwa wamejitolea kufundisha Sekondari zile muwape nafasi ya kufanya *interview* na baadaye wafundishe huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofit*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Sasa nina matangazo machache. Kwanza, Wizara ya Elimu na Ufundi, vitabu mlivyotoa havikutosha. Kwa hiyo, kuna wengi waliopenda kusoma hivyo vitabu lakini havijatosha.

Tangazo la pili, Wizara hii imeandaa maonyesho pale yalipokuwepo maonyesho ya jana *TPDC* ambapo kuna maandiko mengi ya kazi ambazo zinafanywa na Wizara hii. Kwa hiyo, mnakaribishwa kwenda kuangalia kwa wakati wenu kama tulivyosema, hii Wizara itakuwa na siku mbili na kutokana na umuhimu wake, tunaamua kuahirisha baada ya kipindi cha asubuhi kesho ili kusudi mchana Waziri ajibu halafu tuendelee na Kamati ya Matumizi.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(*Saa 07.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka  
saa 11.00 jioni*)

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Kama mnavyofahamu, kwa jioni hii tunaweza kuwa na wachangiaji 11. Kwa hiyo, tutaanza na Mheshimiwa Abdul Marombwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Prof. Feethan Banyikwa na Mheshimiwa George Mkuchika na Mheshimiwa Shally Raymond, wajiandae.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kwanza kujadili hoja hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu katika kipindi hiki cha pili kwa siku yetu ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja hii, napenda kuwapongeza hasa Mheshimiwa Waziri na Manaibu Mawaziri wake wawili pamoja na Viongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu, wamefanya kazi kubwa sana ya kuandaa kitabu hiki kwa kuchambua mambo ambayo wanadhani wakiyaingiza katika Bajeti ya Mwaka huu yanaweza yakaendeleza nchi yetu vizuri. (*Makofi*)

Pili, niseme tu kwamba, utekelezaji wa Wizara hii unaonekana kwa sasa hivi ni mzuri, kwa sababu viongozi wake wote hasa Mawaziri wako imara, popote pale linapotokea tatizo, wao wako tayari kwenda kulitatu kwa kutembea katika maeneo mbalimbali, hata yale maeneo ambayo kwa muda mrefu yalikuwa hayajafikiwa na Mawaziri wengine. Lakini Mawaziri wa Awamu hii ya Nne wamejipanga vizuri na wamefika. Hasa, nimpongeze Mheshimiwa Mwantumu Mahiza kwa kuwa ni mwanamke wa pili na wa kwanza alikuwa ni Mheshimiwa Getrude Mongella, ndiyе aliyetembelea wakati ule maeneo yale ye Delta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hakuna Waziri mwingine yejote aliyetembelea maeneo ya Delta tokea Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella mwaka 1986 karibuni miaka 20 baadaye Mheshimiwa Mwantumu Mahiza amekwenda kutembelea kule. Kwa hiyo, mimi nawashukuru sana, kwa kweli wamejipanga vizuri na huo ni mfano mzuri wa utendaji wa kazi. Naamini kabisa kwamba kwa jinsi walivyojipanga malengo hayo yaliyokuwa kwenye kitabu hiki yanaweza yakatekelezeka vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na sehemu ya kwanza ambayo nataka kuchangia, ni kuhusu malengo hasa ya mwaka 2006/2007. Nikianzia na malengo ya Idara ya Sera na Mipango yaliyopo ukurasa 42 ya kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Katika malengo yake, lengo lake la kwanza kabisa ni kufanya utafiti wa maendeleo ya taaluma kwa Shule za Msingi na Shule za Sekondari, lakini lengo kubwa ni kuangalia dondoo tofauti kwa Shule zetu za Msingi na Sekondari kuanzia mwaka 1995 mpaka mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina imani kabisa kwamba kama utafiti utafanywa vizuri, basi matokeo ya utafiti huu yanaweza kuboresha sana Elimu ya Msingi na ya Sekondari katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa napendekeza tu kwamba, miongoni mwa maeneo au Wilaya ambazo ninaomba zifanyiwe utafiti wa *drop out*, basi namwomba sana Mheshimiwa Waziri kwamba, wale watakaofanya utafiti, wajumuushe Wilaya ya Rufiji kwa kuangalia maeneo yale ya Delta yenyeye Shule 17 za Msingi na maeneo mengine ya Wilaya ile. Kwa kupata matokeo hayo, yanaweza yakawa kama ni kigezo au sura nzuri ya kuchambua matatizo ya wananchi waliokuwa Vijijini sana ambao hawa ni *underserved* na wale ambao kwa ujumla wanapata elimu nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri atakapopata watu wake, waende maeneo hayo hasa katika Wilaya yetu ya Rufiji wanaweza wakapata mambo mazuri zaidi ya kuweza kuyaingiza katika utafiti wao huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, katika malengo hayo kwenye ukurasa ule ule ni kukamilisha andiko la pili la Mpango wa MMEM. Katika Mpango huu wa MMEM, katika Awamu ya Kwanza ya MMEM kulikuwa na ujenzi wa madarasa, ujenzi ule gharama zake, darasa moja lilikuwa na thamani ya Shilingi milioni tatu kama na laki moja hivi na nyumba za Walimu ilikuwa ni milioni tatu na laki sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli nilikuwa naomba Wizara ikae katika kuandika huu Mpango wa Pili wa MMEM, waangalie upya bei au gharama za ujenzi wa Shule zetu hizi za Msingi, ujenzi wa Darasa na nyumba za Walimu. Kwa ujumla, gharama sasa hivi zimepanda sana, basi gharama hizo ziendane na huu Mpango wa Pili wa MMEM ambao unatakiwa uandikwe Mwaka huu wa Fedha 2006/2007.

Sambamba na hilo, kuna tofauti kubwa sana ya ujenzi wa madarasa ya Shule za Msingi na yale ya ujenzi wa madarasa ya Shule za Sekondari. Hali kadhalika, ujenzi wa nyumba za Walimu wa Shule za Msingi na ujenzi wa nyumba za Walimu wa Shule za Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia tofauti iliyopo, mimi sijui ni kigezo gani ambacho kinatumika kwa darasa moja la Shule ya Msingi kupewa Sh. 3,100,000/= wakati darasa la Shule ya Sekondari kupewa Sh. 7,000,000/=. Madarasa na kuta ni zile zile, labda kuongezeka vitu vichache mno. Lakini hii tofauti ni kubwa mno na hata kwenye nyumba za walimu. Nyumba moja ya Mwalimu wa Shule ya Msingi ni Sh.3,600,000/= lakini nyumba ya Mwalimu wa shule ya Sekondari ni Sh. 9,000,000/= karibuni mara tatu zaidi ya ile gharama ya nyumba ya Mwalimu wa Shule ya Msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia idadi ya vyumba katika zile nyumba zinalingana na vitu vingi tu vinalingana mle ndani. Sasa mbona hii tofauti ni kubwa mno?! Nilikuwa naomba sana Wizara iangalie hilo, kama ujenzi wa madarasa haya pamoja na nyumba za Walimu, mimi nadhani gharama za ujenzi isiwe na tofauti kubwa sana kati ya Shule za Msingi na zile za Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, katika hili andiko la pili, nizungumzie jambo ambalo napenda tuliiingize katika hilo andiko ni kuhusiana na Ikama ya Walimu. Sasa hivi tuna matatizo makubwa sana ya Walimu. Tuna matatizo makubwa

sana ya Walimu, kwa sababu idadi ya Walimu waliokuwepo ni wachache sana. Lakini Ikama yetu nayo inatupa matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mwalimu. Katika ufundishaji kwenye Kitabu cha Uongozi wa Shule za Msingi cha mwaka 1978, kulikuwa na hati ya Wizara ya Elimu iliwekwa pale inaonyesha wazi kabisa. Shule ambayo ina mkondo mmoja mmoja wanatakiwa wawepo Walimu saba. Kama Shule ina mikondo saba panatakiwa wawepo Walimu nane, Walimu saba wa darasani na Kiongozi wao, Mwalimu Mkuu. Darasa lilitambulika kama likiwa na wanafunzi kuanzia saba, hilo ni darasa limekamilika na lilitakiwa liwe na Mwalimu mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika huu Mpango uliokuja wa MMEM, kwa kiasi kikubwa hiki, Ikama ya Walimu ikaondolewa, ikawekwa kwa kuangalia au kwa kulinganisha idadi ya wanafunzi na idadi ya Walimu. Imewekwa kwamba, katika kila wanafunzi 40, basi Mwalimu mmoja ndiye atakayekuwa anafundisha darasa hilo. Sasa kama Shule ina wanafunzi 80 na ina mikondo saba, basi Walimu wanaotakiwa wawepo pale Shuleni ni kutokana na idadi hiyo ya *ratio* ya Walimu na wanafunzi, wanatakiwa wawepo Walimu wawili tu. Hivi kweli walioandaa Sera hii ni Walimu kweli! Hivi ni Mwalimu gani anayeweza kufundisha Shule ya Msingi yenze madarasa saba, walimu wawili? Watafundisha namna gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hili ni tatizo. Ukienda kuomba Walimu, kwa sababu Shule zimeanzishwa nydingi, zina wanafunzi 80. Shule nydingine zina wanafunzi 100, wanatakiwa wapeleke Walimu wawili na nusu, sijui Mwalimu nusu mwingine atapatikana wapi? Lakini idadi hii ya Walimu wawili kufundisha Shule ya Msingi kuanzia Darasa la Kwanza mpaka la Saba, hicho kitu hakiwezekani! Kama hao wanaoandaa sera hizi wangelikuwa wao kweli tuwapatie madarasa hayo waende wakafundishe hayo madarasa kwa muda wa wiki mbili tu, mimi nina imani kabisa wengine wangeliacha na kazi yenyewe. Huwezi ukafundisha Shule ya Msingi yenze madarasa Saba, Walimu wawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba Wizara sasa iangalie upya uwiano baina ya Walimu na Wanafunzi. Cha msingi ni kuangalia mikondo, kwa sababu unapokuwa Darasa la Kwanza, hata kama lina wanafunzi saba, inabidi uandae *lesson plan*, uwe na *lesson notes*, uandae *Schemes of Work*, vitu vingi vinatakiwa uvifanye hapa na usahihishe madaftari yao. Sasa huyu Mwalimu ukimwekea mzigo huo mkubwa wa kufundisha madarasa hayo eti kwa sababu idadi ya wanafunzi katika Shule hiyo ni wachache, kwa hiyo walimu watabakia Walimu wawili. Kwa kweli ni kuwapatia mzigo usiobebeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu iangalie upya Ikama ya Walimu mashulen i pamoja na shinikizo tunalolipata kutoka kwa wenzetu hao wanaotufadhili fedha hiso. Lakini sisi kama Watanzania, tuliangalie hivyo. Shule za Vijijini hazifaushi wanafunzi. Mimi ninao mfano wa Shule ya Msingi inaitwa Mbawa. Ile Shule wanafunzi wake wapo 60 tu. Lakini katika Shule

ile mpaka sasa hivi hakuna anayefaulu. Walimu wawili watafundisha namna gani? Hilo nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri liangaliwe upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, katika yale yale malengo hasa kwa upande wa Wakala wa Uongozi wa Maendeleo ya Elimu (*ADEM*) ukurasa wa 51, wanazungumzia kwamba kwa mwaka huu watatoa mafunzo kwa Waratibu wa Elimu Kata 2,300 na wametaja Wilaya pale ziko 34. Inawezekana ni matatizo ya kiufundi au ya uchapishaji, Wilaya zile 34 hazina Waratibu Elimu Kata 2,300, haiwezekani Wilaya 34 kuwa na Waratibu Elimu Kata 2,300 na kama kweli hao Waratibu Elimu Kata 2,300 ndiyo wanaotakiwa kupewa mafunzo. Basi nilikuwa naomba kwamba, hiyo itajumuisha karibuni Wilaya nyingi sana za Tanzania na zitakazobakia ni chache sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba kama hili la tatu kwamba, lengo ni kutoa mafunzo kwa Waratibu Elimu Kata 2,300, basi ziongezwe na Wilaya nyingine, zisiishie tu kwenye Wilaya hizo ambazo zimetajwa na hivyo hawafiki hata Waratibu Elimu Kata 1,000, kwa Wilaya hizo 34.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie Idara ya Ukaguzi. Idara ya Ukaguzi ndiyo Idara ambayo inaangalia mwenendo mzima wa Elimu katika Shule zetu. Lakini Idara hii kwa kwa muda mrefu sana imekuwa Idara ambayo imewekwa pembeni. Bajeti yake ni ndogo, wale Wakaguzi, hasa wa Shule za Msingi wanatembea kwa miguu, posho zao hawalipwi, wanafanya kazi kwa mkopo, leo wanakwenda kukagua Shule fedha zao mpaka itakapokuja *OC* baada ya miezi miwili au mitatu ndipo wanapolipwa. Hali hii itaendelea mpaka lini? Kwa nini Idara hii haipewi fedha za kutosha? Kwa sababu wao ndiyo wanaangalia elimu katika Shule zetu na ndiyo wanaokagua ubora wa elimu. Kwa nini wasipewe fedha za kutosha kabisa ziwasaidie kufanya Ukaguzi huu mara kwa mara katika Shule zetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri aangalie Kitengo hiki cha Ukaguzi. Mwaka huu nimeona idadi ya fedha zilizowekwa ni Shilingi milioni 200. Nilikuwa naangalia kwenye vifungu vile, sina uhakika kama kuna vifungu vingine. Lakini imewekewa Shilingi milioni 200 kwa Wilaya zote za Tanzania. Kwa kweli sidhani kama inawezekana Wakaguzi wa Shule wakaweza kufanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala dogo tu la posho ya madaraka kwa Walimu Wakuu. Kwa muda mrefu sana Walimu wetu Wakuu wameondolewa posho ya madaraka. Hao Walimu Wakuu miaka ya nyuma walikuwa wanapewa posho zile na walikuwa wanafanya kazi vizuri tu na mpaka sasa wanaendelea kufanya kazi vizuri. Lakini ukiangalia majukumu waliokuwa wamepewa sasa hivi Walimu Wakuu ni makubwa mno. Kama Wizara imeamua kabisa kuwapatia Maafisa Elimu wenye sifa ya kuwa Maafisa Elimu wa Wilaya kiwango kikubwa cha mishahara kwa sababu ni Wakuu wa Idara, kwa nini hao Walimu Wakuu wa Shule ya Msingi wanaofanya kazi kubwa sana ya kuleta maendeleo ya Shule kitaaluma wasipewe fedha za posho za madaraka?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Waziri aliangalie hilo kwamba posho za madaraka hasa kwa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi zirudishwe upya kama zilivyokuwa hapo mwanzoni. (*Makofisi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize tu kwa kusema kuwa, mwenzetu asubuhi alizungumzia suala la Elimu Mjumuisho. Elimu hii imeanzishwa, kuna Wilaya kama nne za *Pilot*. Katika *Exclusive Education*, kwa kweli Wilaya nne za *Pilot*, maendeleo yake bado hayajawa mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kama Serikali kweli ina lengo la kutaka kuboresha *Exclusive Education* ili kuwaweka watu wote wenye ulemavu na wasio na ulemavu katika darasa moja, basi ninaomba yale ambayo yaliwekwa katika mapatano ya mwanzo ili elimu hiyo iweze kutolewa katika zile Wilaya za *Pilot* na wengine tujifunze huko. Basi naomba vifaa hasa vya ufundishaji vipelekwe katika Wilaya zile nne za majaribio na katika zile Shule 16 za majaribio ambazo zinajulikana, Wizara yako Mheshimiwa Waziri inazielewa zile Shule wapewe vifaa ili waweze kufundisha vizuri wale Walimu na pia wapatiwe mafunzo Walimu wahusika. Walimu wengi katika Shule zile hawana sifa za kufundisha *Exclusive Education*, basi na wao wapelekwe wapate mafunzo, siyo kumchukua tu Mwalimu wa Darasani kwenda kufundisha *Exclusive Education*, haiwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, kwa kuwa muda wangu umekwisha, ninaomba kusema kwamba ninaunga mkono hoja hii. Nashukuru. (*Makofisi*)

**MHE. PROF. FEETHAN F. BANYIKWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniruhusu kuzungumza kwenye hoja iliyotolewa na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa niseme kwamba Mheshimiwa Waziri ameitoa kwa ufasaha mkubwa sana. Kwa hiyo, nampa pongezi na kwa sababu ameitoa kwa ufasaha, ni dhahiri kwamba amepata msaada wa Manaibu Mawaziri wawili, Mheshimiwa Mwantumu Mahiza na Mheshimiwa Ludovick Mwananzila. Kwa hiyo, nao wanawapa pongezi kubwa sana kwa kumsaidia Mheshimiwa Waziri. Vilevile, nawapa pongezi Katibu Mkuu, Prof. Hamisi Omar Dihenga na Wakurugenzi wote kwa kumsaidia Waziri kutengeneza *speech* nzuri. (*Makofisi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu kwa kusema kwamba, naunga mkono hoja hii iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri. Naunga mkono hoja hii kwa sababu imeeleza mambo ambayo niliyategemea kuyasikia kutoka kwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundii. Mchango wangu utahusu Wilaya ya Ngara kwa sababu ndiyo nina uzoefu nayo kwa muda wa miezi sita ambayo nimekuwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuchangia kuhusu Elimu ya Awali. Hapa inabidi nimpongeze Mheshimiwa kwa kuona umuhimu wa Elimu ya Awali, yaani *Nursery School*. Ni muhimu vijana kabla hawajaingia katika Shule ya Msingi wapitie kwenye Elimu ya Awali, kwa sababu wale waliopitia Elimu ya Awali wanakuwa na

uzoefu wa kukaa Shulen na wanakuwa wamewazoea wanafunzi wenzao na inawawia rahisi kufuata masomo ya Shule ya Msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye Elimu ya Msingi, yaani MMEM. Kusema kweli natoa pongozi kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii kwa kuanzisha Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi, yaani MMEM. Mpango wenyewe ulikuwa ni mkubwa na kwa sababu nchi yenyewe ni kubwa kuna matatizo mengi ambayo yamejitokeza. Lakini matatizo siyo mwisho wa safari.

Mheshimiwa Spika, tatizo la kwanza ambalo nimeliona katika Wilaya ya Ngara ni kuhusu Walimu. Kusema kweli programu nzima haikuzingatia idadi ya Walimu ili kuhitimisha mpango wenyewe. Walimu ni wachache sana. Mpango wenyewe wananchi waliuitikia, wakajenga Shule na zipo, hasa madarasa. Lakini Walimu, hawatoshi! Karibu kila Shule katika Wilaya ya Ngara ina upungufu wa Walimu wa Shule za Msingi. Kwa hiyo, wananchi wa Ngara wanasema angalau tuongeze *training* ya Walimu ili tuweze kukabiliana na ongezeko la idadi ya wanafunzi. Kwani Walimu waliopo inabidi wapewe *Refresher Course* ili waweze kutoa elimu bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho nimeona katika Wilaya ya Ngara hasa katika Kata za Murusagamba, Kata za Keza, Kata za Muganza ni kwamba madarasa yaliyojengwa kusema kweli hayana ubora. Matatizo yanatokana na kiwango cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya ujenzi wa madarasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nizungumzie labda *implementation problem* ya mpango mzima. Shilingi milioni tatu kujenga darasa Dar es Salaam - Kinondoni ni sawa, lakini Shilingi milioni tatu kujenga darasa Ngara siyo sawa, kwa sababu Dar es Salaam mfuko wa sementi ni Sh.10,000/=, mfuko wa sementi huo huo Ngara ni Sh. 20,000/=. Sasa haiwezekani ukajenga darasa lenye ubora ule ule wa Dar es Salaam na darasa lenye ubora ule ule Ngara, haiwezekani! (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, madarasa mengi yaliyojengwa kusema kweli ubora wake una walakini. Inabidi labda tuyaboreshe na hii inaendana hata na mabati. Bati moja Dar es Salaam ni *cheap*, lakini bat moja Ngara ni ghali sana. Kwa hiyo, vifaa vyote vya ujenzi ni ghali sana. Sasa haiwezekani kujenga darasa kwa milioni tatu na hilo darasa liwe bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, inabidi kwenye MMEM ya awamu ya pili, turekebishe haya mambo angalau pale ambapo gharama za ujenzi ni afadhali kidogo, basi wapewe fedha labda Shilingi milioni tatu na kule kwingine ambako ni mbali zaidi ya *source of production* ya hivyo vifaa vya ujenzi, basi waongezewe fedha ili *ku-compansate* zile gharama za usafirishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho naona hakikuzingatiwa vizuri ni ule mchango wa wananchi. Kwa sababu MMEM inabidi wananchi wajitolee. Sasa katika nchi hii, kuna tofauti kubwa sana ya kipato. Zile Wilaya ambazo kipato chao ni kikubwa, madarasa *invariably* yatakuwa ni bora kwa sababu watachangia. Yale mazingira ambayo kwa kweli wananchi uwezo wao wa kipato ni mdogo, madarasa

yatakuwa hafifu na siyo bora. Sasa tuangalie, kuna mahali pengine siyo kosa lako ila kipato chao ni kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, *next time around* tutakapotengeneza mradi mwininge, tuangalie zile *areas* ambazo uwezo wao wa kipato ni mdogo, basi tuwaongezee fedha kwa sababu hawawezi kuchangia kwenye kujenga madarasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho nimekiona katika mpango huu ni nyumba za Walimu. Kusema kweli katika Shule za Msingi Walimu wana nyumba ambazo sio nzuri. Sasa kama Mwalimu anakaa katika mazingira mabaya, siyo rahisi kufanya kazi vizuri. Kwa hiyo, tuboreshe nyumba za Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho napenda kuzungumzia ni *drop out*. *Drop out* katika Wilaya ya Ngara iko juu mno na nilishazungumza na Mheshimiwa Waziri, nilipokuwa kwenye Kamati na walimtuma mtaalam kwenda kuhakikisha tatizo hili na ripoti imeandikwa. Lakini ninachopenda kusema ni kwamba, tujitahidi kupunguza *drop out*. *Drop out* zikifika asilimia 30, kwa kweli inatisha na ikiwa asilimia 30 na hasa iwe ya wasichana, inatisha zaidi. Wasichana wako *disadvantaged*, sasa kama wana *drop out* mapema ndiyo kabisa hawawezi kupata *advantage* ya kupata masomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho naweza kuzungumzia ni Ukaguzi wa Shule. Hii Idara ya Ukaguzi wa Shule ni hafifu sana. Ni hafifu kwa sababu hawana vitendea kazi, hawana magari na mara nyingi Afisa anakuwa mmoja kwa Wilaya nzima na wakati mwininge anafanya kazi katika Wilaya ya jirani, sasa inakuwa vigumu kwake kusafiri kwenda kukagua hizo Shule. Kwa hiyo, Walimu wanazorota kwa sababu hakuna *supervision*. Naishauri Wizara iongeze idadi ya Wakaguzi wa Shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho nataka kuzungumzia ni masomo ya Hisabati na Kiingereza katika Shule za Msingi. Sayansi haiwezi kwenda mbele kama huna msingi wa hisabati, haiwezekani! Nimeona hii *area* ni hafifu sana kwenye Shule za Msingi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningelipenda kusositiza kwamba Kiingereza vilevile hakitiliwi msisitizo. Lakini kijana anapomaliza Shule ya Msingi kuingia *Form One* katika Shule ya Sekondari ni kazi kubwa kumfundisha. Mimi nimefundisha *Form One*, najua matatizo niliyoyapata, inabidi uzungumze Kiswahili kwanza miezi sita ya mwanzo ndiyo uanze kuingiza Kiingereza. Sasa inamchelewesha mwanafunzi kuelewa. Kwa hiyo, labda tujitahidi kuweka mkazo tangu mwanzo ili Kiingereza kiweze kufundisha katika Shule za Msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES). Tunashukuru kwamba Serikali imeweka Mpango mzuri wa MMES na kusema wamejitalidi madarasa yamejengwa. Lakini sasa tatizo ni lile lile, Walimu hawatoshi. Kwa hiyo, tuweke mkazo ili tuweze kutafuta Walimu wa kutosha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunafundisha sayansi, ni lazima tujenge Maabara, Shule nyingi zilizojengwa kwenye Kata, hazina Maabara, hatuwezi kuboresha Elimu ya Sayansi kama hatuna Maabara. Kwa hiyo, tujitahidi kujenga Maabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mitaala, itakuwa siyo vizuri kuzungumzia Elimu ya Sekondari bila kugusia mitaala. Kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Margaret Sitta kwa kurudisha mitaala ya zamani. Ninalisema hili kwa uchungu. Nilipokuwa kwenye Kamati, kusema kweli nilisema maneno ambayo wengi hawakupenda. Hii ilikuwa ni *sabotage* ya hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi kutegemea kupata *Scientist* baada ya *High School* kama unafundisha *physics with chemistry*, haiwezekani!

Ina maana kwamba, wale wanafunzi wote ambao wamefanya *physics with chemistry* hawawezi kwenda mbele kufanya *physics* Chuo Kikuu na hawawezi kwenda mbele kufanya *Chemistry* Chuo Kikuu. Sasa tulikuwa tunafanya nini? Vilevile kama huwezi kufundisha *Chemistry* na *Physics* Chuo Kikuu, huwezi kupata watu wanaokwenda kwenye *medicine*. Sasa sijui ilikuwaje? Inabidi tujiulize kwa makini.

Vilevile, kwenye hili tuwe waangalifu na *consultants*. *Consultants* wengine wa *World Bank* kusema kweli siyo *consultants*. Wapo pale kutafuta fedha. Kwa hiyo, watakuandikia chochote kile *in so far as they make money*. Nadhani ndiyo iliyotokea na watakupambia hiyo ripoti na watatoa Semina wakati tunajua kwamba kilicho huko ndani wala sio *chewable* wala hakina manufaa kwa Taifa.

Kwa hiyo tuwe waangalifu sana na *consultancy* kwa sababu kama mnavyoona kwenye MMES na mitaala, kwa kweli kulikuwa na matatizo ya kubadili mitaala. Namshukuru Waziri ya kwamba amerekebisha mapema bila kupoteza muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nimalizie kwa kuzungumzia namna fedha ya MMES inavyokuwa *administered*. Kuna matatizo makubwa sana ya kupata hizi fedha. Walimu wengi wa Shule za Sekondari ni kama wame-*give up*, hawajui namna ya kuzipata. Vile vile, Mikoa, Wilaya na Kata, sijui wanaunganishwaje katika kupata fedha ya MMES. Tumelizungumzia kwenye Kamati naona hatukupata ufumbuzi. Hili inabidi liangaliwe kwa makini zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naomba Shule za Ngara Mjini, Kabanga Sekondari ipewe Kidato cha Tano na Sita. Wilaya ya Ngara hatuna Shule ya Kidato cha Tano ya Serikali. Ipo moja ya Misheni ambayo ina Kidato cha Tano na Sita. Mimi nadhani tungepata Kidato cha Tano na Sita, katika hizi Shule mbili ya Ngara Mjini na Kabanga Sekondari ingeliinua kiwango cha elimu katika Wilaya ya Ngara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache, naunga mkono hoja.

**MHE. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuzungumza na kuchangia Wizara hii ya Elimu.

Pili, napenda nichukue nafasi hii kuwapongeza Mawaziri wanaoongoza Wizara hii, Mheshimiwa Waziri Sitta na Manaibu wake. Lakini pia nichukue nafasi hii kumshukuru Naibu Waziri, Mheshimiwa Mahiza kwamba baada ya kuteuliwa, hakumaliza miezi miwili alitembelea Mtwara na alitembelea Jimbo langu la Uchaguzi la Newala, nilishindwa kushiriki msafara kwa sababu ndiyo nilikuwa naingia na lori la mizigo kutoka Sumbawanga nilikokuwa nahama. Kwa hiyo, naamini kwamba yale nitakayosema Wizarani, tunaye Balozi mzuri wa kueleza mambo ya Mtwara na Newala Mheshimiwa Mahiza. Lakini kwa jinsi wanavyofanya kazi katika Wizara, naamini haitapita miezi mingi, nitampokea Mheshimiwa Sitta, shemeji yangu, kule Newala kuja kuwatemebelea Walimu na kukagua shughuli zetu za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nataka nichukue nafasi hii kwa kweli kuipongeza Serikali yetu, tukifanyiwa mambo mazuri lazima tuseme, kama vile tunavyosema tunavyofanyiwa mambo ambayo sio mazuri. Sasa mimi leo nataka nianze kwa kupongeza. Kwanza, kuipongeza Serikali yetu kwa mafanikio makubwa ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM). Tumesoma takwimu hapa kiwango cha kufaulu kimepanda, *enrolment rate* imepanda, madarasa mengi yamejengwa, nyumba nyingi za Walimu zimejengwa, kwa hiyo, kuna mafanikio makubwa na mimi nataka niipongeza Serikali kwa hilo.

Pia, katika upande wa MMEM niupongeze Mkoa wangu wa Mtwara kwamba katika Mkoa uliokuwa nambari moja ya utekelezaji wa MMEM ulikuwa ni Mkoa wa Mtwara na ndiyo maana Serikali ikaamua Sherehe za Kitaifa za Uzinduzi wa Madarasa kuzifanyia Mtwara na ndani ya Mtwara zikafanyika katika Jimbo langu la Uchaguzi la Newala, Kijiji cha Mtopwa, Tarafa ya Kitangari na wenyewe waliko wanansikia. Kwa hiyo, nataka niipongeza sana hiyo.

Pia nataka niupongeze Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari. Kule kwetu Mtwara kabla ya huu mpango kuanza tulikuwa na Sekondari 35 tu Mkoa mzima. Baada ya msukumo wa *RC* wetu Mheshimiwa Shirima na naamini huyo aliyejeka naye ataendeleza, tumeongeza Sekondari katika miaka mitatu kutoka 35 mpaka 81.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka pia nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwamba, Mtwara tumejengewa Chuo cha *VETA* kwa fedha zetu wenyewe. Kwa hiyo, tunaipongeza Serikali kwamba Chuo cha *VETA* cha Mtwara nadhani mimi nimetembea Mikoa yote nchi hii, hakuna kama cha Mtwara. Matatizo ya wale wakubwa, kama ulikuwa na mashaka, nikienda Mtwara nitalala wapi, hebu njoo uione *VETA* ya Mtwara, haijapata kutokea. Kwa hiyo, mimi nataka nishukuru kwa hilo pamoja na vifaa ambavyo vimewekwa katika Chuo. Tunafaidika kwa huduma za hoteli za kitalii, pia na huduma za taaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, mimi kama Mwalimu kwa taaluma, naomba nichangie yafuatayo:

Wako wataalamu wawili walio-*define what is education*, mmoja Mfaransa J. S. Farant amesema: “*Education is the process of learning to live as a useful Member of society.*” Kwamba, Elimu ni Mchakato wa kujifunza namna ya kuishi kama mwanachama mwenye faida katika jamii. Jinsi unavyosoma ndivyo unavyokuwa wa faida. Jinsi unavyokuwa mjinga ndivyo unavyokuwa mzigo katika jamii.

Mwingine *All Frair wa Latin America*, anasema: “*Education is for Liberation.*” Kwamba, elimu ni ukombozi. Yule aliyesoma amekomboka na yule mjinga hajakombolewa. Ndiyo maana hata dini zetu zote, Waislamu wanaambiwa watafute elimu mpaka China, Wakristo kitabu cha methali kinasema tafuta elimu mahali popote ukimwona mkamate usimuache.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baba wa Taifa pia mara baada ya kujitawala, alituambia nchi yetu ina maadui makubwa watatu. Nao ni umaskini, ujinga na maradhi. Katika hao watatu mkubwa wao balaa kuliko wote ni ujinga. Ukifuta ujinga una uwezo wa kupambana na umaskini na maradhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nilitaka niseme kwamba hali ya elimu katika Mkoa wa Mtwara, Lindi na vile vile hali ya elimu katika Jimbo langu la Uchaguzi Newala sio nzuri, haiendani na malengo hayo. Tungefanya sensa leo wasiojua kusoma na kuandika wameongezeka, lakini kitu kikubwa zaidi kinachorudisha nyuma jitihada za elimu Mtwara na Newala ni upungufu wa Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni afadhali umsomeshee mtoto chini ya mwembe. Kwa sisi Walimu, darasa ni vitabu, Mwalimu na wanafunzi. Hata akisoma chini ya mwembe, watakenda tu Kidato cha Tano. Lakini ukiwa na madarasa, hata iwe structures za ghorofa, *as long as* hakuna Walimu, tunalangua *education*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baba wa Taifa alituonya kwamba, mkisema huyu Kidato cha Pili aliyehitimu, msilangue elimu, awe ame-*cover syllabus*. Sasa Shule zina upungufu wa Walimu. Tunamshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu ametusaidia sana kuweka msukumo wa ufunguaji wa Shule hizi.

Ma-architecture wanasema, *problem indicates progress*. Sasa *problem* ya Walimu, sisi tunajua *it indicates progress*. Kwa sababu *ikishatatuliwa, that is progress*. Lakini *when? How long?* Juzi Mheshimiwa Waziri Mkuu mimi namshukuru alitualika Wabunge wa Mtwara tumsindikize. Risala ya Mkoa aliyeosomewa juzi, Shule zote zilizofunguliwa hazina Walimu. Wizara ilipeleka Walimu 155 wa Sekondari, walioripoti ni 34 *out of 155*, wengine hawakwenda. Nani aende katika Mkoa ambao wakati wa mvua unalala njiani? *Bus hazipiti!* Ndiyo maana nikasema, katika kutatua haya, *sometimes you have to be revolutionary*, tuchukue hatua za kimapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila ya kuchukua hatua za kimapinduzi katika nchi yetu hii, wale waliosoma wataendelea kusoma sana na wale walioko nyuma watabaki gizani. Mimi natoa ushauri kwa Serikali, Wilayani kwangu tumefungua Shule mwaka huu tano, Chitekete, Mpotola, Michemo, Mikumbi na Mtopwa lakini hazina *Qualified*

*Secondary School Teacher* hata mmoja. Wametafutwa wale Waratibu Elimu Kata ndio wanashikilia. This is July, Kengele mbona inakuja upesi! (Kicheko)

Hii ni Julai, mimi ushauri wangu, Serikali hebu tuambieni, tuorodheshe vijana wa Kidato cha Nne na Sita wanaotoka Mikoa ile muwapeleke Chuoni, wakimaliza wapelekeni, hawawezi kukataa kuja. Cuba, Castro alifunga Shule zote, walikuwa wanapambana na ujinga akafunga Shule zote, wanafunzi wakapelekwa kusomesha watu Vijiini. Cuba was liberated, wote wakawa wanajua kusoma na kuandika. Lazima pale mahali ambapo kuna tatizo, tuchukue hatua ambazo ni *exceptional*. Hawa watoto mwakani wanafanya mtihani wa *National Form Two*, mpaka mwezi wa Julai hawajapa Mwalimu, you expect them watafaulu mtihani wa *National Form Two*, si ndio mwisho wao!

Mimi naiomba Wizara pengine kwa mwakani mtazame. Askari Magereza akienda kozi ya *TPDF*, sijui Uhamiaji halipi karo. Hivyo, kama kweli tuna tatizo la Walimu, kwa nini tusiwapeleke hawa wakalipiwa na Serikali kwenda kusoma? Leo mtoto akitaka kupata Ualimu Daraja la IIIA analipa Shilingi 180,000/=. Tuna shida nao hao, kwa nini tusiwapeleke? Mimi najua Mheshimiwa Waziri hukujiaanda kwa hilo kwa mwaka huu, lakini tazameni mwakani. Is it necessary kwamba lazima anayekwenda kusomea Ualimu alipe hizo, wengine hawana uwezo. Sisi katika Majimbo tunajua. Wengine hawa wanafika Kidato cha Nne kwa sababu Mbunge na Mifuko ya Elimu ya Wilaya imesaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nataka kusemea Walimu wapya. Hakuna watu wanapata taabu katika nchi hii kama Walimu wapya wa Shule za Msingi. Anaajiriwa miezi sita, saba, nane, hajapata mshahara. Why should it happen? Why? Kibali kimetoka Utumishi kwamba Halmashauri iajiri. Halmashauri imeajiri, wamepeleka taarifa, kwa nini huyu akae miezi nane hajapata mshahara? Mimi naomba Utumishi, TAMISEMI, Elimu, Fedha kaeni pamoa mlitazame hili.

Suala la upelekaji wa fedha za MMES, mwenzangu amelisema. Tumepata matatizo sana kusimamia ujenzi wa madarasa haya ya MMES. Mimi nilikuwa Gavana Rukwa. Shule ilikuwa inajengwa Karema Ziwa Tanganyika kilomita 135 fedha zinakuwa administered na Headmistress wa Mpanda ambaye naye mwenyewe hana gari, kwa hiyo, hata communication kati ya ye ye na Karema was a problem.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuangalie uwezekano wa fedha kuzipeleka kwenye site kule ambako kunajengwa. Kama zilivyokwenda za MMES, MMEM zilikuwa zinakwenda kwenye Kamati ya Ujenzi, zilikuwa zinakwenda kwenye Halmashauri, mimi nadhani tukifanya hivyo, tunaweza tukaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, Wizara imetuahidi tunaoendesa Shule za *Private* ruzuku. Hii ni Bajeti ya tatu kusomewa. Mwaka 2004 tuliahidiwa hazikutoka, ilikuwa Sh.10,000/= kila mwezi kwa kila mtoto. Mwaka 2005 tumeahidiwa, hazikutoka. Nakuomba Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufund, Mheshimiwa Sitta sisi tuandike historia kwamba wewe ndio ulikuwa Waziri wa mwanzo kutoa hiyo ruzuku ya Sh. 10,000/= kwa Shule za *Private*. Nilivyokuona umeingia, sisi

wenzio tumeingia kwa ari mpya, wewe umeingia pia kwa *speed* na *standards*, mimi najua hili hushindwi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, mimi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Imetupa matumaini, lakini tunaomba sana haya matatizo tuliyoyaeleza yatazamwe. Mimi najua Serikali yetu ina nia nzuri, uwezo tu wa kifedha wakati mwingine ndio unaotukwamisha, lakini watazameni wale ambao wako taabani zaidi tuwasaidie ili na wao wapate kusoma kama wanavyosoma katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana sio tu kwa kunipa nafasi hii, bali kwa jinsi ambavyo unatulea sisi akina mama hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa pungezi za dhati kabisa kwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundiki kwa hotuba yake nzuri na alivyoiwasilisha hapa mbele yetu kwa umahiri mkubwa na kwa sauti ya utulivu, nyororo iliyokuwa na mvuto na kumfanya kila mmoja aisikilize.

Mheshimiwa Naibu Spika, simpongezi yeze peke yake, kwa sababu kwa jinsi alivyokuwa anaiwasilisha hii hotuba, nimeona dhahiri kwamba wakati anaiandaa alipata msaada kutoka kwa Mheshimwia Spika. Kwa hiyo, nampongeza sana Spika kwa matayarisho hayo na jinsi ambavyo ilikuwa imefanyika vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Wakikudai ushahidi utakuwa nao? (*Kicheko*)

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Nitakuwa nao. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza pia Manaibu Waziri wa Elimu na Katibu wa Elimu pamoja na Watendaji wote wa Wizara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa najiuliza, hivi elimu inaanzia wapi kwa kiumbe duniani? Nikapata jibu kwamba elimu binadamu anaipata mara ya kwanza kwa mama. Kwa sababu toka mtoto anazaliwa, mama yake anakuwa ni Mwalimu wake wa karibu sana, atamfundisha vitu vyote na mama huyo atamlea mpaka pale ambapo atakwenda kupata elimu ya vitabuni. Hata kuzungumza, ni mama na jinsi ambavyo akina mama walivyo wakarimu, hawaanzi kumfundisha mtoto kuanza kusema mama, mama, hapana. Wanaanza na ba, ba, ba. Kwa hiyo, mimi niwaombe tu akina baba hapa kwamba wakati wa elimu ya awali huko nyumbani washirikiane na mama kwa sababu sisi neno la kwanza kwa lugha zote hata ikiwa ni ile ya kienyeji ya baba anaitwa tata, itaanza ta, ta, ta. Ikiwa ni ile ya Kizungu baba anaitwa *dady*, mtoto ataanza kusema *da, da, da..*

Sasa niwaombe kabisa nyie akina baba mtusaidie sana sisi akina mama wakati wa malezi ya awali, kabla ya mtoto hajakwenda shulenii. Mtoto anapofikia kwenda shulenii ni kitu gani haswa ambacho tunataka mtoto aelimishwe? Tuone hii elimu wanayopata

shuleni itamsaidiaje? itamwendelezaji na itamwezeshaji yeje kuja kumudu maisha wakati wa baadaye? Hapa kunakuwa na tatizo kwa sababu watoto hawafanani. Watoto wanatofautiana. Wanapoanza Shule, kila mtoto anakuwa na vipaji vyake tofauti. Ni kazi sasa ya Walimu kutambua vipaji vya watoto hawa na kuviboresha. Wavinoe vizuri na waelekeze mtoto katika vipaji ambavyo yeje ni bora kuliko wengine. Watoto wana vipaji tofauti. Kuna watoto wenye vipaji vya lugha, kuna watoto wenye vipaji vya kuchora, kuna watoto wenye vipaji vya kuimba, kuna watoto wenye vipaji vya hesabu, akiona chochote tu yeje ataandika *figure*, lakini je, watoto wetu wanasaidiwa kukuza vipaji vyao? Hili ni jambo muhimu sana kwenye Shule za Msingi na ningewaomba sana na hususan hii Wizara ya Elimu itambue vipaji vya watoto wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niupongeze sana Mpango wa MMEM na MMES. Hivi majuzi lilitokea tatizo kwamba vijana wamefaulu, lakini hawakupata mahali pa kwenda Sekondari. Mheshimiwa Waziri Mkuu alilipa jambo hilo umuhimu wa kipekee na juhud zikafanyika, madarasa yakajengwa. Lakini eneo ninalotoka mimi ambapo ni Kilimanjaro maeneo ya kujenga madarasa hayo yalikuwa ni finyu sana kiasi ambacho sasa yale maeneo ya kuchezza, *recreation places*, yaani kama ule uwanja wa michezo yamejengwa majengo ambayo yamemaliza zile nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa napendekeza hivi, inapotokea kwenye eneo kama hakuna nafasi kubwa zijengwe ghorofa. Lakini shida ni moja kwamba, ili maghorofa yajengeke ndugu zangu, inabidi pia hicho kiwango cha fedha zinazotolewa kiongezwe. Kwa hiyo, nilikuwa naomba, kule kwenye mfinyo wa maeneo, waweze kuongezewa fedha ili waweze kujenga maghorofa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watoto wetu wanafundishwa na Walimu ambao kwa kweli miaka ya nyuma walikuwa na heshima ya kipekee na Mwalimu alikuwa akiingia mahali anatambulika kama Mwalimu. Mwalimu anapishwa Kiti, Mwalimu ananunuliwa soda, Mwalimu anafanyiwa kila kitu. Lakini sasa hivi Walimu hawa hawapati tena heshima ile.

Nilikuwa naomba Wizara iweze kuwapa hawa Walimu motisha ili nao waweze kujua kwamba wanatambulika. Huenda ikawa vigumu kwa Wizara zenyewe kufanya, lakini nakumbuka kabisa ilielekezwa hata kwenye Halmashauri zetu Walimu hawa waweze kupatiwa chochote ili kuweza kuwapa hali nzuri kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapendeza sana kwamba, wakati Wizara, kama Wizara ya Elimu inakuwa na majadiliano yaliyo wazi, ningeomba majadiliano hayo yasiishie tu kwenye kujadiliana, majadiliano haya yaishie kwenye muafaka. Vitu ambavyo vinajadiliwa vifanyiwe kazi na inapojadiliwa na watu kwa mfano tunapojadili hapa Bungeni sisi Wabunge na wao Walimu pia wapewe nafasi ya kujadili mambo yao.

Hapa inanikumbusha wakati ambapo Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu amechaguliwa kuwa Waziri, nilisoma katuni moja kwenye gazeti kwamba na mtaniwiwa radhi ilikuwa inasema “Kichaa kapewa rungu.” Hapo ilikuwa na maana kwamba mkereketwa haswa wa Walimu amepewa ile Wizara ambayo sasa atakutana

nayo ana kwa ana. Sasa mimi naamini atatatua matatizo hayo na wao Walimu pia wataweza kupidisha shida zao kwake kirahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu na malezi ni kama mapacha. Huwezi kusema kwamba unaelimisha watu au vijana bila ya kuwalea. Imefikia kipindi sasa vijana wetu sio kama miaka ya nyuma tulikokuwa tunalelewa sisi, kulikuwa hamna *video, television*, kulikuwa hamna vitu vingi kutoka nje. Makanisa au Shule za Serikali ziliwu zikitoa mwongozo, unasimamiwa. Sasa hivi zaidi ya elimu inayopatikana darasani, vijana wanajifunza kwenye *internet*. Jambo likitokea Marekani sasa hivi, kesho kwetu limeenea kuliko pale lilipoanza na hapa natoa mfano. Unakuta vijana wa kiume wanasuka nywele, wametoga masikio, wanaishia kwenye baa, wanacheza *pull table*, hayo yote ni mambo ambayo yanawapotezea muda, yanapotosha maadili, lakini Mwalimu akimwuliza, anasema, Mwalimu huyu amechelewa! Sasa sielewi Mwalimu anayemfundisha kijana huyu amechelewa wapi?

Haya mambo inabidi tuyakemee. Lakini haitoshi kukemea kwa kuwa vijana hawa wanafanya mambo mengi bila ya kudhamiria. Nasema hivyo kwa sababu vijana wetu wengine wanalelewa au na mzazi mmoja bila kupenda au wazazi wote wameondoka labda kwa magonjwa au kwa *accident* au jinsi gani, vijana hawa wanaingia kwenye kunywa pombe wengine wanakunywa mpaka gongo, vijana hawa wanavuta sigara, wengine mpaka bangi. Sasa mimi naona tatizo hili tunaweza kulitatta kama tutakuwa na Walimu wa kunasihi, yaani *Cancelling teachers*, ili Walimu hawa wakae na vijana wetu waweze kuwaauliza nini haswa kijana kimekusibu mpaka umefikia hatua hii? Kwa sababu huko tunakokwenda sasa, kama tutazungumza tu wafafulu Hesabu, Kiingereza, Sayansi na kadhalika bila kuangalia tabia zao, kwa kweli itakuwa hatujafanya jambo la kupendeza.

Nilikuwa naomba sana hawa Walimu wa kunasihi wawepo mashulenii na waingizwe kwenye ikama. Itakuwa imetusaidia sisi katika kuwalea watoto wetu katika hali ambayo watakuwa ni vijana wenye maadili mazuri, waliokamilika na watulivu. Wakati mwingine tunaweza tukaishia kuwalaumu, lakini pia aina ya vyakula vinavyoliwa wakati huu, sio kama vile vilivyokuwa vinaliwa wakati ule. Vyakula asili vilikuwa vinafanya miili ya watu inapoa. Hivi vyakula vya sasa, kuku wa kisasa, mayai ya kisasa, kila kitu kisasa inafanya vijana wale wanakuwa *hyper*, kwa hiyo, hawana utulivu tena kwenye maungo. Nilikuwa naomba sana hawa vijana wasaidiwe kwa sababu huko tunakoelekeea kwa kweli tutaishia kulaumiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumzia kuhusu vyakula wanavyokula wanafunzi, lakini pia hapo imenikumbusha kuwa nilikuwa nimeorodhesha hapa kuzungumzia lishe kwa vijana wetu mashulenii. Kwa kweli vyakula wanavyopewa sio vyakula ambavyo ni vya kuboresha au ni vya kujenga miili ya vijana katika umri ule. Utakuta vijana wale wanakula ugali na maharage kila siku. Sasa mimi najiuliza hawa ni wanafunzi au ni wafungwa? Tunaambiwa ni wanafunzi. Haya! Kuku, mayai, maziwa, tunakula sisi watu wazima, tunataka nini? Sisi tumeshakua, tumefikia hapa, kwa nini hivyo vitu tusiwape watoto wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, utakuta Wizara ya Mifugo inasema kila mtu anywe maziwa, lakini jinsi gani haya maziwa hayawafikii watoto hawa mashulenii? Nilikuwa

naiomba Serikali iangalie, kwa vile maziwa ni muhimu sana kwa vijana wetu, basi ikiwezekana vijana hawa mashulenii wawe wanapatiwa angalau kikombe cha maziwa kwa siku ili kuwasaidia pia kukuza afya zao na kuwapa *calcium* ambayo itawasaidia pia kufikiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo ya kuzungumza hapa ni mengi, lakini nilikuwa naomba sasa nirudi kwenye taaluma. Huko nyuma tulipokuwa tunasoma sisi, utaanza kufundishwa Kiingereza Darasa la Tatu, Kiswahili unaanza Darasa la Kwanza. Hiyo ilikuwa wote tunatoka nyumbani ambako tunaongea lugha za kienyeji, yaani lugha zetu.

Lakini sasa watoto wetu wenyewe hawajui tena zile lugha za kikabila, watoto wetu wamekuwa ni Waswahili. Sasa kwa vile watoto wetu wote ni Waswahili, wanajua Kiswahili fasaha, kwa nini wanapoingia Darasa la Kwanza wasianze kufundishwa Kiingereza toka Darasa la Kwanza ili wakienda sasa kutoka Darasa la Kwanza, Darasa la Pili na Darasa la Tatu wawe wanakifahamu Kiingereza?

Hapa inanikumbusha Spika wa Kenya, Ole Kaparo, alisema, huko Kenya wao wanauzu ng'ombe kufundisha watoto wao Kiingereza. Sisi hatujui tunauza ng'ombe kuwafundisha watoto wetu nini!

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba sana, Kiingereza kinasaidia watoto wetu wajifunze vitu vingi Shuleni. Kwa hiyo, Kiingereza kiianzie toka Darasa la Kwanza na kiwekewe msisitizo. Wakati ambapo sasa tunapambanisha vijana wetu hapa na vijana kutoka maeneo mengine, nchi nyingine katika ustahili wa kupata ajira pale, kinachofanyika ni jinsi gani mtu anaweza kujieleza tu. Kijana wetu anaweza akawa anafahamu sana, lakini kijana huyo hawezi kujieleza, anaanza mmmm!! Hivyo, hawezi kabisa kuchukuliwa katika ule usaili. Yule ambaye anaweza kujieleza vizuri atachukuliwa katika ile ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona kwamba michezo imerudishwa sasa mashulenii upya. Lakini najiuliza. Hivi hawa vijana watakuwa wanacheza kwenye viwanja vipi? Mashule mengi hayana uzio na wengi amba wana nyumba zao pembeni ya Shule wanamega yale maeneo ya Shule kidogo kidogo hasa hizi Shule za Msingi. Nilikuwa namwomba sana Mheshimiwa Waziri, naona hapa niiombe Serikali itoe tamko kwamba Shule zote ziwekewe uzio. Kwa sababu kadiri watu wanavyomega maeneo ya Shule, maeneo yale yanakuwa finyu na vijana hawapati mahali pa kuchezea, na pia maeneo yale yanakuwa hayatoshelezi katika hali halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba pia nimwombe Mheshimiwa Waziri aangalie kwenye kufanya *rehabilitation*, yaani *ku-repair* Shule. Ni kweli tumepata madarasa mapya ya MMES na MMEM lakini kwa utamaduni wetu, watu hatufanyii *repair* yale tuliyokuwa nayo. Tumeshapata mapya yale ya zamani tumeyasahau.

**NAIBU SPIKA:** Kukarabati.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nilikuwa naomba hata wanapopangiwa hayo mafungu ya madarasa mapya, yasiishie tu kujenga madarasa mapya, litengwe pia fungu la ukarabati kila mwaka, toka jengo likiwa jipyä siku ya kwanza kioo kinaweza kupasuka, kitahitaji ukarabati, lakini kama hakuna fungu, kioo kile kitapasuka, mwisho dirisha litatoka, mlangano nao hata paa litapeperuka. Tuwe na utamaduni wa kukarabati Shule zetu kila wakati, la sivyo, tutaishia tena kujenga upya kila wakati. (*Makofî*)

Namba sasa nizungumzie kuhusu ajira za Walimu. Utakuta kwamba wengi wangependa kuwa Walimu, lakini kinachowakatisha tamaa ni mshahara ambao unaambatana na hiyo ajira. Matokeo yake sasa wanakuwa Walimu, lakini wanakimbilia kwenda kufanya *tuition*. Sasa, endapo Mwalimu huyu amepangiwa vipindi, anafundisha, lakini akiwa na watoto wa *tuition*, kwa vyovyote ataangalia zaidi anakwenda kufundisha nini kule *tuition*? Kwa sababu kule *tuition* wale wazazi wanabanana naye karibu wanamwambia hapa ilikuwaje? Kwanini nilikulipa *tuition* mwanangu hakufaulu? Kule Shuleni akifundisha, anafundisha kundi kubwa la watu na bahati mbaya sana wazazi wengi au mashule mengi hayana mpango wa kukaribisha wazazi siku ya kuangalia vitabu na maendeleo ya watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili watoto waweze kupata usimamizi katika elimu ni lazima wazazi wafike mashuleni, wazazi wajadiliane na Walimu, ni kwanini hapa imekuwa hivi, imekwenda vile na hapo ndio unaweza kumbana Mwalimu mhusika, kwanini somo hili mwanangu alikuwa hafanyi vizuri na hukunishirikisha? Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana, Walimu waboreshewe mishahara yao, watulie mashuleni kwao ili waweze kuwafundisha hao watoto kwa namna ambayo watoto watawaele wa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kusahau, imeonekana dhahiri kwamba Shule za Seminari zinafanya vizuri na wengi wanajiuliza, ni kwanini? Nataka tu hapa nieleze kwamba zile Shule zinafanya vizuri kwa sababu wakiingia pale linaloangaliwa pale ni elimu tu. Elimu na jembe, kwa sababu huko kwenye Seminari kwa kweli vijana wanalima sana. Lakini hakuna mambo mengine ya ziada tofauti sana na Shule zetu nyingine.

Nilikuwa naomba hivi, wote hawawezi kwenda Seminari, wote hawawezi kwenda Shule za *Private*, lakini hao hao vijana wetu ambao wanafanya vizuri, walio kwenye Shule za Serikali, tuwape shughuli chache na tuwapunguzie adha ya kuwarudisha rudisha nyumbani; rudi nyumbani kachukue hiki, kwa kweli hili jambo la kuwarejesha watoto nyumbani mara kwa mara linaleta kero, sio tu kwa mtoto, lakini ni kwa jamii nzima. Huenda mzazi amekosea, basi tuangalie ni namna gani mzazi huyu aweze kuelewashwa kumpatia mtoto wake mahitaji yanayostahili ili asirudi nyumbani. Sasa kuna wale ambao wanarudi nyumbani kwa sababu ambazo zinaleweka, labda hakupata ada, sasa mtoto huyo anaweza akawa na akili sana na inabidi asaidiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono. (*Makofî*)

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia jioni ya leo. Lakini vilevile, napenda tu

kusema kwamba naipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo, kwa hotuba yao nzuri ambayo tumeisikia asubuhi ya leo. (*Makofî*)

Lakini vilevile ninaamini kwamba Wizara zote zinazosimamiwa na wanawake, kwa kweli ziko makini ukisoma hotuba zao. Unajua akina mama mara nyingi hatupendi mambo ya kupindisha pindisha, kwa hiyo, nachukua nafasi hii kupongeza Mawaziri wote wanawake kwenye Wizara zao, wanafanya kazi nzuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu kuwapongeza na Manaibu Waziri na Makatibu wao na wote walioshirikiana nao katika hotuba hii, kwa kweli nawapongezeni sana. Ninayo tu machache ya kuweza kuongezea ongezea, kwa kweli nikiangalia Wizara hii imepanga mambo yake vizuri na inaonekana kwa kweli mambo yatakuwa mazuri katika awamu hii ya nne, ila sasa ni machache tu ya kuongezaongeza ambayo naona kidogo yamemegukameguka, naomba niongeze tu machache.

Kwanza kabisa, naomba nitangulize pongezi. Nilipokuwa nasikiliza hotuba ya Waziri leo asubuhi, amesema kwamba, yale madeni ya Walimu sasa wanatarajia kuwalipa katika mwaka huu wa 2006/2007. Ninawapongeza sana kwa sababu mara nyingi tumezoea sana kuona umekaribia uchaguzi Walimu ndio wanakumbukwa. Sasa nakuwa na wasiwasi kwamba wasipoangalia hapo, naona mambo yanaweza yakawa mabaya. Kwa hiyo, safari hii naona ni mikakati mipya ya Awamu ya Nne hii tunayokwenda kwa kweli nawapongezeni kwa kuwa hilo mmeliona mapema. (*Makofî*)

Vile vile, nitapenda tu kuingia kwenye hoja ya kwanza ambayo inahusu Walimu wanaoajiriwa katika Shule zetu za Msingi. Ninapenda kuchangia hii hoja kwa sababu nimeona mara nyingi Walimu wanaokuwa wameajiriwa katika Shule hizi za Msingi, wanapokuwa wameingia kazini wanakuwa na muda mchache sana wa kukaa kazini, alipoajiriwa *especially* wale wanawake wanaoingia *first appointment*, yaani ni binti ambaye hajaolewa, ametoka Shule, sasa anaingia kazini.

Ninasema hivyo kwa sababu, nimekuwa na uzoefu katika Wilaya yangu ya Maswa, kuna kipindi tumepata Walimu wengi sana, yaani kwa kweli Wizara ilifanya vizuri sana, tulipata walimu wengi na hata tukafurahi kwamba sasa nafikiri hili pengo tunakwenda kupunguza. Lakini baada ya muda sio mrefu nikashangaa kuona kwamba Walimu wengi kweli wamehama. Wengi mno wamehama, yaani haraka haraka wakawa wamehama, wengine hawakumaliza hata miezi sita. Sasa mimi nikawa najiuliza ni kwanini? Ni sawa Halmashauri ndio wanawajibika kuwahamisha na kuwaajiri, lakini je, Wizara inasemaje juu ya hawa watu? Kwa sababu, kweli wale wanaingia kutafuta ajira, baada ya ajira wanahamia wanakotoka.

La kwanza, anapokuwa amepata ajira, ametoka labda Moshi, ametoka labda Mtwara au wapi, anajua Maswa kuna nafasi Mkoa wa Shinyanga, sasa anapokuwa amejichomeka pale, anatafuta ni jinsi gani ya kuchomoka aende pale anapopataka, ni rahisi tu. Si unajua tena rushwa nayo ilikuwa imetangulizwa sana! Kwa hiyo, anaweza akamwona ye yote anayehusika pale akampa kidogo, muda sio mrefu unashtukia Mwalimu kachomoka. Sasa tatizo linakuwa bado liko palepale, Walimu wote

wanasambaa, wanaondoka. Sasa mimi hapa ningependa tu labda niishauri Wizara kwamba, angalau waweke mikakati kwamba, Mwalimu anapokuwa ameajiriwa, anatakiwa akae muda gani pale Shuleni baadaye ahamishwe kutoka pale.

Mimi nilikuwa nashauri hilo kwa sababu limesababisha hata Wilaya yetu ya Maswa tuwe na pengo kubwa sana la Walimu. Lakini Walimu walikuwa wameajiriwa wengi. Sasa hilo nimeliona kwa kweli na nilikuwa karibu sana na nina uzoefu nalo, nimeligundua, lakini kwa sababu sasa Wizara imepanga mikakati mizuri, tusije tena tukarudi nyuma. Inabidi tuwaambie ni jinsi gani mnaweza kuweka mikakati ya kuweza kufanikisha, mnapoajiri Walimu, basi kwa muda kadhaa wawepo pale wale Walimu. Japokuwa wengine bahati nzuri wanakuwa wameolewa, kwa sababu hizo ni baraka, huwezi ukazuia, kuna wengine wanakuja pale haraka haraka unashukia wameshaolewa. Sasa hapo hatuwezi tukajua kwamba ameolewa kwa *technique* ya kuhama au vipi, lakini hilo ni baraka, tuliache livilyo.

Vilevile, ningependa kuongezea kuhusu kuongeza Walimu. Kwa bahati nzuri, wenzangu wamelisema sana kwa sababu hata kule Wilayani kwetu ninakotoka na Mkao mzima wa Shinyanga na mahali pengine kwa faida ya wote, ninafikiri kwamba kuna sababu ya kuongeza Walimu. Kama Wabunge wenzangu walivyotangulia kusema, ni kwamba, kuna mahali pengine kuna Walimu wachache sana kama Walimu wawili, watatu, lakini wale watoto hawafundishwi vizuri. Mtu yoyote! Ukitaka kuchunguza, watoto wanaofaulu kutoka Kijijini, kwa mfano ametoka Kijijini, hawezi kupambana na mtoto wa Mjini hata siku moja. Yule mtoto anakuwa na akili, huwezi kuamini! Lakini kwa sababu wale watoto wanakosa watu wa kuwa-*support*, Walimu hamna, Mwalimu anatoka huko anatangatanga anarudi huku anarudi huku, inakuwa ni tatizo.

Sasa nilikuwa nafikiri kwamba hili nalo Wizara ijaribu kufanyia marekebisho. Shule kwa kweli ni nyingi zimefunguliwa za sekondari, hata wilayani kwa kweli ni nyingi lakini kuna Shule ambazo yaani hata leo nikikupeleke kuna Walimu wawili maskini. Sasa wale Walimu wanapata taabu sana kuwafundisha watoto. Nilikuwa nafikiri hili nalo Wizara ijaribu kuliangalia jinsi ya kulifanyia kazi, angalau Walimu wapatikane, potelea mbali hata kama wakiwa sita sio mbaya sana, lakini angalau wale watoto waweze kupata masomo yao.

Kingine ambacho ningependa kusema juu ya wanafunzi wanaolipiwa ada zao na Halmashauri, watoto yatima. Kuna tatizo, inapokuwa kimefika kipindi cha mtoto kwenda Shule, anahitaji kupeleka ada, labda Halmashauri haijawa tayari kupeleka ile pesa kule Shuleni, kinachotokea, yule mtoto anapokuwa amekwenda Shule, Mwalimu anamwambia rudi nyumbani. Sasa yule mtoto anapata wapi pesa? Maana yake Serikali ndio inamlipia, wewe Mwalimu kama unamwambia rudi, kwa sababu anaporudi nyumbani, haendi kumwomba baba, wala mama wala babu, wala mlezi, anatakiwa aende pale pale kwenye Halmashauri.

Sasa mimi nilikuwa nafikiri kwamba, hawa watoto ili wasipate taabu maskini, tayari wameshapata adhabu hawana wazazi, hawana mtu wakuwahudumia, tusije tukawapa adhabu hata sisi mara mbili ili tuweze kupokea zile baraka na Serikali iendeleee

kubarikiwa na kuinuliwa. Inatakiwa tuwalee hao watoto, Walimu wanapokuwa wanajua muda umefika, waende wakaonane na Halmashauri wamfuate Mkurugenzi, waongee naye, ni vipi hao watoto, wanatakiwa wafanyiwe nini? Sio inafikia mahali watoto wanatangatanga Mijini, ukiwaliza, wanasesma, tumerudishwa. Nani analipa? Serikali inalipa, Halmashauri inalipa. (*Makofî*)

Nilikuwa nafikiri, hili kwa kweli limekuwa ni tatizo kubwa, sijui kama na maeneo mengine lipo, lakini kwangu mimi nimelishuhudia. Hao watoto waendelee kusoma, yule Mwalimu apewe taarifa kwamba Serikali itakapochelewa kuleta pesa au Halmashauri, basi angalau yule Mwalimu aonane na Halmashauri wakati huyu mtoto anaendelea kusoma, asipoteze muda wake wa masomo eti kwa sababu hana ada.

Mimi nafikiri hilo labda Mheshimiwa Waziri, najua yuko makini sana, ameshalichukua, nimeona anaandika. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, napenda kuchangia juu ya Walimu wanaosimamia mitihani. Hao Walimu wanaosimamia mitihani ya Darasa la Saba, ni wale wale, sijui kwingine. Mimi ninapokuwa nasema kama na wewe lipo hilo, hebu jaribu kuliangalia na kama hujaliangalia licheki linafanyika sehemu nyingi sana. Walimu wanaosimamia mtihani ana miaka kumi anasimamia ye. Pale Shuleni wanapomtoa yule Mwalimu, kuna Walimu zaidi ya kumi, kwanini anakwenda yule yule, kuna nini? Kwanini aende yule yule wakati Walimu walioko pale ni wengi na wanaweza kusimamia?

Ukija kusikia mitihani imeliki, unafikiri inaliki kwa sababu gani? Yule ameshazoea, anajua ni jinsi gani afanye. Anaweza akafanya mipango hata na hao Maafisa Elimu huko, kwa sababu isingekuwa hivyo, Walimu wanapokuwa wanabadilishwa angalau mnaepusha vitu vingine ambavyo sio vya msingi kutokea sana.

Kwa hiyo, nafikiri hili nalo mllichukue, Walimu kusimamia mitihani ya Darasa la Saba, mwaka huu ni ye, mwaka kesho ni ye, mwaka kesho kutwa ni ye, utasikia wanalamikiana hata wao na vilevile ukirudi nyuma hao Walimu wengine hawatendewi haki. Maana na ye, anahitaji mwaka ujao apate hiyo posho anayopata mwenzie. Uwepo mgawanyiko! Mbona hiyo kengele imelia mapema? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa napenda nichangie tena kitu kinachoitwa, suala la madawati shulen. Suala hili kwa kweli limekuwa ni tatizo. Serikali imeweka mikakati mizuri sana kwa kweli tuweze kuchangia na tumechangia muda mrefu sana. Mimi nimechangia dawati mwanangu hajaenda Shule, sasa hivi mwanangu yuko *Form Three*. Mimi ninachotaka kujua hapa, hili tatizo la madawati ni lini litakwisha? Kuna mikakati gani ya kumaliza tatizo hili? Ina maana mimi nilivyochangia madawati, nilikuwa sijaza mtoto, nilikuwa nawachangia wenye watoto? Sasa sisi tuna watoto, wale ambao hawana watoto wanapoyachanga yale madawati na wale wenye watoto, mbona hayawi mengi? (*Kicheko*)

Nilikuwa nafikiri hili na lenyewe lisiwe kero ndugu zangu. Naomba Mheshimiwa Waziri, hebu ajaribu kuangalia ni jinsi gani afanye kama madawati yanapatikana, ifikie mahali madawati yamepatikana pale Shule yawepo. Sasa hivi kuna watoto wanaokaa chini. Mtoto kila siku ni mchafu, anafua, mama anafua kila siku, sasa anakuwa na adhabu ya kutoa sabuni kila siku! Hebu na hili lijaribu kufanyiwa mikakati angalau madawati ifikie mahali watu wapate pumzi basi na wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine, nilikuwa nataka kusema kuhusu kupunguza makato kwenye mishahara ya Walimu. Hao Walimu kwa kweli wana makato mengi. Hilo nafikiri limeshaelewaka, limesemwa sana. Nisipoteze muda, labda niharakishe kusema kitu kimoja.

Nilitaka kusema kitu kimoja, juu ya Walimu kufundisha *tuition*. Mimi nilikuwa naona kwamba Wizara iruhusu hao Walimu wafundishe *tuition* kwa Primary Schools kwa sababu hawana marupurupu. Chaki mnazowapelekea Walimu Wakuu, akiuza, watoto wote hawatasoma. Ni dogo mno kule Shulen. Mimi nilikuwa naona kwamba hawa Walimu waruhusiwe wafundishe *tuition* kwa sababu sisi tuna uwezo, watoto wetu kuwapeleka kwenye *tuition* za pesa yoyote, lakini hawa wa hali ya chini, *tuition* yao sio hela ya nyingi. Unasikia Mwalimu anaomba Sh.500/= kwa mzazi, anaomba Sh.1,000/=, lakini anafaidika, mtoto anaelewa!

Mimi nilikuwa nafikiri ili na Mwalimu apate na ajira ya *tuitioni* na mtoto afaidike, itolewe ruhusa basi, Walimu wafundishe *tuition*, tuwaokoe na hao watoto wa wazazi wao ambaa hawana uwezo. Tusiende nao tu tunawaburuzaburuza. Nashakuru mwenzangu amesema kwa kweli kwamba Walimu wanafundisha *tuition* anakuwa na mawazo ya *tuition*, lakini hapa ukichunguza mzazi anafaidika na vilevile na Mwalimu anaongeza kipato kidogo, ile Shilingi mia tano, tano, akifundisha watoto wanapata hela nyingi na bahati nzuri *tuition* inakuwa pale Shule. Kwa hiyo, akipata ile Sh. 500/= angalau inakuwa nafuu.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa nafikiri kwamba angalau lifanyike hili, watoto angalau waelewe, hakuna jinsi ya kufanya, vitabu Shulen havitoshi, madarasa yenyewe ndio hivyo, sasa angalau wakipatiwa wale watoto ka-*tuition* katawasaidia. Mimi nilikuwa nafikiria kwamba kwa mawazo yangu waruhusiwe wapate madarasa yao pembeni popote pale patakapokuwa panawezekana, angalau wapate *tuition* watoto waweze kuelewa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba nilikuwa na wasiwasi kwamba muda wangu umekwisha, naona kwamba sasa hivi kwa kweli nitakuwa nimefikia mwisho. Maana yake nimechangia kwa wasiwasi, najua dakika hazitoshi. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza, nami niungane na wenzangu kumpongeza Waziri, Manaibu Waziri wake kwa kazi yao nzuri

wanayoifanya kuboresha elimu nchini mwetu. Hili ni jukumu zito na nyeti na wanastahili pongezi zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, naomba nichangie haya yafuatayo:-

Bila shaka utakubalina nami kwamba ili tuingie katika karne ya 21 kama washiriki na sio watazamaji, tunahitaji kuwa na elimu bora inayoendana na wakati. Lakini kwa bahati mbaya, kiwango na ubora wa elimu yetu bado vingali chini sana. Hivyo, Serikali inapaswa pamoja na mambo mengine kufanya haya yafuatayo ili tuweze kuinua ubora na kiwango cha elimu yetu. Kwanza, kuhakikisha kwamba tunao Walimu wengi wa kutosha na wenyewe ujuzi na sifa zinazofaa; Kutatua matatizo ya Walimu wetu likiwemo la ukosefu wa nyumba na kuboresha maslahi yao ili kuwavutia wahitimu wengine waweze kuingia katika Sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu sasa vilio vya Walimu wetu vimekuwa havisikilizwi na matokeo yake yamekuwa, madai yao mengi yamekuwa hayatekelezeki. Hii inakwaza kazi wanayoifanya na kuwafanya wakate tamaa na matokeo yake ni kwamba tunawanyima watoto wetu haki ya kupata elimu iliyo bora. Hivyo basi, naiomba Serikali iandae mkakati mahsusuna unaolenga kutatua matatizo ya Walimu ili waweze kufundisha bila bugudha yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni tathimini, yaani *performance evaluation au assessment*. Kuwa na Walimu wenyewe sifa nzuri na wanaolipwa maslahi mazuri, lakini kama hatufanyi *assessment* ya *performance* yao haitakuwa inatusaidia. Hili ni eneo ambalo kwa muda mrefu limekuwa na matatizo na limeonekana kwamba Walimu wengi wamekuwa hawafanyiwi *assessment* na kwa hiyo, ubora wa utendaji kazi yao umekuwa hauonekani. Hivyo, naomba Serikali itilie mkazo *assessment* ili tuweze kujua kwamba: Je, tunakotoka ni wapi na tunakokwenda ni wapi ili tuone kama majukumu na malengo tuliyowekeana yanafikiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni ukosefu wa vitendea kazi, hasa vitabu. Ukienda katika mashule mengi hasa yaliyoko Vijijini, utakuta kwamba hayana vitabu vya kutosha. Utakuta ama Mwalimu peke yake ndiye mwenye kitabu ama wanafunzi kwa wingi wanachangia kitabu kimoja, sasa na hii inawakwaza. Inakuwa kwamba hawapati nafasi ya mwanafunzi mmoja kuweza kusoma katika maeneo ambayo wamepangiwa, yaani *topics* na hivyo inakuwa ni shida kwa wanafunzi kuweza kuelewa au kufuatilia Mwalimu anachofundisha au somo lenyewe.

Hivyo, naiomba Serikali ihakikishe kwamba Shule tulizonazo zina vitabu vya kutosha na nyingine hasa za *private* ambazo zinafunguliwa zina vitabu vya kutosha, vinginevyo Shule hizi zisipewe leseni za kufundisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika pitapita yangu, katika Mawizara nimegundua kwamba Wizara nyingi na Idara nyingi za Serikali zina urasimu wa kutisha katika kutoa maamuzi au kutatua matatizo yanayotukabili. Huo ni mfano ambaa unamhusisha mpiga

kura wangu wa Jimbo la Mwibara. Mwaka huu mwezi wa pili nilijiwa na mpiga kura wangu mmoja.

Tatizo alilokuwanalo ni kwamba binti yake amefukuzwa Shule katika Shule ya Sekondari ya Ngudu. Tatizo lililokuwepo ni kwamba, huyu mwanafunzi mwaka 2004, baada ya kumaliza mitihani ya Darasa la Saba alialikwa nyumbani kwa Mwalimu Mkuu akamsaidie kazi. Alipofika kule, huyu Mwalimu Mkuu akambaka, huyu mwanafunzi akamshitaki yule Mwalimu Mkuu na kesi iko katika Kituo cha Polisi cha Ngudu kule Kwimba.

Baadaye kabla matokeo hayajatoka kuingia Kidato cha Kwanza, huyu msichana akajikuta ana ujauzito. Lakini kabla ya kuingia Kidato cha Kwanza, Mungu nafikiri alimjalia ingawa sikusudii kusema kwamba tatizo alilolipata ali-*miscarriage*, kwa hiyo, alipopata majibu ya *Form One* katika Shule ya Sekondari ya Ngudu hakuwa na mimba tena. Sasa kakaa kuanzia mwezi wa Kwanza mpaka mwezi wa Kumi na Moja akafanya mitihani ya kumaliza *Form One*.

Baadaye akiwa anasubiri shule ifungwe kwa mapumziko akafukuzwa Shule. Sababu iliyotolewa na Mwalimu Mkuu ni kwamba alikuwa na mimba, lakini uhakika ni kwamba kwanza wakati akiingia *Form One*, hakuwa na mimba. Lakini cha pili, huyu msichana hakustahili kufukuzwa Shule. Aliyestahili kufukuzwa kazi ni Mwalimu Mkuu aliyembaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka ninapoongea muda huu, huyu Mwalimu Mkuu anaendelea kubaka mabinti zetu huku akilipwa kodi ya wananchi ambayo ni pamoja na ya baba wa binti aliyebakwa. Sasa mimi ninaiomba Serikali leo itamke wazi kama kosa ni la yule binti kubakwa au ni yule Mwalimu Mkuu aliyembaka.

Kwa kutumia Bunge hili, tukubaliane kwamba tunapopiga makofi huyu Mwalimu asimamishwe kazi mara moja ikiwa tunasubiri matokeo ya uchunguzi utakaofanywa ili tubaini ni ni nini hasa kilitokea, kesi iko Mahakmani, lakini uchunguzi mwengine hauzuiwi kuendelea kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni mojawapo ya matatizo tunayoyaona yanajitokeza na bado hatuyachukulii hatua. Mwezi Februari, 2006 nilimwarifu Waziri wa Wizara hii kuhusiana na tatizo hili, akanieleza kwamba nimwandikie barua, nikamwandikia barua, nikarudi mwezi wa tatu akaniambia kwamba bado analifanyi kazi.

Nikarudi mwezi wa nne akaniambia amesahau, anaomba nimwandikie barua nyingine, nikamwandikia barua nyingine, nikampatia Msaidizi wake *copy*, nikapeleka kwa Mkurugenzi wa Elimu ya Sekondari. Mwezi wa sita kabla ya kuja huku, nikwamona Waziri mhusika, akaniambia bado anaifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefika hapa, kasema kwamba, Mkurugenzi wa Elimu ya Sekondari bado hajarudi. Nafikiri mpaka muda huu, atakuwa hajarudi kwa sababu majibu ya matokeo ya uchunguzi wake sijayapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumza hili kwa uchungu mkubwa kwa sababu mimi nafikiri Walimu wetu ni walezi wetu na wala sio waharibifu wa watoto wetu. Lakini Wizara ya Elimu inatambua wazi ni Walimu gani wazuri na walimu gani wabaya. Sasa kama Wakuu wa Wizara wanashindwa kuchukua hatua za kuwawajibisha watusika, waharibifu wa watoto wetu, hapo tuna tatizo kubwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwamba, hakuna mtu anayeweza kufika Mbinguni bila kufa, lakini bahati mbaya kila mtu anataka kwenda Mbinguni, lakini hataki kufa. Sasa na sisi hatuwezi kuboresha elimu yetu kama hatuwezi kukubali kuwaondoa wale wote ambao tunafikiria kwamba wanatukwaza katika kuboresha elimu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kama walivyosema wengine, wale wote wanaotukwaza katika kuboresha na kufikia malengo yetu, basi waachie njia sisi tuweze kupita.

Naomba Serikali itamke wazi wakati wa kuitisha vifungu vya Wizara hii hapo kesho, nina imani kwamba Wizara ya Elimu ina miundombinu mingi sana, ina Shule, kila Wilaya ina Ofisi zake, kila Kata ina Waratibu wa Elimu na Maafisa wengine wa Elimu. Suala hili haliwezi likachukua miezi sita kuchukuliwa hata kama ni kitu gani, mimi naomba sasa lipatiwe utatuza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pamoja na hilo na barua zangu vile vile niweze kujibiwa. Naomba na mimi leo niwe muadilifu kidogo nisigongewe kengele ya pili, naunga mkono hoja hii, lakini *pending* kupata majibu na tamko rasmi la Serikali kuhusiana na suala hili. Ahsante sana. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, ahsante. Nadhani mchango wako umekuwa ni *emotional* kwa sisi wote. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge naona tumekuwa *full house*, naomba nisome Kifungu cha 88, (9). Tunarudia haya kwa sababu tunategemea kila mmoja atakuwa na Kanuni. Kifungu hiki kinasema hivi:

“Kamati yoyote ambayo Spika atapeleka kwake kama Muswada au jambo lingine lolote, itahesabika kuwa ndiyo Kamati inayohusika kushughulikia Muswada huo au jambo hilo lingine lolote.”

Waheshimiwa Wabunge, asubuhi Mheshimiwa Chacha Wangwe aliwahi kabisa kuleta nyaraka za ushahidi wa maneno aliyoyasema wakati akichangia hapa kwamba kulitokea mauaji kule kwao Tarime yaliyohusiana na uchaguzi na kwamba wale waliokuwa wanampigia kura waliuawa.

Kwa hiyo, tukamundai hapa atoe ushahidi. Amefanya hivyo kwa kuleta hili kabrasha, kwa hiyo, ili tuweze kutenda haki, naagiza Kamati ya Ulinzi ndiyo itakayoshughulikia kupitia *document* hii.

Kwa mujibu wa Kanuni hizi, wanaweza kualika mtu mwengine ye yeyote kuingia ndani katika suala zima. Kwa hiyo, suala hilo sasa litawasilishwa kwa Kamati ya Ulinzi na tutapewa Taarifa kupitia Kamati hii. Tunaendelea na Mheshimiwa Dr. Sigonda.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia, naomba nifafanue jina langu, maana yake inavyoelekea jina langu linawapa shida sana ndugu zangu. Lakini kama ukiamua kuniita jina la kwanza au la mwisho, hayo majina ni rahisi sana. Jina la kwanza ni “*Gido*,” yaani Guido, ni rahisi kabisa na jina la tatu ni Sigonda. Hili la kati kati, kwa sababu linatupa matatizo, mimi nafikiri tungeliacha tu. Sasa matatizo yanakuja katika matamshi na hasa zaidi hawa ndugu zangu, watani zangu hawa Wasukuma, Wanyamwezi na Wanyakusa, badala ya kutamka Sigonda, wanasema Sing’onda. (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Lakini Naibu Spika, hakutamka vibaya. (*Kicheko*)

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba tu kwanza, ndugu zangu wajaribu kutumia yale majina ambayo pengine yatakuwa ni rahisi kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo, naomba vile vile nami niungane na wenzangu, kumpongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundı, Manaibu wake, pamoja na watendaji wake, kwa hotuba nzuri sana, ambayo kwa kweli imefafanua kila kitu. Mwelekeo wake ni ule amba ni matarajio ya kila mmoja wetu hapa tulipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Waziri akitoa hotuba yake, naomba vile vile nitoe salamu, kuna mtu mmoja ambaye alikuwa anamwangalia, ye ye yuko Dar es salaam. Kwa sababu nilimwambia kwamba, jioni hii nitakuwa ni mmoja wa wachangiaji, akanomba nimpongeze kwa niaba yake. Huyo mtu anaitwa Margareth Sigonda. Anampongeza sana Mheshimiwa Waziri na amenitahadharisha, anasema kwamba, kama sitaunga mkono hii hoja, atashangaa sana. Kwa hiyo, nianze moja kwa moja kwa kusema kwamba, naunganaye kwamba, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi yamezungumzwa kuhusu Wizara hii, lakini mimi nitakuwa tofauti kidogo. Nitazungumzia zaidi maendeleo ya elimu katika Wilaya yangu ya Chunya. Maendeleo ya elimu katika Wilaya yangu ya Chunya ni duni sana. Lakini nilikuwa najaribu kutafuta sababu hasa ni nini. Pamoja na sababu nyininge zote, lakini sababu kubwa nimegundua kwamba, ni kutoptaka na Serikali kuiweka pembezoni hii Wilaya ya Chunya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya hii ya Chunya ilianzishwa mwaka 1942. Tangu tupate Uhuru mwaka 1961, ni Viongozi wa Taifa amba mojawapo ambayo nimeona kwamba, inachangia kudumaza maendeleo ya Wilaya hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako, ninaomba niwatambue tu kwa kuwapongeza na kuwashukuru wale ambao tayari walikwisha itembelea hii Wilaya: Mheshimiwa Marehemu Dr. Omar Ali Juma, Mheshimiwa Dr. John S. Malecela, Mheshimiwa Abdallah O. Kigoda, Mheshimiwa Philip Mangula, aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Mizengo P. K. Pinda, Mheshimiwa Joseph J. Mungai na Mheshimiwa Prof. Mark J. Mwandosya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kati ya hao wote, ambaye ametembelea zaidi ya wenzake ni Mheshimiwa Prof. Mark J. Mwandosya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuruni, lakini pamoja na hayo, Waziri Mkuu aliyepita naye alitembela. Kwa hiyo na yeye namshukuru sana. Vile vile na Waziri Mkuu wa sasa, naye ameitembelea Wilaya hiyo ya Chunya, namshukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini, kila mmoja kati ya hao niliowataja, alikuja kwa matatizo na maelekezo, siyo kwa ajili ya kuja kuhimiza maendeleo. Mheshimiwa John S. Malecela, alikuja kwa ajili ya kuhamasisha Uchaguzi Mkuu, Mheshimiwa Waziri Mkuu wa sasa, alikuja baada ya kuona kwamba, kuna matatizo kati ya wafugaji na wakulima. Kwa bahati nzuri au bahati mbaya, siku hiyo alikabidhiwa yule mwenzangu aliyekuwa Mbunge, siku hiyo akaambiwa aende naye huko. Ninachotaka kuonesha hapa ni jinsi gani Serikali imeiweka pembezoni hii Wilaya. Mimi naomba kabisa, Serikali iendelee tu kuamini kwamba, Chunya nayo ni moja ya Wilaya katika nchi yetu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuna mifano mingine ambayo inanipelekea kuamini kwamba, inawezekana pengine Serikali inafanya hivyo sijui kwa nia mbaya au kwa nia nzuri, lakini najua ni kwa nia nzuri tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyo vivutio vingi sana, lakini kwa bahati mbaya, hata ile hotuba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, haikuweza kuainisha Wilaya ya Chunya. Hilo vile vile linanipa wasi wasi kwamba, kwa nini inakuwa hivyo. Sisi, tumeitendea Serikali hii dhambi gani isiyofutika?

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwengine ambao ni mdogo kabisa, jana nilichangia kwa maandishi hoja ya Wizara ya Nishati na Madini, lakini, hata jina langu halikusomwa. Sasa, hata nashangaa sijui kwa nini, wengine wote wamesomwa lakini mimi sikusomwa! Najua kabisa inawezana kwamba, pengine alipitiwa, lakini ndio kupitiwa huko huko, ndio huko huko kupitiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo, naomba sasa niende kwenye matatizo halisi ya kielimu katika Wilaya yangu ya Chunya. Hadi Aprili, 2006, Wilaya ya Chunya ilikuwa na Sekondari nne tu. Wilaya ambayo imeanzishwa mwaka 1942, lakini Sekondari za Serikali ni nne tu. Bahati nzuri, Mheshimiwa Waziri Mkuu, baada ya kutusukuma sukuma hapa na baada ya kuisukuma Serikali, tumeongeza sasa Sekondari nne. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa jitihada hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kwa sababu tumeona, tunaamini kabisa kwamba ni elimu tu ndiyo itakayotuletea mabadiliko. Chunya ni Wilaya lakini ina Wabunge wawili.

Tumeamua mimi na Mbunge mwenzangu wa Jimbo la Lupa kwamba, tuwe na mshikamano ili tuweze angalau kuleta mabadiliko pasipo tofauti, kusema kwamba, Jimbo hili ama Jimbo lile. Namwomba Mwenyezi Mungu, atuongezee nguvu ili tuweze kukamilisha hayo malengo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo, kuna kero mbali mbali ambazo walimu katika Wilaya yangu wanazipata. Kama ilivyo Wilaya yangu jinsi ilivyo, ukweli kabisa ni kwamba, kuna shule nyingine ambazo kutoka Makao Makuu ya Wilaya ni kilometra 200. Sasa tatizo linalowapata hawa ndugu zangu walimu ambao ndio tunawategemea kwamba, watatutengenezea viongozi wa kesho. Kwanza kabisa ni kero ya kufuata mishahara. Mwalimu anatoka Kambikatoto, kwa sababu ya miundombinu mibovu, anasafiri kwa muda wa siku tatu. Mwalimu anayetoka Namkukwe, anayetoka Ngwala, anasafiri kwa muda wa siku nne. Sasa, hizo siku nne ni kuja, lakini, kwenda vile vile anatumia siku nne. Siku nyingine hizi hatuzihesabu za kuhangaika kama mshahara umekuja ama haujaja. Kwa kweli hiyo ni kero ambayo ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri kwamba, labda tufike mahali, Serikali iamue, iweke *Mobile Bank*, ambayo itakuwa inatumika zile sehemu ambazo ni mbali zaidi na Makao Makuu, ambako ziko fedha zao. Ziweze kuwatembalea na kuwapa hiyo mishahara. Nafikiri kuna wakati fulani, nakumbuka miaka ya nyuma, kitu kama hicho kilikuwa kinafanyika. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba, Serikali ifikirie uwezekano huu kwa wale ambao wako mbali zaidi ya Makao Makuu, hii kero ya mishahara tunaweza tukaipunguza kwa kuwapelekea fedha huko waliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kero nyingine ambayo walimu wa eneo langu wamenitura, nayo inahusu Bima ya Taifa. Hawa ndugu zangu walimu, walishauriwa na Serikali wakashawishika, wakahamasika kwamba, kujiunga na Bima ya Taifa. Bima hizo nyingi zimeshaiva, toka mwaka 2005. Sasa tatizo, kila wanapokwenda kudai, wanaambiwa bado. Bahati nzuri na mimi mwenyewe nimefuatilia, lakini jibu nililopewa na Meneja wa Kanda yetu kule, amesema kwamba ni kweli fedha zilikuja, lakini tulilipa Wilaya chache, Wilaya ya Chunya ikawa kama ninavyosema, sijui ilisahaulika, lakini Wilaya ya Chunya, bado tunangojea hela.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa nafikiri kwamba, pengine Wizara ingechukua jukumu la kufuatilia hili suala ili wale walimu walipwe. Wanahangaika sana, mtu anajitolea, mshahara wake tunaujua jinsi ulivyo, lakini hata hiki kidogo ambacho anadai nacho vile vile anazungushwa. Nilikuwa nafikiri kwamba, Wizara ijaribu kuwasiliana na Wizara inayohusika ili tuwaondolee matatizo hao wenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine ambalo limezungumzwa hapa kwa kirefu sana, mimi nitalizungumza katika sura nyingine, wale walimu ambao wanakaa mbali zaidi wenye matatizo na hali ngumu ya kimaisha. Ninafikiri kwamba, Wizara ingefikira hao wawape motisha ya kuwaongezea kile kipato wanachokipata, wawape *endurance allowance*; ili wajisikie kwamba, kweli na wao wanatambuliwa. Kwa sababu inakuwa ni matatizo, mtu unampa pengine shilingi 160,000, kama kweli wanafikia hiyo,

lakini utaona kwamba, hiyo fedha ukitoa gharama za fedha na matumizi mengine, anarudi nyumbani na shilingi 60,000 tu, ambazo hazimsaidii hata kidogo. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri, pamoja na matatizo mengine, tungefikiri kwamba, pengine waongezewe kipato kidogo wanaokaa nje; mbona hawa *Rare Professionals* tunawapa? Kwa hiyo na hawa tuwa-treat vile vile kama wanaweza kuwa ni watu maalum, ambao wanapata matatizo na shida, ili tuweze kuwasaidia kwa njia hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi mojawapo ambayo tayari tunaifanya hivi sasa ni kuongeza shule za sekondari na kwetu kule tumechacharika kweli kweli. Hizo shule sasa hivi tayari tumeshaanza kuzimaliza na nyingine kama nilivyosema, hizo nne tumezimaliza. Tatizo linakuja, hawa watoto ambao mwaka huu ndiyo wako *Form One*, tunategemea kwamba, mwaka kesho watakuwa *Form Two*, tatizo ambalo ninaliona ni jinsi gani hawa wengine ambao watakuja *Form One*, watasomea wapi? Ninajua kabisa kwamba, bado tuna hamasa ile ile, tutahamasishwa na hasa zaidi watu watakao hamasishwa ni wananchi. Nguvu ya wananchi kwa kweli sasa hivi ni ndogo, haitoshi. Ninaiomba Serikali ifikirie angalau kuongeza nguvu katika kutoa ruzuku, ambayo inaweza ikasaidia kuongeza hayo madarasa mengine.

**MHE. GUIDO GOROGOLIO SIGONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii. Kwanza kabisa, naomba niunge hoja asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru Mungu, aliyenilinda hadi leo. Pili, napenda kumpongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundii na Naibu Mawaziri wake, kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Ninawapongeza sana, kusema kweli wanajitahidi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina masikitiko makubwa sana katika Mkoa wangu wa Rukwa, una matatizo ya uhaba wa walimu. Mkoa wa Rukwa, walimu hawaendi kabisa. Nashangaa ni kitu gani ambacho wanakiogopa kule. Mkoa wa Rukwa ni watu wakarimu sana, wana upendo mkubwa sana, lakini mtu akipangiwa kazi anakataa kwenda! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe wito kwa walimu wanaopangia Mkoa wa Rukwa, waje, sisi watu wa Mkoa wa Rukwa ni wakarimu sana. Ule uchawi haupo. Watu wengi wanasema Rukwa kuna uchawi, hakuna. Naomba mje Rukwa, mfundishe watoto wetu hawana elimu. Elimu kila siku Mkoa wa Rukwa iko duni. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe masikitiko ya shule za msingi, walimu wa shule za msingi wana matatizo makubwa sana. Mtu anakaa Ilunde, kutoka Ilunde mpaka Mpanda Mjini ni mbali, anaweza kutembea siku mbili anaifuata mshahara. Akifika

Mjini Mpanda, anakaa siku tano, sita au saba, akisubiri mshahara, madai au akisubiri posho. Hao watoto waliobaki Ilinde, anawafundisha nani? Ni matatizo kwa shule za msingi. Walimu wanapata tabu mno. Walimu wa wakifika Wilayani wanasumbuliwa kwa kila kitu, chochote ambacho wanakuja kudai Wilayani ni lazima watumie siku saba, nane au wiki mbili. Je, wanafunzi huko vijijini nani anawafundisha? Watoto kila siku tunasema elimu yao ni duni, walimu wanapata matatizo Wilayani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Afisa Elimu anaamua lolote atakalofanya yeze ili mwalimu yule amnyanyase pale Wilayani; tutafika kweli? Hatuwezi kufika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja upande wa shule za sekondari. Mkoa wa Rukwa tuna matatizo yote, upande wa shule za sekondari, ndio kabisa Walimu hawataki kuja. Kama safari hii tumepangiwa na Wizara Walimu 47, sasa hivi tumepiga simu wamefika walimu watatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi Mkoa wa Rukwa watu wanauonaje? Wanaishi binadamu na vile vile sisi tunahitaji kufundishwa, watoto wetu wanahitaji elimu. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Serikali ichukue mikakati ya kuwapeleka walimu Mkoa wa Rukwa, maana yake tunasema kila siku walimu hawapo, wakati walimu wapo. Utakuta pale Wizarani wanaenda kwa Mkurugenzi wa Sekondari, kila mtu ana *bargain* kuomba *transfer*, akipewa *transfer* kwenda Rukwa, anaanza kusema mimi nina matatizo ya moyo, nikienda Rukwa nitafanya hivi, ili asiende Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba Serikali iweke mikakati mizuri ili walimu wakipangiwa kila sehemu, wafike mahali walikopangiwa. *lobbying* zimezidi, hatutafika, tutakuwa tunasema Mikoa ya pembezoni hakuna elimu, elimu ipo lakini walimu hatupati na kwa hiyo, hatupati elimu nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nzungumzie Elimu ya Watu Wazima. Naipongeza sana Serikali, mwaka 2005 kulikuwa kuna Mpango wa MEMKWA, kulikuwa kuna walimu ambao walichukuliwa wa Darasa la Saba wakapewa Kozi za Wiki mbili, tatu, ili kwenda vijijini kufundihsa watu wasiojua kusoma na kuandika. Wale walimu wa MEMKWA wamefanya kazi nzuri sana, kuna sehemu ambayo watu walikuwa hawajui kusoma na kuandika, wakaweza kusoma na kuandika. Lakini masikitiko makubwa, wale walimu hawajaliwi. Mshahara ni shilingi 20,000, hiyo shilingi 20,000 anapata baada ya miezi mitatu; aaishije Mwalimu huyo? Ukikuta sehemu nyingine walimu wengine wametoka vijijini kuja kuchukua mishahara yao, mwalimu wa MEMKWA anaingia madarasani kufundisha. Leo hii mwalimu wa MEMKWA hana thamani. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Serikali iwafikirie walimu wa MEMKWA, waweze kulipwa hata ile shilingi 20,000, lakini kila mwezi wapewe haki yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja upande wa Walemavu, shule za viziwi ni chache mno, wanasubiri kila siku kuandikishwa shule. Shule za wasioona, vifaa vya

kufundishia havitoshi, walimu hakuna. Ninaomba Serikali ifanye mikakati mizuri ili waweze kutafuta walimu wa walemavu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie walimu wapya kucheleweshewa mishahara yao. Waheshimiwa Wabunge wengi sana, wamelalamika kutokana na walimu kucheleweshewa mishahara. Kusema kweli inasikitisha, utakuta mwalimu anakaa miezi minane, miezi kumi, mwaka, hana kitanda, godoro, shuka wala sufuria ya kuanzia maisha. Mshahara hajapata miezi kumi. Huyo mwalimu ataishije? Halafu unakuta walimu wanaoajiriwa katika shule, wanakuwa wasichana wadogo au wavulana wadogo, ambao hawajaanza hata maisha. Ninaomba Serikali, ijitahidi walimu wapya wanaoanza wawatayarishie mazingira mazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Mitihani wanafuta matokeo au kufungia matokeo bila sababu za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila Wilaya na Mkoa kuna wakaguzi wa shule za msingi, lakini mimi sijui Wakaguzi wanafanya kazi gani. Maana yake Wakaguzi Wilayani wapo, lakini matatizo ya shule ni mengi. Unakuta sehemu shule ina mwalimu mmoja au wawili na Mkaguzi yupo. Shule mbovu, sasa sijui nani anayetakiwa aende kuripoti Wizarani, si Mkaguzi, lakini Mkaguzi anakaa Wilayani na Mkoani, haendi kukagua shule! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Wizara ifuatilie Wakaguzi waweze kufanya kazi zao ili shule ziweze kuboreka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniruhusu nami nichangie hoja iliyo mbele yetu. Nashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu, kwa kazi nzuri anayoifanya. Mimi nimefanya naye kazi karibu kabla hajawa Waziri, alikuwa Mwenyekiti wetu wa Chama cha Walimu, alifanya kazi nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna imani kubwa sana naye katika nafasi hii aliyonayo, tunadhani mambo mengi anayafahamu. Kwa kweli anafanya kazi nzuri, usahahidi ni kitabu alichokitoa hiki, ni kizuri sana, nadhani ni kwa sababu ya watumishi wazuri vile vile nao. Nampongeza kwa hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda vile vile nimpongeze Mheshimiwa Samuel J. Sitta, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kumshauri na kumwelekeza ndugu yetu. Huwezi ukafanikisha kama nyumbani una matatizo. Anafanikisha tangu awali, tangu mimi nilipoanza kumfahamu akiwa Mwenyekiti wetu wa Chama cha Walimu, nilikuwa najiuliza huyu mama akili nyingi anazitoa wapi. Sasa, nimekuja kulinganisha na Spika,

nikaona hawa watu wanarandana. Mambo ni mazuri sana. Kwa hiyo, nyumbani kuna ushauri mzuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Samuel J. Sitta kwa kazi nzuri anayoifanya, kama hayupo basi nafikiri atapata taarifa. Kumbe yupo, afadhali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitaka kuona nchi inavyokwenda, nidhamu ya nchi, utendaji wa nchi, utekelezaji wa mambo yote katika nchi, maendeleo katika nchi, ni kwa sababu ya elimu yake. Kwa hiyo, tunalolizungumzia leo ni suala nyeti na zito.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niishukuru Serikali kwa kazi ambayo imekuwa ikiifanya na inaendelea kuifanya, kwa kujaribu kuangalia mazingira magumu ya utendaji kazi hasa walimu. Tumepewa majengo, madarasa na leo asubuhi walikuwa wnazungumzia kuimarisha barabara. Lakini, nadhani kuna kitu ambacho tunajaribu kukisahau, kwa hao watendaji kazi amba ni walimu, tunapozungumzia kuimarisha au kuongeza motisha, tunasahau marupurupu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kuna Tume imeundwa na Rais. Nadhani itajaribu kuangalia, katika mazingira kuna mambo ambayo yanaweza kuwa-*solved* kwa kuwapa motisha, kuwaongezea posho labda wanaokwenda kwenye mazingira magumu au kwenye shule ambayo ina wanafunzi wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa huyu mwalimu mwenye kazi kubwa zaidi, afikiriwe kupewa kwa sababu ya kufanya kazi mara mbili, apewe posho zaidi. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri kwamba, tuanze kufikiria hilo, tusiangalie mshahara tu. Mshahara wote ni *flat rate*, kama ni wa Sumbawanga, anapata ule ule, wa Mtware ule ule, wa Mwanza ule ule, wa Dar es salaam ule ule, aliye na tai ule ule, mwenye magari ule ule. Sasa, inaonekana kwamba, nisipoenda huku afadhali niende huku, kama mambo ni yale yale. Lakini kama anaenda Sumbawanga, anaenda Geita, ambako kuna shida, ukamwongezea kidogo, watu watapenda kwenda kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri, tulikuwa wote kwenye matatizo haya, mpaka tumeweza kuunda Tume ya kuweza kuangalia matatizo ya walimu, nafikiri katika hili ataliangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ninataka kuzungumzia ni suala la madaraka katika shule au katika Vyuo. Nadhani tuna haja ya kutuma wajumbe waende Kenya kujifunza, wenzetu kuna taratibu wanazozifanya. Mwalimu Mkuu ana *allowance* yake, *Headmaster allowance* yake, *Principal* ana *allowance* yake, *Director* ana *allowance* yake na wanafuata hivyo. Sasa sisi kwetu hapa, *Principal* aliyepata u-*principal* mwaka 1982 mpaka leo ni *Principal* yule yule, hataki kuhamishwa, ni yule yule. Kenya sivyo, *you can be a Director in a Class Room*, unaweza ukapanda cheo ukiwa darasani, unaenda unaongezea. Sasa ukimtoa *Principal* wa Mpwapwa ukamhamisha kwa kumwadhibu kumpeleka kuwa *Principal* Butimba na akaendelea kuwa hivyo hivyo, hiyo nadhani kuna haja ya kuangalia. Tumekuwa tukilizungumza tangu nafikiri kipindi kilichopita, Serikali inasema tunaangalia marupurupu yao, lakini kuna haja ya kuangalia *Headmaster* apate nini. Wote ni sawa sawa, ni wale wale.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilipokuwa mwalimu, kuna mzee mmoja aliandika balskeli yake hivi: “utazunguka mabucha yote lakini nyama ni ile ile,” akiwa na maana unaenda kusoma, utapata elimu, lakini wote tunalingana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ni vyema kuangalia mishahara ya watu hawa, wanavyo tofautiana kulingana na *seniority*. Ukiangalia *gap* ya walimu katika mshahara ni ndogo sana, wakati mwininge wanalingana. Mtu aliyeanza mwaka 2004 na aliyeanza zamani mwenye miaka 10, utakuta *difference* ni kidogo mno. Nadhani tuangalie hili suala la mishahara ya walimu na kuweza kuangalia inakwendaje.

Tujaribu kuangalia kama mashirika. Walimu tuwalinganishe, si kwamba wafikie ile ya *SUMATRA* au *TAZARA*, lakini utakuta wanafanya kazi, wanaenda kwenye soko lile lile ambalo watu wenyewe mshahara mkubwa wanaenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tujaribu kuangalia, tuwasukume kidogo. Hao walimu wanahitaji kuishi, siyo kwamba wahitaji kushi kwenye nyumba ile ya Serikali, watastaafu na wanatakiwa waende kwao, nao wakutwe na nyumba. Sasa, tuangalie hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuzungumzia suala la michezo. Naona ameandika vizuri, nilitaka tuhujiane kwenye vifungu, sasa sitamuhoji, lakini tunangoja hiyo mikakati.

Bajeti bado ipo na nina amini Mungu ataniweka nitakuuliza. Mimi ni mgonjwa wa michezo, naeleza hivyo kwa sababu michezo kwa wanafunzi ndio uhai na ndio maisha. Michezo ni dawa ya UKIMWI, Michezo ni ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sisi tutakuwa tunaona wenzetu, hivi Mheshimiwa Joel N. Bendera sjui kama yupo? Hivi Waziri wa Michezo, atapata wachezaji kama siyo vijana walio mashulenii na Vyuo Vikuu? Atapata wachezaji kutoka kariakoo, wale wavuta mirungi na bangi, hatutafika popote.

Tunatakiwa tuwapate hawa na katika hilo nilikuwa nazungumza na viongozi wa Wizara kuhusu Chuo cha Butimba, waangalie kwa nini kumekuwa na *enrolment* ndogo katika fani maalum. Fani ya muziki, fani ya sanaa ya ufundi, fani ya sanaa za maonesho na fani ya michezo, waangalie namna gani kuwe na *full enrolment*, siyo darasa liwe na wanafunzi wawili. Naomba hilo wakaliangalie. Michezo ni muhimu, sasa hivi tunapenda kuelewa mkakati huo ukoje, tunangojea mpaka mwaka kesho, bado muda mfupi tu, tukimaliza bajeti hii tunaanza mambo ya bajeti nyingine. (*Makofi*)

Lingine mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, nilikuwa napenda nizungumzie jengo la Baraza la Mitihani. Lile jengo litatuokoa kuondoa uvujaji, kupunguza gharama na limeshaanza limeshafikia kiwango kikubwa. Sasa kinachonisikitisha, nilikuwa naangalia kwenye kitabu hapa kwenye bajeti kitabu cha maendeleo sioni, ingawa tumeambiwa kwamba, kuna kukamilisha; mtakamilishaje kwa hewa? Naomba wakati wa vifungu, mtuambie hizi hela ni ngapi zitakazokwenda pale,

mtalikamilishaje kulijenga? Jengo lile ni zuri hata kama lilipoanzishwa kulikuwa na mgogoro fulani, lakini likamilisheni. Fedha za Serikali mabilioni yameshaenda pale, tuhakikishe linakamilika na linafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisije nikalisha pua, nikasahau mdomo, sasa nakwenda Wilaya ya Geita. Serikali tangu MMEM imeanza, ilitangaza mbele ya Bunge hili, wananchi wajitolee na yenyewe itamalizia kufanyakazi. Sisi na *DC* wetu na Mkurugenzi wetu, tukalala vijiji, wananchi hakuna, tukakamata kuku, tukakamata ng'ombe, watu wakafirisika tuhakikisha mabomba yanafikia angalau zaidi ya *renter* Serikali imalizie. Sasa imekuja zamu ya Serikali, hatuelewi kulitokea nini, Mawaziri wote waliokuja kule walikuwa wanakuta kilio cha maboma. Hata Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, alipokuja kuzunguka alikuta vilio vitatu; cha maji, Barabara ya Usagala kwenda Geita na Maboma na akasema vizuri, Maboma tunawahakikishia ndugu zetu wana-Geita, tuwe pamoja yatakamilishwa. (*Makofi*)

Sasa juzi Mheshimiwa sijui alipitiwa kidogo, akasema labda mliyajenga vibaya, mwenzangu amesema nisingependa kusema lakini sitaki niende huko. Naomba jitihada za makusudi za Wizara, hebu tuunge nguvu wananchi wa Geita, tunawakatisha tamaa, Serikali yetu ni nzuri mno na ninaomba muelewe viongozi wetu, basi katika ahadi za Rais alizozitoa, tuliondoe hilo haraka. Tenga fedha, najua kuna fedha inapelekwa kidogo kidogo, shilingi milioni mbili na kadhaika, zinapelekwa kule lakini hazitamaliza ile kazi ambayo imeachwa. Sasa hivi kwetu Wabunge wa Geita, pamoja na Viongozi wa Geita ni tabu, tunashindwa kufanya maendeleo kwa sababu ya maboma haya. Naomba tena Mheshimiwa Waziri, katika majibu yake, hebu jaribu kusema, angalia mahesabu yako, toa mahali popote pale, hii ni dharura, yakibomoka ni aibu kwa Serikali yetu. Toa mahali popote, tupeleke fedha kule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Mheshimiwa Waziri Mkuu, ndiye mkombozi wa matatizo haya yanapotokea, uliwha kutukomboa kwenye tatizo la barabara, hebu tukomboe katika hili, kama hawaelewi waeleweshwe, sisi elimu kwetu ni muhimu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, unam-*address* Spika.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniongoza, lakini huyu ndiye anayegawa mafungu. Naomba Wizara, iwe angalifu katika kupanga mipango yake. Mimi ni mwalimu, mwaka 1998 tulikuwa kwenye mkutano na washauri, kulikuwa na mtu anayeitwa Peter Williams, tulikaa Arusha tukapanga namna gani vyuo vya ualimu vipunguzwe. Walimu wanatosha kila mahali, ushahidi upo Wizarani pale, vyuo vingine vikaondolewa vikawa Shule za Sekondari na vingine vikawa *FDC*, vikapungua. Lakini mimi nikiwepo kwenye *field*, kinachozungumzwa sikielewi, leo hii tunalia tuna matatizo hayo. Sasa naomba Wizara, pamoja na umaskini wetu, *consultancy* hizi tuziangalie sana, zitatufikisha mahali pabaya. Tunaambiwa juzi tayari imebadilika, labda inawezekana ni ushauri, keshokutwa utaambiwa sasa hivi teremsha au fanya hivi. Kwa hiyo, mimi naomba sana, *consultancy* tuziangalie sana. Narudia tena kwenye mdomo, Mheshimiwa Waziri sisi tumejenga shule zaidi ya 33, kila Kata sasa hivi ina sekondari. (*Makofi*)

Lakini tumefikia mahali, tuna tatizo, sekondari zetu hazina umeme. Ulimwengu wa sasa lazima mtoto ajifunze kompyuta. Tulipokuwa kwenye Kamati tunaelekezwa elimu ya juu, walituambia atakayepata mikopo ni yule aliyepata *division one and two form six* kwa *science* na *arts*, ndiyo watakaofikiwa hao. Lakini vile vile kuna kipengele kinasema kwamba, wataangalia watoto wa maskini. Sasa sielewi hiyo *mini-testing*, sijui itaangalia vipi kwamba, huyu hakudanganya kwa sababu *mini-testing* haiangalii hilo. Tena ninachotaka kusema ni kwamba, tunaomba *at least* kila shule tupatiwe *generator* na kompyuta, vijana wetu waweze ku-*compete* kwa *approach* hiyo. Maana yake shule zote za nje za Dar es Salaam, Arusha na Mwanza, hawatapata mkopo, mtashangaa tunaelimisha watu wale wale wenye uwezo, tunaacha wengine ambao wamesoma shule hizi za kusuasua na wana uwezo mzuri. Kwa hiyo, naomba mtusaidie ambao tumefikia hatua ile na nchi nzima tujaribu kusaidia hapo tulipofikia, wananchi wakishafungua shule mlete walimu, tujaribu kufanya mikakati ya kuweza kuwasaidia angalau vijana wetu wawe wanaelewa hii ni kompyuta. Vijana wetu wakitoka wakienda kule wanasema hii labda ni redio hawaelewi, bila kompyuta ataajiriwa wapi au anaona mtungi? (*Makofi*)

Kwa hiyo, ndugu zangu mimi nawapongeza kwa kazi nzuri mnayoifanya, jaribuni kutufikiria na kutusaidia Wilaya ya Geita. Katika hizo shule 33 hazina magari. Nawashukuru kwanza walishaniahidi kwamba, watanipa gari la ukaguzi, sitaki kuzungumzia nikaharibu mambo, najua hiyo ipo. Lakini shule za sekondari 33 hazina magari. Sasa kwa magari tunayowapelekea shule za sekondari, walete basi kwenye hizo shule 33, *wata-share* hata *headmasters* tunaomba walau gari moja kwa ajili ya *ku-coordinate* shule zote za sekondari, ambayo itakuwa inazunguka angalau inasaidia ikitokea mgonjwa, likitokea tatizo litusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, napenda nikushukuru sana. Naunga mkono hoja hii, naomba Mheshimiwa Waziri aende kuangalia maboma yetu. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia machache katika hotuba hii ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundii. Nianze kwa kumpongeza sana ndugu yangu, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundii, Mheshimiwa Margareth S. Sitta, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, vile vile niwapongeze wakurugenzi walio chini yao na wasaidizi wote, kwa kazi nzuri sana wanayoifanya ya kuendeleza na kuboresha elimu katika nchi yetu. (*Makofi*)

Lakini vile vile niwapongeze sana walimu wenzangu, kwa kazi kubwa wanayoifanya katika maeneo mbalimbali hapa nchini, ukianzia katika shule za awali, za msingi, sekondari vyuo na kadhalika. Kwa kweli kazi ya ualimu kama tunavyofahamu sisi wote, ni kazi nzito lakini hawa wanafanya kazi kwa bidii, kwa niaba ya sisi wote katika kuandaa Taifa letu la kesho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nisije baadaye nikasahau na mimi naunga mkono hoja moja kwa moja. Katika mchango wangu nitapenda nijielekeze zaidi katika Idara ya Elimu ya Sekondari. Nianze na suala la walimu. Napenda nitoe pongezi kubwa sana kwa

Wizara, kwa kuandaa mipango mahususi katika kipindi hiki cha 2006/2007 katika kujenga uwezo wa kupata walimu, ambao wataziba pengo kubwa na watapunguza tatizo kubwa la walimu lililopo katika shule zetu hasa za sekondari. Naamini kabisa kila Mheshimiwa Mbunge, ambaye atasimama na ambaye hatapata nafasi ya kusimama, lazima atalalamikia tatizo la upungufu wa walimu na hili si siri hata kidogo. (*Makof*)

Kutakuwa na utaratibu wa kufundisha walimu katika mpango wa muda mfupi na vile vile mpango wa muda mrefu. Sasa nigosie huu mpango wa muda mfupi, ambao Mheshimiwa Waziri ameugusia katika hotuba yake. Kwamba, mpaka hivi sasa tunavyozungumza hapa kuna walimu ambao wako mafunzoni na watapata mafunzo yao kwa muda wa mwezi mmoja tu na baadaye watakwendwa mashulenii kufundisha. Mimi sina tatizo na hilo, nakubaliana na mpango mzima, lakini ningependa kutoa tahadhari kidogo kwanza, mwezi mmoja wote tunaamini kabisa ni muda mfupi sana. Kwa sisi wengine ambao ni walimu, tunajua kabisa kwamba, ili uwe mwalimu walau kwa kiwango cha chini sana, unahitaji miaka miwili ili uweze kupata taaluma, lakini vile vile uweze kupata utaalam si chini ya miaka miwili, mwezi mmoja hautoshi.

Wizara imeandaa utaratibu kwamba, watawaunganisha vijana hawa na Chuo Kikuu Huria ili waweze kupata *degree* wakiwa kazini. Ni sawa watapata taaluma vizuri sana, lakini je, utalaam itakuwaje? Vile vile nihoji kwamba, je, walimu ambao watapangwa katika maeneo ya mbali, kuna maeneo kama Ludewa, Ukisi, Kamsamba au nichukue Lufilyo huko au Kyela, hawa watapataje kwa usahihi kabisa elimu hii ya Chuo Kikuu? Kwa sababu watakuwa wamesambaa katika maeneo mbalimbali, ambayo yana mahitaji ya walimu. Msifikiri hawa watapangwa mijini tu, watapangwa kwenye maeneo ambayo yana mahitaji ya walimu, ambayo ni mengi sana. (*Makof*)

Sasa kwa ushauri wangu, pamoja na mpango huu mzuri, ambao mimi nakubaliana nao. Ningeshauri kwamba, labda ungeandaliwa utaratibu, si lazima kwa mwaka huu, lakini utaratibu maalum ambao walimu hawa wataendelea kupata mafunzo kazini, jinsi ya ya kuwa walimu, yaani wafundishwe *skills and methodology* yote ya ualimu, wakiwa kazini. Kwa maana kwamba, wanaweza wakawekwa katika maeneo ambayo pengine ni yale ambayo yanatumika na shule za msingi, *resource centres* katika maeneo mbalimbali. Kuna *resource centres* ambazo ni za walimu wa shule za msingi, nao wangkusanywa kwa kutumia walimu wa vyuo au kwa kutumia wakaguzi, wakaendelea kufundishwa *methodology* ya namna ya kuwa walimu. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumepata walimu ambao watatoa elimu iliyo bora. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka nilizungumzie ni suala la malengo ambayo yamewekwa katika kipindi cha mwaka 2006/2007, hususan majengo. Wizara kwa kusaidiana na nguvu za wananchi, itajenga majengo mbalimbali, ambayo mimi nakubaliana nayo. Majengo kama madarasa watajenga, vile vile nyumba za walimu, jambo ambalo kila mmoja hapa ana kilio juu ya nyumba za walimu. Lakini vile vile watajenga maabara 40. Sasa labda nizungumzie kidogo kuhusu suala hili la maabara 40. Ni kweli kabisa kama wengine walivyozungumza, sayansi yoyote ile huwezi ukaikamilisha bila kazi za vitendo, haiwezekani kabisa. Kwa hiyo, ni muhimu sana kuliangalia suala hili kwa undani zaidi kwamba, tujenge maabara za kutosha katika hizi

shule. Ujenzi wa shule za sekondari tunaokwenda nao sasa, lazima uende sambamba na ujenzi wa maabara, ingawa kwa kweli maabara ni gharama. Lakini kwa makusudi kabisa, ni lazima tuamue kujenga maabara, la sivyo tutatoa watoto waliojaa nadharia tupu. Ninaomba hili liangaliwe. (*Makofi*)

Pamoja na hilo ni kweli kwamba, hatuna fedha za kutosha lakini zipo maabara ambazo zilikuwa zimeshaanzishwa huko nyuma na hazijakamilika, kwa mfano, Mkoa wa Mbeya niliwahi kutembelea shule zifuatazo; nilitembelea Shule ya Sekondari Ndalambo Wilaya ya Mbozi, Vwawa Wilaya ya Mbozi, Lufilyo Wilaya ya Rungwe, *Tukuyu Day* Wilaya ya Rungwe, *Kyela Day* Wilaya ya Kyela, Kiwanja Wilaya ya Chunya, huko kuna majengo ya maabara ambayo yalishaanza lakini si maabara hayajakamilika. Kwa hiyo, ninaomba Wizara itakapokuwa inatoa fedha hii, itoe maelekezo kwa Mikoa kwamba, *priority* namba moja iende kwenye maabara ambazo zilishaanza kujengwa na wananchi, ndipo hela hizi zitakapotolewa sasa ziweze kukamilisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majengo haya yaliyotajwa, lakini naomba nitaje na majengo mengine muhimu, ambayo pengine hayakutajwa katika hotuba hii, labda sikusoma vizuri. Ninaomba sana Wizara iangalie kwa undani na iyaangalie kwa umuhimu wake wa hali ya juu, nayo ni majengo kama hosteli kwa ajili ya watoto wa kike. Ujenzi wa hosteli kwa watoto wa kike ni muhimu sana. Wazazi kuanzia sasa wahamasishwe katika shule zote za kutwa kwamba, hebu jaribuni kuangalia uwezekano wa kujenga hosteli kwa ajili ya watoto wa kike. Tuanzie na watoto wa kike, tuwape *priority* kubwa katika elimu ya sekondari, hasa katika *day schools*, ni watoto wa kike ambao wanatembea kwa muda mrefu kutoka majumbani kwao. Kwa hiyo, hili suala la hosteli, ninaomba sana Wizara iliangalie kwa jicho la uzito kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuzungumzia suala la maktaba. Shule zetu hazina maktaba, wananchi wetu hawana utamaduni wa kujenga maktaba, kwa sababu hata sisi wenyewe hatuna utamaduni wa kusoma. Kwa hiyo, suala la maktaba, watu wanaona ni kama jengo labda la ziada. Lakini ukweli ni kwamba, maktaba ni jengo moja muhimu sana katika shule, kwa sababu kama hivi tunavyoona hapa, kuna uhaba wa walimu, kuna walimu wengine pengine hawana taaluma ya kutosha, wanapo-deliver basi mtoto ukombozi wake ni kukimbilia maktaba. Kwa hiyo, ninaomba sana tena sana, suala la maktaba lazima litiliwe mkazo sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo ninapenda pia niungane mkono na wenzangu ni kwamba, tunaipongeza sana Wizara kwa kutilia mkazo elimu ya ufundi. Tunaomba ipewe umuhimu mkubwa, kwa sababu tunaelewa wazi kabisa kwamba, kuna vijana wengi zaidi ya asilimia 50, ambao watamaliza *form four* hawaendi *form five*, watakimbilia wapi? Ni lazima wakimbilia kwenye maeneo ambayo wana ufundi nayo. Kwa hiyo, kuna haja kabisa, kama wenzangu walivyosema, nafikiri Mheshimiwa William H. Shellukindo, alilisema kwa uzito asubuhi kwamba, badala ya kujiimarisha kwenye kanda, najua kwamba, kwenye mipango ijayo tutaendelea mpaka kwenye maeneo ya Mikoa na pengine na Wilaya.

Lakini vile vile tuangalie huko huko kwenye shule za sekondari, tuangalie yale maeneo zamani tulikuwa tunasema michepuo, kwa nini tusiangularie michepuo tukaweka huko ufundi katika baadhi ya shule tuwe tunakwenda hivyo?

Kwa sababu hatuwezi kuwaacha hawa wanafunzi wasipate elimu yoyote. Huko watajifunza mambo ya *agriculture*, ufundi mdogo mdogo wa kutengeneza magari, kutengeneza mambo madogo madogo ambayo yatawasaidia. Lakini vile vile watajifunza elimu, ujuzi na *skills* za namna ya kutunza mazingira. Kwa hiyo, wakitoka pale, watakwenda katika maeneo yao nyumbani, wataanza maisha kwa njia ambayo ni ya uhakika, badala ya kuzunguka tu bila kuelewa wanachofanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango ambayo imewekwa na Wizara ni mizuri kabisa na ninaamini kabisa, watafanya kazi vizuri na mimi nitoe siri moja, nilishamtakia heri nilimtabiria Mheshimiwa Margreth S. Sitta, nikasema wewe utakuwa Waziri, tena Waziri wa Elimu na ikatokea. Mimi nazidi kumwombea katika kazi yake, afanye kazi vizuri, inaonesha kwamba, ana watalaam wazuri sana wa kumsaidia. Dalili hiyo tunaiona, wataalam ambao amepewa kufanya nao kazi ni wataalam wazuri kabisa na watamsaidia na *inshallah* kwa kweli elimu yetu itaboreka na Mwenyezi Mungu, atatusaidia kabisa. Tanzania itasonga mbele katika elimu, tuweze kuondokana na umaskini ambao umebobea kwa sababu watu wengi ni wajinga, hawana elimu ya kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nianze kwa kupongeza kama walivyofanya wenzangu. Hotuba aliyoitoa Mheshimiwa Waziri wa Elimu ni nzuri, imechapishwa vizuri na imesomwa vizuri. Katika speed na *standards*, hakutegemea jambo pungufu kuliko hilo, tunakupongeza sana kwa hii kazi nzuri sana na tunawapongeza wasaidizi wako wote waliokusaidia kuandaa *speech* hii. Hiki kwetu ni kitabu cha rejea, tutasoma mwaka mzima, tukifutilia utekelezaji wa haya mambo mazuri yaliyoelezwa humu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitazungumzia zaidi matatizo ya Dar es Salaam. Baada ya ile semina tulioifanya Ubungo Plaza, Mheshimiwa Waziri Mkuu alitukutanisha, akatusukuma kidogo, maana wanafunzi 17,000 walikuwa wamefaulu, kati yao 4,000 tu ndiyo walikuwa wanachukuliwa. Ikafanyika kazi moja kubwa sana, iliyowezesha wanafunzi wengine karibu 7,000 wakachukuliwa kwenda sekondari. Naomba nishukuru na kupongeza juhudi hizo, japokuwa Wabunge wa Dar es Salaam walilaumiwa kwamba, walishtaki lakini nafikiri fitina za maendeleo ni nzuri. Tutaendelea kusukuma hivyo ili tuendelee kupata maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Wizara, kwa kazi nzuri iliyofanyika. Halmashauri zetu nazipongeza kwa jinsi zilivyo-*respond* haraka, tukaweza kuwachukua watoto hawa. Lakini mafanikio tulioyopata ndiyo chanzo cha matatizo, maana huko mwanzo elimu ya msingi tulikuwa nyuma sana. Nakumbuka mwaka 1997 tulikuwa na shule 60 wakati tulipokuwa tunahitaji shule 600, lakini katika miaka hii mitano, katika

jimbo langu peke yake zimeongezeka shule 30. Tunashukuru sana kwamba, elimu ya msingi sasa inaanza kuendelezwa na watoto wanaanza kupata nafasi za kusoma. Lakini tumeanza miaka hii miwili, kwa hiyo, tunahitaji kuendelea kila mwaka, tukiongeza vyumba vya madarasa pamoja na huduma nyingine zinazohitajika kama vyoo, madawati, vitabu vya kusomea, nyumba za walimu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahi sana kuona Mpango wa MMEM unaendelea na kwamba, umeandaliwa utakaotupeleka mpaka mwaka 2011, maana usipoendelea ndio tumekwama tena. Sisi Dar es Salaam, kuna maeneo mpaka sasa hakuna shule ya msingi. Pale Kibo, ukipandisha kutoka Ubungo mkono wa kushoto hakuna shule ya msingi. Sasa nafikiria wale watoto wakivuka barabara kwenda ng'ambo ili waende Msewe kwenye shule za msingi zilizoko kule, ni hatari tupu. Hata maeneo ya kujenga hatuna, ni matatizo maalum ya Dar es Salaam. Mwenzangu wa Ngara anasema sisi tuna nafuu, angekuwa Kinondoni angejua jinsi tulivyopungukiwa na huu unafuu na yeze alivyo na unafuu mkubwa kule kwake.

Tuna matatizo makubwa sana kule Dar es Salaam ya Elimu ya Msingi, Elimu ya Awali na Elimu ya Ssekondari. Naomba tunapogawa hizi rasilimali kidogo zinazopatikana, tufikirie mazingira maalum ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu za Dar es Salaam wakati mwingine watu hawazijui, zinatisha. Kabla ya huu msukumo kuanza, tulikuwa na Shule za Sekondari za Serikali 21 tu, huu msukumo umetupa shule nyingine 29, sasa tuna shule za sekondari 50. Ninaishukuru Serikali, kwa hii kazi nzuri sana iliyofanyika. (*Makofii*)

Lakini nilikuwa namsikiliza rafiki yangu Mheshimiwa Capt. George H. Mkuchika, anazungumzia shule 64 za sekondari kule kwake peke yake, sasa hivi akipata walimu watoto wanajaa katika shule zile na wanasona bila matatizo. Sisi za Serikali tunazo 50 kwa Mkoaa wa Dar es Salaam, siyo kwa jimbo la Ubungo, maana tunahitaji kwa jimbo la Ubungo. Lakini kwa Mkoaa wa Dar es Salaam tuna shule 50 tu. Ndiyo maana inanibidi nishukuru sana watu walioanzisha shule za binafsi. Bila hao, sisi watu wa Dar es Salaam tungekuwa hatujui kusoma na kuandika. Bahati nzuri, tuna shule za watu binafsi 102 katika Mkoaa wa Dar es Salaam, watoto wetu wengi wanasona katika shule za watu binafsi siyo shule za Serikali, maana za Serikali ni chache sana. Baadhi ya shule hizi ni nzuri kabisa. Shule kama *Johan Girls Secondary School, Mbezi Secondary School, Nsigani Secondary School*, shule ambazo zimejengwa vizuri na ambaa wanaoziedesha, wanaziendesha kwa umakini kuhakikisha kwamba, zinatoa elimu nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachowaomba ni kuzingatia yale maombi ya Rais, aliyowaomba kwamba, waangalie hili suala la ada, maana ada zenyewe zinaweza zikawa juu, kiasi ambacho wanaomudu ni wale tu wenye nafuu, ambaa wanaweza kwenda kwingine. Lakini tunashukuru sana, kwa hii kazi nzuri wanayoifanya ya kutusaidia kupunguza hili tatizo la maeneo ya kusomea. Bila shule hizi za watu binafsi, tungepata matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu wa 2006, zile shule tulizozianzisha zote, tulianzisha vyumba vinne, zinahitaji vyumba vingine vingine mwaka huu, ili watoto wale waende kidato cha pili. Mwaka kesho vitahitajika tena vyumba vingine vinne na mwaka kesho kutwa vitahitajika tena vyumba vinne. Tunaomba hali hii izingatiwe na hasa tuzingatie vile vile kwamba, hata hizi shule tunazojenga kwa kweli hazijatosheleza bado, tuna upungufu mkubwa sana. Katika baadhi ya maeneo, nafikiri Njombe watakuwa wameshajenga shule ya sekondari kwenye kila Kata, sasa labda kwenye kila kijiji pengine. Sisi wa Dar es Salaam hata Kata bado, ukienda pale Kimara hakuna shule ya sekondari, Ubungo hakuna, Mazese hakuna na kuna utitiri wa watu, Makurumla, Mburahati, Mabibo hakuna shule za sekondari katika maeneo yale. Tuna jukumu la kujenga, lakini tuna tatizo linalotokana na miji kutokupangwa. Kila mtu anajenga anavyotaka, bila kuacha maeneo ya kujenga hizi huduma za jamii.

Kwa hiyo Dar es Salaam tuna mahitaji ya shule, hatuna mahali pa kujenga, kwa kuwa hapakutengwa. Sasa naomba haya mambo tuwe tunayazingatia, tunapoandaa mipango sasa ya kuendeleza Dar es Salaam, wakija kuangalia Ubungo Plaza na taa zile zikiwaka, wanafikiri Dar es Salaam kila jambo ni zuri. Lakini ukija kuingia Dar es Salaam kwenyewe, ukaanza kuitazama ni matatizo kweli kweli, hatuna maeneo ya kujenga shule, lakini shule tunazihitaji. Inabidi tulipe fidia ili watu watupishe tuweze kujenga shule, lakini fidia yenyewe sasa unakuta mtu ana eneo na kijumba chake pale anataka shilingi milioni 60, ukienda kwenye Halmashauri shilingi milioni 60 ndiyo umeifilisi. Haya tunasema kwamba, tutafanya *fund raising*, ukiwakaribisha watu, ukiwapa chakula cha jioni wanakuachia hapo shilingi 10,000, hazitoshii kulipa shilingi milioni 60. Kwa hiyo, hali yako inabakia kuwa ngumu vile vile. (*Makofii*)

Mheshimiwa Waziri tunaomba kwa kasi ile tulivoanza nayo, wakati tunapoangalia mambo ya Dar es Salaam, tuangalie na suala hili linalotokana na matatizo ya maendeleo ya Jiji ambalo halikupangwa. Asilimia 75 ya Jiji la Dar es Salaam, kila mtu kajenga anavyojua, ni matatizo makubwa, hata barabara za kwa kupita hakuna. Sasa tukiacha vile vile maeneo ya kujenga shule, katika mikoa yote ukienda utakuta maeneo ya kujenga shule si tatizo, tatizo ni kupata rasilimali ya kujenga shule hizo. Sisi hata maeneo hatuna.

Lakini kuna jambo lingine linalofuatana na hilo kwamba, hizi shule tunazojenga inabidi turudi kwa yale maeneo ambayo angalau tunayo. Maeneo ya Shule za Msingi. Lakini Shule za Msingi tulijenga kama tunavyojenga kama kwa ndugu ya Rwiombwa, ambako wana maeneo makubwa. Tumezisambaza sana zile shule, inabidi turudi tubadilishe ujenzi ili twende juu tuweze ku-*accommodate* Shule ya Msingi na tuweze kuweka Shule ya Sekondari katika eneo lile lile. Sasa gharama za ujenzi ni tofauti, haziwezi kuwa zile zile za kujenga kwa kusambaa tu. Kujenga shule ya msingi inayokwenda juu kama tulivyojengewa na *Tiger* pale Mbezi Luisi, itachukua gharama kubwa zaidi kuliko kujenga kwa kusambaa tu na bila kujali sana kuandika.

Kujenga shule ya sekondari kama tulivyojenga Benjamin William Mkapa, inayokwenda juu, inabidi vile vile kuingia gharama kubwa zaidi. Lakini wakati

tunapopewa hizi rasilimali, mambo haya hayazingatiwi na kwa hiyo, inakuwa ni tatizo kubwa kweli kweli.

Naomba niseme kwamba, wananchi wa Dar es Salaam, wapo tayari kushughulikia mambo haya. Kulikuwepo hisia kwamba, wananchi wa Dar es Salaam hawatachangia maendeleo yao, hii si kweli hata kidogo. Katika shule moja ya Serikali katika hizi zilizoanza juzi, Mwalimu Mkuu aliita wazazi ili azungumze nao juu ya mambo ya maendeleo ya shule na mahitaji ya watoto wao, wazazi wote walikuja, mimi sijapata kuona. (*Makofifi*)

Wazazi wote walikuja kuonesha kwamba, walikuwa tayari kushirikiana na Mwalimu Mkuu, kuhakikisha watoto wao wanapata elimu. Kwa hiyo, wazazi wa Dar es Salaam, wanataka watoto wao wapate elimu kama tunavyotaka katika maeneo mengine. Tatizo ni lazima tuwa-*mobilize*, lakini sasa uwezo nao una kikomo, tunaomba Wizara iangalie jinsi ya kutusaidia.

Kwa hiyo, naomba tusaidiwe katika Shule za Msingi, kuhakikisha ujenzi unaendelea na kuhakikisha kwamba mahitaji ya kuendeleza shule zile yanaendelea kupatikana; nyumba za walimu zinajengwa; samani zinapatikana na kadhalika na kwa sekondari hivyo hivyo. Nikiangalia katika shule za msingi, anatuambia Mheshimiwa Waziri, ametenga shilingi bilioni tatu, lakini nikiangalia kifungu kinachotangulia chini lile fungu la 3001 naona kuna shilingi bilioni 27. Nikafikiri hizi zingekuwa ndizo zinazoendeleza hizo shule za msingi, kasi ingekuwa ni mpya. Lakini kama ni shilingi bilioni tatu tu, itakuwa ni ile kasi ya jana, tutakwenda pole pole.

Kwa hiyo, naomba sana hizi fedha nyingi ndiyo zitumike kuendeleza sasa Shule za Msingi, tuweze kujenga nyumba nyingi zaidi, kama zinavyohitajika. Kwa sekondari, naona tumewekewa pesa kidogo, ambazo zinatia matumaini kwamba, tunaweza tukafika mahali tukaenda vizuri kidogo. Lakini naomba nimkumbushe Mheshimiwa Waziri, sijui kama anakumbuka, katika shule zote tulizojenga, hakuna hata moja yenye *Form Five*. Tunajitahidi kupambana na *Form One* mpaka *Form Four*. Hata zile tulizojenga bado hazijakamilika, maana Jengo la Utawala hakuna, Maabara hakuna, Mama Ngwea anazungumzia na *Library*. Mama hilo wala hatujaliweka kichwani bado. (*Makofifi*)

Tanapambana na haya mengine kwanza, ili watoto wapate mahali pa kukaa, madawati, vyoo, bado hata ile ngazi ya kwanza hatujaikamilisha. Lakini wakati tunaikamilisha hii, inabidi twende kwenye ngazi ya pili ya kuanzisha Kidato cha Tano na cha Sita katika baadhi ya shule. Kwa sababu mpango wetu ni kwamba, ifikapo mwaka 2009 ni lazima nusu ya watoto wanaomaliza Kidato cha Nne, waende Kidato cha Tano. Hicho Kidato cha Tano kiko wapi? Kwa hiyo, tunakuwa tuna Sera isiyotkelezeka, kwa sababu hatukuweka miundombinu ya kuitekeleza.

Sasa namwomba sana Mheshimiwa Waziri, alitazame na hili ili katika mwaka unaokuja, tuteuwe baadhi ya shule ziwe na Kidato cha Tano ili twende Kidato cha Sita na tulifikiri mwaka huu tunganeza na Kiluvya, lakini tumechelewa hatukufanya hivyo.

Kuna Mbezi hii ingeweza ikaanza, Yusuf Makamba nayo ingeweza ikaanza. Tuna shule kadhaa, ambazo ziko katika mazingira ambayo yangeweza yakatuwezesha, tukaanza sasa kuwa na shule zenye Kidato cha Tano ili twende Kidato cha Sita kutimiza hii azma, nusu ya watoto wanaomiliza Kidato cha Nne kwenda Kidato cha Tano. Lakini nasema mwanzo ni mzuri hasa kwetu sisi wa Dar es Salaam, ambao kwa kweli tulikuwa tumeachwa nyuma na kila mtu. Mbunge wa Chunya analalamika, anasema ziko nne. Sisi kwa kweli tulikuwa tumelala mno. Bahati nzuri tumegutuka na naomba kasi hii tuendelee nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kusema, hakuna nchi iliyoendelea bila ya elimu. Elimu ni msingi wa lazima kwa maendeleo. Ukiangalia katika nchi nydingi, idadi ya watu wasiojua kusoma na kuandika, mara nydingi sana inaoana na umaskini uliokithiri. Utakuta ni asilimia 25 wasiojua kusoma na kuandika, asilimia 25 fukara. Kunaelekea kuwepo uhusiano wa karibu sana kati ya kujua kusoma na kuandika na kutokujua kusoma na kuandika. Kwa hiyo, ni lazima tuendelee kuwekeza katika watu kama tulivyoanza. Mimi nafikiri tumpata jeshi zuri katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı, yenye Waziri ambaye ni makini, mjuzi na mzoefu wa elimu, akisaidiwa na Naibu Mawaziri, ambao wanajituma kweli kweli, pamoja na Watendaji ambao wamebobea, wengine wamekuja katika Ubunge humu, watatusaidia kusukuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunategemea kwa kweli kwamba, haya malengo ambayo yanatiliwa mkazo sana na Serikali ya Awamu ya Nne, yatatumiwa kikamilifu. Lakini kuna kujituma ambako lazima tufanye, kuna kushirikiana ambako lazima tuhakikishe kwamba, kila mtu anayehusika, anatoa ushirikiano ili malengo haya yaweze kutimizwa kama inayostahili. Mimi nataka kumhakikishia tu Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wengine wote wa Wizara kwamba, Wabunge wote wa Dar es Salaam, wako nyuma yenu, wako pamoja nanyi, tutashirikiana mpaka tuhakikishe kwamba, tunafanikiwa katika yale tutakayopanga kufanya. Naona kuna wanaoguna, lakini naomba na ninyi mtoe ushirikiano ili kwenu nanyi mpate mafanikio kama tunayoomba kwa Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache, naomba kutamka kwamba, naiunga mkono hoja kikamilifu. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, anasema kutokusoma kunahusiana na umaskini. Amesahau kwamba, ndiyo baba wa umaskini na uharibifu wa mazingira. Alisema Mzee Ali Hassan Mwinyi. Sasa ndugu zangu, naona tunakaribia kumaliza, isipokuwa nina tangazo moja.

Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, anawatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba, kesho tarehe 20 Julai, 2006, saa 7.00 mchana watakuwa na mkutano chumba namba 227. Pia anawaomba mkitoka hapa sasa, mwende kwenye *Pigeon Holes* kila mmoja, kuna makabrasha ya mkutano wa kesho. Kwa hiyo, ukiyachukua makabrasha saa hizi, utajiandaa vizuri kwa kikao hicho cha kesho saa 7.00 mchana, chumba namba 227.

Baada ya hayo, naona shughuli za leo tumekaribia kuzikamilisha. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge na kuahirisha kikao mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.37 usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Alhamisi  
Tarehe 20 Julai, 2006 Saa Tatu Asubuhi)*